Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Ishirini na Tisa - Tarehe 22 Julai, 2003**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania *(TAFIRI)* kwa Mwaka wa Fedha 2001/2002 *(The Annual Report and Audited Accounts of the Tanzania Fisheries Research Institute for the Year 2001/2002).*

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania *(TAFORI)* kwa Mwaka wa Fedha 2001/2002 *(The Annual Report and Audited Accounts of the Tanzania Forestry Research Institute for the Year 2001/2002).*

Hotuba ya Waziri wa Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2003/2004.

**MHE. ANNE S. MAKINDA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Kamati ya Maliasili na Mazingira kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii katika mwaka uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2003/2004

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 279

**Mapato ya Serikali**

**MHE. LEONARD N. DEREFA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali hukusanya fedha na mapato yake kutokana na sheria zilizopo; na kwa kuwa thamani ya fedha ya Tanzania inazidi kuporomoka; je, isingekuwa busara kwa Serikali kurekebisha sheria zinazotumika kukusanya maduhuli au mapato ya Serikali kila baada ya miaka mitano ili kuiwezesha Serikali kupata mapato yanayolingana na hali halisi?

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leonard Derefa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Serikali hukusanya kodi na mapato yake mengine kukidhi mahitaji yake kwa mujibu wa sheria zilizopo na ni kweli kwamba, thamani ya fedha ya Tanzania imekuwa ikishuka mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, ili Serikali iweze kupata mapato yanayokidhi mahitaji yake ya kila mwaka na kukabili tatizo la kushuka kwa thamani ya fedha. Kila Bunge la Bajeti linapokutana, Serikali imekuwa ikiwasilisha Muswada wa Sheria ya fedha wa kurekebisha sheria mbalimbali za kodi ili pamoja na mambo mengine, iweze kukabiliana na tatizo la kushuka thamani ya fedha yetu. Urekebishaji wa sheria hizo hufanyika baada ya utafiti wa kina kuhusu tathmini ya mapato ya Serikali na tatizo la fedha kushuka thamani katika Bajeti ya mwaka husika. Maandalizi ya mfumo wa mapato kila mwaka yanazingatia vigezo halisi vya uchumi ikiwa ni pamoja na mfumuko wa bei, ukuaji wa uchumi na kushuka kwa thamani ya fedha.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mahitaji halisi ya Serikali ya kila mwaka na tatizo la fedha kushuka thamani mara kwa mara, kipindi cha miaka mitano alichopendekeza Mheshimiwa Mbunge ni kirefu. Aidha, Serikali inaona ni busara kuendelea na utaratibu uliopo sasa wa kurekebisha sheria zake za fedha kila mwaka badala ya miaka mitano mitano ili mapato yanayokusanywa yakidhi mahitaji halisi ya Serikali kwa mwaka husika.

Na. 280

**Makusanyo ya Kodi**

**MHE. THOMAS NGAWAIYA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imekiri kukusanya kodi ya shilingi bilioni 100 kwa mwezi; na kwa kuwa Viongozi wa Serikali ni waadilifu, wawazi na wakweli katika utendaji wao:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kutokana na makusanyo hayo kinatumika hapa nchini na kila Mkoa hupata kiasi gani na ni nani anayepokea fedha hizo kwa kila mwezi?

(b) Je, Serikali inaisaidiaje sekta ya kilimo kutokana na kodi hiyo kila mwezi hasa ikitiliwa maanani kwamba kilimo ndiyo sekta mama ya uchumi wetu?

(c) Je, ni fedha kiasi gani inatumika kulipia madeni ya ndani ya nchi kutokana na kodi hiyo?

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mbunge wa Moshi Vijijini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kutokana na Bajeti ya mwaka wa fedha 2003/2004, makisio ya ukusanyaji wa mapato yanayotokana na kodi yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 1.28. Fedha zote zinazotokana na makusanyo hayo hutumika hapa nchini kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali za Serikali za kawaida na za maendeleo. Hata hivyo, kwa kuwa fedha hizi huwa hazitoshelezi mahitaji, Bajeti ya Serikali hutegemea kwa kiwango kikubwa misaada na mikopo ya nje inayotolewa na wahisani. Kwa mfano, asilimia 45 ya Bajeti ya mwaka huu wa fedha inatokana na misaada pamoja na mikopo nafuu kutoka nje.

Aidha, fedha zote zinazokusanywa na Serikali yaani kutokana na kodi, mikopo na mapato mengine, hupelekwa kwenye Mfuko wa Hazina ambako utaratibu wa kuzigawa kwenye Wizara, Taasisi za Serikali na Mikoa hufanyika.

Kwa upande wa Mikoa, fedha zinazotengwa kwa kila Mkoa hupelekwa kila mwezi na kila Mkoa hupata sehemu 1/12 (asilimia 8.3) ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya Mkoa husika. Kwa mwaka

2002/2003, jumla ya shilingi bilioni 13.619 zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida *(OC)* zilipelekwa Mikoani kama zilivyopitishwa katika Bajeti.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali katika kuikuza sekta hii. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2003/2004, hatua zilizotangazwa kwenye Hotuba ya Bajeti ni pamoja na:-

(i) Mipango ya kuendeleza kilimo katika ngazi ya Wilaya;

(ii) Kufidia gharama za usambazaji wa pembejeo muhimu kwa Mikoa minne ya Kusini Magharibi na pia kuendeleza Mfuko wa Pembejeo;

(iii) Kupanua Mfuko wa Udhamini wa Mikopo kwa mauzo ya nje ya nchi *(Export Credit Guarantee Scheme)* na pia Mfuko wa udhamini kwa wakulima/wafugaji wadogo na wanaojishughulisha kibiashara. Pia kuanzisha Mfuko wa kuendeleza sekta ya Mifugo *(Livestock Development Fund).* Fedha za Mfuko huu zitatokana na ushuru wa asilimia 20 utakaotozwa ngozi ghafi zitakazouzwa nje; na

(iv) Kuendeleza shughuli za mafunzo na utafiti, upatikanaji wa madawa, zana za kilimo, umwagiliaji mashamba na kadhalika kama ilivyoelezwa katika hotuba za Mawaziri wa Kilimo na Chakula, Maji na Mendeleo ya Mifugo na Ushirika na Masoko.

Zaidi ya hayo, Serikali imekuwa ikiipa sekta ya kilimo kipaumbele katika mgao wa fedha, kama sekta zingine za kupunguza umaskini kwa kuipatia mgao wa miezi mitatu mwanzoni mwa kila robo ya mwaka wa fedha.

(c) Kiasi cha fedha kitakachotumika kulipa madeni ya ndani na ya nje katika mwaka wa fedha 2003/2004, ni shilingi bilioni 835.1. Kiasi hiki kinajumuisha malipo ya deni la ndani la shilingi bilioni 626.3 na deni la nje la shilingi bilioni 208.8.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Vile vile namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa majibu yake mazuri kama ni kweli inatekelezwa hivyo. Kwa kuwa tunapokopa fedha nje tunaambiwa ni msaada, inakuwaje sasa huo msaada unageuka? Kwa kuwa wao wenyewe wanaotukopesha ndiyo wanao-*detect* kushuka kwa thamani ya fedha yetu au kupanda. Sasa unaitwaje msaada wakati kuna riba na ni deni kwa nini tusiseme tu kwamba huu ni mkopo badala ya kusema msaada?

Pili, kwa kuwa mikopo kama tuliyokopa ya *TANESCO* wakati huo ilikuwa dola moja ni shilingi mia saba na leo hii tunalipa shilingi elfu moja na kitu kwa dola moja, inatuathiri sana kwa sasa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha jambo kama hili halitokei kwa sababu sasa hivi tunapata madhara makubwa hasa kwa malipo tunayolipia madeni ya *TANESCO?*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, mkopo ni mkopo na msaada ni msaada. Nchi wafadhili wanapotupa msaada ni msaada kweli kweli, hauna riba wala kudaiwa baadaye, ni msaada wa kweli kweli. Lakini licha ya msaada, Serikali huwa pia inakopa kwa Serikali nyingine au mabenki duniani. Serikali inapokopa hivyo inakopa kwa masharti ya mkopo wenyewe, yaani yale ambayo yametolewa na mwenye kukopesha. Kwa hiyo, kama riba ni sehemu ya masharti hayo, basi ndiyo mkopo wenyewe lazima uwe na masharti. Lakini inapofika siku ya kulipa huo mkopo maana msaada haulipwi siku ya kurejesha mkopo na ndivyo ilivyo katika makubaliano, Serikali huwa inalipa thamani ya dola ya leo. Kama Serikali ilikopa kwa ajili ya miradi fulani ya *TANESCO* miaka ishirini iliyopita na leo inatakiwa ilipe inalipa kwa thamani ya dola ya leo siyo ya wakati ule tuliokopa, hivyo ndivyo ilivyo. *(Makofi)*

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nchi nyingi sasa hivi zinasamehe madeni katika nchi yetu ya Tanzania na kwa kuwa Tanzania kuna tatizo kubwa la uhaba au shida ya maji huko Vijijini hasa Mkoa wa Mtwara na Vijiji vyake. Je, Serikali zile fedha ambazo inasamehewa madeni isingekuwa vizuri kuwasaidia wananchi hao ili wapate maji ya uhakika? *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli lingekuwa jambo zuri sana kama wenye madeni wangeyafuta au kuyageuza kuwa msaada, lakini kwa bahati mbaya sivyo ilivyo kwa nchi zote duniani sasa hivi. Suala la madeni Serikali yetu imekuwa ikilivalia njuga kwa muda mrefu, baadhi ya nchi hasa zile ambazo ni matajiri (nchi za *G 8*), zimefuta madeni kabisa na baadhi ya nchi zingine zinafuta nusu, wengine wanafuta robo na kadhalika. Lakini bado kuna baadhi ya nchi ambazo hazitaki kufuta madeni, kwa hiyo, tunaendelea kubeba hayo madeni na tutaendelea kulipa kwa sababu uungwana wenyewe ni kulipa madeni. Nakubaliana naye kwamba, kuna haja ya kuendelea kuzungumza katika mikutano na majadiliano mbalimbali ya Kimataifa baina ya nchi kwa nchi ili kuzibembeleza zile nchi zinazotudai kufuta madeni, lakini kazi hii ni ngumu na tunaendelea nayo.

Na. 281

**Benki ya Ardhi *(Land Bank)***

**MHE. JOEL N. BENDERA (k.n.y. MHE. TALALA B. MBISE)** aliuliza:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya kuwepo kwa Benki ya Ardhi *(Land Bank)* na ni kiasi gani cha ardhi kimetengwa kwa lengo hilo na ni wapi?

(b) Je, wananchi watafaidikaje na benki hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Talala Bana Mbise, Mbunge wa Arumeru Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Benki ya Ardhi *(Land Bank)* ni majumuisho ya ardhi itakayotambuliwa nchini kote na kutengwa kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na kutoka nje ya nchi. Kuanzishwa kwa Benki ya Ardhi ni kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Ardhi Ibara ya 4.2.4(iii), inayoeleza kuwa watu wasio raia watamiliki ardhi kwa ajili ya uwekezaji tu na kwa kufuata sheria ya uendelezaji uwekezaji na Ibara ya 4.2.8(i) inayoelezea kuwa, maeneo maalum yatatambuliwa na kutengwa na Serikali kwa ajili ya wawekezaji. Dhana hii pia ipo katika Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999 fungu la 20.2 inayoelezea kuwa ardhi kwa ajili ya uwekezaji itatambuliwa, itatangazwa katika Gazeti la Serikali na itagawiwa kwa Kituo cha Uwekezaji *(TIC)*. Hivyo, uundaji wa Benki ya Ardhi ni sehemu ya kutekeleza Sera na Sheria za Ardhi.

Mheshimiwa Spika, ardhi itakayounda Benki ya Ardhi itachangiwa na maeneo ya ardhi isiyotumika Vijijini na ardhi zinazomilikiwa na watu binafsi ambao wako tayari kuingia ubia katika shughuli za uwekezaji. Serikali imetenga kiasi cha shilingi 100,000,000/= ili kubaini maeneo haya nchini kwa kushirikiana na Halmashauri za Jiji, Manispaa, Wilaya na Miji. Hadi sasa Wizara yangu kwa kushirikiana na TAMISEMI, inaratibu utafiti huu kwa kushirikiana na wadau wengine wa Serikali Kuu.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na kuanzishwa kwa Benki ya Ardhi wananchi watafaidika kama ifuatavyo:-

(i) Wawekezaji wataondolewa kero iliyopo sasa katika upatikanaji wa ardhi kwa kuwa ardhi itakuwa imekwishabainishwa. Hali hii itaongeza kasi ya uwekezaji nchini;

(ii) Wawekezaji hawataweza kuingia Mikataba kiholela na wanavijiji kinyume cha sheria za ardhi kwa kuwa ardhi itakuwepo na itagawiwa kwa wawekezaji kupitia *Tanzania Investment Centre (TIC)* pale inapotakiwa;

(iii) Maeneo yaliyokwishatambuliwa na yanayoendelea kutambuliwa nchini kote yatatumika kwa wawekezaji wa ndani na kutoka nje ya nchi katika shughuli za kilimo, ufugaji, utalii, uchimbaji wa madini

na viwanda. Shughuli hizo zikiimarika, uzalishaji wa mazao utaongezeka na hali ya maisha ya wananchi wengi itakuwa imeboreshwa kwa kuwa watapata ajira, masoko na kadhalika; na

(iv) Kuongeza Pato la Taifa kwa kuwa uzalishaji wa mazao ya biashara na chakula utaongezeka, uchimbaji wa madini utaongezeka, uzalishaji katika viwanda pia utaongezeka, hayo yote yataongeza Pato la Taifa.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo tu moja la nyongeza. Kwa kuwa wananchi wengi nchini Tanzania wanaishi Vijijini na ndiyo wenye ardhi ndogo ndogo ambazo Mheshimiwa Waziri amesema ni lazima kwanza utafiti ufanyike, lakini kimsingi ni kwamba wananchi wengi wadogo wadogo ndiyo wenye ardhi. Je, Wizara hii itafanya namna gani ili wananchi hawa wadogo wadogo wafaidike na benki hii ambapo wakubwa wengi wanaweza kufaidika na benki hii? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, wananchi Vijijini watafaidika kwa sababu mradi huu utaendelea Mikoa yote. Mikoa yenye maeneo makubwa yaliyobainishwa katika hatua ya awali ya kutambua maeneo, yatatengwa kwa ajili ya wawekezaji kwa kuanzia maeneo yenye ukubwa wa hekta 5,000. Kwa mfano, Mikoa tuliyotambua ni Mkoa wa Pwani, Dodoma, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Mara, Morogoro, Ruvuma, Shinyanga, Singida, Tabora, Tanga na Dar es Salaam. Kwa hiyo, sasa tayari Wizara kwa kushirikiana na wataalam kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, Kilimo na Chakula, Maji na Maendeleo ya Mifugo, TAMISEMI, Ofisi ya Rais (Mipango na Ubinafsishaji) na Kituo cha Taifa cha Uwekezaji, wanafanya uhakiki ili kubaini hali halisi ya upatikanaji wa maeneo hayo ili yaweze kupimwa. Baada ya hapo Wizara yangu itakabidhi kwa *TIC* ili yawekwe kwenye hazina ya ardhi kwa matumizi ya uwekezaji. Kwa hiyo, wanakijiji watafaidika tu kwa sababu timu hizi ambazo zimekusanya, Hazina pia na TAMISEMI wanatembea nchi nzima kuweza kutambua maeneo hayo. Kwa hiyo, siajabu na wanakijiji nao watafaidika katika utambulishi huu wa maeneo ambao unataka kuleta hiyo *Land Bank.*

**MHE. ANATHORY K. CHOYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa kwa kawaida wananchi wa Tanzania hawana uzoefu katika uwekezaji wa ndani, hivi Serikali kwa makusudi mazima itawawezeshaje Watanzania ili waweze kushindana na hawa wanaotoka nje? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, itawezekana, ndiyo maana katika jibu langu la msingi nilisema wataalam wanazunguka nchi nzima katika sekta mbalimbali, kuwaelimisha na kuweza kutambua maeneo ambayo tutaiweka hiyo *Land Bank*. Kwa hiyo katika timu hii itakayokuwa inazunguka, nina hakika na wao watashirikishwa. Sasa ufahamu wao itategemea kwa sababu watakuwa hawa wataalam wakiendelea na wao watashiriki, kushiriki kwao ndiyo ufahamu wao. Kwa hiyo, nina hakika watapata faida katika timu hizi ambazo nimesema kwamba, Wizara ya Ardhi yenyewe imo katika uhamasishaji, pamoja na Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Kilimo na Chakula, Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, Wizara ya Maliasili na Utalii na *Tanzania Investment*. Kwa hiyo, timu yote hii nina hakika wananchi watapata tu uelewa mzuri na kuweza kuingia katika uwekezaji huu. *(Makofi)*

Na. 282

**Nafasi za Ajira zinazotangazwa**

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA (k.n.y. MHE. ABDULKARIM E.H. SHAH)** aliuliza:-

Kwa kuwa Watanzania walio wengi sasa wanafahamu kuwa urithi pekee kwa mtoto ni kumpatia elimu; na kwa kuwa vijana wengi wanajitahidi sana kusoma na kufaulu mitihani yao katika ngazi ya shule za msingi, sekondari na hata kufikia Vyuo vya juu vya taaluma mbalimbali na hupata vyeti vyao baada ya kufaulu mitihani husika na kuanza kutafuta ajira kwenye Makampuni/Taasisi mbalimbali ambazo zimekuwa zikitangaza nafasi za kazi kwenye magazeti na kwenye vyombo mbalimbali vya habari; na kwa

kuwa miongoni mwa sifa zinazohitajika kwa mwombaji wa nafasi hizo ni uzoefu wa miaka kadhaa wa kazi inayotangazwa kitu ambacho huyo kijana aliyemaliza masomo yake hana na hivyo kumfanya kukosa nafasi hiyo:-

(a) Je, vijana waliomaliza mafunzo na kuomba nafasi hizo watapataje uzoefu unaotakiwa wakati bado hawajaajiriwa na pindi wale wenye uzoefu watakapokuwa wamestaafu au kuacha kazi, wenye uzoefu wengine watapatikana vipi ikiwa wale wasio na uzoefu hawapati nafasi za ajira ili nao wafundishwe kazi na kupata uzoefu kutoka kwa wale ambao tayari wanao uzoefu kabla hawajastaafu?

(b) Je, waajiri wanaotaka watu wenye uzoefu katika kazi husika hawaoni kwamba inaweza kuwa sababu mojawapo ya kuwa na wazembe, wezi au wabadhirifu katika sehemu zao za kazi?

(c) Je, Serikali imeandaa mpango gani wa kuwawezesha vijana hao kupata kazi na hatimaye uzoefu utakaowawezesha waingie katika soko la ajira au Serikali kuwaelekeza waajiri waondoe kipengele hicho cha uzoefu wa miaka kadhaa?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mbunge wa Mafia, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana linatokana na mfumo mzima wa uchumi kutoweza kuchukua nguvu kazi inayoongezeka na vile vile vijana wetu kutokuwa na stadi ambazo waajiri wangezihitaji mara moja kwa ajili ya kuzalisha mali na kutoa huduma.

Mwajiri mwenye busara atachukua vijana na kuwaweka pamoja na wafanyakazi wenzake wenye ujuzi ili hawa wa zamani watakapostaafu au kuacha kazi, vijana watakuwa tayari wanao uzoefu wa kuwawezesha kufanya kazi hizo.

Kwa kuwa mwelekeo wetu sasa hivi ni kuachia sekta binafsi kuendesha uchumi, suala la kutaka Serikali kuwawekea masharti katika kuajiri linakuwa gumu kutekelezwa. Hata hivyo, Serikali itaendelea kuandaa na kusimamia sera na sheria pamoja na taratibu ambazo zitaweka mazingira mazuri ya watu kuweza kujiajiri na kuajiriwa.

(b) Waajiri wenyewe wanaweza kuwa na majibu sahihi kuhusu athari ambazo zinaweza kujitokeza kwa kuwa na wafanyakazi wazoefu tu. Jambo hili halijafanyiwa utafiti, kwa hiyo, hakuna jibu la uhakika kwa sasa.

(c) Inakuwa vigumu kuwazuia waajiri wasiweke kipengele cha uzoefu kwa vile mwenendo na mpangilio mzima wa uzalishaji na utoaji huduma, wao ndio wanaouelewa zaidi hasa ikizingatiwa kuwa sekta binafsi imeachiwa kuendesha biashara kwa ushindani. Serikali itaendelea kusimamia utaratibu ambao utawawezesha vijana kupata stadi mbalimbali zitakazowawezesha kuajiriwa na hata kujiajiri wenyewe. Tukumbuke kwamba, historia ya waajiri wengi duniani ni wale walioweza kujiajiri wenyewe kwanza.

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niulize swali la nyongeza. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini nina swali dogo. Kwa sababu uzoefu umeonyesha kwamba waajiri wengi wanataka waajiriwa au watu wanaoomba kazi wenye sifa na ambao wana uzoefu. Sasa je, Serikali ipo tayari kuweka utaratibu katika kila Chuo wa kuwa na mafunzo ya vitendo ili kuhakikisha kwamba kila anayemaliza basi pamoja na ujuzi lakini vile vile atakuwa na uzoefu wa kufanya ile kazi kutokana na mafunzo ya vitendo, Serikali itakuwa tayari kufanya hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, utaratibu wa Vyuo vyetu vingi ni huo anaouzungumza wa kuwa vile vile na elimu ya vitendo. Walimu wanakuwa na majaribio ya kufundisha, ndiyo tunaita walimu tarajali, ukienda Chuo Kikuu na wenyewe wanakuwa na elimu kwa vitendo. Hata sasa hivi kufuatia mpango huu wa *HIPC*, Wizara ya Kazi ina fungu maalum la kuwasaidia wahitimu hasa wa mambo ya Uhandisi kutoka Chuo Kikuu ili kuweza

kupata mafunzo kwa vitendo kupitia Vyuo vyetu vya *VETA* kufuatana na elimu waliyoipata Chuo Kikuu. Kwa hiyo, utaratibu huo upo lakini bado kwa ajira hautoshelezi maana wao wanataka uzoefu wa ajira, uzoefu wa utumishi siyo uzoefu tu wa mafunzo ambayo ameyapata katika Chuo chake.

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kumwuliza kwamba, je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba idadi kubwa ya wanaomaliza masomo ambao wanazagaa bila ya kupata kazi na kwamba wao hawakuandaliwa kuanzisha kazi za kujitegemea wenyewe, ni nguvu kazi inayopotea bure na kwa maana hiyo Serikali ndiyo inayopaswa kulaumiwa siyo vijana hawa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba sehemu kubwa ya elimu kwa mfumo tulio nao sasa inakwenda kwenye nadharia zaidi kuliko vitendo. Lakini kufuatana na swali la msingi wanachohitaji hawa waajiri ni uzoefu wa kazi, lakini nadharia ya kazi hiyo vijana wetu wanakuwa nayo. Sasa tunazungumza kwamba ili waweze kuwa na stadi zinazotakiwa kwa mujibu wa nadharia zao, ndiyo Serikali imeanza kuchukua hatua kwa mfano, sasa hivi nimesema katika jibu la nyongeza la Mheshimiwa Iwvatta, anayemaliza Chuo Kikuu akipenda kwenda kuiweka elimu yake katika vitendo, Wizara ya Kazi kupitia Mfuko wa *HIPC* inampeleka kwenye vyuo vinavyohusika ili aweze kupata ufundi huo kwa vitendo zaidi ili kuongezea nadharia yake aliyoipata. Kwa hiyo, tunaanza taratibu na bila shaka tunakokwenda mambo yatakuwa mazuri zaidi. *(Makofi)*

Na. 283

**Ongezeko la Mishahara ya Askari Polisi**

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Bajeti ya mwaka 1999/97 Serikali iliongeza mishahara ya wafanyakazi wakiwemo watumishi wa Jeshi la Polisi; na kwa kuwa kuanzia Askari wa kawaida *P/C* hadi *S/Sgt.* hawakupewa ongezeko hilo la mshahara hata kwa asilimia moja kwa muda wa miaka mitatu:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani hadi leo juu ya limbikizo la fedha zao za nyuma tangu lilipotangazwa ongezeko la mishahara hiyo?

(b) Je, ni lini Askari hao watapewa limbikizo la tofauti ya mishahara yao kwa kuwa wamekaa muda mrefu?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Serikali katika Bajeti yake ya mwaka 1996/97 iliongeza mishahara ya watumishi wa Serikali wakiwemo Askari wa Jeshi la Polisi wa ngazi zote. Katika ongezeko hili la mishahara, Askari Polisi wa kawaida *(PC)* waliongezwa mshahara kutoka shilingi 39,620/= hadi shilingi 46,350/= kwa mwezi. Marekebisho haya yalifanywa kwa Askari wa ngazi zote na wote walilipwa.

Hivi sasa Wizara yangu haijapokea malalamiko yoyote kutoka kwa Askari Polisi kuhusu kutorekebishiwa mishahara au kudai limbikizo kufuatia ongezeko la mishahara la mwaka 1996/97. Iwapo yupo Askari mwenye tatizo la aina hii, tunamwomba ajitokeze na hatua za kumsaidia zitachukuliwa mara moja.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa suala hili si la mtu mmoja mmoja na iwapo ataletewa taarifa kamili kuhusu

nyongeza hizi kwa mwaka 1996 kwamba hazikurekebishwa. Je, Mheshimiwa Waziri atalieleza nini Bunge hili ambalo liliwahi kupitisha suala hili kwa ukamilifu?

**SPIKA:** Kama umelielewa swali Mheshimiwa Waziri jibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kama nitaletewa taarifa hizo na tukahakikisha usahihi wake, tutafanya marekebisho yanayohusika na kama tutatakiwa kuliarifu Bunge kuhusu hatua hiyo tutaliarifu. *(Makofi)*

Na. 284

**Polisi Kuwapiga Watuhumiwa**

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD** aliuliza: -

Kwa kuwa baadhi ya Askari Polisi wanapowakamata watuhumiwa la kwanza ni kipigo hata kama hawakuleta ubishi: -

(a) Je, ni haki yake Askari kumhukumu mtuhumiwa?

(b) Kwa kuwa uongo wa Askari si ukweli wa mtuhumiwa; je, atalindwa vipi ili apate haki yake?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mbunge wa Jang'ombe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Jinai *(Criminal Procedure Act),* hakuna mtu anayeruhusiwa ikiwa ni pamoja na Polisi kumpiga mtuhumiwa wakati wa kumkamata. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, Askari Polisi anaruhusiwa kisheria kutumia nguvu za kadri *(Reasonable Force),* pale tu mtuhumiwa anapokaidi kukamatwa au anapokuwa katika hali ya kuokoa maisha yake au maisha ya mtu mwingine yaliyoko kwenye hatari. Ni dhahiri Askari Polisi, hana Mamlaka ya kutoa adhabu ya aina yoyote kwa mtuhumiwa bali ni Mahakama peke yake ndiyo yenye mamlaka hayo.

Endapo mtuhumiwa ataona kuwa Ofisa wa Polisi hakumtendea haki, anayo haki ya kutoa taarifa ya uonevu huo kwa Kiongozi yeyote wa Jeshi la Polisi aliye karibu naye. Au anaweza pia kufungua kesi Mahakamani dhidi ya Polisi aliyehusika na Mahakama itatoa hukumu kwa kuzingatia Sheria. Hivyo, mkondo wa Sheria ndio mlinzi mkuu wa haki za raia wote.

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pia nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, kule kwetu kuna *fish food* anaitwa pweza, huyo ukitaka kumla kwa raha basi umpige kwa magogo tena kwenye mchanga. Sasa Mheshimiwa Waziri anaweza kunihakikishia kwamba Watanzania sasa hivi wameshakuwa kama pweza lazima wapigwe magogo na baadhi ya Askari Polisi? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nimeeleza katika jibu langu la msingi kwamba, Askari Polisi hawaruhusiwi kuchukua hatua kama hizo za kupiga watuhumiwa. Kwa hiyo, ninalowahakikishia Watanzania ni kwamba, hawajawa pweza na wala hawatakuwa pweza na haki zao zitaendelea kulindwa. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pale inapotokea Askari Polisi akamnyanyasa raia na raia akaamua kufungua kesi, lakini Askari Polisi wakamkatalia kufungua kesi kama ilivyotokea Kibaha, je, Mheshimiwa Waziri anasema nini? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nimeeleza katika jibu langu la msingi kwamba, raia anayo haki ama ya kutoa taarifa kwa Maofisa wa Polisi, akikosa ushirikiano na Maofisa wa Polisi anaweza kufungua kesi Mahakamani. Nadhani hawezi kuzuiwa kufungua kesi Mahakamani. Lakini kwa yote hayo kama hayakuwezekana tupo na viongozi wa siasa ndani ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi tutalishughulikia. *(Makofi)*

Na. 285

**Uimarishaji wa Elimu Nchini**

**MHE. KHALID S. SURU** aliuliza: -

Kwa kuwa Serikali imeamua kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya uimarishaji wa elimu nchini kwa kuanzisha programu kamambe ya Elimu ya Msingi (MMEM) kwa wote ifikapo mwaka 2006 kwa kusisitiza uboreshaji wa madarasa, nyumba za Walimu, maliwato mashuleni, vifaa mbalimbali vya kufundishia na kujifunzia, Walimu wa kutosha na mazingira ya shule kwa ujumla: -

(a) Je, hadi sasa, Serikali na wananchi wameshajenga madarasa, nyumba za Walimu na vyoo vingapi kwenye mashule nchini kote na ni Walimu wangapi wameajiriwa tangu mpango huo mpya uanze hapa nchini?

(b) Je, ni Mikoa na Wilaya gani zinazoongoza katika kutekeleza vizuri mpango huo ukiorodhesha Mkoa wa kwanza hadi wa mwisho na vivyo hivyo kwa Wilaya?

(c) Je, katika Mkoa wa Dodoma ni Wilaya ipi inaongoza katika mpango huo wa ujenzi wa madarasa na ni kwa kiwango gani?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalid Suru, Mbunge wa Kondoa Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa kwanza na wa pili wa utekelezaji wa Mpango wa MMEM, ilipangwa kujenga jumla ya madarasa 27,264 na nyumba za walimu 15,732. Hadi sasa Serikali kwa kushirikiana na nguvu za wananchi katika Halmashauri mbalimbali nchini, jumla ya madarasa 16,464 yamekamilika sawa na asilimia 60.4 ya lengo na mengine yanaendelea kujengwa kutokana na ruzuku ambayo imetumwa kwa Halmashauri mwezi huu wa Julai. Aidha, jumla ya nyumba za walimu 7,085 zimekamilika na nyumba 7,732 zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi na jumla ya mashimo ya Maliwato 72,913 yamejengwa, ambayo ni asilimia 99.6 ya lengo la kuongeza mashimo ya maliwato 75,453.

Aidha, Serikali katika kipindi hicho cha miaka miwili ya mpango ilipanga kuajiri jumla ya walimu daraja la IIIA 20,751, hadi kufikia tarehe 30 Mei, 2003 jumla ya walimu 17,854, ambayo ni asilimia 86.04 ya lengo walikuwa tayari wameajiriwa na jumla ya walimu tarajali ambao bado wako mafunzoni 7,055 wamegawiwa katika Mikoa yote 21, ambao watakapohitimu na kuajiriwa lengo litavuka kwa karibu walimu 4,000.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa sasa bado ni mapema mno kuorodhesha Mikoa na Wilaya zote. Lakini kwa tathmini ya awali Mikoa na Wilaya bora zinazoongoza mpaka sasa katika utekelezaji wa mpango huu ni kama ifuatavyo: -

(i) Ujenzi wa nyumba za walimu kwa wingi ni Mkoa wa Ruvuma, Dodoma, Iringa, Tanga, Mwanza, Shinyanga, Mara, Arusha na Kilimanjaro. Wilaya zinazoongoza ni Songea Vijijini, Mpwapwa, Songea Mjini, Njombe, Muheza, Kwimba, Bariadi na Tarime.

(ii) Kuhusu ujenzi wa vyumba vya madarasa Mikoa inayoongoza kwa ubora ni Mtwara, Ruvuma, Kilimanjaro, Kagera, Mara, Kigoma, Arusha, Lindi, Pwani na Tabora. Wilaya zinazoongoza ni Rombo, Bunda, Newala, Kibondo, Masasi, Mbeya Vijijini, Hanang, Mtwara Vijijini, Kondoa na Biharamulo.

(iii) Kwa ujenzi wa maliwato Mikoa inayoongoza ni Kilimanjaro, Morogoro, Mara, Ruvuma, Mwanza, Mbeya, Rukwa, Arusha, Kagera na Singida. Wilaya zinazoongoza ni Mbinga, Moshi Vijijini, Rombo, Musoma Vijijini, Morogoro Vijijini, Kilosa, Masasi, Same, Manyoni na Karagwe.

Narudia kusema kwamba, hii ni tathmini ya awali kabisa kwa sababu bado ni mapema mno kuweza kutoa taarifa hii kwa usahihi.

(c) Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Dodoma, Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa inaongoza kimkoa katika ujenzi wa madarasa kwa kukamilisha ujenzi wa madarasa 206, ikifuatiwa na Dodoma Manispaa madarasa 105, Dodoma Vijijini madarasa 48, Kongwa madarasa 33 na Mpwapwa madarasa 24. *(Makofi)*

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.

(a) Kwa kuwa mpaka sasa wale walimu walioajiriwa hivi karibuni hawajaanza kupata mishahara wala hawajapata hata posho za kuanzia maisha. Je, Serikali inatoa tamko gani kwa sababu mwisho wa mwezi wa Julai ni mbali wataishije ili waweze kufanya kazi zao vizuri? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa inasemekana kwamba kuna baadhi ya Watendaji wa Halmashauri mbalimbali katika nchi hii wametumia fedha za madarasa, maliwato na vitu vingine kinyume cha utaratibu ulivyokusudiwa. Je, Serikali ipo tayari kufuatilia na kama itabainika watachukuliwa hatua gani? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, la kwanza hao walimu ambao wameajiriwa, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, fedha yao iko katika Bajeti na uamuzi uliofanywa ni kwamba, wakati wakiwa bado ni walimu tarajali, wako katika mafunzo, watalipwa asilimia 80 ya mshahara. Sasa kama kuna kukwama kokote, napenda nichukue nafasi hii kutoa maagizo kupitia Bunge hili na kupitia tamko hili kwamba, wanaohusika wafanye haraka kuhakikisha kwamba fedha za malipo ya mishahara ya walimu tarajali zinatumwa kwa Halmashauri za Wilaya walikopangiwa kufanya kazi haraka kabisa kabla ya mwisho wa mwezi Julai ili waweze kulipwa fedha zinazotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Watendaji ambao wametumia fedha vibaya za mwaka wa kwanza, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali imeshachukua hatua kufanya uchunguzi unaotakiwa. Lakini pia Halmashauri hizo ambazo fedha zake zimetumiwa vibaya, mafungu ya mwaka huu yamesimamishwa hazikutumwa fedha mpaka tupate maelezo ya matumizi yanavyohitajika na tuwe na uhakika kama fedha hizo zimepotea kabisa wahusika wamechukuliwa hatua zinazotakiwa. Kwa hiyo, jambo hili tunalisimamia kwa bidii na nguvu zote za Kiserikali.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, kuhusiana na suala la Uimarishaji wa Elimu ya Msingi nchini na kazi nzuri ambayo inafanywa na Wizara hii, ningependa kuuliza kwamba, lipo eneo ambalo limesahaulika sana nalo ni eneo la Waratibu wa Elimu wa Kata.

Je, Wizara ina mpango gani wa kuimarisha nafasi hii kwa kuhakikisha kuwa Waratibu hawa wanapata ofisi, wanapata pikipiki na wanapata fedha za kufanyia kazi ikiwezekana hata wapate wasaidizi wa kuwasaidia ili kuweza kuimarisha na kuboresha mafanikio mazuri ya Mpango huu wa Maendeleo ya Elimu ya Misingi nchini? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu kulegalega na kutokuwa na vifaa vya kufanyia kazi Waratibu wa Elimu wa Kata, ningependa kumhakikishia kwamba, jambo hili katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi limeanza kusahihishwa. Katika mafungu niliyoyatangaza hapa Bungeni na ikitazamwa katika nyongeza A, B na C ya hotuba yangu

ya Bajeti iliyochapishwa katika kitabu maalum, utakuta fedha za uwezeshaji ambazo zimepelekwa katika kila Wilaya kwa ajili ya ngazi ya Kata, zipo zilizopelekwa katika ngazi ya Mkoa, ngazi ya Wilaya na ngazi ya Kata. Fedha hizo zinalenga kuwapa uwezo Waratibu wa Elimu wa Kata kuweza kutembelea shule na kusimamia mambo yanavyokwenda katika shule zao.

Lakini pia katika sheria ya elimu ambayo nimekwishasema hapa Bungeni, inaandaliwa upya kutokana na kuwa na viraka vingi, ambayo tayari rasimu ya kwanza ninayo ninaipitia. Nafasi hii ya Mratibu wa Elimu wa Kata tunalenga kuiimarisha ili awe ni *Ward Education Supervisor* badala ya Mratibu wa Elimu wa Kata ya Elimu ya Watu Wazima. Kwa hiyo, ni nafasi ambayo itajazwa na watu wenye uwezo zaidi na tunategemea kwamba, nafasi hiyo watakaoijaza wawe na uzoefu na ujuzi wa kusimamia shule na angalau na sifa ya *Diploma* ya Ualimu ili waweze kusimamia vizuri shule za msingi. *(Makofi)*

Na. 286

**Mikopo ya *Tractor* kwa Vikundi vya Vijana na Wazee**

**MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME (k.n.y. MHE. MARTHA M. WEJJA)** aliuliza: -

(a) Je, hadi sasa Serikali imetoa mikopo ya matrekta na fedha kiasi gani kwa vikundi vya vijana nchini kwa lengo la kuendeleza Kilimo na vikundi hivyo vipo kwenye Mikoa ipi?

(b) Je, Serikali haioni pia kwamba umefika wakati sasa wa kuwapa wazee mikopo ya fedha na matrekta ili viwasaidie kuendeleza kilimo baada ya kutoa mikopo hiyo kwa vijana peke yao?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Wejja, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Wizara ya Kilimo na Chakula haina mipango wa kutoa mikopo ya kilimo kwa vikundi maalum. Hata hivyo, Serikali imekuwa ikitoa mikopo mbalimbali kwa vijana kama ifuatavyo: -

(i) Kati ya miaka ya 1994/1995 na 2002/2003, Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, imekuwa ikitoa mikopo kwa vikundi vya vijana yenye jumla ya shilingi 1,622 milioni kwa ajili ya miradi mbalimbali.

(ii) Kati ya mwaka 1998 na 2000, Halmashauri za Wilaya zimekuwa zikitenga asilimia 10 ya mapato yake kwa ajili ya miradi ya Wanawake na Vijana. Hata hivyo, mikopo hiyo haikutengwa maalum kwa ajili ya vikundi vya vijana kununua matrekta. Aidha, kutokana na mahitaji makubwa ya mikopo kwa kulinganisha na fedha zinazotengwa, kiwango cha juu cha mikopo iliyotolewa kwa vijana ni Sh.500,000/=. Kiasi hicho hakiviwezeshi vikundi kununua matrekta.

(b) Hakuna mpango wa utaratibu maalum wa kuwapatia wazee mikopo. Sera ya wazee iliyoandaliwa na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, inatambua nafasi muhimu ya wazee katika jamii na kuweka utaratibu wa kuwahudumia. Kwa sasa Wizara hiyo inaandaa mkakati wa kutekeleza sera hiyo. Suala la mikopo kwa wazee ni kati ya mambo muhimu yatakayozingatiwa katika mkakati huo. Katika mwaka 2003/2004, Wizara ya Kilimo na Chakula itatoa mikopo yenye masharti nafuu kwa ajili ya kununua matrekta kupitia Mfuko wa Pembejeo. Vijana na Wazee wanashauriwa kuomba mikopo hiyo kupitia Halmashauri za Wilaya zao.

**MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

(a) Kwa kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa la Tanzania; na kwa kuwa nguvu kazi kubwa ya Taifa letu ni vijana. Je, Serikali haioni vyema sasa ikatoa kipaumbele katika kukopesha vikundi vya vijana vilivyopo vijijini matrekta kwa ajili ya kuendeleza shughuli za kilimo?

(b) Kwa kuwa Serikali imetoa kipaumbele kutoa mikopo kwa vikundi viwili tu, vikundi vya vijana na kundi la wanawake; na kwa kuwa wazee wanaonekana kwamba ni wazalishaji wazuri sana. Je, sasa Serikali inaweza pia ikatoa kipaumbele kwa kundi la wazee kwa kuwapa mikopo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, ninakubaliana naye kama kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa nchi. Vilevile swali la pili, kuhusu wazee katika kuimarisha uchumi. Narudia tena kwenye swali la msingi ambapo nasema Wizara ya Kilimo na Chakula inawakaribisha vijana na wazee kwa kutambua hilo alilolisema Mheshimiwa Mbunge, waombe mikopo hiyo kwa kupitia Halmshauri za Wilaya zao, wanakaribishwa. *(Makofi)*

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa mikopo hii inataka dhamana na hawa vijana wengi hawana dhamana. Kutakuwa na mpango gani wa kuwasaidia hawa vijana kwa sababu hawana dhamana na wanataka kukopa hayo matrekta kwa ajili ya shughuli za kilimo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, tunatambua kama vijana watapata matatizo ya dhamana. Lakini papo hapo tuna sera nzuri ya Serikali inayosema kama vijana watajiunga katika Ushirika au katika Mifuko mbalilmbali ya Halmashauri za Wilaya au wakiunda Asasi kama *SACCAS* itawezekana. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kuwa aidha wapitie Ushirika au wapitie *SACCAS* au Halmashauri zetu za Wilaya ambazo zipo ziwadhamini.

Na. 287

**Gharama za Kumsajili Mtoto anapozaliwa**

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI** aliuliza:-

Kwa kuwa gharama za kumsajili mtoto anapozaliwa ni shilingi 3,000/=, fedha ambazo ni nyingi mno kwa mzazi kumudu hasa ikizingatiwa hali ngumu ya maisha hasa vijijini; na kwa kuwa mtoto huyo anapokuwa mtu mzima akitaka kupata elimu au ajira hutaabika sana kupata cheti cha kuzaliwa na hatimaye hulazimika kutoa shilingi 10,000/ au zaidi ndipo apate cheti hicho:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali isimsajili mtoto huyo bure?

(b) Je, ni kosa gani alilofanya mzazi huyu hata apigwe faini ya shilingi 3,000/= badala ya kumpongeza kwa kazi kubwa na nzuri ya kumleta Mtanzania duniani salama?

(c) Je, ni kwa nini kila Mganga Mkuu wa Hospitali na Zahanati asiwe na vyeti hivyo vya usajili kwa ajili ya kumkabidhi mzazi pindi mtoto anapozaliwa ili mzazi asisumbuke kufuatilia cheti hicho kwa Msajili wa Vizazi na Vifo?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Major Jesse Makundi, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Serikali haitozi ada yoyote katika kumsajili mtoto anayezaliwa hapa nchini. Kila mtoto anayezaliwa katika Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali, anayo haki ya kusajiliwa bila malipo yoyote iwapo usajili huo utafanyika ndani ya miezi mitatu tangu kuzaliwa kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa. Mganga wa kila Zahanati anapaswa awasajili watoto wote wanaozaliwa katika Zahanati yake na kutoa taarifa ya watoto wote anaowasajili kwa Msajili wa Vizazi. Wasajili wa vizazi wapo katika kila Wilaya, isipokuwa Wilaya chache ambazo mradi wa usajili wa watoto *(Civil Registration System)* bado haujafika.

Hata katika maeneo hayo, bado upo utaratibu unaomtaka Mganga wa Zahanati au Kituo cha Afya, kutoa taarifa ya vizazi kwa msajili wa vizazi wa Wilaya. Watoto waliokwishasajiliwa

wanapokwenda kuchukua vyeti vya kuzaliwa hutakiwa kulipa ada ya shilingi 2,000/=, pamoja na gharama ndogo ya shilingi 1,000/= kwa ajili ya upekuzi. Hivyo, malipo hayo siyo faini.

Mheshimiwa Spika, wale watoto ambao kwa sababu mbalimbali hawakusajiliwa katika kipindi cha siku tisini baada ya kuzaliwa, hupaswa kulipa shilingi 4,000/= na watoto wanaochelewa kusajiliwa baada ya kupita miaka 10 hulipia shilingi 10,000/=.

Malipo hayo yanaweza kuepukwa kama wazazi watajitahidi kuwasajili watoto wao mapema pindi wanapozaliwa, jambo ambalo naamini Mheshimiwa Mbunge, atakubaliana nami kwamba, ni muhimu ili kuweka kumbukumbu sahihi za wananchi wetu, malipo haya pia yana lengo la kufidia gharama za upekuzi unaofanywa ili kudhibiti usajili wa raia wa Tanzania na kuzuia udanganyifu katika zoezi la usajili.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniruhusu kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali amekubali kwamba kuna malipo ya shilingi 10,000/=; na kwa kuwa Watanzania wengi ni maskini na tunazaa sana na si vibaya; na kwa kuwa kuna mpango wa kutoa vitambulisho vya Taifa *(National Identity Card);* sasa huwezi kutoa vitambulisho bila ya kuwa na cheti cha kuzaliwa; je, Serikali haioni kwamba ni busara sasa hati hizo za kuzaliwa zikatolewa bure na kuhakikisha kwamba wanatoa elimu kwa Watanzania wote wajue na kuweza kuzipata kabla *National Identity Card* hazijatolewa? *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli ni azma ya Serikali kuwa na utaratibu wa kutoa vitambulisho kwa wananchi wake, lakini zoezi hilo litachukua muda.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa tunasema tuendelee kuwahimiza wananchi wetu katika maeneo ambayo tayari mradi huu wa *Civil Registration System* umeshafika, ni karibu Wilaya 74 sasa. Lakini kwa mwaka huu wa fedha tunaingia Mkoa mzima wa Mbeya.

Kwa maana hiyo katika Wilaya hizo ni lazima tujitahidi kabisa kuwahamasisha wananchi wetu kwamba, watoto wote wanaozaliwa katika vituo vyetu vya afya, zahanati na hospitali wasajiliwe. Katika maeneo ambayo ni nje ya mradi, tunaendelea kuwahimiza viongozi wetu na wananchi kwa ujumla kwamba, tujitahidi kwa kadri inavyowezekana taarifa hizi za kuzaliwa kwa watoto wetu zipelekwe kwa Msajili wa Vizazi katika ngazi ya Wilaya.

Na. 88

**Mikataba Inayoridhiwa na Bunge**

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA (k.n.y. MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali yetu kupitia Bunge lake imekuwa ikiridhia Mikataba mbalimbali ya Kimataifa na ya Kimkoa *(Regional Agreements):-*

(a) Je, ni Mikataba mingapi imeridhiwa na Bunge katika kipindi cha miaka 10 kuanzia mwaka 1992 hadi 2002?

(b) Je, ni Mikataba mingapi kati ya hiyo imetungiwa sheria na ni mingapi bado haijatungiwa sheria na kwa nini?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Mbunge wa Kuteuliwa, naomba kutoa maelezo mafupi ya jumla kama ifuatavyo:-

Nchi kama sehemu ya Jumuiya ya Kimataifa, ina uwezo wa kuingia Mikataba na nchi nyingine au na Jumuiya za Kimataifa. Ingawa jukumu la nchi kuitekeleza Mikataba ya aina hii linatokana na Mikataba yenyewe, uwezo wa kutekeleza ndani ya nchi, utatokana na Katiba ya Nchi husika.

Zipo nchi ambazo Katiba inatamka wazi kuwa Mikataba ya Kimataifa iliyoridhiwa na nchi inakuwa moja kwa moja sehemu ya Sheria za Nchi. Nchi zenye mfumo wa kutelekeza Mikataba kwa utaratibu huu, hazitungi sheria kutekeleza Mikataba hiyo. Kwa upande mwingine, kuna nchi kwa mujibu wa Katiba ya Nchi hii, Mikataba ya Kimataifa inayoridhiwa na Mamlaka ya nchi haiwi na nguvu ya kisheria mpaka itungiwe sheria maalum kwa ajili ya utekelezaji wake. Tanzania ni miongoni mwa nchi hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Kuteuliwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Bunge katika kipindi cha miaka 10 kuanzia 1992 hadi 2002 limeridhia Mikataba ya Kimataifa ipatayo 62 kati ya hiyo, Mikataba 7 ambayo utekelezaji wake ulihitaji kuwepo na sheria, imetungiwa sheria au sheria zilizopo zimefanyiwa marekebisho ili ziweze kukidhi mahitaji ya utekelezaji wa mikataba hiyo.

(b) Mikataba iliyobaki haijatungiwa sheria kwa sababu utekelezaji wake hauhitaji kutungwa sheria mpya kwani sheria zilizopo zinatosheleza mahitaji ya utekelezaji wa Mikataba hiyo. Aidha, ipo Mikataba kama ile inayohusika na Haki za Watoto, ambayo tupo mbioni kuitungia sheria.

**SPIKA:** Mwuliza swali la msingi ameridhika na muda wa maswali umekwisha. Kwa hiyo, inatuwezesha kuendelea na mambo mengine. Matangazo ya vikao vya leo. Kamati mbili zimepangwa kukutana leo ya kwanza ni Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Sophia Simba, anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane leo tarehe 22 Julai, 2003 saa 7 mchana katika Ukumbi Na. 58 ghorofa ya kwanza.

Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Shellukindo, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane leo tarehe 22 Julai, 2003 saa 5.30 asubuhi hii katika chumba cha Kamati Na. 84 ghorofa ya 2. Mwisho wa matangazo.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2003/2004
### Wizara ya Maliasili na Utalii

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, katika taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, iliyochambua Makadirio ya Matumizi ya fedha ya Wizara ya Maliasili na Utalii, naomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako Tukufu likae kama Kamati ili liweze kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka 2003/2004.

Napenda kumshukuru Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuchambua na kujadili mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Wizara kwa mwaka 2003/2004. Wizara yangu imezingatia mapendekezo ya Kamati na inaahidi kuyatekeleza.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge, waliochaguliwa katika chaguzi ndogo zilizofanyika Mei, 2003. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Wizara yangu iliahidi kutekeleza majukumu muhimu yatakayodumisha uhifadhi endelevu wa Maliasili, mambo ya kale na uendelezaji utalii kwa manufaa ya wananchi. Majukumu hayo yalilenga katika maeneo makuu yafuatayo:-

- Kuandaa Sera ya Mambo ya Kale;
- Kurekebisha Sheria na Kanuni;
- Kuandaa Programu za utekelezaji wa sera;
- Kushirikisha wadau katika shughuli za uhifadhi;
- Kufanya utafiti wa wingi wa raslimali na matumizi yake; na
- Kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha taarifa ya utekelezaji ya mwaka 2002/2003 na malengo ya Wizara kwa mwaka 2003/2004 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, sekta ndogo ya utalii iliendelea kukua na kutoa mchango wake katika uchumi wa nchi. Pamoja na mshtuko wa mashambulizi ya kigaidi ya Septemba 11, mapato yaliyotokana na utalii kwa mwaka 2002 yalifikia Dola za Kimarekani milioni 730, ikilinganishwa na Dola milioni 725 mwaka 2001. Aidha, idadi ya watalii iliongezeka kutoka watalii 525,000 mwaka 2001 hadi watalii 575,235 mwaka 2002.

Mwaka 2003, Wizara inatarajia kuwa watalii 603,990 watatembelea nchi yetu na kuliingizia Taifa Dola za Kimarekani milioni 731. Hata hivyo, lengo hili linaweza lisifikiwe kutokana na athari za vita vya Irak na maonyo yanayotolewa na vyombo vya habari vya Magharibi kuwatisha watalii wanaotarajia kutembelea nchi za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa sera unategemea sana uelewa wa wadau, hasa wananchi. Ili wananchi wengi waielewe, mwaka 2002/2003, Wizara ilichapisha nakala 5,000 za sera ya Utalii katika lugha ya Kiswahili. Katika mwaka 2003/2004, Wizara itaanza kutayarisha Mpango wa utekelezaji wa sera hiyo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003, Sheria ya Wakala wa Utalii namba 2 ya mwaka 1969 na Sheria namba 22 ya Hoteli ya mwaka 1963, zilifanyiwa mapitio kwa nia ya kuhuisha ili kuwa na sheria moja ya utalii. Katika mwaka 2003/2004, Wizara itakamilisha uandaaji wa Sheria ya Utalii kwa kushirikiana na wadau.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Wizara ilibaini na kutathmini vivutio na maeneo ya uendelezaji utalii katika Bonde la Mto Rufiji. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Uongozi wa Mikoa ya Iringa na Tanga, ilifanya mikutano kuhusu uendelezaji wa utalii unaojali mazingira.

Mwaka 2003/2004, Wizara itabaini, kutathmini vivutio na kufanya semina za uhamasishaji katika Mikoa ya Singida, Mwanza, Mara na Kagera. Aidha, itaandaa picha za video zitakazoonyesha vivutio mbalimbali katika Mikoa hiyo. Vile vile, taarifa za vivutio hivyo zitawekwa kwenye tovuti.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2002/2003, Wizara ilikamilisha mapitio ya Mpango Kamambe wa utalii chini ya mradi unaohisaniwa na Jumuiya ya Nchi za Ulaya. Katika kutekeleza mpango huo, uchambuzi wa soko la utalii ndani na nje ya nchi, uandaaji wa mpango kamambe wa utalii wa Zanzibar na ununuzi wa vifaa na vitendea kazi ulifanyika. Aidha, mradi uligharimia uendeshaji wa chombo kinachosimamia shughuli za utalii katika sekta binafsi *(Tourism Confederation of Tanzania).*

Katika mwaka 2003/2004, Wizara itaimarisha mafunzo kwa watumishi wa sekta na kuimarisha chombo kinachosimamia shughuli za utalii katika sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ilikamilisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 14 ziendazo kwenye hoteli za kitalii zilizoko kwenye fukwe za Dar es Salaam. Ujenzi wa barabara ya kutoka Makuyuni hadi Ngorongoro unaendelea.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya *Multilateral Investment Guarantee Agency (MIGA)* na Taasisi nyingine ilifanya mkutano wa wawekezaji Arusha, Oktoba, 2002. Mkutano huo ulihudhuriwa na wawekezaji 280 wa ndani na nje ya nchi. Aidha, kwa kushirikiana na *MIGA* na *DCDM Consulting Limited,* Wizara ilifanya uchambuzi wa miradi sita ya wawekezaji.

Katika kipindi cha 2003/2004, Wizara itaendelea kufuatilia wawekezaji walioonyesha nia ya kuwekeza pamoja na kubaini maeneo mapya yanayofaa kwa Uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2002/2003, Wizara ililenga kukusanya shilingi milioni 698 kutokana na ada mbalimbali za Wakala wa Utalii. Hadi Mei, 2003, shilingi milioni 750 zilikusanywa. Wizara inalenga kukusanya shilingi milioni 855 kutokana na leseni za Wakala wa Utalii na Hoteli za Kitalii katika mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2002/2003, Wizara kwa kushirikiana na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, ilikamilisha vigezo vya kupanga hoteli, migahawa na loji za kitalii katika daraja. Aidha, Wizara ilikamilisha kuorodhesha hoteli zilizopo katika Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Tanga, kama hatua ya awali ya kupanga hoteli katika daraja.

Katika mwaka 2003/2004, Wizara itaendesha warsha ili kupata maoni ya wadau kuhusu vigezo hivyo na kutoa mafunzo kwa wataalamu watakaohusika katika zoezi hilo. Aidha, Wizara itaandaa kanuni za kusimamia utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2002/2003, Wizara ilikagua Wakala wa Utalii 240 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara. Kufuatia zoezi hilo, wafanyabiashara 15 walikamatwa kwa kufanya biashara bila leseni. Kati yao, mmoja alihukumiwa kifungo cha miaka mitatu na wengine walitozwa faini.

Mwaka 2003/2004, Wizara itaendelea kufanya ukaguzi ili kudhibiti Wakala bandia na kufuatilia ubora wa huduma zinazotolewa kwa watalii.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Idara ya Uhamiaji na Benki Kuu, ilianzisha mfumo mpya wa ukusanyaji takwimu za utalii utakaowezesha kupata takwimu sahihi. Katika kuanzisha mfumo huo, utafiti ulifanyika ambapo kampuni 500 za Wakala wa Utalii zilihusishwa na watalii 20,000 kuhojiwa. Aidha, kompyuta 20 zilinunuliwa na kukabidhiwa Idara ya Uhamiaji kwa ajili ya kufanikisha ukusanyaji takwimu.

Mwaka 2003/2004, Wizara inatarajia kufanya tafiti mbili zitakazolenga kupata takwimu na kuendeleza mfumo huo. Tafiti hizo zitatuwezesha kupima kwa usahihi zaidi, mchango wa utalii wa ndani *(Domestic Tourism*) na watoa huduma za kitalii *(Tourism Establishments)* katika kuchangia Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Taifa cha Utalii kilizinduliwa kuwa Wakala tarehe 24 Januari, 2003. Mwaka 2003/2004, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa, inatarajia kujenga majengo ya chuo. Wahisani hao pia watasaidia kuboresha chuo na kutoa mafunzo katika ngazi ya uongozi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Bodi iliandaa mkakati wa utangazaji wa utalii katika kipindi cha miaka 10 ijayo na kushiriki katika maonyesho mawili ndani ya nchi na kumi na nane nje ya nchi. Kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, hususan Ubalozi wetu nchini Urusi na sekta binafsi, Bodi iliwezesha ujio wa Wakala wa Utalii na waandishi wa habari 200 kutoka Urusi. Aidha, mwezi Agosti, 2003 tunatarajia kupata watalii 300 kutoka Japan kutokana na msukumo wa Ubalozi wetu.

Mheshimiwa Spika, 2003/2004, Bodi itaendelea kutangaza utalii na kushiriki katika maonyesho katika nchi za Afrika Kusini, Australia, Japan, Marekani na Korea. Aidha, Bodi itaendelea na mpango wa kutafuta Wakala wawakilishi katika masoko ya zamani na mapya.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2002/2003, Wizara ilikamilisha rasimu ya sera ya Mambo ya Kale. Mwaka 2003/2004, Wizara itaendelea na ukamilishaji wa sera kwa kuendesha warsha za wadau ili kupata maoni yao.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003, Wizara kwa kuwatumia wataalamu wa Mambo ya Kale, ilifanya utafiti wa akiolojia huko Kinole na Kigurunyembe, Morogoro. Utafiti huo umebaini kuwepo kwa mahusiano baina ya Jamii za Bara na Pwani. Aidha, Wizara imeratibu na kusimamia utafiti wa akiolojia katika Bonde la Olduvai, eneo la Laitoli, Ziwa Eyasi, Hifadhi ya Taifa Serengeti, Mafia, Mbeya na Kagera.

Katika kipindi cha 2003/2004, Wizara kwa uhisani wa Serikali ya Ufaransa, itatumia wataalam wa ndani na nje ya nchi, kufanya utafiti ili kuboresha historia ya maeneo ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara. Aidha, Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia tafiti za Mambo ya Kale katika Bonde la Olduvai, eneo la Laitoli, Mbeya, Dodoma na Morogoro.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2002/2003, Wizara ilianza ujenzi wa vituo vya kumbukumbu na habari vya Isimila, Iringa na Kolo, Kondoa. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Sweden, ilianza ukarabati wa jengo la Caravan Serai, Bagamoyo, ili pia kiwe kituo cha kumbukumbu na habari. Katika mwaka 2003/2004, Wizara itakamilisha ujenzi wa vituo hivyo na ukarabati wa jengo la Caravan Serai, Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali za Japan na Ufaransa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni *(UNESCO),* imeanza kutekeleza mpango wa uhifadhi na uendelezaji wa eneo la Kilwa Kisiwani na Songo Mnara, kwa kukarabati nyumba ya Kijerumani, kujenga gati na kukarabati Msikiti Mkuu wa Kilwa Kisiwani.

Katika kipindi cha 2003/2004, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau inakusudia kuikamilisha kazi zilizokwishaanza na kuanza kuweka umeme utokanao na mionzi ya jua, kukarabati jengo la kihistoria la Wareno na kufanya utafiti wa kina katika nyanja za uhifadhi, akiolojia, historia, mazingira na Elimu ya Jamii huko Kilwa Kisiwani na Songo Mnara.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Sweden, iliimarisha baadhi ya majengo yaliyokuwa katika hali mbaya katika Mji wa Bagamoyo kama hatua ya dharura.

Katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu itakamilisha mazungumzo na Serikali ya Sweden juu ya namna bora ya kuimarisha na kuboresha vituo vilivyopo kwenye njia ya kati ya biashara ya utumwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Wizara yangu iliwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa historia na umuhimu wa kuhifadhi Mambo ya Kale kwa kutumia vipeperushi, vipindi vya Redio na Televisheni. Aidha, mkakati wa kushirikisha jamii katika uhifadhi na uendelezaji wa maeneo ya Mambo ya Kale umeanza kutayarishwa.

Katika kipindi cha 2003/2004, Wizara yangu itakamilisha mkakati wa kushirikisha jamii katika uhifadhi na uendelezaji wa maeneo ya Mambo ya Kale na itaendelea kuandaa na kurusha vipindi vya Redio na Televisheni na kusambaza vipeperushi. Aidha, Wizara itaandaa na kuendesha mikutano, semina na warsha mbalimbali za kuelimisha jamii.

Katika mwaka 2002/2003, Wizara iliweka lengo la kukusanya shilingi milioni 97. Hadi Mei, 2003, shilingi milioni 111 zilikusanywa. Ukaguzi uliolenga kuimarisha ukusanyaji maduhuli ulifanyika katika vituo vya Bonde la Olduvai, Isimila, Bagamoyo, Kaole, Kolo na Mapango ya Amboni. Wizara inatarajia kukusanya shilingi milioni 125 katika mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003, Shirika la Makumbusho ya Taifa liliimarisha usalama katika Makumbusho ya Taifa Dar es Salaam na Elimu Viumbe, Arusha kwa kununua silaha na kujenga uzio.

Aidha, Mazingira ya Makumbusho hayo yameboreshwa kwa kufunga viyoyozi na kuongeza mukusanyo *(Artifacts)*. Pia Shirika lilishirikisha jamii ya Wamwera katika kuandaa Tamasha la Utamaduni wa Mtanzania.

Shirika liliendesha warsha kwa washiriki kutoka Mikoani kuhusu uanzishwaji na uendelezaji wa Makumbusho na Mambo ya Kale. Katika kipindi hicho watumishi 7 wliajiriwa katika makumbusho ya Mwalimu J. K. Nyerere iliyoko Butiama, Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003, Shirika kwa uhisani wa Mfuko wa Utamaduni, limeandaa mpango wake wa maendeleo. Aidha, lilifanya upembuzi yakinifu wa mradi wa ujenzi kwa Jumba la Utamaduni katika makumbusho ya Dar es Salaam kwa uhisani wa Serikali ya Sweden.

Mhehsimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, shirika litaendelea na programu ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo wenye lengo la kuboresha na kusogeza huduma za makumbusho karibu na wananchi na kuimarisha usalama wa makumbusho zake.

Katika kuendeleza ushirikishaji wa jamii, shirika litashirikiana na makabila ya Wakerewe na Wabena katika kuandaa Tamasha la Utamaduni wa Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Sheria ya Makumbusho ya Taifa ya mwaka 1980 yameanza na rasimu ya kwanza imekamilika. Katika mwaka 2003/2004, Shirika litakamilisha marekebisho ya sheria hiyo.

Mhehsimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Sheria ya Uvuvi Namba 6 ya mwaka 1970 ilifanyiwa mapitio kwa lengo la kuandaa sheria mpya ya uvuvi. Rasimu ya sheria hiyo tayari imeidhinishwa na Baraza la Mawaziri. Mwaka 2003/2004, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, itaandaa Muswada wa Sheria hii na kuuwasilisha Bungeni. Aidha, Kanuni na Sheria ya Uvuvi zitaandaliwa kwa kushirikisha wadau.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003, utekelezaji wa mpango kamambe wa kuendeleza sekta ya uvuvi ulianza kwa kufanya Mikutano Miwili ya Kitaifa iliyoshirikisha wataalamu wa uvuvi kutoka ngazi za Wilaya, Mikoa na wadau wengine ili kuweka mikakati ya utekelezaji. Miradi 15 iliyo chini ya mpango huo ilichambuliwa na kupewa kipaumbele kwa kuzingatia uwezo wake katika kuongeza Pato kwa wananchi.

Mwaka 2003/2004, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Japan inatarajia kujenga Soko la Kisasa la Samaki Kirumba katika Jiji la Mwanza, ukiwa ni mradi mmojawapo chini ya mpango kamambe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003, Wizara ilikuwa na lengo la kukusanya shilingi bilioni 4. Hadi Mei, 2003 shilingi bilioni 5.7 zilikusanywa. Aidha, wahamasishaji wa ukusanyaji wa maduhuli ulifanywa katika Mikao ya Mbeya, Rukwa, Mtwara, Lindi na Mwanza na ushirikiano na Mamlaka ya Mapato Tanzania uliimarishwa. Katika kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli, kituo kipya cha Kasumulu, Wilayani Kyela kilifunguliwa.

Katika mwaka 2003/2004, Wizara inatarajia kukusanya shilingi bilioni 6.4 kutokana na mazao ya uvuvi.

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, wawekezaji wengi wanajitokeza kuomba/kutaka kuwekeza katika ukanda wa uchumi wa bahari, yaani *Exclusive Economic Zone (EEZ).* Mwaka 2002/2003, meli 44 zilipata leseni ya kuvua katika ukanda huu ikilinganishwa na meli 17 mwaka 2001/2002.

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ilikamilisha mazungumzo na Serikali ya Shelisheli kuhusu mpaka wa Ukanda wa uchumi wa Bahari.

Katika mwaka 2003/2004, Wizara itaendeleza majadiliano na Serikali ya Comoro kuhusu utata wa mipaka katika eneo hili.

Mhehsimiwa Spika, mwaka 2002/2003, Wizara ilitoa mafunzo ya ufugaji samaki na ukulima wa viumbe katika maji kwa wananchi 4,208 kutoka mikoa 9. Aidha, wataalam 90 walipata mafunzo ya ugani. Pia Wizara ilichimba mabwawa sita ya mfano katika Mikoa ya Tabora na Mbeya.

Kituo cha maendeleo ya Ufugaji Samaki Kingolwira - Morogoro kilizalisha vifaranga vya samaki 100,000. Kati ya hivyo 30,000 vilisambazwa kwa wafugaji na 70,000 vilipandikizwa katika mabwawa ya kituo. Kituo hicho kimeimarishwa kwa kupatiwa vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, Wizara itaandaa miongozo ya uwekezaji katika ufugaji wa samaki na ukulima wa viumbe katika maji. Huduma za ugani zitaboreshwa na mafunzo kutolewa kwa wadau. Aidha, Wizara itaendelea na utafiti wa kuzalisha mbegu bora na ufugaji wa samaki aina ya kambare na perege.

Katika kipindi cha 2002/2003, doria 61 zilifanyika katika maji chumvi na 57 katika maji baridi. Kufuatia doria hizo watuhumiwa 187 walishtakiwa. Aidha, makokoro 1,043, nyavu 8,285 za macho madogo chini ya inchi 5, nyavu 257 za dagaa zenye macho chini ya milimita 10 na boti 67 zilikamatwa na kutumika kama vielelezo kwenye Mahakama.

Katika ukanda wa Ziwa Victoria, vikundi 511 vya ulinzi wa raslimali na mazingira vilishiriki katika ulinzi. Kati ya hivyo 16 vimekasimiwa kukusanya mapato yatokanayo na uvuvi katika Halmashauri za Wilaya za Musoma, Magu, Geita, Sengerema, Misungwi na Muleba.

Mwaka 2003/2004, Wizara itaimarisha doria kwa kushirikiana na vikundi vya ulinzi na kuhamasisha uanzishwaji wa vikundi vingine.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003, Wizara iliweka mfumo utakaosaidia kugundua na kudhibiti vyanzo vya uharibifu wa ubora na usalama wa mazao ya uvuvi kutoka eneo la uvuvi hadi kwenye viwanda. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo kuhusu usafi, uhifadhi wa mazao ya uvuvi, usafirishaji na utunzaji bora wa mialo kwa wadau 1,469. Vile vile Wizara iliimarisha Mialo kwa kuweka matishari kumi katika Wilaya za Tarime, Ilemela, Ukerewe, Muleba, Musoma Vijijini, Sengerema na Geita.

Mhehsimiwa Spika, ujenzi wa maabara ya kisasa ya uvuvi, Nyegezi upo katika hatua za mwisho kukamilika. Maabara hii itakapokamilika itatumika katika uchunguzi wa Mazao ya uvuvi badala ya kufanyia nje ya nchi kama ilivyokuwa hapo awali.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003, Wizara ilitoa mafunzo kuhusu uvuvi endelevu kwa wavuvi wadogo wadogo 132 katika Mikoa ya Lindi, Mtwara, Kigoma, Rukwa na Mbeya. Aidha, wavuvi hao walihamasishwa kuanzisha vyama vya ushirika vya kuweka na kukopa.

Katika mwaka 2003/2004, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu uvuvi endelevu, ufugaji bora wa samaki, kilimo cha mwani na usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, 2002/2003, Wizara ilinunua boti saba ili kuimarisha ulinzi katika hifadhi za bahari na maeneo Tengefu Dar es Salaam, Mafia na *Mnazi Bay*. Aidha, wananchi walishirikishwa katika kuendesha doria na uvunaji endelevu wa raslimali ndani ya hifadhi na maeneo yanayozizunguka kama njia muhimu ya kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara itashirikiana na Benki ya Dunia kukamilisha upembuzi yakinifu, kuona jinsi gani hifadhi za Bahari na maeneo Tengefu zinaweza kuchangia katika juhudi za kupunguza umaskini. Aidha, Wizara itaimarisha vivutio vya utalii katika Jiji la Dar es Salaam kwa kujenga Kituo cha Taarifa *(Visitors Information Centre)*. Pia, Wizara itashirikiana na wadau katika kuimarisha usimamizi wa fukwe na visiwa vidogo katika juhudi za kuendeleza utalii wa mwambao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Taasisi ilifanya utafiti wa kutambua mtawanyiko *(distribution)* na kupevuka kwa kamba katika Ukanda wa Pwani. Utafiti huo umeonyesha kuwa zipo aina tano za kamba katika maeneo ya Pwani ya Bagamoyo, aina mbili katika Pwani ya Saadani na aina nne katika maeneo mengine. Aidha, utafiti umeonyesha kuwa mwezi Machi kamba wengi wanakuwa hawajapevuka na kuwa kiwango kikubwa cha kamba kinapatikana katika Pwani ya Bagamoyo na Kilwa. Utafiti katika maziwa madogo na mito uliohusisha Mikoa ya Kagera, Mara, Mwanza, Tabora na Singida umebaini kuwa bioanuai kubwa inapatikana Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Spika, aidha, utafiti umeonyesha kuwa aina za samaki wa asili walioanza kupungua katika Ziwa Victoria hususan jamii ya sato wanapatikana katika Maziwa madogo yanayozunguka Ziwa hilo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, taasisi itaendelea kutathmini wingi wa kamba katika Bahari ya Hindi, pamoja na kuendeleza utafiti katika mabwawa madogo, mito na maziwa. Aidha, ujenzi wa Makao Makuu na Kituo cha Utafiti Dar es Salaam utaanza.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Programu za Misitu na Ufugaji Nyuki Wilayani, Wizara iliandaa mpango wa uhifadhi na usimamizi wa raslimali za misitu na nyuki unaohusisha Wilaya za Mtwara Vijiji, Masasi, Liwale, Muheza, Nachingwea, Handeni na Korogwe. Aidha, Wilaya 24 ziliwezeshwa kuandaa mipango yake ya utekelezaji. Katika kuendeleza ufugaji nyuki, Wizara kwa kushirikiana na Wilaya za Kibondo, Tabora, Manyoni, Kondoa na Handeni, ilianzisha hifadhi za nyuki katika vijiji vitatu kila Wilaya.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2002/2003, Wizara ilianza kutafsiri Sheria za Misitu na Ufugaji Nyuki kutoka lugha ya Kiingereza kwenda Kiswahili na kutayarisha Kanuni na Taratibu za kutekeleza sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, Wizara itakamilisha tafsiri ya Sheria za Misitu na Ufugaji Nyuki, pamoja na Kanuni na Taratibu za Sheria hizo na kuzitangaza.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003, Wizara ililenga kukusanya shilingi bilioni 4.8, hadi Mei, 2003, shilingi bilioni 4.5 zilikusanywa. Katika kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli, warsha iliyoshirikisha Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya 12 kutoka Mikoa ya Kilimanjaro, Tanga, Arusha na Mwanza, ilifanyika. Wizara imeandaa mpango wa kukasimu majukumu ya kukusanya maduhuli ya mazao ya nyuki katika Wilaya zote za mpakani.

Katika mwaka 2003/2004, Wizara inalenga kukusanya shilingi bilioni 4.8 kutokana na mazao ya misitu na nyuki.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Wizara iliviwezesha vijijji 11 kuandaa Mipango ya Usimamizi Shirikishi wa misitu ya vijiji katika Wilaya za Kondoa, Dodoma Vijijini na Kongwa.

Mwaka 2003/2004, Wizara itaandaa mafunzo ya usimamizi shirikishi wa misitu itakayojumuisha vijiji 200. Vile vile itaviwezesha vijiji 49 kuandaa Mipango ya Usimamizi wa misitu na hifadhi za nyuki.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, uvunaji wa miti uliendelea. Hadi Mei, 2003, magogo yenye mita za ujazo 19,020 yalivunwa katika misitu ya asili na mita za ujazo 315,853 katika mashamba ya miti.

Katika mwaka 2003/2004, magogo yenye mita za ujazo 25,000 yatavunwa katika misitu ya asili na mita za ujazo 350,000 katika mashamba ya miti.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003, mazao ya misitu na nyuki yenye thamani ya shilingi bilioni 3.9 yalitarajiwa kuuzwa nje ya nchi. Hadi Mei, 2003 mazao ya misitu na nyuki yenye thamani ya shilingi bilioni 7.2 yaliuzwa.

Katika mwaka 2003/2004, inatarajiwa kuwa mazao ya misitu na nyuki yenye thamani ya shilingi bilioni 9.8 yatauzwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003, Wizara iliendelea kusimamia na kuendeleza mashamba ya miti. Hadi Mei, 2003, miche 7,376,733 ilikuzwa na hekta 2,275 kupandwa miti. Aidha, miti katika hekta 881 ilipunguzwa na heta 1,650 ilipogolewa matawi katika mashamba 16. Shamba la Miti la *Sao Hill* limebuni mpango wa kuendeleza miti ya mikaratusi kwa kuvuna miti iliyokomaa na baadaye kuruhusu machipukizi ili kuzuia moto usiingie katika miti ya misindano.

Mwaka 2003/2004, Wizara itakuza miche 9,000,000 na kupanda miti hekta 4,000. Pia, itapunguza miti katika hekta 3,700 na kupogoa matawi hekta 3,600. Aidha, taratibu za kushirikisha wadau katika kusimamia mashamba ya miti ya *Sao Hill*, Kiwira, Buhindi, Meru na Kilimanjaro Kaskazini zitaandaliwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003, taasisi kwa kushirikiana na taasisi nyingine za Kitaifa na Kimataifa, ilianzisha mradi wa matumizi ya mianzi asili kwa ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu Mkoani Mbeya. Chini ya mradi huo, vitalu vya mianzi vilianzishwa katika Wilaya za Mbeya Vijijini na Rungwe. Aidha, taasisi inaratibu utunzaji wa mianzi asili ili kuhakikisha upatikanaji wake. Vile vile, taasisi iliendelea kufanya utafiti wa aina nane za miti ya asili kwa ajili ya kilimo misitu na uzalishaji kibiashara.

Katika mwaka 2003/2004, taasisi itatekeleza mradi wa matumizi ya mianzi katika ujenzi wa nyumba bora. Aidha, taasisi itachapisha nakala 2,000 za toleo la tatu la Kitabu cha *Commercial Timbers of Tanzania* na itaendelea na utafiti wa miti ya asili na kilimo misitu.

Mheshimiwa Spika, tarehe 24 Januari, 2003, Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania ulizinduliwa. Madhumuni ya Wakala huu ni kukusanya na kutoa, kwa ufanisi zaidi, mbegu bora za miti kwa ajili ya kuhakikisha upatikanaji endelevu wa mazao ya misitu na uhifadhi wa mazingira nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, kazi ya kurekebisha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Na.12 ya mwaka 1974 iliendelea kwa kuendesha warsha tisa zilizoshirikisha wadau. Warsha hizo zilibainisha maeneo ya kufanyiwa marekebisho na maeneo mapya yanayotakiwa kuingizwa kwenye sheria hiyo.

Kipindi cha 2003/2004, Wizara itaendesha warsha ya Kitaifa ya kukusanya maoni ya wadau. Aidha, taratibu za kuandaa Muswada wa Sheria hiyo zitaanza.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Wizara ilikamilisha kanuni za uanzishaji na usimamizi wa maeneo ya Jumuiya ya Uhifadhi wa Wanyamapori *(WMAs).* Kanuni hizo zilitangazwa katika Gazeti la Serikali Na.543 na zitaanza kutumika katika maeneo 16 ya majaribio. Wizara itahamasisha utekelezaji wa kanuni hizo katika maeneo ya majaribio katika mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Wizara iliimarisha ulinzi wa wanyampori kwa kununua magari 18, risasi 11,151, sare jozi 1,680, mahema 20, magodoro 1,000 ya safari na kutoa mafunzo maalum kwa Askari wanyamapori 94 na wanavijiji 78.

Katika kipindi cha 2003/2004, Wizara itaimarisha ulinzi kwa kuwapatia Askari wanyampori 150 mafunzo juu ya mbinu mpya za kupambana na ujangili na itaongeza vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003, siku za doria 557 zilitumika kusaka wanyamapori wakali na waharibifu katika Wilaya 24. Aidha, risasi 3,337 zilipelekwa katika mikoa 20 kwa ajili ya ulinzi wa maisha na mali za wananchi.

Katika kipindi cha 2002/2004, Wizara itaendeleza jitihada za ulinzi wa maisha na mali za wananchi dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu ikiwa ni pamoja na kuhamasisha wananchi kuwa waangalifu na kushirikiana na Askari wanyampori katika kudhibiti wanyama hao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Wizara ililenga kukusanya shilingi bilioni 8.2, hadi Mei, 2003 shilingi bilioni 7.8 zilikusanywa. Kampuni 40 za uwindaji na wageni 1,599 walishiriki katika uwindaji wa kitalii msimu wa mwaka 2002. Kati ya hao, 1197 walikuwa wawindaji na 402 watazamaji.

Aidha, Wizara imeandaa kipeperushi kinachoelezea maeneo ya uwindaji, ada na taratibu za kuendesha biashara ya uwindaji wa kitalii nchini na utalii wa picha.

Mwaka 2002/2003, Wizara ilitoa leseni 279 za biashara ya nyara na hati za kusafirisha wanyama hai mbalimbali nje ya nchi. Hadi Mei, 2003, wanyama na ndege 234,465 walisafirishwa na kulipatia Taifa shilingi milioni 98.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003, Rasimu ya Mipango ya Uendeshaji wa Mapori ya Akiba ya Burigi/Biharamulo na Ibanda/Rumanyika ilikamilika. Aidha, mapori ya Mpanga/Kipengele na Kimisi yalipandishwa hadhi kuwa Mapori ya Akiba. Barabara mpya zenye urefu wa kilomita 1,045 zilitengenezwa katika Mapori ya Akiba matatu na nyingine zenye urefu wa kilomita 831 zilikarabatiwa katika Mapori ya Akiba saba.

Aidha, viwanja kumi na moja vya ndege vilikarabatiwa katika Mapori ya Akiba manne. Vile vile, kilomita 736 za mipaka zilikarabatiwa katika Mapori ya Akiba na alama za kudumu 152 ziliwekwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara italima barabara mpya zenye urefu wa kilomita 2,150 kwenye Mapori ya Akiba ambapo kilomita 1,800 ni katika Pori la Akiba la Selous na kufanyia matengenezo ya kawaida barabara zenye urefu wa kilomita 1,700, kati ya hizo kilomita 900 zitakuwa katika Pori la Akiba la Selous. Pia, mipaka ya mapori yenye urefu wa kilomita 3,000 zitafyekwa na kuwekewa alama za kudumu.

Aidha, Wizara itakamilisha mipango ya uendeshaji wa Mapori ya Akiba ya Moyowosi/Kigosi, Burigi/Biharamulo, Ibanda/Rumanyika, Usangu na Mpanga/Kipengele.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2002/2003, Wizara ilitoa mafunzo ya uhifadhi wa wanyamapori kwa wanavijiji 138 kutoka Wilaya za Babati, Kilombero, Ulanga, Masasi na Pangani. Aidha, ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa wahitimu ulifanyika katika Wilaya hizo.

Mwaka 2003/2004, Wizara itaendesha jumla ya kozi za sita za ushirikishaji wa wananchi katika uhifadhi wa wanyampori.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003, taasisi ilifanya sensa za kawaida za wanyampori katika maeneo ya Mikumi, Kilombero, Selous, Katavi, Ruaha na Rungwa. Aidha, Kitengo maalum cha kuhifadhi takwimu na ufuatiliaji wanyampori kilianzishwa. Taasisi kwa kushirikiana na *Zoological Society of London* inatekeleza mradi unaoitwa *Carnival Monitoring Project* unaohisaniwa na *Darwin Initiative.*

Katika mwaka 2003/2004, taasisi itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kuhesabu idadi ya wanyamapori ndani na nje ya maeneo ya hifadhi, kuimarisha miundombinu na kuongeza vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Mfuko ulitarajia kupata mgao wa shilingi bilioni 3.3, hadi Mei, 2003, Mfuko ulipokea mgao wa jumla ya shilingi bilioni 3.6, kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 3.4 zilitumika katika kuimarisha shughuli za uzuiaji ujangili, hima sheria, utafiti na mafunzo. Aidha, Mfuko uligharamia shughuli za maendeleo katika Mapori ya Akiba na ushirikishaji wananchi katika uhifadhi.

Mwaka 2003/2004, matarajio ya Mfuko ni kupokea mgao wa shilingi bilioni 3.7 ambazo zitatumika kugharamia kazi mbalimbali za kuhifadhi wanyampori na mazingira yake.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003, Shirika la Hifadhi za Taifa *(TANAPA),* lilisimamia uhifadhi wa maliasili na mazingira kwa kufanya doria na kukagua mwenendo wa shughuli za kitalii. Hadi Mei, 2003, wanyampori 172 wa jamii mbalimbali waliuawa na majangili. Aidha, majangili 639 na silaha 27 za aina mbalimbali zilikamatwa.

Mheshimiwa Spika, hadi Mei, 2003 Shirika lilipokea watalii 381,747 waliotembelea Hifadhi za Taifa na kuliingizia shilingi bilioni 19.5, kati ya watalii hao, 120,486 walitoka hapa nchini na 261,261

walitoka nje ya nchi. Idadi hii ni ongezeko la watalii 118,127 au asilimia 45 ikilinganishwa na mwaka 2001/2002, ambapo watalii 263,620 walitembelea Hifadhi hizo.

Katika kipindi hiki kulikuwepo na ongezeko la mapato la asilimia 54.4 ikilinganishwa na mwaka 2001/2002. Ongezeko hili lilichangiwa hasa na kuongezeka kwa idadi ya watalii, ongezeko la viwango vya ada katika hifadhi za Taifa za Mlima Kilimanjaro na Serengeti na shughuli mpya za utalii katika Hifadhi za Tarangire na Ziwa Manyara.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003, Shirika lilikamilisha Mpango kamambe wa Usimamizi wa Hifadhi za Katavi na Ziwa Manyara. Rasimu ya kwanza ya Mipango Kamambe ya Usimamizi wa Hifadhi za Arusha na Rubondo ilikamilishwa.

Mwaka 2003/2004, Shirika litakamilisha maandalizi ya Mipango Kamambe ya Usimamizi wa Hifadhi za Mahale, Serengeti, Ruaha na Mikumi. Vile vile, Mapori ya Akiba ya Saadani, Uwanda wa Kitulo, Msitu wa Marang', Hifadhi ya Misitu ya Asili ya Meru, Ngrudoto, Kilimanjaro, Mashamba Na. 1 - 3 Majimoto, yatapandishwa hadhi na kuwa Hifadhi za Taifa.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ilishiriki maonyesho mbalimbali ya utalii ndani na nje ya nchi. Hadi Mei, 2003, watalii 256,625 walitembelea Hifadhi ya Ngorongoro. Kati ya hao, 118,341 ni kutoka nje na 138,284 ni kutoka ndani ya nchi. Idadi hii ni ongezeko la watalii 34,188 ikilinganishwa na watalii 222,437 mwaka 2001/2002. Mamlaka ilikusanya shilingi bilioni 6.7 ikilinganishwa na matarajio ya shilingi bilioni 5.5.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ilichangia shilingi milioni 988.7 katika kazi za maendeleo ya wananchi. Shilingi milioni 550 kati ya hizo zilitumika kama mchango kwa wananchi waishio ndani ya eneo la hifadhi, milioni 80 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro, milioni 290 kwa ajili ya Mradi wa *Ngorongoro Pastoralist Project - ERETO*, shilingi milioni 11.7 mchango kwa taasisi nyingine na shilingi milioni 57 mchango kwa maeneo yanayozunguka hifadhi.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa vituo vya nje vya Nainokanoka na Endulen umekamilika kwa asilimia 50. Ujenzi wa barabara ya Lemala hadi Empakaai unaendelea ambapo kilomita 38 zimekamilika. Katika mwaka 2003/2004, Mamlaka inatarajia watalii 255,555 ambao wataingiza shilingi bilioni 6.9. Mamlaka itakamilisha ujenzi wa barabara ya Empakaai na Olbalbal. Pia, Mamlaka itaanza ujenzi wa barabara kutola Olpiro mpaka Kakesio.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Wizara ilitarajia kuajiri watumishi 145 ili kujaza nafasi mpya na watumishi 58 kujaza nafasi zilizoachwa wazi. Katika kipindi hicho, watumishi 157 waliajiriwa.

Katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Wizara inatarajia kuajiri watumishi 166 wa kada mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, jumla ya watumishi 358 walipandishwa cheo na Mamlaka mbalimbali za ajira na mapendekezo ya kuwapandisha cheo watumishi 142 yaliwasilishwa katika Mamlaka husika za ajira.

Katika mwaka 2003/2004, watumishi 2,086 wa Wizara wanatarajiwa kupandishwa cheo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003, Wizara ilitarajia kuwapeleka mafunzoni watumishi 350 wa kada mbalimbali. Hadi Mei, 2003, watumishi 488 walikuwa wamehudhuria mafunzo mbalimbali ndani na nje ya nchi. Idadi hii imevuka lengo kwa kiasi cha 39% kutokana na hatua za dharura zilizochukuliwa kutoa mafunzo ya mbinu za kupambana na ujangili kwa Askari Wanyamapori 96 na baadhi ya watumishi kupata udhamini kutoka Taasisi mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Aidha, Wizara iliendeleza jitihada za kuviboresha vyuo vyake ili viweze kutoa mafunzo yanayoendana na Teknolojia ya kisasa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa vinafikia viwango vya kuweza kusajiliwa na Baraza la Taifa la Usajili wa Vyuo vya Elimu ya Ufundi *(NACTE)* na Mamlaka ya

Vyuo vya Ufundi Stadi *(VETA)*. Jumla ya walimu 11 wa Chuo cha Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi walipatiwa mafunzo yanayohusu mbinu bora za ufundishaji. Mwaka 2003/2004, Wizara inatarajia kuwapeleka mafunzoni watumishi 350 wa kada mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa vitendo vya rushwa ulitekelezwa kwa kuweka bayana taratibu za ajira, mafunzo, upandishaji cheo na utoaji wa leseni mbalimbali. Aidha, Wizara iliendesha warsha kuhusu kukabiliana na vitendo vya rushwa katika vituo vyake mbalimbali. Kama sehemu ya kukabiliana na vitendo vya rushwa, Mkataba wa Huduma kwa Mteja umeainisha wajibu wa watumishi wa Wizara kwa umma katika kutoa huduma. Vile vile, Mkataba umeainisha taratibu za kufuata iwapo mteja hataridhika na huduma aliyopewa.

Katika kipindi cha 2003/2004, Wizara itaendesha warsha za uhamasishaji katika vituo vyake katika jitihada za kukabiliana na vitendo vya rushwa pamoja na kusambaza nakala za Mkataba wa Huduma kwa Mteja kwa wadau.

Mheshimiwa Spika, katika kupambana na janga la UKIMWI, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali, iliendesha semina na mafunzo kwa watumishi wa Makao Makuu, Vituo vya *Sao Hill* na Ukanda wa Ziwa Victoria. Pia, Taasisi za Wizara, miradi na vyuo viliendesha semina za aina hiyo. Wizara iliendelea na juhudi za kuwahimiza watumishi kujiunga na Mfuko wa Bima ya Afya. Hadi Mei, 2003, watumishi 680 na wategemezi wao walikuwa wamepatiwa vitambulisho vya kuwawezesha kupata huduma za matibabu katika hospitali na vituo vya Afya vilivyoteuliwa. Katika mwaka 2003/2004, Wizara itaendeleza uhamasishaji na utoaji wa elimu kwa watumishi wake juu ya umuhimu wa kujiunga na Mfuko wa Bima ya Afya.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa 2003, Mashirika 21 kati ya 33 yalikuwa yamerekebishwa kimuundo au kubinafsishwa. Aidha, Wizara imeandaa taarifa ya utekelezaji kuhusu hatua iliyofikiwa kuhusu Mashirika ya Umma yaliyorekebishwa au kubinafsishwa.

Mwaka 2003/2004, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma, itaendelea na zoezi la kukamilisha urekebishaji na ubinafsishaji wa Mashirika yaliyobaki, pamoja na kufuatilia maendeleo yake.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, wananchi na Taasisi mbalimbali, kwa ushirikiano walioutoa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu.

Vile vile napenda kushukuru nchi wahisani na Mashirika mbalimbali kwa michango yao ya kifedha na kitaalamu kama ifuatavyo: Denmark, Norway, Finland, Marekani, Sweden, Japan, Ufaransa, Ujerumani, Ubelgiji, Uingereza, Jumuiya ya Nchi za Ulaya *(EU), ADB, AWF, FAO, FZG, GTZ, IUCN, KfW, Trade Aid, MIGA, UNESCO, UNDP, World Bank, WWF* na mengineyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kumshukuru Katibu Mkuu, Ndugu Solomon Odunga, Wakurugenzi na watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake, kwa juhudi na ushirikiano walionipa na kuiwezesha Wizara yangu kutekeleza majukumu yake katika mwaka 2002/2003. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa mwaka 2003/2004, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha makadirio ya matumizi ya Shilingi 57,853,038,200/=. Kati ya fedha hizo shilingi 31,477,786,800/= ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na shilingi 26,375,251,400 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. ANNE S. MAKINDA - MWENYEKITI KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Maliasili na Mazingira, kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Maliasili na Utalii katika mwaka wa fedha uliopita wa 2002/2003, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, kufuatana na kifungu namba 81, kifungu kidogo cha Kanuni za Bunge, nachukua fursa hii kukushukuru kwa kuniruhusu kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Maliasili na Mazingira, kuhusu Utekelezaji wa Shughuli za Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha uliopita wa 2002/2003, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, huu ni mwaka wa kwanza kupata nafasi ya kupitia, kujadili na kuchambua Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii, chini ya mfumo mpya wa Kamati za Kudumu za Bunge, ambao ni wa Kiwizara. Aidha, katika kupitia Wizara hii masuala yafuatayo yalijadiliwa:-

- Dira ya Wizara ya Maliasili na Utalii;

- Muundo wa Wizara;

- Taarifa ya Utekelezaji wa Maagizo yaliyokuwa ya Kamati ya Kisekta ya Biashara kuhusu Wizara hii kwa kipindi cha mwaka 2002/2003;

- Mapitio ya Utekelezaji wa mpango wa mwaka wa Maendeleo na Bajeti ya mwaka 2002/2003 hadi mwezi Aprili, 2003;

- Mpango wa Maendeleo wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2003/2004 na;

- Maoni, mapendekezo na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliieleza Kamati kuwa dira ya Wizara ambayo ni uhifadhi endelevu wa Maliasili, Mambo ya Kale na Uendelezaji Utalii wenye kuwajibika kuleta maendeleo kwa wote. Inatafsiriwa kwenye sera zake Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2003/2004. Aidha, sera hizo ni pamoja na Sera ya Wanyamapori, Sera ya Misitu, Sera ya Ufugaji Nyuki, Sera ya Utalii na Sera ya Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika tulielezwa kuwa muundo wa Wizara wenye Idara 5 za Kisekta ndio unaiwezesha Wizara hii kutekeleza malengo na majukumu yake kwa ufanisi kufuatana na sera nilizozitaja hivi punde. Idara hizo ni pamoja na Idara ya Utalii, Idara ya Uvuvi, Idara ya Wanyamapori, Idara ya Mambo ya Kale, Idara ya Misitu na Nyuki, Idara ya Sera na Mipango, Idara ya Utawala na Utumishi, Vitengo vitatu na Taasisi na Shirika, Wakala na Vyuo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa kutekeleza maagizo yaliyokuwa ya Kamati ya Kisekta ya Biashara kwa kipindi cha mwaka 2002/2003. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya mwaka 2002/2003, Kamati imeridhika na utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika mwaka huo. Wizara imekusanya maduhuli hadi Aprili, 2003 ya Sh.18,300,687,505/= ukilinganisha na makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka mzima wa 2002/2003 ya Sh.17,773,046,400/=. Hili ni ongezeko la asilimia 16. Kwa hiyo, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuvuka lengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ilitengewa Sh.10,927,341,200/= kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali. Lakini hadi Aprili, 2003 matumizi halisi yalikuwa Sh.2,409,204,456/= yaani asilimia 22.05. Wizara imeeleza kuwa matumizi hayo madogo yanatokana na kuchelewa kukamilika kwa taratibu za kusaini mikataba na hivyo kusababisha baadhi ya wahisani kushindwa kuwasilisha fedha hizo kwa wakati. Kamati haikuridhika na maelezo hayo hivyo, kuitaka Wizara itafute utaratibu mzuri zaidi wa kushughulikia miradi ya maendeleo kama inavyopangwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa pongezi za dhati kwa Wizara kwa mafanikio iliyoyapata katika kipindi cha 2002/2003. Mafanikio haya ni kama yafuatayo: -

- Ushirikishwaji wa wadau katika usimamizi, uhifadhi na matumizi ya Maliasili nchini;

- Ulinzi wa uhifadhi wa maliasili na mambo ya kale;

- Kuhimiza ushirikiano na uwekezaji wa Sekta binafsi;

- Kuridhia itifaki za maendeleo ya utalii, wanyamapori na uvuvi katika nchi za *SADC;*

- Ongezeko la ukusanyaji wa maduhuli;

- Kufanya mapitio ya sera mbalimbali;

- Urekebishaji wa Kanuni na Sheria mbalimbali;

- Kutayarisha mwongozo wa *Wildlife Management Areas* ili kuwezesha Wananchi katika Vijiji kushiriki katika shughuli za uhifadhi na kufaidika na maliasili hizo;

- Uendelezaji wa utalii; na

- Kuimarisha utendaji wa watumishi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, Wizara katika utekelezaji wa majukumu yake imekuwa ikipambana na matatizo yafuatayo: -

- Uvunaji na matumizi haramu ya mazao ya maliasili na utalii kama vile uvuvi wa kutumia makokoro, uvunaji holela wa misitu na uchomaji moto ovyo katika misitu;

- Kuchelewa kupata vifaa/zana za kufanyia kazi mbalimbali kutokana na urasimu na utaratibu mpya wa manunuzi yaani kwa kuzingatia *Procuremet Act, 2002;*

- Upungufu wa Askari wa Wanyamapori kwa ajili ya kudhibiti ujangili katika hifadhi;

- Lipo tatizo la kutokuwa na alama wazi la mipaka ya Hifadhi ya Taifa na hivyo kuleta migongano kati ya Vijiji na hifadhi hasa katika maeneo ambayo ushiriki wa Vijiji vinavyozunguka hifadhi ni dhaifu;

- Pia, ipo migogoro na mizozo kwenye baadhi ya hoteli zilizobinafsishwa, hivyo kuikosesha Serikali mapato na ajira;

- Hali kadhalika lipo tatizo la magari kuua ovyo wanyamapori katika barabara kuu kwenda Hifadhi ya Mikumi. Kwa mwaka mmoja tu wa 2002 waliuawa jumla ya wanyama mbalimbali 103 kwa kugongwa na magari yaliyopita katika barabara hiyo. Hapo sikuhusisha ndege na aina nyingine ya wanyama wadogo wadogo. Sasa hivi kuna matuta barabarani, lakini bado wanyama wanauawa. Idadi hii kwa miaka mingi wanyama watapotea. Upo pia utalii wa bure, hivyo kuifanya Serikali kukosa mapato ya kutunzia hifadhi hii. Kamati inafahamu ugumu wa suala hili, hivyo Vyombo husika vyote vikae ili ufumbuzi upatikane; *(Makofi)*

- Wizara inakabiliwa na upungufu wa watumishi kwenye hifadhi ya misitu na wanyamapori;
- Upo ukosefu mkubwa wa miundombinu, barabara na vitendea kazi; na

- Kamati ikiwa kwenye ziara yake katika hifadhi ya *Sao Hill* ilielezwa wapo wafanyakazi ambao kwa zaidi ya miaka minane hawajalipwa mishahara, marupurupu wala kupandishwa vyeo, Wizara iharakishe hatua ambazo wanaendelea nazo kuwalipa watumishi hao.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004, umezingatia mpango endelevu wa miaka mitatu unaoanzia mwaka 2003/2004 hadi 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha, Wizara imepanga kutekeleza malengo ya jumla ambayo yamepewa kipaumbele kulingana na majukumu ya Wizara kama nilivyotaja hapo awali.

- Lengo ni kukusanya maduhuli ya kiasi cha Sh.21,370,892,000/= ikilinganishwa na Sh.17,773.046,400/= za mwaka 2002/2003;

- Kurekebisha Sheria mbalimbali kwa kuzingatia Sera za Wanyamapori, Misitu, Nyuki, Utalii, Uvuvi na Mambo ya Kale;

- Kuweka mazingira mazuri zaidi ya kuwawezesha wadau kushiriki katika uhifadhi na uendelezaji utalii. Kuimarisha ulinzi wa Maliasili, mambo ya kale na vivutio vya utalii;

- Kuweka mazingira bora zaidi kwa wawekezaji katika Sekta ya Maliasili na Utalii; na

- Kuboresha utendaji wa watumishi kwa kusimamia marupurupu yao ya mishahara.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia na kutambua kwa makini taarifa ya Wizara hii, yafuatayo ni maoni, mapendekezo na ushauri wa Kamati:-

(a) Wizara iendeleze ushirikishwaji wa Wadau na Wananchi katika kusimamia, kuhifadhi, kulinda na kuendeleza maliasili na utalii. Kwa kufanya hivyo, tutaweza kupunguza uchomaji moto ovyo, migogoro ya mipaka kati ya hifadhi na Vijiji vinavyopakana nayo, ujangili na uvuvi haramu.

(b) Wizara ifikirie utaratibu mzuri zaidi wa kifuta machozi kwa Wananchi wanaoumizwa au kuuliwa na wanyamapori. *(Makofi)*

(c) Kutokana na matumizi kidogo ya fedha za miradi inayofadhiliwa na Wahisani iliyofanyika mwaka 2002/2003, Wizara ibuni utaratibu mzuri zaidi wa kutumia fedha za miradi ya maendeleo zinazotokana na Wahisani.

(d) Wizara ifanye uchunguzi kuhusu malalamiko ya Wananchi, mtu yule yule kulipa kodi ya *VAT* mara mbili *(Double Taxation),* kwani analipia wakati anapokata mti msituni, halafu hulipa tena wakati anapopasua mbao. Suala hili lilijitokeza wakati Kamati ikiwa *Sao Hill.*

(e) Migogoro ya hoteli zilizobinafsishwa zipatiwe ufumbuzi kwa sababu Serikali inapoteza mapato mengi na ajira kwa Wananchi. Hoteli hizo ni ile ya Mikumi na sasa tunafurahi kwamba Hoteli ya Kilimanjaro imepatiwa ufumbuzi na nyinginezo. *(Makofi)*

(f) Wizara iimarishe doria baharini, pamoja na kuwa inatoa taarifa za utafiti unaofanywa kuhusu aina za idadi ya samaki wanaopatikana baharini, ziwani, mabwawani na nchini pote.

(g) Kutokana na kuuawa kwa wanyama kwa magari katika Mbuga za Hifadhi za Mikumi, Kamati inashauri Serikali kupata ufumbuzi wa kudumu wa kuokoa wanyama hao.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii, ina uwezo wa kutoa mchango mkubwa zaidi katika Pato la Taifa kuliko inavyofanya sasa. Mkakati mahsusi uandaliwe wa kuendeleza utalii kwa kuboresha vivutio vya utalii. Pia, tunaweza kuongeza Pato la Serikali kutokana na kusimamia vizuri zaidi mazao ya misitu, wanyamapori na mazao yatokanayo na bahari, maziwa, mabwawa na mito. Nchi kama Mauritius inapata mapato yake kutokana na utalii.

Mheshimiwa Spika, mwisho, baada ya uchambuzi wa kina, Kamati yetu inakubaliana na Mpango, pamoja na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004. Hivyo, Kamati inaomba Bunge lako liyapitishe makadirio ya Wizara hii.

Aidha, fedha zinazoombwa na Wizara chini ya fungu la 69 ni Sh.57,853,038,200/= ambazo zimegawanyika kama ifuatavyo: Matumizi ya kawaida ni Sh.26,375,251,400/= na matumizi ya maendeleo ni Sh.31,477,786,800/=.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wanakamati wenzangu, napenda kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Wizara hii ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Zakia Meghji, Katibu Mkuu wake, Ndugu Solomon Odunga, pamoja na Wataalam/Watendaji wa Wizara yake, kwa kazi nzuri waliyoifanya kuandaa mpango wa Bajeti hii kwa makini na ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira tuliohusika na zoezi zima la kujadili na kuchambua maelezo ya Bajeti ya Wizara hii ni pamoja na Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Aziza S. Ali, Mheshimiwa Shaibu Ahmada Ameir, Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mheshimiwa Sharifa Mbarouk Khamis, Mheshimiwa William J. Kusila, Mheshimiwa Ernest G. Mabina, Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mheshimiwa Muttamwega B. Mgaywa, Mheshimiwa Bernadine R Ndaboine, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa Abdulkarim E. H. Shah, Mheshimiwa Mohammed Rajab Masoud, Mheshimiwa Esha H. Stima, Mheshimiwa Issa Mohammed Suleiman, Mheshimiwa Mathew T. Ole- Timan, Mheshimiwa Martha M. Wejja na juzi ameongezeka Mheshimiwa Masoud Abdul Salim, pia mimi mwenyewe Mheshimiwa Anne S. Makinda, Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru sana Waheshimuwa Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano walionipa hadi kuniwezesha kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Namshukuru pia Katibu wa Bunge na Katibu wa Kamati hii Ndugu Sam Manamba kwa kazi nzuri aliyofanya ya kuratibu shughuli za Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi hii kutoa maoni kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2003/2004 kwa mujibu wa kifungu cha 43(5) (b) (c) cha Kanuni za Bunge toleo la 2003. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwashukuru wapiga kura wote wa Jimbo la Mtambile Pemba, kwa kunichagua kwa kura nyingi kuwa Mbunge wao, ninawahakikishia kuwa nitawatumikia kwa kazi zao kwani mimi ni mtumishi wao kama nilivyowaahidi. Pia, ninawapongeza Wabunge wenzangu wote wapya wa vyama vyote viwili *CUF* na CCM kuingia katika Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitamshukuru Mheshimiwa Zakia Hamdan Meghji, Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa msaada wake wa kufanikisha hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi ya pekee kuwapongeza Wabunge wenyeji wote wa Bunge hili Tukufu waliotupokea tarehe 10 Juni, 2003 kwa kutushangilia kwa hoihoi na vigelegele vya aina yake wakati wa kula kiapo cha uaminifu mbele ya Spika. Mlituonyesha kukomaa na kupevuka katika demokrasia, haijapata kutokea! Hivyo, ahsanteni sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ingependa kutoa mchango wake katika Bajei hii kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ya Maliasili na Utalii ni Wizara yenye umuhimu mkubwa kusaidia kuongeza Pato la Taifa na kupunguza hali ya umaskini nchini. Kambi ya Upinzani kutokana na kuona

umuhimu wa Wizara hii, inapenda kutoa mchango wake katika Bajeti ya Wizara hiyo kwa kutoa maelezo yake katika makundi mawili ya kisekta ambayo ni Sekta ya Maliasili na Sekta ya Utalii.

Mheshimiwa Spika, tukianza na Sekta ya Maliasili, Kambi ya Upinzani ina mchango ufuatao juu ya Sekta hii. Kambi ya Upinzani inaipongeza Wizara kwa juhudi zake ambazo zimetokana na mafanikio yafuatayo: -

- Makusanyo ya Wizara kuongezeka, kwa mfano mwaka 2000/2001, Wizara ilikusanya jumla ya Shilingi bilioni 6.8 wakati malengo ya makusanyo kwa mwaka 2000/2001 ni Shilingi bilioni 5.6. Hivyo, makusanyo katika mwaka huo yameongezeka kwa asilimia 18. *(Makofi)*

- Wizara imeimarisha ulinzi zaidi dhidi ya majangili katika Mbuga za Wanyamapori kwani imetoa mafunzo kwa walinzi wake, pia imekamata nyara za Serikali, bunduki, risasi na kuwatia mbaroni baadhi ya majangili. *(Makofi)*

- Wizara imejaribu kuchukua hatua za makusudi za kuzuia uvuvi haramu katika maeneo ya Bahari ya Hindi, Maziwa Makuu (Victoria, Nyasa, Tanganyika na kadhalika) kwani mwaka 2001/2002, Wizara ilinunua boti mbili za kufanyia doria katika Bahari ya Hindi na huku maandalizi ya ununuzi wa boti nyingine kwa sehemu za Maziwa yanafanywa. *(Makofi)*

- Wizara imeonyesha jitihada nzuri za kusimamia ubora wa mazao yatokanayo na uvuvi ambao umeanza mwaka 2001/2002.

- Wizara imeanzisha mfuko maalum wa kuinua ushiriki wa Watanzania katika utafiti wa wanyamapori.

- Wizara katika mwaka wa fedha 2001/2002, imeanzisha dira yake ambayo inasema "uhifadhi endelevu wa maliasili ambayo inaendeleza mambo ya kale na uendelezaji utalii wenye kuwajibika kuleta maendeleo kwa wote".

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa ufafanuzi juu ya mambo ambayo yameelezwa hapa chini.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka kupata maelezo kutoka kwa Waziri juu ya utekelezaji wa mikakati iliyowekwa na Wizara ya kuanzisha mradi wa hifadhi za bahari na maeneo endelevu, mradi ambao umeanza toka mwaka 2000/2001.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetilia mkazo sana Wananchi wajishughulishe na ufugaji wa samaki, uvunaji na ulaji wa samaki. Mafanikio ya wananchi katika sekta hiyo ya uvuvi itatoa mafanikio katika masuala yaliyoelezwa hapo juu ikiwa kuna vyombo muhimu vya kufanya utafiti wa kina juu ya ufugaji, uvunaji na ulaji wa samaki sehemu mbalimbali nchini. Je, Wizara inasimamia vipi suala hilo la utafiti ili liweze kuleta mafanikio kwa bidhaa zitokanazo na samaki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2002/2003, Wizara ilijiwekea malengo kuwa itapanua, kuuza na kutangaza maeneo ya uwekezaji katika shughuli za Wizara yake (Maliasili na Utalii). Je, Wizara inaweza kulieleza Bunge hili ni kiasi gani imefanikiwa katika utekelezaji wa suala hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Wizara kutoa maelezo ya mafanikio ya malengo iliyojiwekea mwaka 2002/2003 juu ya mpango kamambe wa kuendeleza Sekta ya Uvuvi hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Wizara kutoa maelezo juu ya tatizo la Wanakijiji wa Nyamuma Wilaya ya Serengeti, ambao wanadai kuwa Serikali imewachomea na kuwabomolea nyumba zao bila ya sababu zozote kama inavyoonyesha nakala ya lalamiko lao kwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, lalamiko namba 103 la mwaka 2002. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa nchini Taasisi ya Uchunguzi wa Wanyamapori iko moja, nayo iko *Njilo Hill* Arusha, wakati Mbuga za Wanyama na Hifadhi za Wanyama ziko kote nchini. Je, Wizara haioni hili ni tatizo kubwa na ina mpango gani wa kuongeza vituo hivyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2001/2002, Wizara hiyo ilisema kuwa itaandaa maeneo ya Jumuiya ya Uhifadhi wa Wanyamapori. Je, ni kiwango gani Wizara imetekeleza suala hilo na maeneo yapi hapa nchini yamejumuishwa katika suala hilo?

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tatizo kubwa la wavuvi kuzama mara kwa mara kwenye Maziwa au Bahari na vyombo vyao vya kuvulia kama vile mitumbwi na kadhalika. Je, Wizara imefanya jitihada zipi za kupunguza ajali hizo ambazo zinawapata wavuvi hao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara inafanya jitihada zipi kuwawezesha Wananchi kuboresha afya zao kwa kuwafanya wajishughulishe na kuvuna samaki walioko kwenye Mito, Maziwa na Bahari hapa nchini, hata kujipatia fedha zaidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko mengi sana ya baadhi ya maeneo hapa nchini ambayo yanapakana aidha na hifadhi ya Taifa, kuwa kuna wanyama kama simba, tembo na mamba, ambao husababisha vifo pamoja na uharibifu wa mazao katika sehemu hizo.

Wizara hiyo imeanzisha Mfuko wa Wanyamapori ambao kila mwaka hukusanya takribani Shilingi bilioni 3, fedha hizo hutumika kwa mafunzo na utafiti yahusuyo wanyamapori; je, Wizara haiwezi kuongeza katika matumizi ya fedha hizo, kuwa pia zihudumie kutoa fidia kwa Wananchi wale ambao mashamba yao huharibiwa na wanyamapori?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapenda pia kuishauri Wizara hiyo juu ya mambo muhimu yafuatayo ambayo yakifuatwa yanaweza kuinua Sekta ya Malialisi hapa nchini. Mambo hayo ni kama yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, Wizara inavyo vituo ambavyo vinajihusisha na uandaaji wa mbegu za miti na miche ya miti, kwani Wananchi hupenda kukata mbao/miti katika misitu asilia au iliyopandwa bila kupanda miti mingine katika sehemu zile ambazo miti imekatwa. Miti hiyo isambazwe kote nchini, vilevile Wizara isimamie kwa karibu shughuli zifanywazo na *TAFORI*, ili matokeo ya tafiti zake ziwafikie Wananchi wote kwa wakati muafaka. Katika mwaka wa fedha 2001/2002, ilielezwa na Wizara hiyo kuwa *TAFORI* imeanza kusambaza vijitabu vielezavyo juu ya *Commercial Timber of Tanzania*. Vijitabu hivyo tunaomba viongezwe na visambazwe kwa haraka na vipelekwe sehemu zote nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Wizara iwahamasishe Wananchi zaidi katika shughuli za ufugaji wa samaki na kilimo cha mwani, pia ijitahidi kuwapatia mbegu bora za bidhaa hizo. Vile vile, Wizara ipange na iendeleze elimu ambayo inaitoa kwa Wananchi kupitia vipindi vya redio na vipeperushi kama ilivyoelezwa katika Bajeti ya mwaka 2001/2002. *(Makofi)*

Mheshismiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhamasisha Wananchi kuhusiana na uvuvi mdogo mdogo ili waunde vyama vyao vya ushirika vya uzalishaji wa bidhaa za uvuvi, vile vile waunde vyama vya ushirika vya kuweka na kukopa. Ili kuwezesha shughuli zihusuzo maliasili ziende kwa ufanisi, ni vyema Wizara ifanye mpango wa kuanzisha Bodi Maalum ambayo itasimamia masuala yote yahusuyo maliasili, Wizara ibakie na utungaji na usimamizi wa sera zihusuzo maliasili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapenda kuishauri Wizara kuwa ishirikiane na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhamasisha Wananchi kwa kuwaelemisha juu ya athari za kukata miti iliyoko kwenye vyanzo vya maji, uchomaji moto wa misitu na ukataji ovyo wa miti kwani kwa kutowaelimisha Wananchi hao tatizo la uharibifu wa mazingira linaweza kuwa kubwa na hata kuiletea nchi, Mkoa au Wilaya kutokuwa na aidha maji ya kutosha au mvua za kutosha.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani vile vile inapenda kuweka msisitizo kwa Wizara hiyo kuwa ianzishe mfuko maalum wa fedha ambao utatumika kuwasaidia Watanzania wazawa, ambao wako

tayari kupata mikopo ya kujihusisha katika biashara ya uwindaji Wanyamapori au uvunaji na uuzaji wa bidhaa za misitu, nyuki, samaki na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaishauri Wizara kuwa sehemu zile ambazo wananchi walio karibu na mipaka ya Hifadhi za Taifa na kadhalika, wapatiwe Askari wa Wanyamapori, pia vijana ambao wanaishi katika maeneo hayo wapatiwe mafunzo maalum ya kujilinda dhidi ya wanyamapori ambao wataleta usumbufu na uharibifu katika Vijiji hivyo. Vile vile, vijana hao watasaidia kulinda hifadhi dhidi ya majangili ambao huvamia hifadhi hizo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Wizara kupanua kiwango cha uvunaji wa wanyamapori wa hatari kama vile mamba na kadhalika, badala ya kuvuna kwa kipindi cha miezi sita, wavune kwa mwaka mzima, hasa sehemu zile ambazo wanyama hao wako wengi na wanaleta madhara makubwa kwa Wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ihamasishe Wananchi kupanda miti mara kwa mara hasa wakati wa kipindi cha mvua, vile vile Wananchi wapewe elimu ya kutosha juu ya faida ya kutunza misitu na kupanda miti. Pia, Serikali inaombwa kuhakikisha kuwa uvunaji wa misitu na wanyamapori unawanufaisha Wananchi wote waishio karibu na misitu hiyo au hifadhi hizo za wanyamapori kwa kuimarisha huduma zote muhimu za jamii kama vile shule, maji, barabara, hospitali na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani katika kumalizia ushauri wake juu ya Sekta ya Maliasili, inaomba Wizara husika kuwa inapotoa vibali vya uwindaji wa wanyamapori na uvunaji wa misitu ambayo iko karibu na makazi na mashamba ya Wananchi, inabidi Wananchi waelezwe kabla na baada ya kuwapata wawindaji na wavunaji, ili kuepusha migogoro kati ya makundi hayo mawili ya Wananchi wazungukwao na hifadhi au misitu na wavunaji wa bidhaa za misitu au wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inachukulia uzito mkubwa Sekta ya Utalii, kwani Sekta hiyo ni ya pili kwa umuhimu katika mpango wa uchumi wa Taifa, Sekta hiyo inachangia asilimia 16 ya Pato la Taifa *(Gross Domestic Product).* Katika Sekta ya Utalii kama nafasi nzuri kwa wauzaji wa bidhaa/ huduma za utalii, kwani bei za bidhaa hizo hupangwa na wauzaji wenyewe, lakini kwa upande wa Sekta ya Kilimo bei za bidhaa katika soko hupangwa na walaji (wanunuzi) ndiyo maana Sekta hiyo maendeleo yake ni ya kusuasua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Sekta hiyo tunapenda kuipongeza Wizara katika mambo yafuatayo ambayo yanaonyesha mwelekeo mzuri wenye matumaini kwa Sekta hiyo. Kambi ya Upinzani inapongeza Wizara kwa kufanya mambo muhimu yafuatayo: -

- Ukamilishaji wa tafsiri ya Sekta ya Utalii katika lugha ya Kiswahili.

- Urekebishwaji uliofanywa juu ya Sheria ya Wakala wa Utalii ya mwaka 1969 na Sheria ya Hoteli ya mwaka 1963.

- Ongezeko la ukusanyaji maduhuli katika mwaka 2001/2002. Makusanyo ya maduhuli yalikuwa Shilingi milioni 718 kiasi ambacho kimevuka lengo lililowekwa kwa mwaka 2001/2002 la Shilingi milioni 657, hivyo makusanyo yalivuka lengo kwa asilimia 9.3.

- Uanzishwaji wa Utalii wa Utamaduni *(Cultural Tourism)* ambao unaonyesha matumaini makubwa ya mafanikio.

- Uanzishwaji wa Chombo Maalum cha Kushughulikia Utalii ambacho kinaitwa *Tourism Confederation of Tanzania.*

- Imeandaa mpango kamambe wa utalii nchini.

- Kuweka uzito juu ya utafiti wa kuboresha takwimu zihusuzo utalii nchini.

- Kuweka uzito wa uwekezaji katika utalii.

- Kuifanya Sekta ya Utalii kuwa na mwelekeo wa utalii unaojali mazingira.

- Upanuzi na uimarishaji wa barabara ziendazo kwenye vivutio vya utalii.

- Uimarishaji wa ukaguzi wa Wakala wa Utalii, suala ambalo lilianza mwaka 2001/2002.

- Ongezeko kubwa la watalii waingiao nchini na mapato yapatikanayo kutokana kuingia kwao kama ilivyoonyeshwa kwenye Gazeti la Mwananchi la tarehe 16 Julai, 2003 kwa miaka ya 1998 mpaka 2002.

Mwaka 1998 idadi ya watalii ilikuwa ni 482,331 na mapato yalikuwa ni Shilingi bilioni 3.70. Mwaka 1999 idadi ya watalii ilikuwa ni 627,325 na mapato ya utalii yalikuwa ni Shilingi bilioni 7.33. Mwaka 2000 idadi ya watalii ilikuwa ni 501,669 na mapato ya utalii yalikuwa ni Shilingi bilioni 7.39. Mwaka 2001 idadi ya watalii ilikuwa ni 525,122 na mapato ya utalii yalikuwa ni Shilingi 7.25. Mwaka 2002 idadi ya watalii ilikuwa ni 575,235 na mapato ya utalii yalikuwa ni Shilingi bilioni 7.30.

- Wananchi wengi sasa wanafaidika na mapato yatokanayo na shughuli za utalii hasa wale Wananchi wanaoishi karibu na sehemu za utalii kama vile Hifadhi za Taifa za Serengeti, Ngorongoro, Manyara, Mikumi na kadhalika. *(Makofi)*

- Ongezeko la wafanyakazi kuajiriwa katika mahoteli ya kitalii kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali namba D katika Kitabu cha Bajeti cha mwaka 2002/2003 kama ionyeshwavyo hapa chini: -

- Idadi ya wafanyakazi kwenye mahoteli ya kitalii mwaka 1996 ilikuwa ni 100,000, mwaka 1997 idadi ya wafanyakazi ilikuwa ni 110,000, mwaka 1998 idadi ya wafanyakazi ilikuwa ni 132,000, mwaka 1999 idadi ya wafanyakazi ilikuwa ni 148,000 na mwaka 2000 idadi ya wafanyakazi ilikuwa ni 156,000.

- Mwaka wa fedha wa 2000/2003, watalii toka Urusi waliingia wengi sana kuliko miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe ufafanuzi juu ya masuala yafuatayo: -

- Kwa nini Mashirika mengi ya kigeni yanayotoa huduma za utalii yanapenda kuajiri watumishi watokao nje ya Tanzania? *(Makofi)*

- Kwa nini Wizara haifanyi utaratibu wa kuweka viwango maalum vya bei za huduma ya utalii kwa wazawa kwani Wananchi wanapenda kutembelea Mbuga za wanyama, lakini uwezo wa kifedha ni mdogo mno ukilinganisha na watalii watokao nje ya nchi hii? *(Makofi)*

- Hatua zipi Wizara inachukua katika Tanzania kuzuia wizi unaofanywa dhidi ya watalii kama ilivyotokea hivi karibuni Jijini Dar es Salaam na Wilayani Ulanga watalii kuibiwa fedha na mali zao? *(Makofi)*

- Wizara inajihusisha vipi katika kuinua kiwango cha elimu ya utalii katika vyuo vile vifundishavyo kozi zihusuzo shughuli za utalii?

- Malalamiko ya wafanyakazi wa iliyokuwa *Hotel 77 Ltd.* ya Mjini Arusha, waliopunguzwa bila kufuatwa utaratibu hapo mapema mwaka 2000 yanashughulikiwa vipi na Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaishauri Wizara hiyo katika sekta hiyo ya Utalii juu ya mambo yafuatayo:-

(a) Wananchi waelimishwe kwa upana zaidi juu ya faida ya shughuli za utalii.

(b) Kuweka mfuko maalum wa kuwasaidia wazawa kupata mikopo nafuu ihusuyo biashara ya utalii.

(c) Wizara kwa kupitia Bodi yake ya utalii ifanye *promotion* kubwa ya zile Hifadhi za Taifa, ambazo bado hazijafahamika ulimwenguni hasa zile ambazo haziko katika Ukanda wa Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani kwa kuhitimisha mchango wake juu ya Bajeti hiyo ya Wizara, inaipongeza Serikali kwa kutilia maanani mahitaji ya maendeleo ya Wizara ya Maliasili na Utalii, kwani kipindi cha 2002/2003 na 2003/2004, imeongeza Bajeti ya maendeleo ya Wizara hiyo kwa shilingi bilioni 20.6, kiasi ambacho ni sawa na ongezeko la asilimia 18.9 toka Bajeti ya mwaka 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii niweze kuchangia katika hoja ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Naomba nianze kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Ni lazima tuunge mkono kwa sababu kama Kambi ya Upinzani wanatuunga mkono hivyo na sisi wenyewe CCM lazima tuunge kwa bidii kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii vile vile kuipongeza Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa taarifa yao nzuri na kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya katika Wizara ile. Imeainishwa wazi katika hotuba na katika majedwali. Lakini vile vile nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa kuendelea kuwa Rais wa *Africa Travel Association (ATA),* ambayo kwa kweli ni heshima kwa Tanzania, imetujengea sifa sisi kama Watanzania na hasa Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Vile vile niipongeze Wizara kwa sababu katika miaka miwili mfululizo wamekuwa washindi katika mabanda ya maonyesho kule kwenye Uwanja wa Sabasaba. Ni dhahiri kwamba kazi ya Wizara ya Maliasili na Utalii inakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri nina na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, Wizara ya Maliasili na Utalii shughuli zake zinahitaji ushirikiano wa karibu katika kila Sekta ya Wizara nyingine katika nchi hii. Ili Utalii uweze kuendelea ni lazima tuwe na barabara nzuri, tuwe na viwanja vya ndege ili tuhakikishe watalii wanafika kwa urahisi. Tuwe na huduma za simu kwa ajili ya kurahisisha huduma za mawasiliano, tuwe na *internet services* kwa ajili ya kurahisisha kujitangaza. Sasa pamoja na mipango mizuri na kazi nzuri ambayo inafanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii, kama haitapata ushirikiano na Wizara nyingine za Serikali inawezekana kabisa ikakwama katika kujiendeleza.

Kama alivyosema ndugu yetu Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba, utalii umeongezeka vizuri sana. Pato linalotokana na shughuli za Utalii, lingeweza kabisa kusaidia na kuongeza Pato la Taifa vizuri sana. Lakini bado kuna maeneo hayajawa *taped* na si kwamba si vivutio lakini ni kwa sababu hayafikiki kwa urahisi. Sasa tukiachia Wizara ya Maliasili na Utalii peke yake inaweza kuwa kazi ngumu.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili niipongeze Wizara hii kwa kuendeleza Kilwa Kisiwani na Songo Mnara. Wilaya ya Kilwa Mkoani Lindi, ina vivutio vingi. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwamba, tulikuomba uende Lindi na umekwenda kujionea na tunashukuru kwa juhudi zinazoonekana za kuendeleza Kilwa Kisiwani na Songo Mnara na Majengo ya Wareno. *(Makofi)*

Lakini vile vile tunayo mapango kule Kipatimu ambayo pia ni kivutio. Lakini kufika Kipatimu toka Kilwa ndiyo tatizo. Lakini vile vile tunalo Bwawa la Viboko kule Kilwa sehemu za Kilanjelanje. Hivi vyote ni vivutio lakini kinachotukwamisha ni barabara. Kwa hiyo, ningependa kuishauri Serikali iisaidie Wizara hii, vivutio hivi vifunguke na vikifunguka vitaweza kabisa kuongeza pato katika Mkoa wa Lindi na hasa Wilaya ya Kilwa, ambayo kama barabara hii ikifunguliwa tutachohitaji ni kuhakikisha kwamba, Uwanja wa Ndege wa Kilwa unapata ndege za uhakika ili watalii waweze kuja na kuweza kuwavutia

wawekezaji waweze kutumia fukwe nzuri zilizopo Kilwa, kujenga Mahoteli na watalii waweze kuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ambalo ningependa kugusia liko katika ukurasa wa 20 hadi 21 juu ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu. Katika ukurasa wa 21 Mheshimiwa Waziri anasema, Wizara kwa kushirikiana na Wadau katika kuimarisha usimamizi wa fukwe na visiwa vidogo vidogo itaongeza juhudi na kuendeleza utalii wa mwambao. Sasa naomba juhudi za kuendeleza utalii wa mwambao zisifanyike Dar es Salaam tu, ninaomba waje kwenye Fukwe za Mkoa wa Lindi na Mtwara. Fukwe zilizopo katika Mkoa wa Lindi na Mtwara ni nzuri mno. *(Makofi)*

Tatizo lingine Mkoani Lindi ni barabara ya kufika *Airport* ni mbaya. Kama barabara ile ikitengemaa na tukapata wawezekaji katika hoteli, basi tunaweza na sisi tukapata watalii wengi. Ninaomba Wizara katika kuendeleza utalii wa mwambao, waje waangalie na Fukwe za Lindi na Fukwe za Mtwara.

Mheshimiwa Spika, eneo la nne niungane na Kamati ya Maliasili na mazingira juu ya Hifadhi ya Mikumu. Mimi kila siku nasema kitu ambacho naweza kuwashukuru wakoloni ni kutufundisha kuhifadhi, lakini mambo mengine siwashukuru. Tumshukuru pia Baba wa Taifa kwamba, alikubali tutenge maeneo na tukawa na Hifadhi za Taifa. Sasa hifadhi hizi ni urithi wa watoto wetu, wajukuu na kivutio kwa wageni wanaokuja. Hifadhi ya Mikumi ina barabara inayopita katikati. Kama walivyosema kwenye Kamati, wanyama wengi wanauliwa kwa sababu magari, madreva wanakwenda kasi wakati wameingia kwenye eneo la Hifadhi. Kuna mabango yamewekwa, ukiingia kutoka Morogoro au ukiingia kutoka Iringa kuna mabango yamewekwa pale wazi kabisa, yanayokueleza kwamba sasa unaingia kwenye Hifadhi ya Taifa ya Mikumi punguza mwendo. Lakini sisi wengine tunaopita barabara ile kwenda kwa wakwe zetu Mbeya, unakuta magari yanakimbia pale ni hatari. Yanakwenda *speed* nafikiri zaidi ya ile 50. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi ninaungana na Kamati ya Maliasili na Utalii kwamba, tuangalie *alternative* nyingine. *Alternatives* zilizopo mimi nadhani ni mbili. Moja kuondoa ile barabara ili ipite eneo lingine isiingie kabisa katika eneo la hifadhi ambayo ni ghali sana. Lakini tungeweza kufuata mbinu wanazofanya nchi nyingine tujenge *gate* pale magari yanapoingia kwenye Hifadhi, Serikali au wasimamizi wa Hifadhi wana-*note* kwamba, gari namba fulani limeingia kwenye *gate* la Hifadhi kutokea Morogoro. Kwa sababu *speed* ya 50 kutoka unapoingilia na inapokwenda kutokea upande wa pili, wanaweza kufahamu muda uliotumika. Wakiwahi kufika kule wanatozwa faini. Sasa *of course* hata wakitumia ujanja inawezekana, lakini hiyo itasaidia Hifadhi kwanza kusimamia vizuri na zile *speed gun* ambazo wangetumia askari wa traffic ambao wanaweza kuogopa kukakaa kwenye eneo la Hifadhi, lakini hifadhi wanao askari wao wa wanyama pori na sheria zipo ambazo zinasimamia maeneo haya, wanaweza kutumia *speed gun* hizo kusimamia magari yanayopita pale. *(Makofi)*

Kwa njia hiyo, kwa kuanzia ndiyo pekee tunaweza tukaokoa wanyama wale. Hata kuokoa huu utalii wa bure ambao unafanyika na wengi wanaopita eneo la Mikumi. Ukipita pale unapunguza *speed* uangalie kwanza twiga wanavyopendeza, pundamilia, ukiangalia tembo unavutiwa. Lakini utalii wa bure. Lakini vile vile tukiweka utaratibu wa geti utatusaidia kuhifadhi usafi ndani ya hifadhi ya Mikumi, kwa sababu hivi sasa magari mengine yakipita pale wanatupa takataka ovyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu sikumbuki katika Wizara gani nilisema tuwashauri wenzetu wanaotembeza magari ya abiria waweke mifuko ya lambo ya kuhifadhi uchafu, lakini wawe na eneo ambapo wakifika hapo zile takataka wazitupe. Wenzetu wanapoingia kwenye Hifadhi ya Mikumi wanafika wanatupa tu. Lakini tungekuwa na *gate* wanapoingilia kunakuwa na chombo ambapo wanatupa takakata, abiria wote wanatupa takataka zile halafu magari yanapita na kwa njia hiyo hatuwezi kuwa na uchafu uliozagaa na hata ukiwepo hautakuwa mwingi kiasi hicho. Kwa njia hiyo, tutaendeleza Hifadhi ya Mikumi, maana ukiangalia hata unapoingia Ngorongoro pale pana *gate* na unapoingia Ngorongoro unalipa na si vibaya hata *gate* la Mikumi tukiweka watu walipe kwa ajili ya kusaidia ulinzi na kusaidia katika kuhifadhi usafi. *(Makofi)*

Eneo la tano ningependa kuzungumzia juu ya mambo ya Kale. Naipongeza Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuhifadhi mambo ya Kale. Mambo ya Kale yanatuwekea kumbukumbu za historia za mababu zetu ili watoto wetu, wajukuu zetu, wajue tumetoka wapi hadi hapa tulipo. Kwa hiyo, mimi

ninashauri Wizara katika Jumba la Makumbusho la Mwalimu Nyerere, tuwe na eneo maalum la kuweka kumbukumba za Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Maana sasa hivi ukiingia pale Makumbusho unakuta mambo ya *Governor,* unakuta kuna wanyama na vitu vingine mbalimbali. Lakini sijui kama tumeweka kumbukumbu kamili za Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, kumbukumbu zile ni muhimu kwa ajili ya kuendeleza Historia ya Taifa letu jinsi tulivyopigania uhuru bila kumwaga damu, jinsi Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alivyoshirikiana na wananchi wengine, jinsi alivyofuta Uchifu na kadhalika mpaka hapa tulipo. Kwa hiyo, mimi pamoja na kuliita lile jengo la Makumbusho la Mwalimu Nyerere, basi tuwe na eneo ambalo litaweka kumbukumbu sahihi za mwalimu. *(Makofi)*

Eneo la sita ningependa kugusia suala la ufugaji wa nyuki. Naipongeza tena Wizara kwa kazi yake nzuri inayoifanya. Lakini mimi naomba basi kwa sababu ufugaji nyuki unatupatia asali na asali ni moja ya bidhaa ambayo ina soko zuri nje, kwa sababu asali yetu haijachanganywa na kitu chochote ni ya asili kutoka kwenye miti, basi tungeendeleza sekta hii kwa bidii zote. Kwanza itasaidia ajira kwa vijana na hasa akina mama. Mimi napigia debe kwetu Mkoa wa Lindi kwa sababu sisi tuna misitu ya asili mingi mno na kule tunaweza tukapata asali nzuri sana.

Hivi sasa wafugaji wapo lakini siyo wengi. Naomba Mheshimiwa Waziri, uje ukatembelee safari hii ukapitie miradi yetu midogo midogo iliyopo ya ufugaji wa nyuki ili uone jinsi gani Serikali kwa kushirikiana na *NGOs* au sekta nyingine zozote, watusaidie kujenga uchumi wa wananchi wetu kwa kutumia malialisi ya nyuki. *(Makofi)*

Eneo la saba ni kuhusu uhifadhi wa misitu yenyewe ambayo inakuwa kwa kweli chanzo kikubwa cha upatikanaji wa maji. Tunaona wenzetu wa Kilombero wanapata maji mengi kwa sababu Milima ya Udzungwa imehifadhiwa. Lakini maeneo mengine miti inakatwa ovyo. Sisi wakati tunatoka kwetu Lindi tunakuja Dar es Salaam, tunakutana na malori makubwa, mazito, yamebeba magogo. Mimi sijui magogo yale yanakatwa kwa vibali vya tani ngapi, maana hakuna siku ambayo hukutani na magari yenye magogo. Mimi nina wasiwasi kwamba, magogo haya tusije tukamaliza misitu yetu. Ninaomba vibali vinapotolewa basi Wizara ifanye utaratibu wa kufuatilia waone kwamba, ukataji ule unafuata viwango walivyoruhusiwa. Maana tukiwaachia tu hivi hivi hawa wakataji wanaweza wakakata miti ovyo kupita kiasi ambacho wameruhusiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile ningeomba kama mtu anapewa kibali kutoka Makao Makuu ya Wizara basi ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kumalizika)*

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja hii.

Kwanza kabisa, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Zakia Meghji, Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa hotuba yake nzuri. Vile vile nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu wake bwana Odunga na wafanyakazi wote wa Wizara hiyo kwa kazi nzuri waliyofanya katika mwaka 2002/2003. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza katika kudhibiti vitendo vyovyote ambavyo vingeweza kuwazuia watalii wasije katika mbuga zetu licha ya ugaidi uliofanyika tarehe 11 Septemba, huko Marekani, lakini Mheshimiwa Waziri na Wafanyakazi wake waliweza kuhakikisha kwamba, hatuathiriki kiutalii. Hii imeonyesha kwamba mwaka 2002 ambapo ni baada ya yale matukio, watalii waliendelea kuongezeka. Mfano mwaka 2002 kulikuwa na watalii 575,000 walikuja nchini, *compare* na 2001 ambapo watalii walikuwa 525,000 kwa hiyo, waliongezeka zaidi licha ya ugaidi tulipata watalii 50,000 zaidi. Vile vile kimapato tulipata dola milioni 25 zaidi. Kwa hiyo, hii ni kazi nzuri ambayo Mheshimiwa Waziri na Wafanyakazi wake walifanya, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo mimi nataka kuunga mkono hii hoja kwa asilimia mia kwa mia kwa sababu imeonekana kwamba hawa ndugu zetu wamefanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nina machache ya kusema. Msemaji Mkuu wa Upinzani, amegusia jambo ambalo nisipoliongelea nitakuwa sijamtendea haki Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Msemaji Mkuu wa Upinzani, amesema kwamba, kuna nyumba zilichomwa moto Nyamumwa kule Serengeti. Mimi kama Mbunge wa Jimbo la Serengeti, nakubaliana na alivyosema Mheshimiwa Mbunge. Hili analosema ni kwamba, Wizara ya Maliasili haikuhusika na hilo jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niweke bayana hili jambo. Wakati kitendo hicho kilipotokea hizo nyumba zilichomwa na *DC* wa Jimbo la Serengeti na mimi niliiarifu Serikali na sijawahi kumpelekea hiyo shida Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Jambo hilo mimi nililipeleka kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, nikalipeleka kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, nililipeleka katika Utawala Bora, Tume ya Haki za Binadamu na sikulifikisha kwake. Kwa hiyo, napenda kum-*clear* Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwamba, hahusiki na hilo, ningeshampa *copy*.

Nimefuatilia jambo hilo Serikalini, kinachonishangaza ni kwamba, Serikali haijachukua hatua yoyote wakati wanajua kabisa muafaka, nyumba zilichomwa watu wamekuwa wanaumia hawakusaidiwa lolote, watoto wao wanakufa, wazee wanakufa hakuna chochote. Lakini kinachoshangaza *DC* yupo na wala hawajachukua hatua yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sababu gani mimi sijui. Kweli tuseme huo ni Utawala Bora? Naomba Serikali ifuatilie hilo jambo kwa vyombo vya usalama nilivyo-*contact* navyo, vina ushahidi wa kutosha. Kwa nini huyu mtu hajachukuliwa hatua? Kwa hiyo, naomba kwamba hilo halimhusu Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Kwa hiyo, nafikiri katika kulijibu hakuna mtu atakayemwomba kwamba bwana jibu hilo swali. Serikali inajua na tunategemea kwamba itachukua hatua za kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Vyombo vya Habari vya Magharibi vimekuwa vikitoa taarifa katika vyombo vyao kwamba, ugaidi unataka kufanyika Tanzania, Serikali inakataa, wanasema tena wakati ambapo kuna sikukuku zinakuja na watalii wanataka kuja kwa wingi. Naomba Serikali yetu iwasiliane na Serikali zao ili iweze kuviambia hivyo vyombo vya habari kwanza kabla havijatoa habari hizo viwe vimewasiliana na Serikali. Kwa hiyo, wanaposema kuna kitendo cha kigaidi kinataka kufanyika kusiweko na mabishano. Ama sivyo wanatuharibia utalii wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kuhifadhi wanyama, lazima watu waweze kufaidi. Mimi nataka kuwashukuru sana Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kuweka Kitengo cha Ujirani Mwema. Kitengo cha Ujirani Mwema kimeweza kuwa-*sensitize* watu kujua umuhimu wa wanyama na sasa siyo kwamba ukimwona mnyama umuue, bali unazuia jangili asimuue ili mtalii aje amwone, aweze kuendelea kuja na kutoa hela. Vile vile napenda kushukuru sana kitengo hiki kwamba, kinasaidia kimaendeleo badala ya wananchi kuona wanyama wanatusaidia lakini kimetusaidia sana kimaendeleo, ukichukua Wilaya ya Serengeti, tumepata shule, tunapata maji, tunapata barabara. Kwa kweli kitengo hiki ni ukombozi wetu sisi. Kwa hiyo, tunaomba tena kitengo kiendelee kuimarishwa ili kitusaidie, ili watu wajue kwamba mnyama hayupo pale kwa ajili ya kuliwa. Enzi za kula vimuru imepita! Vimuru maana yake ni nyama iliyokaushwa. Mnyama ukimwona unaua, unakausha nyama, unaweka kwenye ghala unakula mwaka mzima. Sisi hatutaruhusu hilo na tunaomba sana kitengo hicho kiendelee kuimarisha ili wananchi wajue umuhimu wa wanyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaongelea kuhusu mambo ya misitu. Mimi kabla sijaja Bungeni nilikuwaTabora, nilikuwa nasafiri sana na treni. Ukipita leo unakuta msitu, kesho unapita msitu umekatwa watu wamepanda tumbaku. Wakati wa kuvuna anaendelea kufyeka misitu ili apate kuni za kukaushia tumbaku. Baada ya muda ya mfupi yule mkulima anahama pale anaelekea sehemu nyingine na kuendelea kukata miti. Tunaomba sana Serikali iweze kutoa elimu kwa wale wakulima wa tumbaku kwamba eneo hilo hilo kama utatumia ukulima wa kisasa kama Zimbabwe wanavyofanya, unaweza kulima miaka 10 bila kuathiri misitu. Tunaomba mbinu za kisasa zitumike ili misitu yetu isiathirike sana. *(Makofi)*

Vile vile tunaomba wale wanaolima tumbaku wapande miti. Nchi zingine kama unalima tumbaku unapanda miti, kilimo cha tumbaku siyo kibaya kinategemea unakilimaje, unapanda miti yako ya mikaratusi, wakati unavuna unakata ile miti yake unakaushia tumbaku yako na inaendelea kuchipua miaka hadi miaka. Lakini kitendo cha kukata misitu ya asili kwa ajili ya tumbaku unaendelea kukata, maeneo yakiisha rutuba halafu unakata na kukaushia, misitu itaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, alipitisha Kanuni za kuanzia *WMA*, ina maana kwamba yale maeneo wananchi wanayopakana nayo ambayo yana wanyama sasa watatakiwa wayamiliki. Sisi tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kufanya hivyo kwa sababu sasa wananchi watafaidika na wanyama hao moja kwa moja. Kama unatakiwa kuja kuwinda pale basi itabidi uje ukutane nao ili wakupe *quarter* na kile kipato kitaingia kwao. Kwa hiyo, sasa wataweza kusimamia na kuhakikisha kwamba, majangili hawaui wanyama. Hii teknolojia hii ni ngeni, kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Waziri, ajaribu kuhakikisha kwamba, watalaam wanakuja kuelimisha kama sisi pale Serengeti wawe wanakuja mara kwa mara wanatuelimisha ili tusije tukaathiri uhifadhi wa wanyama. Vile vile tunaomba katika *process* yote watoe ushauri kwa wanakijiji ili wababaishaji wasije kule kuyachukua yale maeneo na wananchi wakawa wanatumikia kama vibarua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeongelea mambo ya misitu, kwa ujumla unakuta kwamba misitu mingi inakatwa kila sehemu. Kama ulikuwa mtoto pale ukienda sasa hivi hakuna misitu imekatwa yote. Kwa mfano, Mlima Uluguru, mimi nimesoma Morogoro kulikuwa na swali moja tulikuwa tunaletewa. Ule mlima ulikuwa umejaa misitu, sasa tunaletewa swali unaulizwa ukitaka kukata miti pale utakataje? Sisi tulikuwa tunasema kwamba, lazima uanzie huku chini unakwenda juu, kwa sababu utakapofika juu hapa chini miti itakuwa imeota tena kwa hiyo ule mteremko wa maji hautaleta mmomonyoko. Leo hii hilo swali huwezi kulitunga tena kwa sababu ule mlima hauna miti. Kwa hiyo, tunaomba vyanzo vya maji vitunzwe. Halafu tunaomba upandaji wa miti uendelee kupewa kipaumbele, halafu tuhamasishe watu kutumia majiko sanifu. Takwimu zilizopo zinaonyesha waziwazi kwamba, Hifadhi ya Mikumi inaathirika. Mfano mwaka 2002 wanyama 1,000 walipoteza maisha pale, nyoka 500 walikufa, ndege 700 waliuawa na magari yanayokimbia. Wanyama wengine walikula plastiki kwa mfano tembo anachukua anaingiza kwenye mkonga halafu anakufa. *(Makofi)*

Tunaomba utaratibu upatikane kama vile msemaji aliyetangulia aidha tuweke *gate* kwa ajili ya kudhibiti *speed*. Pale *TANAPA* imeshaanza kufagia mahali kuondoa makaratasi. Lakini *speed* kwa kweli ni kazi ya *traffic.* Tunaomba Serikali iweke *long term plan* ya kupitisha barabara kando ya ile Mbuga, kwanza itasaidia watu wengi.

Napenda tena kumpongeza Mheshimiwa Zakia Meghji, Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa hotuba yake nzuri na kazi waliyoifanya nzuri, namwombea afya njema ili apate nguvu za kuendeleza hii kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia na mimi katika Wizara ya Maliasili na Utalii. Nadhani ni mara yangu kwanza kuchangia kwenye Wizara hii katika vikao vyako. Kwanza nianze kwa kusema mambo mema kwamba, ninaunga hoja mkono asilimia mia kwa mia. Si jambo ambalo ni la kuficha ni kwamba, Wizara imempata Waziri. Huyu Waziri kwa kweli ile ndiyo Wizara ambayo imepata hasa Waziri, kwa sababu Mheshimiwa Zakia Meghji, amefanya kazi kubwa sana katika Wizara hii. *(Makofi)*

Napenda kwa kweli niseme tunamshukuru na kumpongeza Rais kwa kumwacha pale kipindi kingine cha pili. Nafikiri Rais mwingine atakayekuja naye atapenda pia aendelee kuwa pale kwa sababu kwanza ameitangaza Tanzania Dunia nzima, kwa kuwa wamekuwa wakifanya maandalizi mazuri sana ya kushiriki katika kongamano mbalimbali zinazohusu Wizara yake, wametoa vipeperushi na machapisho mbalimbali ambayo ukiingia ndani ya ndege unakuta, ukienda kwenye balozi unakuta tofauti na zamani. Yeye mwenyewe amejitahidi kutoa maelezo mengi sana. Tumemwona mara nyingi sana kwenye kongamano za kimataifa akitoa maelezo na hali kadhalika amejitahidi sana kutetea kama Mlima Kilimanjaro uko Tanzania hauko Kenya. Kwa hiyo, tunampongeza kweli ndiyo maana tunamuunga mkono katika hoja hii. *(Makofi)*

Lakini jingine ambalo naomba niseme wazi ni kwamba, hapo zamani tulikuwa tunadhani utalii uko Mikoa ya Kaskazini. Ukitaka kutalii maana yake unakwenda Kaskazini Arusha kwenye mbuga za wanyama. Lakini yeye ameingia amejitahidi sana kusambaza shughuli za utalii sehemu mbalimbali za nchi yetu ambayo hiyo ni sifa kubwa.

Kwa sababu sasa maeneo mengine kweli hayana wanyama, lakini yana mambo ya kale na yeye amejaribu kufufua maeneo mbalimbali. Kuna sehemu nyingine anakwenda tu kuangalia kitu fulani ambacho ni cha pekee cha aina yake, kwa hiyo, amejitahidi. Hata kule kusema tu kwamba hicho Kituo cha Wanyama Tanzania ambacho kilikuwa kinakaa kule Serengeti, kinajulikana kama ni cha Serengeti peke yake, kujitahidi kuunda sheria ambayo itaitwa ni *Authority* ya Tanzania nzima kwa utalii. Nayo ni jitihada kubwa na ujasiri mkubwa. Kwa kweli tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitaka kusema kama wenzangu walionitangulia, suala la misitu na mkaa. Hili nilishazungumza na Mheshimiwa, kidogo linaonekana kama jambo dogo. Nimejaribu kupitia kitabu chake mwenyewe cha hotuba, ukurasa wa 24 ibara ya 46, inaelezea tu juu ya usimamizi shirikishi wa misitu, Vijiji 200 ndio anataka kufanyia majaribio. Nasema hivi Vijiji 200 ni kidogo sana, ni afadhali iwe ni kwa nchi nzima. Mkakati ufanyike iwe ni kwa nchi nzima kwa sababu kila Kijiji kitahitaji kuwa na miti.

Lakini nimesoma kwenye taarifa ya Mwenyekiti wetu, tumeona ukurasa wa tatu, ukurasa wa sita, kumi na kumi na mbili, wanaongea juu ya sera, wametaja vizuri, juu ya watu wasichome moto, wametaja juu ya kushirikisha watu, basi na kwamba kwa sababu ya shida, wanaongeza kipato. Sijaona, na vile vile kwenye upinzani kwenye ukurasa wa sita imezunguzia juu ya wananchi kuhamasishwa, kupenda miti na hivi. Sasa sikuona *seriously* kabisa mahali panazungumza juu ya uharibifu wa miti kwa kuchoma na hasa kwa kuchoma mkaa kwa kiwango ambacho si cha kawaida. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wote mtakumbuka tunavyosafiri barabarani. Siku moja nikamtania Mama Meghji nikasema, je, sasa kumeanzishwa Ushirika wa Mkaa? Kwa sababu kwenye Ushirika kuna Vyama vya kawaida vidogo halafu kuna *Union.* Sasa hivi kama vile kuna Vyama Vidogo vya Mkaa. Ukitembea kutoka Morogoro au kutoka Dodoma kwenda Morogoro au Morogoro kuja Dodoma au kutoka Chalinze kwenda Segera au kutoka Mikumi kwenda Iringa au unakuja *the other way opposite,* lakini hasa Segera unakuta kila nyumba mlangoni kuna magunia kumi, ishirini. Lakini ukifika eneo fulani, unakuta magunia hata mia mbili mia tatu yaani kule ni *Union* sasa. kuna nyumba mtu ameweka magunia kumi, sita lakini kwa kweli unakuta kuna *Union* hasa, Chama Kikuu cha Ushirika wa Mkaa.

Hili sasa si suala la Mheshimiwa Waziri. Waziri amejitahidi kutoa sera na yeye kama tulivyosema ni mchapakazi mzuri, lakini Watendaji hawamsaidii kwamba vibali vinatolewa namna gani. Sasa hivi inaonekana hakuna kibali. Kwa sababu kama kwa Mheshimiwa Eliachim Simpassa, kuna mkaa, kwa Mheshimiwa Philip Marmo kuna mkaa, kwa mzee Makwetta kuna mkaa, kwa Kagonji kuna mkaa, kwa Mzee Spika kuna mkaa, kila mmoja ameweka magunia kumi, ishirini, hapo hakuna kibali. Hapo ni kibali cha kila mtu. Ndio maana yake! Lakini kama kweli kuna vibali, tunajua kwamba nishati ni ngumu sana kwa kutumia umeme, tunatumia mkaa. Lakini kiwango hiki cha ukataji ni kikubwa kiasi ambacho kama hakiwezi kutawaliwa, kama hakiwezi kurekebishwa misitu itakwisha, ile *course of ten years to come* hakutakuwa na misitu. Kwa kweli utakuta watu hawajali.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine imeonekana wazi kwamba wale wale wasisimamizi wanaoitwa Mabwana Misitu ndio wana miradi yao wao wenyewe. Unakuta sehemu nyingine ameruhusu watu wanakata lakini anapata chochote au yeye mwenyewe ni Wakala wa Mkaa. Sasa hali hii katika nchi ni hatari. Halafu inaleta aibu kwa sababu tunaongelea juu ya kupanda miti na Mheshimiwa Rais amekazania sana juu ya kupanda miti kila tarehe moja, lakini tunapanda na tunavuna mara tano ya tuliyopanda. Sasa ni kama tunapingana sisi wenyewe kwa wenyewe. Huku tunapanda, huku watu wanafyeka.

Sasa unapita barabarani sisi tunazungumza mambo yetu hapa kwamba misitu itunzwe, lakini wale wanawaonyesha barabarani tena wala hawaogopi. Wanasema mikaa ni hii hapa, hapa ni Chama cha Ushirika, hapa ni *Union.* Mheshimiwa Waziri na wewe si unapita barabarani na watu wako? Unaonaje

hali hii? Sasa hii hali sehemu nyingi ndio anasemea Mheshimiwa Dr. James Wanyancha. Anasema misitu imeadhirika kwa sababu wao hawana kuathirika. Imeathirika sio imeadhirika. Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, tunataniana. Anasema msitu ule wa Ulugulu umeathirika sio umeadhirika, umeathirika. Kila mahali imeathirika yaani imeumia, imepata taabu, hakuna tena msitu, yamebaki mawe. *(Kicheko)*

Tukienda pale Iringa, zamani milima yote ilikuwa inapendeza, unakuta sasa hivi ni mawe tu. Ukienda pale Mbeya ile *Mbeya Peak* ilikuwa inapendeza sana sasa hivi ni mawe tu. Kila unapopita, ukienda Lushoto kwa akina Mheshimiwa Charles Kagonji, ilikuwa milima ile ni misitu, sasa hivi ni mawe tu. Kila unapokwenda ni mawe *and nobody* anashituka.

Sasa hii ni hatari sana, ni lazima kile kitengo cha misitu sasa watafute utaratibu. Ni kweli tunahitaji mkaa katika matumizi ya nyumbani, lakini sio kwa kiwango hiki.

Mheshimiwa Spika, unajua hali ilivyo ni kwamba, hivi kama kweli kuna kukata mti tu na kuchimba shimo ukatumbukiza na ukaacha moto unawaka na kesho asubuhi ukapata mkaa ukauza na hii habari ya kutaka kujipatia kipato cha kwenda kufyeka shamba, ulime mwaka huu uvune mwaka kesho ndio upate mazao, ungechagua kwenda wapi?

Mimi nadhani ungechagua mkaa, maana ndio *the cheapest employment.* Ndio rahisi kwamba unakata leo, baada ya siku mbili tatu unauza. Kwa hiyo, kila mmoja amejiajiri katika hii ajira rahisi. Kila mmoja anajiajiri katika ajira rahisi. Kitu mara moja tayari. Kama watu wanaochoma mahindi siku hizi. Serikali inasema msichome mahindi, Mheshimiwa Charles Keenja anapiga kelele, msichome mahindi. Kikija chakula wanasema Mheshimiwa Charles Keenja upige kelele zako tu.

Mimi nikiuza mahindi, hindi moja shilingi 100/=, nikiuza mahindi mia moja napata shilingi ngapi? Je, nikija nikiyavuna hayo nikiweka kwenye gunia nikauze napata shilingi 3,000/= tu! Kwa hiyo, mtu anaangalia *which is the cheapest.* Sasa mkaa unakata mti unaweka, unaungua. Ukimaliza, kesho unapata hela. Kama *employment* ya Watanzania itakuwa ni mkaa, ndio nasema mimi naogopa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amejitahidi ameweka sera. Lakini wasimamizi wake kutoka kwenye Vijiji, kwenye Wilaya mpaka huko Makao yake Makuu, bado hawajamsaidia Waziri.

Mimi naomba sana tusaidiane katika hili maana miti ni yetu wote. Kwa nini mtu mwingine anafaidi miti peke yake wakati ni mali yetu sote? Hilo mimi nimeona niseme kwenye Wizara hii kwa sababu inatisha na kwa kweli inakera. Tunaomba katika hili Mheshimiwa Waziri atoe maagizo kabisa na usimamizi uonekane. Waziri anafanya kazi nzuri tunampongeza sana hapa na ametujengea heshima sana na tunamwombea Mungu ampe afya azidi kutusaidia.

La mwisho ni hili aliloongea Mheshimiwa Maria Watondoha. Sisi Waafrika nafikiri hatuna utaratibu wa kuweka kumbukumbu. Hata mtu binafsi tu! Hatuwezi kuandika historia yako binafsi, ukimwuliza mtu ameweka vitu vingapi, ameandika mpaka wapi hata mambo yanayomhusu yeye mwenyewe, hatuna! *We live at random.* Hata ukifa leo mtu hawezi ku-*trace* hivi huyu fulani au ndugu yangu Madina amefanya mambo gani, aliandika kitu gani kinachomhusu, hakuna! Mheshimiwa Eliachim Simpassa, hamna!

Tukupongeze Spika wewe angalau kuna vitu unatuandikia tunaona. Angalau *you have a record,* watu watapitia kwamba hiki kiliandikwa na Mheshimiwa Pius Msekwa. Lakini sisi wengine ni watu tu wa kupita hata ukikuta kumbukumbu unapita tu. Lakini nasema, kumbukumbu za viongozi wa Kitaifa, Mwalimu Julius Nyerere, Mzee wetu Abeid Karume, Edward Sokoine, akina Mzee Rashid Kawawa hawa, tuna watu wazito humu na akina Salim Ahmed Salim, wamefanyakazi kwenye *OAU,* wanahitaji kumbukumbu kwamba kunakuwa na eneo kuna *status* zao pale na maelezo mbalimbali na vitabu mbalimbali. Hii sisi hatuna.

Mheshimiwa Spika, wewe umekuwa Mwenyekiti wa Mabunge ya *Commonwealth.* Ukiingia kwenye ile *House of Commons* unasoma historia ya Uingereza yote kwenye kuta tu, huhitaji kitabu. Sisi hakuna kitu, ni hivi hivi maisha yetu, kila mahali hakuna kumbukumbu. Tunaweza tusiweke huku kwa sababu jengo hili halijakaa kwa ajili ya kuweka kumbukumbu yoyote. Lakini kuwe na mahali mtu akitaka

kusoma habari za Edward Sokoine, historia yake na amefanya nini, unakwenda unasoma. Kwa Mheshimiwa Hayati Julius Nyerere, unakwenda unasoma. Hivi hakuna, wala kuandika vitu tu kwamba tuna Watanzania na hiki na hiki na kuna mahali fulani nenda kavione, hakuna!

Lakini tunashukuru Mwenyezi Mungu kwamba kwa vinyago kwa kweli hapo hatujambo. Vinyago kwa kweli hapo tunashinda nadhani dunia nzima. Hiyo tunasema ahsante kwa mambo ya vinyago na Mungu azidi kuwabariki wale wanaochonga vinyago, hiyo nashukuru. Lakini kwa maandishi na kuweka kumbukumbu, sanamu, nini vitu muhimu na maelezo, kwa kweli bado tuko nyuma.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa muda huu mzuri. Nampongeza Waziri, Mheshimiwa Zakia Meghji, aendelee na moyo wake wa kusaidia nchi hii kwa kupitia Utalii, tunampongeza kwa makusanyo mazuri ya fedha, tunampongeza kwa kutujengea heshima ya nchi yetu. Naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza kabisa nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika hoja hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Pili, ningependa kutumia nafasi hii kumpongeza Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Zakia Meghji na wataalamu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kusimamia maliasili ya nchi hii. Kama walivyosema wenzangu, Wizara hii imeshikwa na Waziri shupavu na ametujengea heshima Watanzania na hotuba yake hii inaonyesha wazi kwamba ana dira, kuna mwelekeo. Kuna miongozo, kuna uchambuzi, kuna taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, samahani, Mheshimiwa Zakia Meghji ni mama lakini nadhani hapa kwa kweli hakuna jinsia, ni utaalamu mtupu. Kuna mtaalam mmoja aliwahi kusema kwamba katika dunia ya sasa ni wale watu wanaothubutu kuona mbali ndio wanaoweza kujua uwezo walionao. Nadhani Mheshimiwa Zakia Meghji, anathubutu kuona mbali na ndio maana anajua uwezo wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kuchangia mambo makubwa mawili. Moja nakubaliana na mawazo yote yaliyosemwa na wenzangu waliotangulia hasa Mheshimiwa Eliachim Simpassa, Mheshimiwa Anne Makinda na Mheshimiwa Dr. James Wanyancha. Lakini ningependa kusema tu kwa lile la Mheshimiwa Eliachim Simpassa, labda nipendekeze tu kwamba ili kutatua hili tatizo la kuni, tutoe mwongozo kwamba kila Kijiji, kila Taasisi iwe na shamba la kuni, iwe ni *wood plantation.* Bila kuwa na hivyo, maadam *demand* ya mkaa ipo, tutakuwa tunahangaika tu, wataendelea kukata miti kwa sababu wanahitaji. Kwa hiyo, tuanzishe mashamba ya miti ya kuni kila Mji.

Hapa Dodoma tungechagua eneo la eka 10,000 tukapanda miti na tukawa na *fuel shade* kwenye Mji wetu. Kwa hiyo, watu watakuwa wanatatua tatizo hili. Napendekeza hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kusema mambo makubwa mawili. Moja ni kwamba Watanzania tuwekeze katika raslimali muhimu yaani jiografia yetu. Kwa mahali hapa tulipo kwa sababu ya *location* ya Tanzania ilivyo katika Afrika tunaweza tukavuna na tukafaidika kutokana na jiografia yetu. Kwa mfano nchi za jirani, nchi nane zinazotuzunguka hasa zile saba zinatumia Bandari ya Dar es Saalam. Kwa kuendeleza barabara, kujenga barabara imara na nzuri zinazounganisha Tanzania na nchi hizo za jirani, tunaweza tukaimarisha biashara kati ya nchi hizo kwa kujenga reli imara zinazounganisha Tanzania na nchi hizo. Tunaweza tukapata faida ya kufanya biashara na nchi hizo na wanapoagiza mazao yao kwenda nje au kutoka nje, basi lazima wapitie Dar es Salaam. Kwa kutumia jiografia tu hata bila ya kulima mahindi, nchi inaweza ikafaidika kwa kutumia jiografia yake. Ni kama mgodi ambao hauwezi kuondosheka.

Watanzania tumieni jiografia hii, ni mgodi ambao haumaliziki, uko pale ulipo na Wizara hii ndio inayohusika. Utakuta fedha zinazopatikana ni kutokana na kuuza jiografia. Mlima Kilimanjaro, Mbuga, Bandari, Viwanja vya Ndege na Vituo vya Mikutano, watu wanakuja hapa wanaleta fedha za kigeni bila kulima mahindi na bila kulima kahawa. Tutumie jiografia yetu kama raslimali ya kujenga nchi hii. *(Makofi)*

Tanzania ipo hapa kwa sababu ipo na hatukuiweka hapa. Kwa hiyo, kuna bahati ambayo huwezi ukaiunda kama gari. Sasa kwa bahati mbaya hatujui raslimali hii. Kutokana na hizi *hinterlands* ambazo zinapakana na nchi yetu, hivi sasa nasikia katika Ziwa Tanganyika wenzetu kwa upande fulani wameanza kuimarisha Bandari ya Mpulungu katika Ziwa Tanganyika na wanataka wajenge reli kati ya Mpulungu na Kasama ili bidhaa za kutoka Uganda, Rwanda, Burundi, Kongo na Zambia ziende upande mwingine ule na kuua reli ya Kati na Bandari ya Dar es Salaam. Sisi tumebaki hivi hivi kama Twiga, *docile.* Tumebweteka na wanataka kumaliza kabisa mali yetu. Tutazame mikakati ambayo itatujengea nchi hii. Namshukuru Waziri ameanza kutambua umuhimu huu.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ambayo tungeweza tukafaidika ni pamoja na kufufua historia ya nchi yetu. Kwa mfano, Bagamoyo kama alivyosema. Nyumbanitu katika Wilaya ya Njombe inaaminika kwamba ni chimbuko la makabila ya Nyanda za Juu Kusini. Ukiweka mnara pale, watu watapenda kuona pale au makambi ya wakimbizi, wapigania Uhuru katika Tanzania ya Mgagao, Kongwa na Mazimbu, tukiyajengea na kuweka historia pale, watu wa kutoka nchi hizo watapenda kwenda kuangalia pale na kufanya hija na kumbukumbu ya ukombozi wao. Lakini tumenyamaza kimya tu. *(Makofi)*

Wenzetu kule *South Africa* pale walipomfunga Mandela sasa pamegeuzwa kuwa ni Kituo muhimu cha utalii na wanapatia pesa pale. Sisi hapa tumebaki hivi hivi. Lazima tubuni maeneo mapya ya kutengeneza fedha kwa kutumia akili. Hii ni njia mojawapo ninayopendekeza hapa. Nasikia kwamba kama walivyosema wenzetu hapa, tumejenga kaburi la Sokoine liko Monduli, la Baba wa Taifa liko Butiama na hao watakaokuja sijui tutakwenda kwao.

Mimi nimewahi kwenda Uchina, nilipata heshima ya kwenda kuona maiti ya Hayati Mao, iko pale. Kwa sisi hapa sijui kama ndio kutukuza au vipi, lakini haya ni baadhi ya mambo ya kuangalia kadri tunavyozidi kwenda mbele.

Mheshimiwa Spika, vile vile nimesimama hapa kuchangia wazo la pili nalo linahusu uchafuzi wa mazingira katika nchi yetu. Ukiangalia nchi hii, hizi barabara za kutoka Dar es Salaam kwenda Mbeya, Dar es Salaam kwenda Arusha, Dar es Salaam kwenda Mwanza na kufuata hizi njia za Reli pembeni mwa njia hizi utaona tabia ya Watanzania. Yamejaa makaratasi, marambo, chupa za maji, maganda ya matunda na kila takataka. Nchi imechafuka na mtu hajali. Katika baadhi ya magari, kwenye magari huwa wanagawia *biscuits,* maji na makaratasi ya kuwekea uchafu kwa sababu wanataka usichafue gari lao, lakini wanataka uchafue nchi yetu, mali yetu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napendekeza kwamba Wizara hii na Wizara nyingine zinazohusika zifanye kampeni maalum ya kuondoa takataka hizi katika barabara hizi na kuziangamiza halafu kuweka utaratibu wa kudumu wa kuzuia wenye mabasi wasiruhusu wasafiri kutupa takataka nje ya magari yao na kuwe na Vituo kama Morogoro na kila mahali ambapo wakifika, wanatupa takataka zao na waelekeze Chama cha Wenye Mabasi Tanzania kuanza kutunza nchi hii. Nchi iwe safi. Kama Wizara ya Ujenzi kwa makusudi kila mwaka huwa inapita inakata nyasi kando kando ya barabara yake, kwa nini isione hili? Kama huwa inazibua maji na matakataka kwenye mifereji kwa nini isione hili? Wakati umefika wa kuiweka Tanzania iwe safi. *(Makofi)*

Katika Mlima Kilimanjaro kwa bahati nzuri binti yangu anafanya kazi pale, wale wanapopanda Mlima ule wanakuta mlima wote umepambwa kwa mifuko ya rambo na makaratasi. Wanakuja kuangalia mlima, sio mifuko ya rambo na makaratasi na chupa za bia. Tuanze kutazama na kujenga tabia ya usafi katika kudumisha mazingira ya usafi katika nchi yetu. Kwa hiyo, napendekeza kwamba kuwe na kampeni ya makusudi ya Kitaifa ya nchi nzima ya kuondoa takataka katika nchi nzima na Wizara ya Ujenzi vile vile iwe na utaratibu au iajiri watu kuondoa takataka hizi kandokando ya barabara kabla ya kuweka utaratibu wa kudumu na kwamba wenye magari, basi vile vile wajulishwe kwa kuandikiwa barua kusudi wazuie tabia hii. Vile vile, mashuleni na kila mahali elimu ya usafi iimarishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile ningependa niseme kwamba pamoja na mikakati ambayo naipongeza sana, sisi pia tutazame namna ya kupata hela kwa njia nyingine. Kwa mfano, tukijenga barabara na reli, tukaimarisha viwanja vya ndege fulani, hata viwanja vya Mikutano tu, sasa hivi ni Arusha tu au viwanja vya michezo ya mipira, hii nayo inaingiza hela katika nchi kuliko hata kiwanja kingine chochote kile.

Lakini tumebaki hapa hapa tunaangalia Arusha tu. Kwa mfano mchezo wa *Golf,* watu wanasafiri dunia nzima kwenda kucheza mahali fulani ambapo kuna viwanja vizuri. Kwa nini tusiunde Kamati Maalum ikaangalia maeneo mapya ya kuwekeza ili tuweze kupata fedha za kigeni ili nchi yetu hii isibaki inaangalia chai na kahawa na pamba, ikaangalia haya maeneo ambayo yanatokana na jiografia yetu. *We are in Tanzania, we happened to be born in Tanzania,* tutumie raslimali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakoloni waligundua tabia ya Watanzania ndio maana walitupatia alama ya Twiga, Kenya waliwapa alama ya simba na wenzetu Uganda alama ya ndege. Ukiangalia tabia ya Twiga pamoja na uzuri wake wote ule lakini watu wanamwangamiza kwa urahisi kwa sababu ya kuzubaaau upole wake ambao unapita mipaka. Ni mnyama asiye *aggressive* ni *docile* na *passive!* Ni vizuri na Watanzania tukaangalia hii tabia yetu katika dunia hii ya mashindano ambayo haijali nani ni nani. Kwa kweli tukiendelea na tabia hii ya *docility* tutakuwa watu wa mwisho kabisa katika dunia hii ya mashindano. *(Makofi)*

Kwa hiyo, napendekeza na kutoa angalizo kwa upande ufuatao, moja, hili suala la misitu, kukabidhi wananchi watunze baadhi ya misitu, tuwe waangalifu, tunaweza tukaangamiza nchi kama alivyosema mwenzetu Wanyancha pale. Pili, Wizara iangalie madhara ya misitu hii ya Misindano maana kila inapoota inaua miyaa mingine yote. Tupate ushauri katika hili. Mimi nimeona kwenye kitabu cha Waziri ukurasa wa 50, nafurahi kwamba hata Wasukuma sasa wameanza kupanda miti. *(Makofi)*

Vile vile tutilie mkazo watalii wazalendo. Mimi sijafika Ngorongoro wala Manyara wala Serengeti siijui, sembuse wengine! Kwa hiyo, kuna haja ya kutazama mikakati ya ku-*encourage local tourists.*

Lingine ni kwamba Wizara izuie wananchi kuwatupia wanyama chakula. Wananchi wakifika Mikumi wanawatupia wanyama ndizi. Tabia hii inasababisha magonjwa ambayo hayakuwepo na wanaua nguvu ya asili ya wanyama wale ya kutafuta chakula wenyewe. Kutokana na tabia hii, wanaua silika ya wanyama kutafuta chakula. Sasa wananchi wasipotupa chakula, basi wanabaki wanasubiri tu mngurumo wa magari, hawawezi kutafuta chakula, kwa hiyo wanakufa. Kwa hiyo, mtoe maelekezo ya kuzuia tabia kama hii ya kuwatupia chakula wanyama isiendelee.

Lingine la mwisho ambalo nilitaka niliseme kwa Wizara hii, napendekeza kwamba katika suala la kukuza utalii, Wizara ifikirie mara mbili. Niliwahi kutoa kwa maandishi, hivi kwa nini nchi hii hatuna mahali pa kuzika *heroes.* Lakini Watanzania tumepoteza damu zetu na miili ya Askari wetu katika nchi nyingi. *South Africa,* Zimbabwe, Msumbiji, Comoro, Guinea Bissau, kote huko. Lakini hakuna mnara hata mmoja wa kumbukumbu unaoonyesha kama hapa ndipo *heroes* wa Tanzania waliofia nchi mbalimbali.

Tukiweka kitu cha namna hiyo kitaleta maana kwetu na sisi ndiyo tulikuwa nchi ya *liberation* ya kwanza katika Afrika. Tutawavutia watalii vile vile. Tubuni vitu! Maajabu yote saba ya dunia yameumbwa na binadamu. Kwa hiyo, tu-*create* vitu, tusitegemee mbuga tu. Kama huna mbuga *create* vitu vingine kama vile *pyramids,* ule Ukuta wa Mkuu wa Uchina na mambo mengine. *(Makofi)*

Mwisho, napenda kushukuru jitihada za Wizara za kuhimiza watu kupanda miti. Katika ukurasa wa 50, nashangaa hata wasukuma sasa wameanza kuelewa thamani ya miti. Kwa kweli nimepata faraja kubwa sana. Mwaka ule uliopita ilikuwa ni 10,000 sasa wamefikia 12,000, wanakaribiana na Iringa. Tabia hii nadhani ni muhimu. *(Kicheko/Makofi)*

Lingine nimpongeze vile vile Waziri kwa kuamua kufanya Tamasha la Utamaduni wa Wabena na Wakerewe katika Tanzania, ukurasa wa 14. Tabia hiyo ya Mheshimiwa Zakia Meghji ni tabia nzuri kwa sababu Taifa lisilo na utamaduni wake ni kama kivuli tu. Wabena kwa taarifa yenu ni *Parent Stock* ya makabila ya Nyanda za Juu Kusini na ndio chimbuko la makabila ya Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Spika, nina maandishi hapa yanayothibitisha usemi huu. Kwa msingi huo, hapa ukitaka utamaduni wa Nyanda za Juu Kusini, basi ndio penyewe.

Kwa hiyo, kwa uamuzi huu, unaweza ukaendeleza utamaduni wa nchi hii na kuwahusisha wanaohusika. Mimi niko tayari kushirikiana na Wizara hii ili kukidhi lengo hili la kuanzisha Tamasha la Utamaduni wa makabila katika Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Spika, kwanza natoa shukurani sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Lakini pia nampongeza sana Waziri, Mheshimiwa Zakia Meghji, kwa umahiri wake katika kazi zake za uwaziri. Anajitahidi sana na anastahili kabisa kupigiwa makofi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nampongeza Katibu Mkuu, Makamishna , Wakurugenzi na Wasaidizi wake wote waliofanikisha kujenga hii hoja mpaka ikapendeza na ikawa nzuri na ikawa inasifiwa. Tunawapongeza sana. Bila ajizi, naunga mkono hoja hii ili niweze kutoa michango yangu vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nataka nichangie eneo la mambo ya Kale. Kama unavyofahamu kihistoria kule Kondoa Irangi, hiyo michoro ni mingi sana. Nataka niikumbushe Serikali kwa sababu naona inasahaulika sana ile michoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule Kondoa kuna mapango zaidi ya 30 yenye michoro ambayo ni urithi wa dunia. Lakini katika michoro hiyo, mapango hayo kama 15 hivi ndio yanatambulika. Lakini zaidi ya 15 hayatambuliki kwa sababu hayana mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, hakuna mtu anayefanya utundu wa kufuatilia na kuyapata yote kwa ujumla. Yakifuatiliwa yatapatikana mengi kabisa yatasaidia sana kuwepo katika urithi wa dunia. Kwa hiyo, namwomba sana Waziri hilo alifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine katika hilo ni kwamba mara baada ya Uhuru mapango yale yalihifadhiwa vizuri sana, yalijengewa *fence,* waliokuwa wanakwenda pale, wanafunguliwa milango ndio wanakwenda wanaangalia na kadhalika. Lakini sasa hivi *fence* zile hazipo na yale mapango yanatishia kupoteza thamani yake na baadaye yatakwisha kabisa na tutapoteza historia.

Kwa hiyo, naomba kabisa mapango yale yahifadhiwe, yajengewe *fence* na yawe na ulinzi ili yawe yanakwenda kuangaliwa kwa nidhamu na utaratibu unaoeleweka. Tusiyaache hivi hivi tu kama hayana mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, zamani yalikuwa chini ya Wizara ya Elimu na Utamaduni, lakini sasa yamehamia katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii na nina uhakika yatahifadhiwa vizuri ili iwe ni kumbukumbu na urithi wa dunia ya sasa na dunia inayokuja.

Mheshimiwa Spika, katika mapango maarufu kabisa kule Kondoa yako mengi lakini ninayoyajua ni yafuatayo, ambayo yako katika hatari ya kutoweka ili Waziri aweze kuweka msimamo na ayatilie maanani, ayafuatilie ili yaweze kuwekwa katika hali ya Ulinzi vizuri. Kolo ambapo kuna Ofisi ile ya Mambo ya Kale, yapo mapango zaidi ya manne.

Kwa hiyo, lazima yafuatiliwe ili yawekwe katika hali nzuri zaidi. Kuna sehemu moja inaitwa Pahi, yako zaidi ya matatu, nayo lazima yafuatiliwe na yahifadhiwe zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuna sehemu moja inaitwa Kesese, yapo yasiyopungua mawili. Itororo yapo yasiyopungua matatu, Kandaga yapo yasiyopungua mawili, Cheke yapo yasiyopungua mawili na vile vile Changaa yapo yasiyopungua mawili na mengine mengi yale ambayo hayatambuliki, yafuatiliwe ili tuweze kuweka kumbukumbu zetu na watalaii wanakuja, lakini kwa sababu wanakuta mambo hovyo hovyo, wamepungua sana katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, baada ya Uhuru tu watalii walikuwa wanafika sana kutembelea mapango yale, kwa sababu yalihifadhiwa vizuri. Lakini sasa yameachwa tu hivi hivi, wakija wanaona kama kitu ambacho sisi hatukijali.

Mheshimiwa Spika, nisisitize yafuatayo kwa Serikali katika hayo, katika hifadhi hiyo ya Michoro ya Mapango ya Kondoa Irangi, hata katika historia na mambo mengine yanatajwa.

Naomba Serikali itambue na kujali mapango hayo yenye urithi wa dunia ili yahifadhiwe vizuri, yatambulike, yahifadhiwe kwa ajili ya historia yetu ya baadaye. Lakini pia yajengewe *fence* yarudishiwe kama zamani. Kwa sababu tumewahi kufanya hivyo. Sasa sijui ni kwa nini tumelegea tukaacha tu hivi. Lakini sina shaka na Mheshimiwa Zakia Meghji, kwa sababu ana umahiri huo wa shughuli mbalimbali, atafuatilia na ataona kwamba inakuwa katika hali iliyo bora zaidi na iliyo nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile tuongeze walinzi. Kuna walinzi wawili tu katika Ofisi ile ya Mambo ya Kale pale Kondoa na mapango ni mengi na ndiyo maana huku kuna kunatokea uharibifu katika mapambo mengine kwa sababu hakuna ulinzi wala wananchi hawajashirikishwa waweze kujua vizuri zaidi kwamba yale mambo ni yao. Kwa hiyo, tunaomba kazi hiyo Mheshimiwa Waziri ashirikiane na wadau mbalimbali ili tuweze kuyaimarisha hayo na kuyakuweka katika hali nzuri.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile tuimarishe Ofisi ya Mambo ya Kale iliyopo pale Kondoa ambapo ndiyo kituo, watalii wanafika pale na wananchi wengine wanaokwenda pale kwanza wanaripoti pale. Sasa Ofisi yao haijakarabatiwa siku nyingi imekaa ovyo ovyo mpaka uulizie ni wapi, ndiyo uweze kujua. Tunataka Ofisi ya Mambo ya Kale ionekane hata kwa mbali na ni kilomita 24 tu kutoka Kondoa Mjini.

Pia nilikuwa naishauri Serikali ingejenga kambi katika maeneo yale ambako kuna hii michoro kwenye hizi kumbukumbu ili wanaotembelea waweze kuwa na sehemu ya kufikia, kule kabisa karibu na michoro yenyewe. Hiyo itasaidia sana, itavuta watu wengi na tutaingiza fedha za kutosha.

Nakuomba Mheshimiwa Waziri ufike ukajionee mwenyewe. Ukifika ukajionee mwenyewe, utavutika. Yako mambo mengine huyajui wewe lakini ukiyaona lazima utajichochea kuyafanyia kazi. Kwa hiyo, naomba ufike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naomba nizungumzie eneo la uhusiano baina ya *TANAPA* na vijiji jirani na hifadhi hiyo. Vijiji vinavyopakana na hifadhi ya Tarangire kule *TANAPA* kule Kondoa Kaskazini vipo kama 13. Kuna Kijiji cha Chubi, Kisaki, siyo Omar Chubi Mheshimiwa hapa, ni kijiji cha kule. Lakini na yeye Chubi, anafahamu kwa sababu aliwahi kufika. Anakijua kijiji hicho.

Pili, Kijiji cha Kisaki, tatu, kuna kijiji cha Ata, kuna kijiji cha Keikei, kuna kijiji cha Ikaswi, kuna kijiji Hurui, kuna kijiji cha Isongolo, kuna kijiji cha Idindiri, kuna kijiji cha Kerere Chang'ombe, kuna kijiji cha Mauno. Kuna kijiji cha Madisa, kuna Ikengwa na kwa Kwadelo. *(Makofi)*

Hivi vijiji vyote vinapakana na vinashirikiana sana askari wa hifadhi kulinda wanyama na wanajitahidi sana. Wakati fulani wanyama wanavuka mipaka, lakini wanarudishwa tu bila kuuwawa. Kwa hiyo, wananchi ni wazuri sana hawa wanatakiwa kubembelezwa na kusaidiwa sana katika mambo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kimsingi uhusiano ni nzuri sana. Wananchi na jamii nzima wanashiriki, wanalinda wanyamapori kama nilivyoeleza vizuri kabisa wanapambana na majangili wanaojitokeza vizuri kabisa, wananchi wapo mstari wa mbele na wanawarudisha wanayama wanaovuka vizuri tu kwa upole bila matatizo yoyote na pia wanashirikiana vizuri sana na walinzi bila ugomvi, bila matatizo yoyote na vile vile sasa hivi wananchi wanaanza kutambua kwamba ile ni mali yao na ni mali ya nchi siyo mali ya mtu binafsi au siyo mali ya hifadhi peke yake. Ni mali ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, lakini wamenituma mambo yafuatayo ili kuimarisha uhusiano na kujaribu kwenda pamoja na hao wadau ambao ni wananchi ili na wao wajisikie wajitume vizuri zaidi. Baadhi ya

vijiji hivyo huunganishwa na Kata yao na Tarafa yao na Wilaya yao kwa barabara moja tu. Waziri anaijua, sasa nataka nimkumbushe kidogo ili kuitilia mkazo ndani ya Bunge hili Tukufu. Ni barabara inayoitwa kutoka Kijiji cha Chubi ambacho ndiyo kipo kabisa inapakana na hifadhi hii ya Tarangire, Itaswi, Kisaki. Kama kilomita 14 hivi. Kijiji cha Chubi ndicho ambacho kipo mpakani kabisa na ndiyo wanashirikiana na watu wa hifadhi katika ulinzi wa kila siku katika mbuga hii ya wanyama.

Mheshimiwa Spika, mvua zikinyesha vijiji hivi sasa vinatengwa kwa miezi sita, miezi saba, miezi minane hawapati huduma na kadhalika na mwaka 1999, 2000, 2001, 2002, *TANAPA* iliwahi kuahidi kuchangia ili kuweza kuchangia waweze kushirikiana na Halmashauri kujenga hiyo barabara. Lakini bahati mbaya kwa sababu kulitokea matatizo kule *TANAPA* miaka hii yote *TANAPA* hawakushiriki kuikamilisha hiyo barabara. Lakini sasa tunaihitaji kwa sababu mambo ya *TANAPA* sasa yamenyooka Halmashauri ipo tayari na nina uhakika *TANAPA* wapo tayari. Wao wenyewe wamesema wanaweza wakaikwangua ile barabara kwa greda katika kilomita zote hizo 14.

Mheshimiwa Spika, lakini liko tatizo la msingi ambalo ndiyo tunatakiwa tushirikiane tulitatue. Tukishalitatua hilo hakuna matatizo. Ni kwamba kuna kipande cha barabara ambacho kinapita kwenye mbuga cha kilomita 3 mpaka 4 hivi, mvua ziminyesha hapo ndiyo kivumbi, magari hayapiti. Sasa katika kipande hicho kunahitaji *bulldozer* la kuinua tuta, kumwaga *moram* na kuweza kujenga makalvati. Tukifanya tu hivyo, hata maeneo mengine bila kuchonga barabara itapitika wakati wote.

Mheshimiwa Spika, sasa gharama ni kubwa lakini kwa *TANAPA* si kubwa kama wananchi wanaweza wakashiriki usiku na mchana kulinda wanyama wale sasa wale watashindwaje kusaidia tu kilomita hizo chache kumwaga moram na kufanya wananchi wale wapite. Wapate huduma katika upande kwenye Kata, Tarafa na Wilaya. Hii ni lazima na *TANAPA* nao wajue.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, awakomboe wananchi wale lakini pia namwomba Mheshimiwa Mzee Lusinde, Mwenyekiti wa Bodi namwona yupo pale. Namwomba sana washirikiane na Mkurugenzi wake watatue tatizo hilo. Wakitatua tatizo hili wananchi watapenda sana kwa kweli. Watajitahidi sana kuendelea kumiza na kulinda wanyama hawa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, baada ya hapo Mheshimiwa Spika, nina uhakika Mheshimiwa Waziri atatilia mkazo na wale wanaomsaidia watatilia mkazo. Lakini pia wananchi wanamwomba, amewahi kuahidi mara mbili hivi hajafika, na safari hii aliniambia huenda nafikiri ikiisha basi twende ili tukaone hiyo hali. Ukishaiona tu utaridhika mwenyewe. Utasema hawa kweli wanastahili kusaidiwa. *(Makofi)*

Baada ya hapo nashukuru sana. Naiunga mkono kabisa hoja hii ipite bila matatizo ili tuweze kuchapa kazi katika kipindi hiki cha 2003/2004. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba radhi kidogo nilikuwa naendelea kufanya maandalizi mazito kidogo kabla sijaja hapa. Naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, lakini ya pili nitamke mapema kwamba kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Ulanga hasa kabisa Jimbo langu la Ulanga Mashariki, napenda kutamka kwamba naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wilaya yetu ya Ulanga ni Wilaya ambayo tuko Wabunge wawili na mwenzangu *Comrade* Dr. Juma Ngasongwa, haya matamshi ninayatoa kwa niaba yake, kwamba tunaunga mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa jinsi alivyoweza kujieleza vizuri kwenye hotuba yake. Nimefurahi kwa sababu yako mambo fulani ambayo napenda niyaseme nayo ni kwamba hotuba hii imeandaliwa vizuri nina hakika kwa uzoefu wake yeye pamoja na wataalam wake ndiyo sababu mambo mengi katika Wizara hii yamekwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwetu sisi wa Wilaya ya Ulanga, ningependa kwanza kushukuru kwa kazi moja nzuri ambayo imefanywa na Wizara hii. Wananchi wa Wilaya hasa katika Jimbo la Ulanga Mashariki tumepata bahati ya kupata mradi wa kutengeneza barabara ya kisasa ambayo inapitika wakati wa masika na wakati wa kiangazi, tumepata mkopo kutoka *ADB* sasa hivi ninavyozungumza barabara inatengenezwa kutoka Mahenge kwenda Isongo kwenda Kijiji cha Zelezi, kwenda Chirombola, kwenda Mwaya, kuelekea mbuga ambako kwenye mbuga ya *Selous*.

Kazi ni nzuri na kwa niaba ya wananchi, nasema tena kwamba Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana kwa jinsi ulivyokuwa karibu na wananchi wa Wilaya ya Ulanga hasa Vijiji vilivyokuwa kando kando ya *Selous*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina jambo moja nalo ni kwamba kwa kipindi nadhani kilichopita tulikuwa na Semina, tulikuwa na warsha kama 9 zimefanywa na Idara ya wanyamapori. Ningependa kwa dhati kabisa kumpongeza sana sana Ndugu Severe ambaye ndiyo Mkurugenzi wa Wanyamapori katika nchi yetu. *(Makofi)*

Nasema kwa dhati kabisa zile semina zimetusaidia sana, zimetupa nafasi ya kujua nini maana ya wanyamapori na nini kinatakiwa kurekebisha zile Sheria. Tumeshiriki pale Dar es Salaam na maeneo mengine. Kwa kweli tumepata upeo na sasa hivi hata nikisimama hadharani kuzungumzia nini maana ya wanyamapori, kwa kweli nitazungumza vizuri zaidi na yote ni elimu ambayo tumeipata kutoka kwenye semina ile. Ndugu Severe, kwa kweli nakushukuru sana. Nakupongeza na nakuomba uendelee vizuri katika Idara hii ya Wanyamapori. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo langu liko ukurasa wa 29. Ukurasa wa 29, Wizara imezungumzia habari ya mapato waliyopata kwa kipindi cha mwaka huu hasa kabisa 2002 mpaka 2003 na hadi Mei 2003, wamekusanya kutoka uwindaji shilingi bilioni 7.8. Kazi ile ni nzuri, inapendeza sana. Ni dhahiri kwamba tutaendelea kupata mapato vizuri kwa kupitia wawindaji hao. Lakini tatizo langu ni kwamba Kampuni za Uwindaji ambazo katika ukurasa huu wa 29 imesema pale kwamba zipo Kampuni 40 za uwindaji hapa nchini. Kampuni hizo zinafanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini lipo tatizo ambalo nadhani ni vizuri kama haya nitayasema yatakwenda sambamba na maelezo yaliyoko ukurasa wa 27 inayozungumzia kurekebisha Sheria. Sasa hivi wawindaji wote wanaopewa maeneo ya kuwinda katika nchi yetu, wawindaji hao hawapitii maombi yao kwenye kijiji chochote. Wanaomba moja kwa moja kwenye Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu hivi sasa, nchi yetu imegawanyika kwenye vijiji na vijiji vyetu vinakuwa na hati. Nchi yetu imewanyika kwenye Kata na nchi yetu imegawika kwenye umbile la utawala kiwilaya, kimkoa na Taifa. Wawindaji hawa ambao wamepewa nafasi ya kwenda kuwinda maeneo mbalimbali. Sheria zetu haziwaambii kabisa kwamba wanaomba kupitia kijiji chochote, wao wanaomba moja kwa moja Wizarani, matokeo yake kuna mgongano. Kuna mgongano kati ya wananchi ambao wanapenda kujua. Wanapenda kujua maeneo ya vijiji kujua hawa wanakuja kuwinda kwa naufaa yetu. Lakini mbona hatuelewi.

Mheshimiwa Spika, yametokea haya kule kwangu. Kule Mahenge mwindaji mmoja amekwenda kwa nia nzuri kabisa kupita maeneo ya vijiji, Kata ya Lukambe, amekwenda Kijiji cha Gombe, amekwenda Kata ya Mbuga, amekwenda Kijiji cha Iputi, ametembelea Vijiji na viongozi wake, Makao Makuu ya Tarafa wamezungumza na kuonekana kwamba yeye kweli ni mtu ambaye alikuja kuwasaidia na alikuwa tayari kuwasaidia katika miradi ya kujenga *dispensary* kuwaletea mashine ya kusaga, kuwasaidia wanyama waharibifu na ameandaa makontena mawili kuleta madawa kusaidia vijijini.

Mheshimiwa Spika, maombi yake yamekwenda Wizarani hayakuzungumzwa, akapewa mtu mwingine. Napenda kusema kwamba huyu aliyepewa kule ana haki zote. Nazungumzia utaratibu kwa nini mwombaji atoke moja kwa moja alipo na Kampuni yake na anaomba eneo ambalo wako wana vijiji. Matokeo yake nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri si jambo la kawaida lakini nadhani ndiyo maana nasema ipo haja ya kulitazama Sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, yule mwindaji alipokwenda hivi karibuni wananchi wa Lukande, Gombe, Mbuga, Iputi wanamwuliza, mwenzetu umetoka wapi? Anasema nimetoka Arusha. Arusha maana yake nini? Sisi hapa ni wananchi wa Tarafa ya Mwaya, umekuja kwa ajili ya uwindaji. Inawezekane kutoka Arusha mpaka Mbuga, mpaka Ikuti? *Off course* ni nchi yetu, haina matatizo, lakini wananchi wale walikuwa wanapata matatizo ya huyu kaomba kupitia wapi? Wakati vijiji vyao havina habari.

Mheshimiwa Spika, nasema mwaka jana katika Bunge hili hili tumeondoa Sheria ya kulipa ada unapoingia kwenye *gate* la hospitali. Sisi hapa ni watungani wa Sheria na tuliona Sheria ina matatizo tunaiondoa. Mheshimiwa Waziri, nafasi yako katika Chama Cha Mapinduzi, Mama Meghji ni Mjumbe wa *Central Committee. (Makofi)*

Ni mwenzetu, huyu ni Mjumbe wa Kamati Kuu, ni mtu mzito. Si mtu ambaye naweza kusema ya kwamba wanaomsaidia wasirekebishe. Warekebisho hiyo Sheria ili wote wanaoomba uwindaji wapitie kwenye ngazi za Wilaya, wapitie kwenye Kata, wawe ni sehemu ya wananchi. Kwa mfano, hivi sasa tumeondoa kodi ya mapato. Wananchi hawa wanategemea hawa wawindaji angalau washiriki kwenye miradi yao huko kijijini.

Mheshimiwa Spika, lakini wanakuja moja kwa moja. Kwa hiyo, ninachokisema ni kwamba hakuna mwenye tatizo isipokuwa naomba wakati tunafanya marekebisho ya Sheria eneo hilo lifanyiwe marekebisho, ili wote washirikishwe hasa vijiji. Haijapata kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nasema, vipi unapokea maombi ya mwindaji huku juu wakati wenzako kule chini hawamwelewi.

Kwa hiyo, nasema sitaki kuilaumu Serikali, Serikali ni ya kwangu. Mimi ni Kada wa Chama, ninachosema ni kwamba yatakapokuja marekebisho ya Sheria tubadilishe Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, naona kuna kengele inalia. La mwisho katika maelezo yangu ni juu ya kule Mahenge ipo barabara ambayo wananchi wanaitumia, kutoka kijiji cha Chikuti, unapita kando kando ya mlima Ndololo unafika mpaka Lukande. Njia ile ni njia ambayo wananchi wanaitumia lakini iko kabisa ndani ya msitu, msitu wa *Selous.*

Sasa nimejaribu sana kuzungumza na rafiki yangu mmoja anaitwa Kibonde, anakuwa mgumu sana kuelewa. Lakini ninachosema ni kwamba hayo maendeleo ya watu wakati mwingine si lazima yaende wakati unaotakiwa. Lakini ionekane kwenye mpango ile barabara ni nzuri, wananchi wanaipenda sana na wanaizungumzia sana na endapo Wizara hii itaanza kushughulikia barabara ya kutoka Chikuti kwenda Lukande nina hakika na Waziri wa Ujenzi na yeye atachukua nafasi yake kusaidia.

Kwa hiyo, nadhani ni suala la kuanza tu na wakianza Wizara ya Maliasili na Utalii, nina hakika na Wizara yetu ya Ujenzi watakuwa tayari kutusaidia, kwa sababu ile barabara ni nzuri inafanya usiende Mahenge inakufanya uende kwenye mbuga za wanyama bila kupitia Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nasema tena kwamba ninafahamu uwezo mzuri wa Mheshimiwa Waziri, nafahamu sana kwa sababu nina habari kwamba hata wakati fulani Mama Zakia Meghji, alikwenda kwenye mkutano akakaribishwa kwenye Mkutano vizuri, wakati anamaliza mkutano ule basi wale waliomwita wakaamua kwamba watafuta *bill* yote, alikataa, kwamba mimi ni Waziri, nimekuja kwenye kikao na gharama ya usafiri, malazi, chakula ni gharama za Serikali yangu.

Kwa hiyo, nasema nazungumzia Wizara ambayo naijua. Naijua kwamba ina mtu mwenye uwezo mzuri sana. Naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MATHEW T. OLE-TIMAN:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Aidha, nichukue nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Zakia Meghji kwa kazi nzuri anayofanya yeye pamoja na timu nzima au safu yake nzima ya wataalam. Nampongeza sana. *(Makofi)*

Kwa sababu hotuba nimeisoma, nimeipitia nikaafiki kwamba ni nzuri, siwezi kupata kigugumizi cha aina yoyote kusema kwamba naiunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

Baada ya hayo, kama utangulizi tu, niseme kama rafiki zangu na jirani zangu Wakurya pamoja na Wasukuma kwa maneno ya Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, wanakubali kwamba wanyama sio wa kuliwa tu bali ni wa kuhifadhiwa. Sasa nina hakika tutafanikiwa na shughuli za uhifadhi, na vile vile watapunguza harakati za kuiba mifugo kwa kupitia maeneo hayo yaliyohifadhiwa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naomba kuchangia maeneo mawili katika hoja ya Mheshimiwa Waziri. Eneo la kwanza ni eneo la uwindaji wa wanyamapori. Nafikiri mwezi uliopita tulisoma kwenye magazeti kwamba kuna vijana 300 wa Kimasai wameenda kuzuia ndege ya Mwarabu kutua uwanjani Loliondo. Imeandikwa hivyo kwenye magazeti na mimi kwa kupitia Bunge lako Tukufu naomba niseme kwamba vijana hawa wa Kimasai hawakwenda pale kwa madhumuni ya kuikataa au kukataa hiyo ndege kutua bali walienda pale kutafuta ajira. Walienda pale kutafuta ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kwamba vijana walioenda pale kwa lengo na madhumuni ya kutafuta ajira *FFU* waliwapokea kuwatandika viboko na kuwafukuza pale. Mimi nafikiri ni aibu na inasikitisha. *FFU* ni askari wa Kitanzania, Watanzania na sidhani kama ni jambo jema wao kutumika kulinda mali ya mtu mmoja. Mali ya mtu binafsi hata wakati ambapo mfalme wa wafalme hawapo. Nafikiri hilo halikuwa jambo jema na ninatumaini halitaendelea. Kosa la hao vijana ni kutafuta ajira na mimi nasema kwa niaba yangu na kwa niaba yao kwamba wana haki ya kupata hiyo ajira kwa sababu au kutokana na sababu zifuatazo.

Moja, wanyama hao wanaowindwa ni mali ya Serikali ya Tanzania na wao ni Watanzania. Pili, eneo la uwindaji ni eneo la ardhi ya kijiji au ardhi ya vijiji, vijiji vya Arashi, Oluipiri, Olorieni, Maaloni, Sottsambu na Ololosokwai. Kwa hiyo, vijana kutoka vijiji hivyo wana haki ya kupata ajira. *(Makofi)*

Tatu, kwa sehemu kubwa wananchi hao wameshiriki na wanaendelea kushiriki katika jitihada za uihifadhi wa wanyamapori hivyo wana haki ya kupata ajira. *(Makofi)*

Nne, wanyamapori kwa sehemu kubwa wanasababisha madhara kwa mifugo kwa watu na kwa mashamba kupata ajira walau ni namna moja ya wananchi hao kufaidi kutokana na wanyama hao. Kwa hiyo, hao vijana walikuwa na haki ya kwenda kule kutafuta hiyo ajira na narudia ni masikitiko makubwa kwamba vijana, maaskari wetu wa *FFU* walitumika kuwapiga viboko na kuwafukuza hao vijana ambao kosa lao tu ni kutafuta ajira. Naomba hili Wizara isilifumbie macho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba na namshauri Mheshimiwa Waziri kama inawezekana kutoa tamko kwa wawindaji wote kutoa kipaumbele kwa suala la ajira kwa vijana wanaotoka maeneo yale au yanayozunguka maeneo ya uwindaji. Vingenevyo tutaendelea na tatizo hili la kufukuzana na kupigwa viboko ambalo ni jambo lisilofaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo napenda kulichangia ni eneo la Sheria za Hifadhi ya Mamlaka ya Ngorongoro. Eneo la Ngorongoro ni eneo la Hifadhi ya Wanyamapori pia ni eneo la maskani ya watu. Kuna zaidi ya wananchi 52 wanaoishi katika eneo lile na hao wananchi kwa bahati mbaya na kwa sehemu kubwa wanatawaliwa na Sheria za Wanyamapori. Hawapo pale kama wavamizi, wako pale kwa mujibu wa sheria lakini sheria zinazotawala eneo lile kwa sehemu kubwa ni sheria za uhifadhi ni sheria za wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa mifano michache ambavyo sheria hizo kwa sehemu kubwa inampa mamlaka makuu au mamlaka makubwa muhifadhi mkuu. Kwa mfano, mhifadhi mkuu ana nguvu, ana uwezo wa kutunga sheria ndani ya eneo lile. Pili mhifadhi mkuu ana nguvu, ana uwezo wa kuadhibu yeyote yule anayevunja sheria katika eneo lile.

Mheshimiwa Spika, tatu, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, ana nguvu na ana uwezo wa kutekeleza sheria hizo. Kwa maneno mengine sheria jinsi zilivyo zinampa mhifadhi mkuu nguvu kama za kibunge kwa maana ya kutunga sheria, nguvu za Kiserikali maana ya kutekeleza sheria hizo. Na nguvu za

kimahakama, *the Legislative Powers, Executive Powers* na *Judicial Powers.* Siyo mara yangu ya kwanza kuzungumza mambo haya katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, mimi ninachosema ni kwamba kuna uwezekano wa nguvu hizo au mamlaka ya namna hiyo kutumika vibaya. Sisemi kwamba mhifadhi wa sasa Bwana Chausi anatumia vibaya, hapana! Bali kuna uwezekano wa nguvu hizo nyingi namna hiyo, kutumika vibaya.

Kwa hiyo, napendekeza namwomba Mheshimiwa Waziri kwamba wakati umefika wa kupitia sheria hizo kwa upya kuzibadilisha ili nao hawa wananchi walioko pale nao wapate haki zao za kidemokrasia kwa sababu tukiangalia nyakati tulizopo ni wakati wa kupanuka kwa demokrasia na utawala wa Sheria. Ili na wao waweze kufaidi kikamilifu na kushiriki kikamilifu katika harakati za demokrasia na kupanuka kwa utawala wa Sheria.

Nafikiri kuna ulazima wa kubadilisha Sheria hizi. Nafahamu kuna mjadala ambao umeanza wa kubadilisha Sheria hizi lakini naomba mfanye haraka. La muhimu zaidi wananchi wahusika katika eneo lile na wao washirikishwe ili waweze kutoa mawazo, waweze kutoa pendekezo na hatimaye pendekezo hilo lije Bungeni na wote kwa pamoja tulipitishe kwa manufaa ya wananchi hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. EDWARD N. NDEKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Katibu wake Mkuu pamoja na timu ya Maafisa wote, wataalam katika Wizara hii, kwa kufanikisha hoja hii nzuri na kuiwasilisha kwenye Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuipongeza Wizara hii kwa kuwasilisha hotuba hii nzuri mbele yetu, napenda nijielekeze moja kwa moja katika Sekta ya Uvuvi. Baada ya kupitia ukurasa wa 15 mpaka ukurasa wa 22 unaozungumzia Sekta ya Uvuvi, napenda kusema kwa masikitiko kidogo kwamba sekta hii inaonekana haijapewa uzito na kipaumbele inachostahili.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Uvuvi ya mwaka 1997 imeainisha vyanzo mbalimbali vya uvunaji wa raslimali hizi katika Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria na Ukanda wa Pwani kwa Bahari ya Hindi. Jumla ya tani zilizoonyeshwa zinazoweza kuvuliwa katika vyanzo hivi ni tani 730,000. Katika hizi Ziwa Tanganyika lina uwezo wa kuvuna tani 300,000 kila mwaka bila kuharibu chanzo cha raslimali hiyo.

Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanywa na Shirika la Chakula Duniani *(FAO)* kati ya mwaka 1973 na 1976 ulionyesha kwamba Tanzania katika kiasi hicho cha tani 300,000 ina uwezo wa kuvuna tani 122,000 kwa mwaka bila kuharibu chanzo cha raslimali hiyo. Katika kiasi hicho Mkoa wa Kigoma una uwezo wa kuvuna tani 98,000 na kiasi kilichobaki cha tani 24,000 ni Mkoa wa Rukwa kwa sababu ndiyo Mikoa miwili inayopakana na Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ukiangalia uwezo huo wa Mkoa kuweza kuzalisha kiasi cha tani 98,000 na uwekezaji unaofanyika katika sekta hiyo katika Mkoa unakuta ni vitu viwili tofauti. Vyanzo vilivyobaki ambavyo ni Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa na Ukanda wa Pwani, kiasi kinachoweza kuvuliwa kikagawanywa kwa Mikoa inayoshiriki katika uvunaji huo, hakuna Mkoa wenye uwezo au fursa hiyo ya kuweza kuzalisha tani 98,000.

Mheshimiwa Spika, sasa nadhani kwa kuzingatia ukweli huo, Wizara inapaswa kutoa kipaumbele kwa maeneo yale ambayo yana *potential* yana fursa ya kuweza kuzalisha kiasi kikubwa. Ni kwa kufanya hivyo mpango kamambe ambao umeelezwa katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri utakuwa na maana, kwa sababu ukichukua Mikoa ya Ukanda wa Pwani iko Mikoa 10 ambayo ikigawana tani 100,000 za samaki zinazoweza kuvuliwa Ukanda wa Pwani kila mmoja utapata tani 10,000 kila mwaka. Kwa hiyo, mwito wangu hapa ni kwamba katika kukamilisha huo mpango kamambe, ni dhahiri maeneo ambayo yana uwezo wa kuzalisha kiasi kikubwa yakapewa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilifurahishwa na kauli ya Mheshimiwa Waziri mwaka 2002 mwezi Mei, alipotembelea Mkoa wa Kigoma. Katika kuhitimisha ziara yake aliwaambia Maafisa katika Kituo cha Uvuvi kwamba: "Wasaidieni wavuvi si kutafuta Shahada tu" na vyombo vya habari vilimnukuu akitamka hivyo. Hilo lilikuwa ni tamko zuri sana kwa sababu wavuvi wana haja ya kusaidiwa ili waweze kuvuna raslimali ambazo ziko katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wavuvi watafaidika kama hizo tafiti zinazofanyika zitawafikia. Katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri ameonyesha katika ukurasa wa 20 kwamba katika utekelezaji mwaka 2002/2003 kiasi cha wavuvi 132 wadogo wadogo walipewa mafunzo kuhusu uvuvi endelevu na wavuvi hao ni wa kutoka Mikoa ya Lindi, Mtwara, Kigoma, Rukwa na Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, idadi ya wavuvi 132 ni kiasi kidogo sana hasa wanapotawanyika katika Mikoa hiyo iliyoonyeshwa. Mkoani Kigoma wavuvi wadogo wadogo wanakadiriwa kuwa kati ya 6,000 na 10,000. Sasa kama kiwango cha kutoa elimu ni hicho basi itakuwa ni kazi ngumu sana kuwawezesha hao wavuvi kuweza kupata elimu wanayoihitaji kwa ajili ya kuiendeleza sekta hii ya uvuvi. Kwa hiyo, wito wangu ni kwamba Wizara na Serikali kwa ujumla iwekeze zaidi katika kutoa elimu kwa wavuvi wadogo wadogo katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo wavuvi wanalihitaji, ni katika kuboresha zana za uvuvi. Wavuvi wadogo wadogo hasa katika Mkoa wa Kigoma na Mheshimiwa Waziri alibainisha katika ziara yake kwamba bado wanatumia zana duni za uvuvi na hususan Karabai. Sasa ni vema kuanzia hapo katika jitihada za kuwasaidia wavuvi kwa upande wa zana muhimu. Katika hotuba hakuna mahali ambapo misaada kwa wavuvi wadogo wadogo imetajwa hususan katika vikundi vyao ambamo wangeweza kusaidiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho wavuvi wanahitaji ni sera bayana zinazohusu zana wanazozitumia. Kumekuwa na tatizo kuhusu aina ya nyavu wanazozitumia. Mfano katika baadhi ya nyavu zinaruhusiwa za macho ya inchi nane wakati maeneo mengine jirani nyavu za *size* hiyo zinakatazwa na kuagiza zitumike za inchi kumi. Sasa nadhani Wizara na Idara ya Uvuvi zingefanya utafiti zaidi ili kuangalia hizo nyavu ambazo wanazikataza katika maeneo fulani kwa ajili ya aina fulani ya samaki kwa mfano, dagaa. Dagaa wana kimo na ukubwa usioongezeka baada ya kupevuka kwa hiyo nyavu ambazo zinastahili katika maeneo hayo zinaweza kuwa ni hizo zinazokatazwa kwa ajili ya uvunaji wa raslimali za aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, wavuvi kadhaa katika Mwambao wa Ziwa Tanganyika hususan katika Jimbo langu la Kigoma Kusini, wamelazimika wengi kukimbia kutoka kule kwa sababu ya uvamizi ambao umefanywa mara kwa mara na majambazi na kulazimika kwenda Mwanza katika Ziwa Victoria. Sasa huko nako wanapambana na Maafisa wa Maliasili na kufanyakazi inakuwa ngumu sana. Kwa hiyo, nadhani wanapaswa wasaidiwe katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani pia ni vizuri kwa sababu hotuba ya Mheshimiwa Waziri inaonyesha mwelekeo wa mabadiliko, mwekeleo huo uwe katika kuwasaidia wavuvi hawa kutoka katika matumizi ya zana duni na kwenda katika zana za kisasa zaidi. Hayo yataandamana na utafiti kuwafikia na kuwezeshwa pia katika vikundi vyao katika suala la zana wanazozihitaji kwa kuvulia samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba nikiri kabisa kwamba hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii naiunga mkono kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika Wizara iliyo mbele yetu, Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, mimi kwanza niseme kwamba naunga mkono hoja ya Wizara na Bajeti yake kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye ufasaha na malengo mazuri katika dira nzima ya mwekeleo wa kusimamia uchumi wa nchi hii na kuweza kutekelezwa mambo mengi ambayo yatasaidia kuwaendeleza wananchi wetu kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, labda kwa utangulizi niseme kwamba ingekuwa Mheshimiwa Rais leo aseme kwamba ninaiteua Wizara ya Maliasili na Utalii peke yake ili iweze kuchangia Pato la Taifa hili na kuchangia Bajeti ya nchi nzima kama Wizara peke yake, tukafunga migodi yote na Wizara nyingine zote zinazoleta uchumi katika nchi hii, mimi naamini kwamba Wizara yako Mheshimiwa Waziri ni kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii inaweza kubeba mzigo huu peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni Wizara ambayo ni *very potential,* ina mambo mengi ambayo yanatosheleza kabisa ukilinganisha na baadhi ya nchi ambazo ni ndogo sana lakini zinaweza kumudu kwa utalii peke yake na kuendesha Bajeti ya nchi nzima, sembuse Wizara hii yenye mambo mengi ya utalii lakini hayo hayafanyiki kwa sababu ya *mismanagement.* Sasa mimi nadhani kutokana na *mismanagement* hii ndiyo maana hatufikii malengo halisi ambayo Wizara inategemewa na nchi hii kwamba ingetufikisha mahala pazuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nisimkatishe tamaa Mheshimiwa Waziri, aendelee kujitahidi na kuiendeleza Wizara hii angalau basi tufike mahala tuone kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii inakidhi haja katika kuchangia Pato kubwa sana la Taifa hili katika Bajeti yetu. Wizara inategemea kukusanya shilingi milioni 855,000,000/=, hii ni *fraction* katika Bajeti yetu ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa napenda niingie katika hoja yenyewe ya Wizara. Kwanza, napenda nizungumzie kuhusu Katiba yetu. Katiba inasema wazi kabisa na ime-*define open areas,* tena ime-*define* kwa ufasaha kabisa kuwa hizi *open areas* ni maeneo kwa ajili ya wananchi wa Tanzania kuwindia.

Sasa Katiba inapoandika katika kitabu hiki cha Katiba, tafsiri yake ni pana sana, bila shaka kuna Sheria mbalimbali zimetungwa kufuatana na maelezo haya ya Katiba lakini ndiyo nasema hayatekelezwi. Kwa kweli tunakuwa hatuwatendei haki wanavijiji ambao wanatakiwa wafaidike na maeneo kama haya. Hapa Katiba inawasema Watanzania bila ya kuwabagua wale wa Vijijini au wale wanaoishi Mjini kwa vile wako katika eneo lile lile kwa hiyo na wale ambao wako *Urban areas* wana haki ya kwenda kuwinda katika maeneo ya Vijiji vyao ambavyo viko karibu nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hii inasababisha kwamba pengine Wizara inaingia katika maeneo haya kuwagawia *professional hunters* wa nje. Hii mimi nahisi tunakwenda kinyume kabisa na Katiba.

Naomba Mheshimiwa Waziri uitazame vizuri ili tuweze kunufaika na maelezo haya na wananchi wanufaike kwa ujumla. Bila shaka wewe unaielewa zaidi na una wataalam ambao wamepitia hilo na utaweza kutuarifu vizuri au kutoa maelezo mazuri ili kuweka wazi na bayana katika masuala haya. Waheshimiwa Wabunge wengi wamelizungumzia suala hili la *open areas* na jinsi gani wanavijiji kwa ujumla wanaweza kufaidika na maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, napenda niongelee sasa hivi suala la Hifadhi ya Saadan. Suala la Hifadhi ya Saadan, niliwahi kulizungumza hapa kwamba ni eneo ambalo tayari limekwishaiva kiutalii.

Mimi napenda niishukuru Wizara yake kwamba imekwishawaleta watu wa *TANAPA* wako kule, wamekwishaanza kujenga *infrastructure* ndogo ndogo, taratibu za kuweza kuifanya Hifadhi ya Saadan kuwa Hifadhi ya Taifa kama kwa upande wetu wa Wilaya na Wilaya ya Bagamoyo nafikiri imekwishatekeleza, tuna matumaini kwamba Serikali kwa haraka sana itaweza kuleta Muswada hapa Bungeni ili tupitishe ili Hifadhi ya Sadani iwe ni Hifadhi ya Taifa. Hii itatusaidia kukuza uchumi kwa mwananchi mmoja mmoja wa Wilaya ya Pangani na Mkoa wa Tanga, Wilaya ya Bagamoyo na Mkoa wa Pwani na Watanzania kwa ujumla na vile vile kwa watalii wanaokuja nchini katika kutembelea hifadhi zetu na mbuga zetu za wanyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba hili eneo limekwishaiva kiuchumi, kuna mambo mengine muhimu ya kuzingatia ili tuweze kukamilisha na kuweza kunufaika kwa asilimia karibu mia moja

na utalii kwa maana ya Taifa kuongeza uchumi. Ndiyo yale niliyosema kwamba Wizara yako *is very potential* katika suala la utalii. Basi tuyatazame haya maeneo ambayo yamekwishaiva. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, suala la barabara. Barabara ni kitu muhimu sana kwa sababu watalii wengine wanataka waje wa-*spend* labda *weekend*, siku tatu au siku nne, kama barabara ni nzuri watakuja kwa programu zao na kuweza kuja katika viwanja vya Kimataifa kwa ndege na kuondoka kama programu zao walivyozipanga, hii itawasaidia kwa upande mmoja.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile barabara hiyo ni *alternative* kiusalama katika nchi yetu. Tuna barabara ya Segera – Chalinze ambapo tuna daraja la Mto Wami na tuna daraja lingine kwa barabara ya kutoka Dar es Salaam kwenda Morogoro, daraja la Mto Ruvu. Mungu apishie mbali tunaweza tukapata matatizo mbalimbali ya *climate*, madaraja haya yakibomoka kwa mfano hatuna *alternative* inabidi sijui tupite wapi. Ukipitia upande wa Handeni utapambana na daraja la Mto Ruvu na pia ukipitia Segera – Chalinze kuna daraja la Mto Wami lakini basi tuwe na *alternative* nyingine kwa kupitisha barabara hii ambayo ni barabara ya kwanza kabisa ya zamani sana kabla ya uhuru. Ndiyo barabara muhimu ambayo ilikuwa inatumika kuunganisha maeneo kama Dar es Salaam na maeneo ya Kusini na kwenda Kaskazini kwa kupitia Bagamoyo – Sadani – Pangani – Tanga na kuendelea na safari.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuna haja ya Wizara yako, Wizara ya Maliasili na Utalii iwe ina uhusiano wa karibu sana na Wizara ya Ujenzi, waweze kupanga mikakati ni jinsi gani watawezesha barabara hizi ziweze kufunguliwa kwa maana ya kuongeza kipato kwa Taifa hili kwa ajili ya kusaidia Bajeti ya nchi hii ili tuondokane na matatizo mbalimbali ambayo tunayo katika nchi hii katika huduma za jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuipa Hifadhi ya Taifa ya Saadan mnao ninyi na sisi ni matumaini yetu tu kwamba muda sio mrefu mtatekeleza hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba bila shaka tukiwa na maeneo kama hayo kuna faida zake na kuna mambo mengine ambayo wananchi watakuwa hawajazoea yataleta usumbufu lakini pole pole itafika wakati yataweza kutatuliwa baada ya wananchi wenyewe kuelewa umuhimu wa kuwa na hifadhi hii ya Taifa. Sasa hivi tuna matatizo ya wanyama waharibifu, sisemi wanyama waharibifu lakini ni wanyama ambao wanaingia katika mashamba ya wananchi kule Pangani kama tembo na kuanza kuvunja minazi na kuharibu mashamba ya wananchi. Lakini kama *TANAPA* itakuwa imeanza kazi rasmi, itaweza kusaidia katika kudhibiti hali hiyo na hatimaye wananchi waweze kufanya shughuli zao kwa usalama na amani kwa maana kwamba na wao pia watakuwa wamekwishapewa mafunzo kama Mheshimiwa Waziri ulivyosema katika hotuba yako, kuweza kuwashirikisha moja kwa moja na wao washiriki katika kulinda hifadhi hizo. *(Makofi)*

Napenda pia nizungumzie suala la uvuvi. Uvuvi ni moja ya vyanzo vya mapato kwa ajili ya kusaidia uchumi wa nchi hii. Bado tunapenda kusisitiza, kuiambia Wizara kwamba wale wavuvi wanaovua katika zile boti zinazojulikana kama *trollers*, wajaribu kufuata taratibu na Sheria zilizowekwa. Wanasogea karibu mno na fukwe za bahari na kutuharibia mazingira ya bahari yetu kwa sababu wanakwenda kwenye kina kifupi na nyavu zao zinavunja miamba ya mazalia ya samaki na hatimaye kuvua samaki ambao wao hawawahitaji na wanakwenda wakati wa usiku. Lakini pamoja na kwamba kuna *patrols boots* bado zinatakiwa ziimarishwe kwa sababu hizikidhi haja kutokana na urefu wa fukwe zetu za bahari. Kuna haja ya kuongeza juhudi za kuweza kuongeza *patrol boat* ili kuweza kudhibiti hizi *trollers* ambazo zinavua.Wananchi wetu wanalalamika, wao ndio wana nafasi ya kuvua katika maeneo haya ya karibu na hao wengine basi waende katika yale maeneo waliyopangiwa ili wasiyaharibu mazingira hayo. Lingine ni suala zima la *polluter fees* kwenye Viwanda vya Samaki kule Mwanza. Mimi nafahamu kwamba sheria hii imetungwa mwaka 1974 lakini kwa taarifa nilizozipata ni kwamba kupitia *discharge permit* hakuna hata moja iliyotolewa. Kwa hiyo, mpaka sasa hivi Ziwa la Victoria linakuwa *polluted*. Kwa maana hiyo, sheria haitekelezwi.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba Mheshimiwa Waziri hili suala alitazame upya ili kutilia mkazo kwa sababu hii *pollution* itakayofanywa katika Ziwa Victoria athari zake zitakuja kuonekana baadaye sana. Hii ndiyo inayosababisha kuongezeka kwa magugu maji katika maeneo haya kwa sababu kuna mambo

mengi yanayotupwa mle mtoni pengine ni *chemicals* nyingine ambazo zina *activate* na yale magugu maji yanapata nguvu, kukua kwa kasi zaidi. Sasa hili linatakiwa litazamwe ili tusiyaharibu mazingira ya Ziwa Victoria kwa sababu Ziwa Victoria linategemewa na karibu nchi nyingi katika Bara letu la Afrika.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na niseme tena kwamba naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mpaka hapo ndiyo tunafikia mwisho wa kikao cha asubuhi.

Kwa kipindi cha mchana watakaochangia ni watano. Kwa kuwa Wizara hii haina Naibu Waziri, kwa hiyo tumeweza kuwapanga Waheshimiwa Wabunge watano badala ya wanne wale wa kawaida. Hao watano ni hawa wafuatao Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Job Ndugai na Mheshimiwa Ireneus Ngwatura. Waliopata nafasi katika hoja hii ni wale waliokwishachangia mara moja na mara mbili. Wapo walioomba lakini wamekwishachangia mara tatu, naona hao hawatapata nafasi kwa utaratibu huo wa kutendeana haki.

Sasa baada ya maelezo hayo nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.56 Mchana Bunge Lilifungwa Mpaka saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11:00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kabisa jioni hii ili niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, wataalam wote wa Wizara kwa hotuba nzuri na yenye kuleta matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalazimika kuunga mkono hotuba hii kwa sababu ina mpango wa kuendeleza Hifadhi ya Akiba Lipalamba. Fedha za kuendeleza hifadhi hiyo iko katika bajeti hii kwa ajili ya ujenzi wa ofisi, ununuzi wa gari na vifaa vingine na kwa ajili ya kumteua na kumgharamia Meneja wa mradi. Kwa hayo yote mazuri inanilazimisha niunge mkono moja kwa moja hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Itakuwa ni ajabu kabisa kwa wananchi wangu wa Wilaya ya Mbinga kama nitaikataa hotuba nzuri kama hii yenye mpango mzuri wa kuendeleza sehemu yetu ya Wilaya ya Mbinga. Naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ingekuwa wakati mwingine ningeachia hapo hapo na kukaa chini lakini itakuwa sio vizuri. Nataka niongelee mambo mawili tu ambayo ni utalii Kusini na uvuvi. Sekta ya utalii imekwama sana Mikoa ya Kusini ya Ruvuma, Mtwara na Lindi. Sekta hii haikuenea kule sio kwa sababu Mikoa hii mitatu haina vivutio vizuri bali ni kutokana na ubovu wa miundo mbinu mfano barabara ni mbovu, umeme hakuna kama upo sio wa uhakika na maji sio ya uhakika. Kutokana na ubovu wa miundo mbinu hii imefanya vivutio vya Kusini vyote visitumike katika sekta hii ya utalii. Kwa sasa naipongeza sana Serikali kwa jumla mipango yake kwa upande wa barabara ya kutoka Dar es Salaam – Mtwara, Mtwara – *Mamba Bay* ina lengo la kuimarisha utalii Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mipango hii yote kukamilika kama vile barabara, umeme na maji vivutio vyote vya Kusini vilivyojaa Lindi, Mtwara na Ruvuma vitatumika kwa ajili ya utalii. Nichukue mfano mmoja tu wa Wilaya ya Mbinga. Mbinga tuna vivutio vingi tu vya utalii tuna jiwe kubwa sana ninavyoamini linaongoza kwa ukubwa Afrika ukiamua kulizunguka unaweza kutumia saa nyingi kama sio siku. Jiwe lile tunaliita mbuji, hii ni sehemu mojawapo ya kivutio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuna Milima ya Matengo ambayo imepambwa na kahawa, miti ya kupanda ni vivutio vya pekee kabisa. Jambo lingine tuna Ziwa Nyasa ambalo lina maji safi, ufukwe mzuri, maji baridi na tuna samaki wa mapambo ambao hawapatikani mahali pengine popote wakipelekwa Ulaya wazima wanauzwa si chini ya dola tano. Kwa hiyo, kama miundo mbinu yote ikikamilika naamini sekta ya utalii Kusini itashamiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ana mpango wa kutengeneza barabara 2150 ili zihudumie hifadhi mbalimbali hapa nchini. Mheshimiwa Waziri nakuomba sana katika kilomita hizi 2150 barabara ya kutoka Mbinga kwenda Hifadhi ya Lipalamba ikawa mojawapo ili barabara hii iimarike ili huyu Meneja atakayeteuliwa kusimamia mradi huu tumpunguzie matatizo. Naomba sana katika barabara zilizofikiriwa kutengenezwa mojawapo iwe barabara ya kutoka Mbinga kwenda katika Hifadhi ya Akiba ya wanyamapori Lipalamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache juu ya utaliinizungumzie sasa uvuvi. Ziwa letu Nyasa kama Mheshimiwa Waziri alivyosema halina samaki. Hii ni wazi kabisa kwa sababu wananchi wa mwambao wa Ziwa Nyasa wanakula dagaa wa kutoka Mwanza kama Ziwa lile lingekuwa na samaki sidhani kama wangekula dagaa wa kutoka Mwanza. Kuna kero moja wavuvi wa Ziwa Nyasa wanatumia zana duni mfano mitumbwi na samaki wenyewe hawapo wanachovua ni kwa ajili ya chakula tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna wataalam wanaitwa watalaam wa samaki hawa wataalam wa samaki sio kwamba wanawasaidia wavuvi ili waweze kuvua zaidi, sio wanawaelimisha wavuvi ili waweze kuboresha maisha yao au shughuli zao za uvuvi, kazi kubwa wanayofanya ni kukimbizana na wenye mitumbwi kwa ajili ya kukatia leseni, ni kukimbizana na wale wachuuzi wanaonunua samaki chini ya shilingi elfu tano ili walipe ushuru kwa kweli ni kero kubwa. Naomba sana Serikali leseni ya mitumbwi pamoja na ushuru ufutwe kwa kuwa ni kero kubwa kwa wananchi. Wananchi wenyewe kipato wanachokipata kwa mwaka mzima hakifiki hata shilingi 50,000 katika kipato hicho ulipie leseni kwa kweli ni kichekesho.

Kwa hiyo, ni vema kero hiyo Serikali ikaiondoa kwa wananchi wanaoishi katika mwambao wa Ziwa Nyasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mito yetu mingi sana inayoingiza maji Ziwa Nyasa zamani ilikuwa na samaki wengi tu lakini karibu miaka minne haina samaki. Watu tunafikiria baada ya kuibuka shughuli ya uchimbaji wa madini Mito ile midogo midogo kwa mfano Mto wa Ruhuu inatumika kwa ajili ya kusafishia madini. Tunavyoelezwa huwa wanatumia *mercury* kwa ajili ya shughuli hiyo na *mercury* ina sumu kwa viumbe vyote vyenye uhai ikiwemo na binadamu. Nafikiria kupungua kwa samaki katika Mito hiyo na Ziwa Nyasa inawezekana ni kutokana na uchafuzi huo. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri ashirikiane na Wizara ya Nishati na Madini ili wafanye uchunguzi juu ya suala hili tusije tukahatarisha maisha ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mto Ruhuu kwa kawaida ulikuwa unachafuka wakati wa masika tu wakati wa kiangazi maji yalikuwa safi lakini siku hizi iwe masika au kiangazi maji yanakuwa machafu sana wakati wote. Naomba sana Wizara hii pamoja na Wizara ya Nishati na Madini wafanye utafiti waone hali halisi inayosababisha kupotea kwa samaki katika Ziwa Nyasa na Mito inayoingiza maji Ziwa Nyasa wakati miaka ya nyuma kulikuwa na samaki wengi inawezekana hilo likachangia, naomba uchunguzi ufanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, sipendi kugongewa kengele ya pili, naunga tena mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyo mbele yetu jioni ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nianzie pale alipoachia Mheshimiwa Simpasa mchana juu ya ukataji hovyo miti kwa ajili ya mkaa na kwa ajili ya uchongaji vinyango kwa mfano mipingo. Sisi watu wa Mtwara hasa vijijini tunaongoza kwa kukata miti kwa kuchoma mkaa na kuchonga vinyango lakini sio kwa makusudi bali ni kwa shida. Wala si ajabu Mtwara ikachukua wiki nzima hakuna dizeli wala mafuta ya taa na wote tunajua kwamba hakuna umeme sasa usiku ndani ya nyumba unatokaje kutembea kwenye *corridor* kwenda kujisaidia wakati una watoto ni lazima upate jiko kubwa la mkaa uweke kwenye *corridor* pale basi kila anayetoka chumbani huchota mkaa kuweka pale moto angalau uwe unatoa mwanga kidogo. Sasa kwa nini tusinunue mkaa kwa wingi, dhiki! Serikali tukieleza habari za umeme wa Mtwara basi taabu sasa tunafanya hivyo kwa shida. Tunaiomba Serikali kusikia kilio chetu hiki ili tuweze kuinusuru misitu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vinyango, tunajua umuhimu wa kuweka kumbukumbu tena basi kwenye maandishi na kurembamba vizuri ujumbe ulio nao lakini ukikaa kwenye *computer,* wachache walio na computer kabla hujamaliza umeme umekatika mpaka mwezi ujao. Sasa nataka niweke kwenye kumbukumbu jambo langu nafanyaje kama sio kuingia porini kukata mti kuchonga kinyango vizuri kuwasilisha nililo nalo? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nimepokea kinyago kizuri vijana walitaka waweke kwenye maandishi safi kumpa Mzee Malecela juu ya ndoa yake Tukufu lakini hawana *computer.* Sasa sijui Mzee Malecela ataniruhusu kuonyesha jinsi walivyowasilisha hisia zao kwenye kinyango badala ya kuweka kwenye maandishi, kwa ruksa yako ukikubali niwaonyeshe…

**WABUNGE FULANI:** Sawa.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Kwa sababu ya shida sio kwa makusudi, amekataa? Aah, amesema nionyeshe. *(Kicheko)*

*(Hapa Mheshimiwa Abdillahi O. Namkulala*
*Alionyesha Kinyago kilichochongwa kutokana na mti)*

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ujumbe huu ulitakiwa uwekwe kwenye maandishi juu ya pingu ya maisha lakini hakuna umeme wakaingia porini kukata miti kuchonga ili kuwasilisha ujumbe wao wa kumtakia Mzee Malecela ndoa yao iwe ya maisha kama walivyofungana mke na mume kwenye kinyago hiki. Mara nyingine tunafanya hivi kwa shida kutokana na kukosekana umeme. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Bunge lako Tukufu naomba kumuarifu Waziri wa Maliasili na Utalii kwamba kijiji changu cha Nalingu kuna mgogoro mkubwa sana. Wiki tatu zilizopita magazeti yalitoa habari kwamba watu wasiopungua 300 wamewekwa ndani, Mwenyekiti wa CCM na *DC* walifukuzwa kijijini kule, watu zaidi ya 2000 wanatishia kurudisha kadi za Chama cha Mapinduzi kwa nini kwa sababu hawataki *Marine Park* na wanamtaka Mbunge wao arudi Jimboni mara moja, nilitii. Nilienda kuzungumza nao nilichogundua pale hawajaelimishwa vya kutosha juu ya *Marine Park.*

Kuna mtu mmoja tu kasema *Marine Park* ikiwepo hapa Mtwara mtu kugusa maji tu risasi au miezi sita watu hawavui, mitumbwi yao itapasuliwa kwa hiyo wakadai kwamba kama mtindo wenyewe ndio huu na *Marine Park* yenyewe hatuitakii. Kwa hiyo, hawakumtaka *DC,* Mwenyekiti wa CCM, hawataki gari ya kupelekewa madawa hakuna walichokuwa wanakitaka isipokuwa Mbunge wao tu awaeleze je, *Marine Park* hii ikiingia hapa haki zao na mipaka yao itakuwaje katika shughuli za uvuvi?

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri kwa kupitia Bunge hili leo aielimishe jamii vilivyo faida na haki zao kama wavuvi juu ya mpango huu wa *Marine Park* . Pia ikiwezekana watusaidie watu kama 20 au 30 waende Mafia wakajifunze kule ilikoanza *Marine Park* . Wanasema kuna watu 18 sijui waliuawa ni kweli Mafia watu waliuwawa? Naomba waende Mafia wakajifunze juu ya mpango huu.

**MBUNGE FULANI:** Si kweli hawajauwawa.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la shamba la mkonge Kabisera yule mwekezaji anataka iwe *zoo* afuge simba na chui pale. Wanakijiji ndio hawataki kabisa wanasema kama mmeshindwa kulima katani turudishieni shamba hili tulime mtama na korosho…

**MBUNGE FULANI:** Na muhogo.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Na muhogo, naam! Sasa msimamo wa Serikali katika suala hili ukoje maana naulizwa maswali kule nashindwa kujibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimwombe radhi Mzee John Malecela lakini alishaniruhusu, naunga mkono hoja kwa asilimia mia, ahsanteni. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika hotuba iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Zakia Meghji, kwa jinsi alivyoiwasilisha hoja yake vizuri tukaweza kuielewa sawasawa; lakini zaidi nimpongeze kwa kazi nzuri aliyoifanya katika Wizara hii hata kufikia kuvuka lengo alilolikusudia kwa asilimia 18. Vile vile naomba pongezi hizi ziende moja kwa moja kwa Katibu Mkuu wa Wizara husika pamoja na wasaidizi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie dira ya Wizara na nichukue yale maneno ninayoyahitaji. Katika malengo ya dira ya Wizara ni pamoja na uhifadhi endelevu wa maliasili kwa lengo la kuleta maendeleo kwa wote ambavyo wameitafsiri katika Sera ya Uvuvi. Napenda nizungumzie upande wa uvuvi na hasa wavuvi wa Ziwa Victoria na hasa wavuvi wa Jimbo langu la Muleba Kaskazini hasa visiwa vya Bumbile na Goziba. Haya ni maeneo ambayo yako katikati ya Ziwa Victoria lakini maarufu kwa uzalishaji mkubwa wa samaki na vina wavuvi wanaotoka katika Jimbo la Muleba Kaskazini, Wilaya ya Muleba na maeneo mengine mbalimbali kwa sababu ni maeneo yaliyo na samaki wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru sana Serikali kwa kazi inayofanya kuboresha uvuvi katika Ziwa Victoria na sisi ni miongoni wa wale waliopata bahati ya kupata wawekezaji au wavuvi wakubwa ambao kwa kweli wameboresha sana uvuvi kwa kuvua wale samaki ambao wavuvi wadogo hawawezi kuwavua kwa sababu hata maeneo yale ambayo wavuvi wakubwa wanaweza kufika kwa kawaida wavuvi wadogo hawawezi kwenda kule kwa sababu zana zao ni duni hawawezi kuthubutu kwenda kwenye maji yenye kina kirefu. Kwa hiyo, nashukuru kwa sababu mchango wao umeonekana katika Serikali na wamechangia uchumi na kuinua pato la Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia samaki kwa sababu mwananchi wa Mkoa wa Kagera hasa yule anayekaa maeneo yanayopakana na Ziwa samaki kwake ni kitoweo, ni ajira, ni kuinua kipato kiasi ambacho inamwezesha kuchangia na kuendeleza maisha yake yeye mwenyewe. Baada ya Ziwa Victoria kupata wawekezaji katika Visiwa viwili nilivyovitaja ambavyo ni sehemu ya Jimbo langu, kuna jumla ya visiwa 19 na wakazi wapatao 11,000 kumetokea kutokuelewana kwa hali ambayo haileti amani kwa hawa ambao ni wakazi wa muda mrefu katika visiwa hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa naangalia ni mkakati gani umefanyika kuwaendeleza wavuvi hawa wadogo wadogo wa Ziwa Victoria kwa sababu baada ya kuwa wamekuja wavuvi wakubwa kumetokea ghasia na kutokuelewana miongoni mwao na njia pekee ya kuyasahihisha matatizo hayo ni kuwainua hawa wavuvi wadogo ambao wamekuwepo pale kwa muda mrefu lakini sasa wamegeuka ndio vibarua.

Kuna matatizo mengi ambayo ninapokwenda kule ninayakuta tunajitahidi kuyarekebisha lakini kulingana na mazingira magumu ya kufanya kazi katika maji hakuna barabara, hakuna viwanja vya ndege kama unataka kwenda sharti utafute mtumbwi tena wa kujitegemea kwa sababu mtumbwi wa abiria ni mgumu kwa mtu kama mimi ambaye sina mazoea ya kusafiri ndani ya maji mara kwa mara kwa hiyo yale mazingira ni magumu kiasi ambacho imenipasa leo niombe nafasi nizungumze nikiwa nalenga kuwazungumzia wavuvi wadogo wadogo katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri waliyoifanya wavuvi wakubwa kwa kuchangia uchumi lakini wamekuwa wakikiuka taratibu walizopewa. Wanawashambulia wavuvi wadogo, wanakata nyavu zao, wanavunja mitumbwi yao na wakati mwingine wanawafanya washindwe kufanya kazi yao ya uvuvi. Napenda kuomba suala hili liangaliwe kwa makini sana ili isionekane kwamba wavuvi wakubwa wamekuwa ni tishio kwa wavuvi wadogo hasa katika suala la amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa uwezo wa kufanya kazi mvuvi mdogo hawezi kushindana na mvuvi mkubwa lakini amani ikiwepo kila mmoja ataweza kutumia nafasi ile kujipatia kipato chake cha halali kwa jasho lake halali bila kuwa amembugudhi mtu yeyote yule. Kwa sababu wavuvi wakubwa wana uwezo mkubwa basi wakiwakuta wale watendaji wadhaifu wa Serikali mazingira yanazidi kuwa ni mabaya kwa yule mvuvi mdogo kwa kushindwa kutetewa hata pale ambapo ana haki yake, mazingira ni ya uhasama, kutafuta na kuumizana na kuna kesi nyingi. Hata leo mtu angepata taarifa za Muleba Polisi atakuta kuna kesi kati ya wavuvi wakubwa na wavuvi wadogo haya sio mazingira mazuri ambayo tunayokusudia yaweze kuboresha uvuvi katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashawishika kuiomba Serikali katika bajeti ambayo tutaipitisha leo, nilikuwa natazama katika kitabu hiki nimeona kwa wale wenzetu wa Mikoa ya Kigoma, Lindi, Mtwara, Mbeya na Rukwa walibahatika kupata mafunzo lakini wale wavuvi wa Mwanza, Kagera, Mara sikuwaona katika orodha ya wale wavuvi wadogo wadogo waliopata mafunzo.

Kwa hiyo, naomba pia wavuvi wa Kanda ambayo nimeitaja ambao wanashughulika na uvuvi katika Ziwa Victoria wapewe mafunzo ili waweze kushiriki ipasavyo katika uvuvi huu endelevu. Pia na wao waweze kujua namna ya kuweza kushirikiana kwa karibu na wavuvi wakubwa na iondoe ile hali ya uhasama inayojitokeza kwa sababu kila mmoja katika nafasi yake ana mchango mzuri na tunamhitaji katika uchumi wa Taifa letu lakini mazingira haya ni ya matatizo makubwa.

Vile vile waweze kuanzisha ushirika wao wa kuweka na kukopa lakini waelimishwe namna watakavyoweza kufaidika na ushirika huo. Kama inawezekana pia waweze kusaidiwa misaada na kupewa uangalizi wa karibu ili waweze kushiriki ipasavyo katika uvuvi wa samaki katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nashawishika kusema kwamba wale Maafisa Uvuvi wanaozunguka Ziwa na hasa Mabwana Samaki wanaokaa katika visiwa hivi ya Goziba na Kerebe waangaliwe kwa karibu kwa sababu mazingira ya kufanya kazi katika maji na katika maeneo ambayo hayajaendelezwa lakini kuna utajiri mkubwa pale lakini kuna ugumu sana wa kufanya kazi. Lakini utakuta hawa wafanyakazi ambao ni watendaji wa Serikali walioajiriwa hawana mishahara ya kutosha, hawana vifaa vya kutosha, inabidi mtu mwenyewe aanze kudandia usafiri ama kutafuta namna nyingine ya kumwezesha kufanya kwa kukodi mtumbwi kwa mtu mwingine mwenye uwezo. Haya ni mazingira mabaya na wakati mwingine inashindikana kufanya kazi ipasavyo. Naomba suala hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuweka ulinzi mzuri katika visiwa vyetu. Kwa upande wa ulinzi wa mazingira kwa kweli visiwa hivi vinafanya kazi nzuri sana katika kipindi cha mwaka 2000 mazingira yalikuwa machafu wala yalikuwa hayavutii lakini sasa hivi visiwa hivyo ni safi, wananchi wameelimika.

Kwa hiyo, ulinzi umekuwa mzuri na umepiga hatua kuondoa tu tatizo la ulinzi kwa wanaotaka kuiba samaki kwa sababu kuna boti zinazotoka nje kuja kuiba samaki katika visima hivi vya Goziba na Kerebe ambavyo viko mbali na ndivyo vyenye samaki wengi. Boti nyingine zinatoka nje kujaribu kuiba samaki kwa sababu eneo hilo ndio bado lina samaki wengi kwa upande ule wa Muleba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo wavuvi wanaomba kulifahamu ni bei ya minofu ya samaki. Bei ya minofu ya samaki kwa kweli haiko wazi. Wakati mwingine wanapokwenda kwenye biashara wanakuta bei nzuri siku nyingine wanakuta bei imeshuka sana lakini kwa sababu wao katika eneo lao mtu anayenunua ni yule yule mmoja wanashindwa kujua bei hiyo inakuwaje.

Kwa hiyo, kama inawezekana ni vizuri bei zikawa zinajulikana kama zilivyo kwenye vituo vya mafuta unakuta bei zimetundikwa ili mtu awe na uhuru wa kuona kwamba siku hiyo anaweza kuuza au asiuze.

Lakini iondoke ile dhana ya kufikiria kwamba ni yeye peke yake yule anayenunua samaki. Ikiwa pamoja na kwamba kuweka pia uangalizi wa karibu, ununuzi wa samaki ufanyike nchi kavu, usifanyike kati kati ya Ziwa kwa sababu wengine wameweka mizani yao katikati ya Ziwa.

Kwa hiyo, inabidi yule mwenye kwenda kununua ni lazima apeleke mtumbwi wake mpaka pale kati kati ya Ziwa. Sasa jambo hilo wakati mwingine linaweza kuwa si zuri lakini hata katika mazingira ya kutokuwa na amani ambayo yapo yanaweza kupelekea kuhatarisha maisha ya hawa wananchi wanaoshughulika na kazi ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia lingine ninaloomba lifanyike ni hili la kuwezesha kuanzisha na kuimarisha ufugaji bora wa samaki kwa watu wa Kanda ya Ziwa. Kulingana na kazi kubwa ambayo sasa inafanyika kwamba samaki ni wengi katika Ziwa Victoria. Kwa hiyo, ni lazima kutafuta wavuvi wenye uwezo wa kuweza kuwavua ili tupate biashara na kitoweo.

Lakini sasa unakuta wananchi wengi wanaona kwamba kama hawezi kuvua samaki ndani ya Ziwa Victoria hana maisha mengine ambayo anaweza kuyaishi. Pia kama samaki wanavuliwa kiasi kikubwa maana yake ni kwamba wale wavuvi wadogo hawapati kitoweo cha kupeleka kwa wananchi wa kawaida. Sasa hali hii inaleta udhaifu wa hapa na pale.

Kwa hiyo, nilikuwa nashawishi pia Serikali ione uwezekano wa kipindi kijacho kusimamia huu ufugaji bora wa samaki katika maeneo ya Kanda ya Ziwa ili wavuvi na wananchi wa kawaida waweze kushiriki katika hiki kilimo cha samaki nchi kavu iwe ni njia mbadala ya kuweza kuendesha maisha yao, lakini vile vile kupata kitoweo, kuongeza kipato na kuwa na maisha mengine. Kwa sababu kipato cha mwananchi wa Kagera kwa mwaka kinakisiwa kuwa ni shilingi laki moja na elfu kumi ni kidogo mno kwa kuweza kumwezesha mwananchi huyu kuendesha maisha yake kwa namna yoyote ile. Kwa sababu baada ya kahawa kuwa imeshuka sana bei na baada ya kutokuwa na ule wepesi wa kupata zao mbadala hali hii imeendelea kuwa ni tishio kwa maisha ya wananchi wanaotegemea mazao haya ambayo soko lake limeteremka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naona samaki inawezekana ikawa ni namna moja pia ya kusaidia kuinua kipato cha mwananchi wa Kagera lakini sio kuendelea kung'ang'ania tu katika ziwa. Tupate mabwawa na mito inayoweza ikazalisha samaki, wananchi wakafuga kule samaki na wakaweza kupata kipato kingine ukitilia maanani kwamba Mkoa wa Kagera ni mmoja ambao una vyanzo vingi vya maji baridi.

Kwa msingi huo hakuna tatizo la kuweza kupata mahali pa kupata maji isipokuwa tu yanaweza kuwa mbali kwa sababu ya *plateaus* zinazotengeneza Mkoa, maeneo mengine unakuta maji yanakuwa mbali lakini vyanzo vya maji vipo na mambo mengine ni mazuri hayana matatizo yoyote ya kuweza kupata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ni usafiri. Ziwa Victoria litaweza kuboreka sana na kuchangia uchumi wa Taifa kwa upande wa samaki na hata mazao mengine kama linaweza kupata usafiri. Kwa hiyo, wanaohusika naomba pia wasaidiane na Wizara ya Maliasili kuona kwamba Ziwa Victoria nalo linapata vyombo vya usafiri kwa vile wananchi usafiri wao wenyewe, mizigo yao na bidhaa mbalimbali hasa ya samaki na mazao yake iweze kutoka kule kwenye visiwa kwenda nchi kavu. Lakini pia na watu wa nchi kavu wapate urahisi wa kwenda kupata mazao kama wanahitaji hasa samaki na biashara nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuwatakia kila la kheri Wizara hii ya Maliasili na Utalii, nikiwatakia afya njema na mafanikio makubwa katika kazi hii kubwa iliyopo mbele yao. Ninaamini kabisa kwamba Mwenyezi Mungu atawatangulia na wataweza kufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia kwenye hoja iliyo mbele yetu ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Kwanza nianze kwa kutoa pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara hii, Wakurugenzi na wasaidizi wao wote kwa kazi nzuri ambayo inaendelea kufanyika kama ambavyo Kamati ilivyokuwa inawasilisha mapendekezo yake hapa imepongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ambayo tumepewa na Mheshimiwa Waziri leo asubuhi inatoa ushahidi wa mambo hayo hasa ukiangalia kuwa idadi ya watalii wa Kimataifa imeongezeka sana. Mapato kwa dola za Kimarekani yameongezeka, wastani wa siku kwa mtalii umeongezeka ambapo sasa hivi wastani ni karibu siku nane. Mtalii kukaa siku nane katika nchi yetu siyo jambo dogo na kwa hiyo waajiriwa kwenye sekta ya utalii kwa ujumla nao wameongezeka.

Kwa hiyo, kitu muhimu tunachokitarajia kutoka kwenye sekta hii kwa ujumla wake ni kwamba maskini wa Tanzania watafaidika zaidi moja kwa moja kwa kuuza bidhaa zao ndogo ndogo na kwa namna nyingine ya ajira na kadhalika katika kufaidika na mapato haya ya utalii ambayo yanaendelea kuongezeka. Kwa hali hiyo nzuri nalazimika kuanza mazungumzo yangu kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nianze tu kwa kusema kwamba mimi nililelewa na Wizara hii kabla sijaingia katika Bunge hili kwa miaka karibu kumi na tano hivi. Ni Wizara ambayo ilinilea vizuri na kwa kiwango kikubwa ndiyo imenipa uwezo wa kuwa Mbunge na kuweza kuchangia hoja na kadhalika, nilijifunza mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wakati anaingia kwenye Wizara hii ilikuwa imejaa *Maloliondo Gate* na Ma-*gate* na ma-*gate* lakini ninyi wote ni mashahidi kwamba sasa hakuna cha *gate* wala nini, hali ni nzuri tunahitaji kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri. Kazi yote hii anaifanya yeye peke yake kwa maana kwamba Waziri asiyekuwa na msaidizi, kwa maana ya Naibu, unamwona yuko peke yake pale.

Kwa hiyo, ni lazima tumpongeze kwa kweli kuna kila sababu na hii ni Wizara ngumu, Wizara ya Utalii ina-*deal* na masuala ya Kimataifa kwa hiyo, ni ngumu si mchezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Wizara hii kwa kuendesha uhifadhi wa daraja la juu. Tunazo hifadhi za Taifa za *quality* ya juu kabisa duniani. Hifadhi ambazo ukilinganisha na nchi jirani kama Kenya na Uganda haziwezi kutukaribia hata kidogo japo kabla Mheshimiwa Waziri hajaingia walikuwa wanatutambia sana Waganda na Wakenya kwa maana ya idadi ya utalii. Lakini sasa wanahangaika sana kutufikia kwa sababu hifadhi za Tanzania karibu zote ni hifadhi ambazo ukifika kwenye *gate* unakutana na wanyama wa kila aina kwa wingi kabisa. Jambo ambalo huwezi kulipata katika nchi nyingi duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewahi kutembelea Kenya wakati fulani kwenye hifadhi yao moja kubwa wanayoitegemea ya Tsavo, wameweka tangazo wanasema Mheshimiwa mgeni katika hifadhi hii wanyama wa hifadhi hii wanafanana sana na mazingira yaliyopo humu kiasi kwamba ukiweza kumwona mmoja jipongeze sana. Inabidi uwe na macho mazuri na mtafiti sana lakini hiyo ni janja ambayo wameiweka kwa sababu wanyama hakuna lakini wa kwetu huhitaji kuweka bango la namna hiyo kwa sababu ukifika getini unakuta wanyama wa kila aina. Sasa wanyama hawa wa kujiweka wenyewe ni dhahabu ya Tanzania na inatunzwa na inaonyesha kazi nzuri ambayo imekuwa ikifanywa na Wizara hii chini ya Mheshimiwa Waziri wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kazi hii imekuwa ikifanywa na shirika la umma au mashirika ya umma kwa maana ya *Ngorongoro Conservation Area* na *Tanzania National Parks* kwa maana ya Mashirika nazungumzia kwa kuendesha hizi hifadhi zetu. Mnajua jinsi ambavyo mashirika ya umma mengi Tanzania yalivyoboronga mambo, yakaharibu uchumi, yakafa, lakini shirika hili la umma *(TANAPA)* chini ya uongozi wa Mzee Job Lusinde, Mwenyekiti wa Bodi, ni shirika la umma *grade one,* linaendesha mambo yake vizuri na ushahidi upo wazi kabisa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, baada ya hifadhi za Taifa tunayo mapori ya akiba kwa Kiingereza yanaitwa *Game Reserve* ambazo nazo zimeendelea kuongezeka idadi yake siku hadi siku na uhifadhi kwenye *Game Reserve* pia ni mzuri sana. Tunayo hifadhi ya bahari, tuna hifadhi za misitu ambazo nazo zinaendelea vizuri. Kinachohitajika sasa hivi kushughulikia katika maeneo haya ya hifadhi zetu za nchi nzima ni kuangalia kuhusu suala la idadi ya watumishi, ni wachache mno.

Kwa hiyo, ni kuangalia suala la posho maalum wanazostahili kupata watumishi hawa kwa sababu wengi wao wanakaa maeneo ambayo yako porini sana, yanahitaji *commitment* kubwa mtu kuweza kuishi katika maeneo yale. Vile vile panahitajika marekebisho ya Sheria ya Wanyamapori, Sheria ya Hifadhi za Taifa ya *TANAPA* na sheria ya Ngorongoro kurekebisha tu hapa na pale kwa maana ya kuweza kufikia malengo yao vizuri zaidi na natumaini hilo ni jambo ambalo Wizara inashughulikia litakuja wakati muafaka utakapofika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2002 kulikuwa na mkutano mkubwa wa dunia kule Johannesburg ambao uliweka malengo ya kupunguza umaskini wa dunia kwa nusu ifikapo mwaka 2015 na nafurahi kwamba mwaka huu Bajeti yetu kwa kiwango kikubwa imelenga zaidi katika kumtazama mtu maskini Mtanzania. Kwa jinsi hiyo tumeona jinsi ambavyo Bajeti ya Ujenzi, Elimu, Kilimo na Wizara zingine zimekuwa kwa kiwango kikubwa zimekwenda chini kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningeshauri sana pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii, vile vile kuiga utaratibu huu kwa kutobaki Wizarani kwa kiwango kikubwa kujaribu kuteremka chini na kuwianisha mipango yake na mipango ya Halmashauri za Wilaya kwa sababu katika Halmashauri za Wilaya zilizo nyingi Idara ya Elimu inapata fedha kutoka Halmashauri na Serikali Kuu, Idara ya Afya, Idara ya Ujenzi, Kilimo na kadhalika, lakini idara za maliasili za Halmashauri za Wilaya ni Idara ambazo ni maskini mno, zinafanya kazi katika mazingira magumu sana.

Kwa hiyo, hatuwezi kuwa na uhifadhi mzuri wa maliasili ya nchi yetu endapo hatutaangalia utaratibu wa namna ya kuwa na mipango ya nchi nzima kama ilivyo kwa elimu, kilimo, afya na kadhalika. Ipo haja ya kusaidia sana idara hizi ili ziweze kupata pikipiki kama magari hayatapatikana waweze kupata mafungu, watumishi ambao kwa sehemu kubwa hawapo. Wilaya nyingi hazina maafisa uvuvi, hazina maafisa wanyamapori, baadhi hazina maafisa misitu wenye sifa zinazotakiwa. Upo umuhimu mkubwa sana wa kuimarisha eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kupambana na umaskini tumekubaliana kwamba maeneo ya kipaumbele makubwa sana ni kama matatu, lakini yapo na mengine. Moja, ni kuwekeza katika maendeleo ya watu kwa maana ya elimu, afya, maji na chakula na bajeti ya mwaka huu imetoa ushahidi huo kwa kuongeza zaidi nguvu ya Serikali kimafungu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni kuwasaidia wananchi kuongeza uzalishaji kwa maana ya kilimo, mifugo na hifadhi ya maliasili ikiwa ni pamoja na hifadhi ya ardhi ili kuwa na ardhi yenye rutuba, hewa safi, maji, wanyama, samaki na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu kwa mpangilio wangu mimi ninavyoangalia kwa umuhimu wake ni masuala ya miundo mbinu na tumeona hapa kwenye masuala ya barabara. Tunatarajia masuala ya mawasiliano yatakuwa mazuri, umeme Vijijini, yakifanyika haya yatakuwa yametusogeza sana mbele katika kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ili kupambana na umaskini vizuri ipo mitego, wazungu wanaita *Poverty Trap* ambayo ndiyo inawakamata watu wasiweze, kutokana na umaskini ule. Zipo tafiti zimefanyika mbalimbali katika nchi kwa nchi na ndani ya nchi. Ndani ya nchi utakuta kwamba wastani wa Kitaifa unapotumika mahali pengi unatudanganya sana. Kwa sababu wastani ule hauonyeshi hali halisi ya tofauti za Mkoa kwa Mkoa na Wilaya kwa Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo Mikoa ambayo inafanya vizuri na zipo Wilaya ambazo zinafanya vizuri zaidi ya nyingine na hizi ni nyingi kuliko zile ambazo hazifanyi vizuri. Lakini sasa ili kuepukana na mitego hii ya umaskini lazima kuwe na kitu wanakiita *take off* namna ya kusaidia hizi Wilaya ambazo ziko

nyuma ili kuondokana na pale walipo na eneo kubwa katika jambo hili ni elimu. Yupo mtaalam mmoja alisema ukiwa na asilimia kumi ya wakazi wako wana elimu angalau ya sekondari basi una mtaji mzuri sana wa kuweza kuendelea.

Kwa hiyo, zipo Wilaya katika nchi yetu zina shule za sekondari mpaka 30 au zaidi na zipo Wilaya kama ya kwangu ya Kongwa ambayo ina shule za sekondari tatu kwa watu 240,000. Hawa watu hawajafanya makusudi kutokuwa na sekondari nyingi ndiyo zile nilizokuwa nasema zipo *Poverty Trap,* yapo mambo yanambana mtu katika umaskini anabakia pale. Sasa juhudi za Serikali lazima zisaidie kuwezesha watu wa aina hii waweze kutoka pale walipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwaachia tu tukisema wajenge wao wenyewe itakuwa ni vigumu na tusiposomesha watu wetu ndiyo nakuja pale pale kwenye suala la hifadhi ya maliasili na mazingira itakuwa ni vigumu sana kwa sababu umaskini unaendana na kuharibu mazingira na kuchafua mazingira.

Kwa hiyo, tunatumaini kabisa Serikali mwakani italeta ule mpango ambao imeuongea kwa muda mrefu wa *Secondary Education Programme(SEDP)* ili itusaidie sana tulio wengi kuondokana na matope ambayo tumekwama nayo katika upande wa elimu ya sekondari na itatusaidia sana katika kukwamuka na hifadhi ya mazingira na hifadhi ya maliasili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, niongelee kidogo kuhusu masuala ya kumbukumbu ambazo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walitaja kidogo asubuhi. Harakati za ukombozi wa Afrika zikiongozwa na Kamati ya Ukombozi ambayo Makao yake Makuu yalikuwa hapa Tanzania ilifanya kazi nzuri sana. Sisi Wanakongwa tuliishi na wakombozi hawa wa Angola, Zimbabwe, Namibia, Msumbiji-*FRELIMO* na bado ndugu zetu hawa wanakumbuka sana Kongwa na tumekuwa na mawasiliano nao na wapo tayari kushirikiana na Serikali yetu kuona namna bora zaidi ya kuweka kumbukumbu ya ukombozi wa Afrika na ukombozi wa Mwafrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ushauri wetu ni kwamba pale Kongwa iwe ni moja ya sehemu ambazo patawekwa kumbukumbu fulani kama ni chuo, shule au kitu kingine na Jumuiya ya *SADC* naamini katika jambo hili tunakubaliana bila tatizo ili vizazi vijavyo watakapokuwa wakifuatilia historia ya ukombozi wa Mwafrika waweze kufika pale na kujifunza matatizo gani aliyapata Mwafrika na aliishi katika mazingira gani, pia alifanya mbinu gani kuweza kujikomboa. Hilo ndilo pendekezo langu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa kwa sababu wakati umekwisha nirudie tu kuitaka Wizara na kuiomba kabisa kwamba mwakani iangalie uwezekano wa kuleta mpango kamambe kabisa wa nchi nzima kama jitihada za Serikali za kupambana na umaskini kwa kuweka fedha nyingi katika uhifadhi wa maliasili ambazo zitakwenda mpaka Wilayani kama ilivyo kwa Kilimo, Ujenzi, Elimu ili yale malengo ya dunia *(Millenium Development Goals)* zile saba mojawapo ikiwa ni masuala ya hifadhi ya mazingira yaweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nawaomba Waheshimiwa Wabunge tumpitishie Mheshimiwa Waziri Bajeti yake na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja hii ambayo ipo mbele ya Bunge lako Tukufu.

Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mama yetu Zakia Meghji, kwa kazi nzuri anayoifanya, kadhalika napenda nichukue vile vile nafasi hii kumpongeza Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote walioshiriki katika kuandaa hotuba hii kwa makini na umahiri mkubwa sana. Hongereni sana. Aidha, niungane na Wabunge waliotangulia pamoja na wa upande wa Upinzani kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafanya hivi kwa misingi kwamba karibu maagizo yote ambayo Wizara hii ilishauriwa na Kamati ya Bunge yametekelezwa kwa kiwango kikubwa. Mafanikio haya yanayozungumzwa kwa kweli yameletwa kwa ushirikiano mkubwa kati ya Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji na hasa wale watendaji wa chini wanaofanya kazi kwenye mapori, misitu pamoja na bahari na maziwa. Mimi nimekulia katika Wizara hii kwa miaka zaidi ya 30. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafahamu mazingira magumu ya kazi hii. Lakini inasikitisha kwamba bado mpaka leo hii Serikali yetu inawaona hawa vijana wanaokaa maporini sawasawa na watu wanaofanya ofisini. Matokeo yake ni kukatisha tamaa na pindi watu wanapocheleweshewa malipo yao wanajilipa wenyewe. Sasa ninachosema hapa ni kwamba ipo haja kubwa sana ya kuhakikisha kwamba hawa watu wanaangaliwa katika aina ya kipekee kwa sababu wamekabidhiwa raslimali kubwa sana.

Sasa ndugu yangu ukiangalia sana watu wanaofanya kazi katika mapori siyo tu wao wenyewe wanapata matatizo lakini vile vile familia zao, watoto wao wengi wanachelewa kwenda shule. Kwa hiyo mimi ningependekeza na kushauri kwamba Wizara hii iangalie sana na kutilia mkazo suala la elimu kwa watoto wa wafanyakazi ambao wanakaa mbali karibu na shule hasa za sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningependa nichangie vile vile katika eneo lingine kuhusu maduhuli.

Kwanza ningependa kwa ujumla nipongeze tu kwamba Wizara imefanya vizuri sana katika kukusanya maduhuli. Lakini ni budi niseme sekta ya misitu na nyuki ingekuwa na uwezo mkubwa sana wa kuchangia katika eneo hili. Taarifa ya Umoja wa Mataifa inaonyesha kwamba Idara ya Misitu na Nyuki wana uwezo wa kuchangia kati ya shilingi bilioni ishirini mpaka thelathini, lakini sasa wanachangia bilioni 4.5.

Mimi nashauri kwamba ipo haja ya kuipa motisha na kufanyia tathmini ya kina sekta hii ili iweze angalau kufikia nusu ya kiwango hiki. Ukiangalia sana matumizi ya mazao ya misitu ni makubwa sana kuliko kile ambacho kinakusanywa na pengine tunatumia zaidi kuliko kile ambacho kinatakiwa kitumike.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya ningependa sasa nizungumzie jambo moja ambalo kwa kweli halijatajwa katika hotuba hii wala hata Kamati haikuligusia lakini mimi nadhani nimeona nichukue nafasi niliseme. Kama mnakumbuka jana nilikuwa nimeuliza swali Na. 278 kuhusu rasilimali ya meno ya tembo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati biashara ya meno ya tembo ilizuiliwa Serikali ya Tanzania ilikuwa na kiwango kikubwa sana cha meno ya tembo ambacho kwa bei za wakati ule ilikisiwa kwamba ingeweza kuiingizia Serikali mapato ya kati ya shilingi dola za Kimarekani milioni tano mpaka milioni nane. Naamini sasa shehena hii imeongezeka kutokana na wanyama tembo kufa na kadhalika. Sasa mpaka leo shehena hii ipo na inagharimu fedha nyingi kuilinda, kuhifadhi kinyume na sera endelevu kwa sababu meno siyo ya kuendelea kuyahifadhi bali meno ya kuyauza na kutumia hizo fedha kwa ajili ya shughuli za uhifadhi. Ninaelewa matatizo ambayo yapo kama Mheshimiwa Waziri alivyokuwa anaeleza katika jibu lake la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningependa Bunge lako Tukufu angalau likafahamu ni kiasi gani cha meno hayo tunayo na yana thamani kiasi gani na kama thamani hiyo inaongezeka au inapungua ili tuweze kuamua, je, tuendelee kuyaweka au tuyaondoe. Shehena ambayo Tanzania tulikuwa nayo ilikuwa ni kubwa na yalikuwa meno mengi zaidi kuliko meno ya nchi zote ambazo zilikuwa na meno wakati huo ikiwemo nchi ya Botswana, Zimbabwe, Afrika ya Kusini, Zambia na nchi nyingine. Baadhi ya nchi hizo zimeweza kufanikiwa kuuza shehena zake kwa kutumia Mkataba wa *CITES* ikumbukwe kwamba Tanzania ilikuwa ni moja kati ya nchi ambazo zilikuwa zinaunga mkono kusitisha biashara hii kwa lengo la kujiandaa ili tuwe na mipango mizuri hatimaye tuwe na biashara endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nasikitika kwamba sasa ni miaka kumi na nne tangu tusitishe na bado yanaendelea kutugharimu na mimi nashauri kabisa Bunge lako Tukufu tuiombe Serikali itupe sasa *time frame* ni lini meno haya yatauzwa. Kwa sababu wenzetu wameuza na mimi naamini tunachohitaji ni kushirikiana kwa karibu na nchi za *SADC* kufanya *lobying* inayotakiwa kwa sababu uko *CITES* nawaambieni kabisa pamoja na kwamba taasisi au asasi inayodhibiti biashara ya viumbe adimu, lakini vile vile chombo hiki kinaweza kikatumika kukandamiza nchi maskini. Mimi nawaambieni kabisa hapa kwamba kama meno haya yangekuwa ni ya Amerika au Uingereza sasa hivi yangekuwa yameshauzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tunaambiwa kwamba tembo sasa wameongezeka kuanzia 52,000 na kufikia 83,000 na kama wengi mlivyoona mimi naamini kwamba kiwango cha uhifadhi katika nchi hii kinazidi nchi nyingi sana za Afrika, kwa hiyo, tunastahili kupewa kibali kuuza haya meno mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aandae mikakati ya kuhakikisha mkutano unaokuja wa *CITES, agenda* yetu iwe ni hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi ijiandae vizuri kama nchi ianze kufanya *lobying* sasa na nchi nyingine na haki za *SADC* kwa sababu nchi za *SADC* na sisi sera zetu za uhifadhi zinafanana. Lakini sera ya wenzetu Kenya inatofautiana wao hawataki masuala ya matumizi kama uwindaji wanataka utalii. Kwa hiyo kama *lobying* yote inayopinga suala la biashara katika Afrika lazima itakuwa inapitia Kenya.

Kuna kundi moja la *NGO* inayoitwa *Animal Welfare Group* hiyo inasambaa kila mahali kupita kushawishi wanachama kwamba waache hizo mali zikae hapa hapa. Lakini hawasaidii chochote katika uhifadhi. Kwa hiyo mimi ningeomba kabisa kwamba nchi yetu sasa ijenge mikakati madhubuti kuhakikisha kwamba meno haya yanauzwa ili hizo fedha zitumike kuhifadhi tembo walio hai.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ningependa nimalize kwa kusema kwamba imefikia sasa wakati Wizara iandae mikakati na iwe na lengo la kujua nchi yetu tunahitaji tembo kiasi gani. Kwa sababu ikizangatia kwamba idadi ya watu nayo inaongezeka, itafikia mahali lazima migongano itaongezeka. Kwa hiyo, lazima pawe na lengo kwamba tunahitaji tembo kama 100,000 na wanabaki tembo 100,000 ile nyongeza inavunwa na yale meno yanauzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ningependa Waheshimiwa Wabunge niwaombe tuunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Nikiamini kwamba Mheshimiwa Waziri ni msikivu sana anautendea kazi ushauri wa Waheshimiwa Wabunge. Naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ABU T. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sera ya wanyamapori hususan athari kwa binadamu na mali zake katika mchango wangu nashauri uwekeji wa wigo ili kutenganisha hifadhi ya wanyama na makazi ya binadamu.

Hapo zamani kwenye miaka ya sabini *Ngurdoto National Park* walikuwa wanatumia teknolojia hii ya uwigo wa nyaya za umeme, umeme ufuliwao na *battery* za kawaida tu. Umeme mdogo *(voltage* ndogo) ambao humstua tu mnyama bila kumuathiri ila tu humfanya arudi kwenye hifadhi badala ya kuelekea kwenye makazi ya watu kwenye Vijiji vile vya Ngurdoto, Segiruki, Ngabobo, Ngarananyuki, Oldonyosambu na kadhalika. Tatizo la Hifadhi ya Mikumi pia lingeangaliwa kwa mtizamo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu hapa ni kuomba mabadiliko ya mgao upatikanao na uwindaji wa kitalii. Mgao wa asilimia 25 kupewa Wilaya na asilimia 7.5 kupewa Vijiji ni kudumaza elimu kwa wananchi wa Vijijini kuwa wao ndio wenye jukumu zaidi la kuhifadhi wanyamapori. Hali hii ibadilike ili waweze kuchangia zaidi kwenye kutatua kero zao kama vile ujenzi wa shule, Zahanati na matengenezo ya barabara zao za Vijijini. Wilaya kwa kuwa itakuwa na Vijiji vingi kwa ujumla asilimia 7.5 ni kubwa zaidi kuliko asilimia 25 pekee itakayopata Kijiji. Ningeshauri mabadiliko haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Zakia Meghji, kwa kazi yake nzuri na hasa kabisa kwa kipaji chake kizuri cha usikivu. Nampongeza sana yeye binafsi, Katibu Mkuu wake na Watendaji wakuu wake wote. Naipongeza pia Kamati ya Kudumu ya Bunge kwa kuiwezesha kwa ushirikiano mzuri unaojitokeza kwenye ripoti yake, Wizara kutoa hoja nzuri na fasaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, asilimia mia moja.

**MHE. ALLY A. KARAVINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata fursa ya kuchangia hoja hii. Yangu ni mafupi tu na ni katika nyanja zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maskini wengine katika Taifa hili, misitu ndiyo raslimali pekee waliyonayo. Katika hali hiyo ni muhimu wakaruhusiwa kuvuna mali asili hii kama njia mojawapo ya kondoa umasikini. Lakini gharama kubwa ya leseni ya mbao na hata miti ya kujengea sasa hivi ni kubwa sana na pili, suala la uvunaji kwa ajili ya nishati ni kwa sababu hakuna *alternative* kwa sasa. Inatakiwa Serikali ielewe hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa nyuki upo lakini ubora wa asali si mzuri, ugani juu ya uzalishaji unatakiwa Tabora - Urambo na Sikonge ili watu wazalishe asali bora. Pia mashine za kusafisha asali na *packages* za kukidhi Soko la Kimataifa. Elimu ya soko isibaki kuwa hazina ya Ofisi tu bali elimu hii ipelekwe kwenye sehemu za uzalishaji ili itoe motisha kwao. Pia Serikali isajili vikundi vya wazalishaji wa asali ili kuwasaidia.

Mheshimwia Naibu Spika, *WMA* zisaidiwe pamoja na juhudi wanazofanya wananchi na wale wanaowasaidia, inabidi pia msaada wa Serikali uwepo. Pia inabidi *WMA* ziongezwe ili hata zile sehemu ambazo in *potential parks* (Hifadhi) zianze kutunzwa kutoka sasa na wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. DR. JUMA A. NGASONGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naungana mkono na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri Zakia Meghji kwa hotuba nzuri na yenye mwelekeo sahihi na uhakika. Naiunga mkono hoja hii ya Waziri wa Maliasili na Utalii.

Namwomba Mheshimiwa Waziri, wakati akitekeleza mradi wa barabara katika eneo la Kusini mwa *Selous Game Reserve* katika eneo la Tarafa ya Malinyi katika Wilaya ya Ulanga na lile la Tarafa ya Kitanda upande wa Wilaya mpya ya Namtumbo, naomba kwa niaba ya wananchi wangu ile barabara ya *Selous Game Reserve* inayoanza kitanda kuingia *Selous Game Reserve* iendelee hadi Kijiji cha Kilosa Mpepo kilichopo katika Tarafa ya Malinyi iliyomo Jimboni mwangu. Kama atavyokumbuka, Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, Mbunge wa Namtumbo, jirani yangu na Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula, alikuandikia kuomba msaada/mchango wako ili tutengeneze barabara hii ya Kilosa Mpepo - Kitanda, barabara mpya, yaani itafungua eneo hili la kilimo na wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii itasaidia sana kuimarisha uhifadhi wa wanyamapori wa eneo hili ambao sasa majangili wanaingia na kuwinda tembo na kuchukua nyara za Serikali bila kuhofia sheria. Kiutawala, barabara hii inaunganisha Wilaya ya Ulanga, Namtumbo na Songea pamoja na Mikoa ya Morogoro na Ruvuma. Hivi sasa Wilaya ya Ulanga na Namtumbo wanaendelea kuzifyeka sehemu zao husika ili kuwezesha barabara hii kutoboka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri uchangie ujenzi wa barabara hii. Nawasilisha ombi hili kwako kama pia Mwenyekiti wa Kamati ya Viongozi wa Wilaya za Ulanga na Namtumbo/Songea inayosimamia ujenzi wa barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. Namtakia mafanikio Mheshimiwa Waziri katika hoja yake hii.

**MHE. PROF. PIUS P. MBAWALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kushirikisha wananchi katika uhifadhi misitu nakumbusha tena tulichojadili pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafadhali naomba Waziri akigeuze Chuo cha Maliasili Likuyu Sekamaganga (Namtumbo - Ruvuma) kifanye vile vile shughuli zifuatazo:-

(i) Kutengenza mizinga ya kisasa ili nyuki waweze kurinwa na kusambazwa katika misitu ile kuzunguka chuo;

(ii) Kuwapo mashine ndogo za kurinia asali na kusindikwa kwa ajili ya soko la ndani na nje;

(iii) Wanafunzi wajue pia jinsi ya kutengeneza mishumaa. Soko lipo Mkoani na kwingineko nchini;

(iv) Kwa kuweka mizinga kuzunguka misitu ya Vijiji itawahamasisha watu kutochoma moto;

(v) Chuo cha Likuyu kitumike pia kufunza *Porters*/Wapagazi wa Utalii ili watekeleze huduma hiyo kwa umakini zaidi; na

(vi) Je, lile wazo la kuweka samaki katika mto Likuyu toka Mto wa Kilombero limeishia wapi?

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ninatoa mchango wa maandishi katika kuboresha Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kukosa mapato stahili kutokana na utalii unaohusisha Mlima Kilimanjaro, kutokana na ukweli kwamba Watalii wanapitia tu Tanzania. Watalii hao hufikia Kenya na shughuli zao nyingi pia hufanyia Kenya. Biashara ya utalii unaohusiana na mlima huu, imeshamiri zaidi Kenya na ni Kenya inayonufaika zaidi kupitia viwanja vyake vya ndege, mahoteli ya kitalii, mawakala wa utalii, Kampuni za usafirishaji na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kenya bado inautangaza Mlima Kilimanjaro katika nchi za Ulaya Magharibi, Marekani, Australia na New Zealand, pia Japan kama vile mlima huo upo Kenya. Kenya iko *very aggressive* katika kuutangaza Mlima Kilimanjaro kuliko Tanzania ambayo bado ipo nyuma sana katika biashara nzima ya utalii na hasa katika suala zima la utangazaji wa vivutio vya utalii na hata utoaji wa huduma bora kwa watalii. Hivi sasa itatuwia vigumu sana kuweza kuwapiku Kenya kutokana na kuchelewa kwetu katika kuutangaza mlima huu na kuonya kuwa sio mlima wa Kenya ni wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali Kuu kukusanya fedha nyingi kutokana na utalii wa Mlima Kilimanjaro, zingepaswa kuwa nyingi zaidi kama zisingepokonywa na Kenya. Bado Halmashauri ya Wilaya ya Moshi na Jimbo zima la Ubunge la Moshi Vijijni hakuna chochote kikubwa linachopata moja kwa moja kutokana na mapato hayo ya Serikali Kuu ambao ni watunzaji namba moja wa Mlima Kilimanjaro na mazingira yake yote na ni pamoja na kufanya shughuli za kuzima moto mara utokeapo na pia ndiyo walinzi wakubwa wa Maliasili mbalimbali zinazohusiana na Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kila sababu ya watu wa Moshi Vijijini kupewa kifutajasho fulani kikubwa na pia kupewa motisha stahili kwa kuwa mstari wa mbele katika kuilinda raslimali hii muhimu ya Taifa na ya Kimataifa (Mlima Kilimanjaro) kwa niaba ya Watanzania wote na wapenda mazingira wote waliopo duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri atakumbuka malumbano ya mara kwa mara kuhusiana na sheria Na.32 ambayo ni tangazo la mwaka 1994 ambayo nimeambatanisha kivuli chake kuashiria kuwa sheria hiyo haijafutwa kwa kuwa Wizara imegoma kutekeleza sheria hiyo, basi Wiziri aagize kufutwa kwa sheria hiyo kama anao uwezo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima Mlima Kilimanjaro uwe na manufaa ya moja kwa moja ya kiuchumi na kijamii kwa watu wa Moshi Vijijini kwanza na baadaye kwa wenzetu wengine katika Tanzania. Si jambo jema watu walioko Kenya, Ulaya na Marekani, wakaneemeka zaidi na Mlima Kilimanjaro ulioko Moshi Vijijini na wananchi wa Moshi Vijijini wakiishia kusindikiza watalii tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inawajibika kimsingi kabisa kuchangia maendeleo ya Moshi Vijijini kutokana na mapato ya Utalii wa Mlima Kilimanjaro. Ni lazima Serikali ifanye uamuzi wa makusudi kabisa wa kutenga asilimia nzuri tu ya mapato hayo ili iende moja kwa moja kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Moshi. Sababu kubwa ni moja tu, wananchi wa Moshi Vijijini ndio askari wa

mstari wa mbele katika utunzaji wa mazingira ya Mlima Kilimanjaro. Siku zote Askari wa Mstari wa Mbele hufikiriwa kwanza kabla ya askari wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nategemea ushirikiano mwema siku zote ili tuweze kunufaisha Taifa hili, nami sitachoka kuwakumbushia.

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Waziri wa Maliasili na Utalii kwa juhudi zake za kiongozi na utendaji katika Wizara hii nyeti ambayo imekuwa na mafanikio makubwa. Pia nampongeza Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujangili wa wanyamapori umezidi kiasi kwamba hata twiga huwindwa. Uwindaji huu haramu hufanyika zaidi nje ya Hifadhi za Taifa. Huenda ni kwa sababu ya watumishi wachache.

Napendekeza kwamba Serikali iwaajiri watumishi wa kutosha ili kuhifadhi raslimali hii adimu. Pili, kuanzisha askari wa wanyamapori wa Vijijini *(Village Game Scouts)* na tatu, kuanzisha *WMAs* katika maeneo yanayozunguka Hifadhi za Taifa.

Kuhusu uwindaji wa kitalii napendekeza kwamba wanaopewa vitalu vya uwindaji yapatikane kwanza maoni ya wananchi wanaoishi katika maeneo hayo ili kujua wanavyoshiriki katika maendeleo, wapewe sharti la kushiriki katika maendeleo katika Vijiji vilivyopo katika eneo hilo, naomba vitalu vya Wilaya ya Simanjiro viingizwe katika *WMA* na wapewe sharti katika kupambana na ujangili katika vitalu vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mikutano ya kutangaza utalii wetu yatazamwe yafuatayo:-

(a) Tangazo letu lililozaoeleka ni bango kubwa lenye picha ya Mlima Kilimanjaro lililoandikwa *Tanzania Land of Kilimanjaro and Zanzibar.* Hii imebadilishwa na kuandika *Tanzania Authentic Africa* (Tanzania - Afrika Halisi).

Kila nchi Afrika ni halisi lakini hakuna nchi ya Afrika yenye Mlima Kilimanjaro wala yenye Visiwa vya Zanzibar. Pia itakuwa kwa pamoja umetangaza pande zote mbili za Jamhuri.

(b) Madhara yake ni kwamba nchi jirani itaanza tena kutangaza Serengeti na Kilimanjaro iko kwao, hii pia itasababisha uhasama na nchi nyingine za Afrika na watu wengi kwenye maonyesho hutafuta Tanzania *Land of Kilimanjaro and Zanzibar* wasipoona huondoka kwa hivyo huchukua muda mrefu hilo la sasa kuzoeleka.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, misitu ni raslimali kubwa ambayo ni budi kuihifadhi na kama tunatumia, basi tutumie kwa uangalifu. Nashauri yafuatayo:-

(a) Vibali vinavyotoka Makao Makuu vipitie Mkoani na Wilayani ili Maafisa Misitu wa eneo husika wawe na taarifa na waweze kufuatilia;

(b) Wanaokata miti kwa vibali wawekewe chombo ambacho kitaonesha idadi ya miti inayokatwa; na

(c) Uwekwe utaratibu wa uvunaji miti ili kuhakikisha kila mti unaokatwa kuna miti inapandwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utalii wa Tanzania unatangazwa sehemu nyingi ulimwenguni. Naipongeza Wizara kuwa inashiriki katika maonesho mbalimbali katika kutangaza utalii na vivutio vya Tanzania. Katika kufungua tovuti ya utalii wa Tanzania nimekuta Tanzania inajitangaza kama *Authentic Africa.* Sikuelewa maana yake nini. Ni nchi gani ya Afrika siyo *authentic?*

Nashauri kuwa Tanzania ina vivutio ambavyo havipatikani nchi nyingine yoyote ile ila Tanzania kama Mlima Kilimanjaro, Serengeti na Visiwa vya Zanzibar. Hukuti mlima mrefu wa pili duniani ila

Tanzania. Nashauri turudie *logo* yetu ya Tanzania nchi ya Kilimanjaro na Zanzibar. Tukiacha kutangaza Tanzania na Kilimanjaro kuna hatari nchi jirani wakauteka mlima wetu na kuutangaza wao. Tusiache raslimali mali yetu hii ikatumiwa na wasiohusika. Nashauri Wizara iwe makini na wataalamu wa nje, maana sio wote wanaitakia mema Tanzania. Wizara ya Maliasili na Utalii imepiga hatua kubwa sana, basi tuendeleze utalii wetu kwa kutangaza vivutio asilia. Naunga mkono hoja.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja ya Waziri wa Maliasili na Utalii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nampongeza Waziri na timu yake. Nampongeza pia kwa jinsi alivyoshughulikia kwa haraka sana tatizo la uharibifu wa mazingira, hasa ukataji holela wa mti wa Msandali (Kipaati) katika msitu wa Marang japo bado sijapata matokeo ya hatua alizochukua.

Kwa vile mti huo, magamba, mizizi na mbao yake huhitajika sana na kutengenezea manukato na mti huo umekatwa sana maeneo ya Dongobesh na msitu wa Tumati na inasemekana umemalizika na sasa wakataji (wavunaji) wamevamia msitu wa Marang:-

(a) Je, Wizara ina utaratibu gani kuhifadhi miti na raslimali adimu kama hii hasa ikizingatiwa kuwa leseni za ukataji inasemekana zimetolewa Wizarani na pia Wilayani?

(b) Je, wakati utafiti unandelea kuchunguza uhalili wa taratibu zilizotumika Wizara inatoa kauli gani kunusuru mti huu adimu hadi hapo utaratibu mzuri utakapowekwa na hasa kwa vile *TANAPA* hawana mamlaka ya kisheria kulinda uharibifu katika msitu wa Marang ambao uko chini ya Idara ya Misitu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile kuna uchimbaji wa madini wa muda mrefu unaoendelea ndani ya msitu wa Marang ambao unaleta uharibifu mkubwa kwa kuacha mashimo makubwa; Je, Wizara inatoa kauli gani juu ya uharibifu huu hasa tukizingatia kuwa kuna Wizara mbili tofauti zinazohusika na eneo hilo ikiwa ni pamoja na tatizo la mpaka wa kiutawala kati ya Wilaya ya Mbulu, Babati na Karatu? Ni lini matatizo hayo yatamalizwa kwa lengo la kunusuru uharibifu katika msitu huu muhimu ambao ni raslimali ya Taifa?

Kwa vile uwindaji katika maeneo ya Matala ya Hifadhi ya Akiba ya Yayeda Chini (Mbulu) umefungwa na kwa taarifa tuliyonayo hata Wizara imefunga uwindaji katika maeneo hayo na kwa kuwa kuna taarifa kuwa kuna Kampuni moja iliyoko Arusha ambayo *Directors* wake ni pamoja na Bwana Peter Kersten (Mjerumani) na Bwana Udo, pia Mjerumani wamiliki pia wa mashamba ya kahawa na Udo anamiliki *Lodge* ya Kitalii, Karatu na kuwa wamegawiwa *Hunting Blocks* maeneo ya Hifadhi ya Akiba ya Yayeda Chini na Matala: -

(a) Je, Serikali inayo taarifa ya *Hunting Blocks* hizo na kama inayo; Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya jambo hilo na leseni wamepewa na nani?

(b) Kwa vile Halmashauri ya Wilaya ya Karatu haina taarifa ya kuwepo kwa *Hunting Blocks* hizo na kwa vile tayari kuna malalamiko kuhusu kuwepo kwa *Hunting Blocks* hizo na au uwindaji haramu unaoendelea katika hifadhi hiyo ya Akiba na kwa kuwa Halmashauri ya Karatu inayo Bwana Wanyamapori mmoja tu na hana nyenzo za kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Wizara iko tayari kuchunguza jambo hilo na au uwindaji huo haramu na kuchukua hatua madhubuti kuzuia jambo hilo na kuwachukulia hatua za kisheria wahusika ikiwa ni pamoja na kutafuta leseni zao iwapo walipewa kinyume na utaratibu?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa tuliwasiliana na Waziri, natumia tena nafasi hii kwa vile wataalamu wake wote wako hapa leo. Natanguliza shukrani za dhati nikitegemea majibu ya kina.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi nyingi sana kwa Waziri, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara wote pamoja na Wenyeviti wa Bodi za Taasisi za Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kinole na Kigurunyembe na Mlima wa Mindu ni historia inayovutia. Ninaomba sana Wizara ishirikiane na Chifu *Kingalu 19th MwanaBanzi* katika kujua historia hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Morogoro Vijijini kuna kipindi cha msimu wa kilimo, lakini wanyama waharibifu husumbua sana wananchi. Tunaomba risasi na wananchi Vijijini wamilikishwe silaha. Vijiji vimilikishwe bunduki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mamba wa Mto Ruvu. Matukio kadhaa kwa wananchi wa Morogoro Vijijini wanaoishi kandokano ya Mto Ruvu Vijiji vya Kibulumo, Kidunda, *K Stand,* Tununguo, Bwakira Chini, Bwakira Juu, Kiganila na kadhalika, tunaomba Wizara iende kuwavuna mamba hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maombi mawili. Kwanza, tunaomba atusaidie daraja la waenda kwa miguu Kidunda kwa wananchi wanaotumia kuvuka kwenda *TAZARA* . Pili, tunaomba barabara za *Selous,* ingiza Kwaba- Kidunda kilometa 40, Kwaba - Usangwe, kilometa 15.

Mwisho, kuwatakia kila la kheri mkafanye kazi kama kawaida yenu, Wizara hii ni wachapa kazi. Hongera Odunga na timu yako. Naomba sana barabara hizi mbili tu.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mludikano wa pembe za ndovu katika *Ivory Room,* yasemekana Tanzania inashindwa kujenga hoja ya kuuzwa pembe za ndovu kama walivyofanya wenzetu wa Namibia, Afrika Kusini na Zimbabwe kwa vile Wanaharakati wa Haki za Wanyama Duniani hawaelewi hali ilivyo nchini Tanzania, hivyo kuwa shinikizo kwa *CITES* ambayo hudhibiti biashara hiyo. Je, kuna mikakati gani ya kuwaelimisha wanaharakati wa Haki za Wanyama Ulimwenguni kuelewa hali halisi ya Tanzania katika uhifadhi wa tembo nchini na mlundikano wa pembe za ndovu?

Mheshimiwa Naibu Spika, misitu *(catchment forests)* ya Hhassama na Nown, Wilayani Mbulu. Baada ya sera ya sheria mpya ya misitu kupitishwa sasa nini hatma ya misitu hii miwili muhimu katika maendeleo haya ya Bonde la Ufa? Wananchi na Taasisi za Wananchi sasa zitashirikishwa namna gani katika uhifadhi wa misitu hii?

Msitu wa Hhassama siyo msitu mkubwa sana lakini ni msitu nyeti kwa vile ni chanzo cha mito inayopeleka maji katika Ziwa Manyara. Kwa vile Serikali haijihusishi na msitu huu (kwa maana ya ulinzi). Je, Wizara iko tayari kukabidhi msitu huu aidha kwa Vijiji vinavyozunguka msitu huu au Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu?

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu nitaanza na kuunga hoja mkono. Naunga hoja mkono asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu, Mwenyekiti wa Bodi na Watendaji wote Waheshimiwa hawa nawapongeza sana, nawatakia kazi njema na Mwenyezi Mungu awape afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeomba msaada wa visima vitano Mikumi nimeambatanisha na gharama za kisima @1,800/= mambo hayo yamezingatia tatizo la maji Mikumi. Tunayo Kampuni ya Maji na Mradi wa Maji hauna uwezo wa gharama hizo, iko tayari kuhamasisha wananchi mchango wa nguvukazi na kazi za mikono.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la mipaka bado halijapata ufumbuzi wa kurekebisha mipaka katika Vijiji vya Kata ya Ruembe na Kidodi Mikumi. Vijiji vifuatavyo:- Kijiji cha Kitete, Kielezo, Rumango na Mikumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mhifadhi wa Mikumi apatiwe fungu la kumwezesha atoe kero hiyo ya upimaji mipaka katika Vijiji hivyo. Zoezi hili Mhifadhi Muro hakutenda haki katika zoezi hilo kwa fedha iliyotengwa. Naomba kusikilizwa kwani ni ombi la siku nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa ombi tena kuhusu Hoteli ya Mikumi. Hoteli hiyo kwani mwekezaji hakufanya ukarabati wowote na amekuwa akidai Serikali madai ambayo siyo kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya barabara ya Dar es Salaam - Mbeya ambayo imepita katikati ya Hifadhi ya Mikumi, barabara hii huua wanyama wengi sana kila siku. Tunaiomba Serikali ichepushe hiyo barabara, ianzie Mikumi, Kilosa, Dumila. Jambo hili litakuwa limeokoa mapato makubwa sana kama alivyochangia Mwenyekiti wa Kamati ya Mazingira. Naomba maombi yangu yaendelee kufikiriwa.

Mkoa wa Morogoro tumekaa na kupendekeza na tumekutana na Waziri wa Ujenzi, tumepeleka mapendekezo yetu. Naomba Wizara ikutane na Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata matatizo ya kutomaliziwa Mradi wa Bwawa - Kijiji cha Kiduhi - Bwawa limeanzishwa mwaka 2001 mpaka leo halijakwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru mahusiano ambayo tunapatiwa na Mheshimiwa Waziri wetu, Serikali yetu inavyopambana na rushwa, tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, nategemea kupata majibu mazuri asilimia mia.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri kwa utaratibu wa kushirikisha wananchi katika uhifadhi wa Wanyamapori Wilayani Babati (kifungu 59, ukurasi wa 31 wa hotuba ya Waziri). Hata hivyo, elimu zaidi kwa wananchi kuliko hata viongozi wao hasa katika maeneo ya mipaka kati ya Vijiji na maeneo ya hifadhi ni muhimu sana.

Katika baadhi ya maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya *Wildlife Management Areas* yapo malalamiko kwa baadhi ya Vijiji kuwa zoezi zima la kutenga maeneo halikuzingatia ushirikishwaji wa wanakijiji wote kwa sababu Serikali za Vijiji hivyo, hazikuzingatia uitaji wa Mikutano Mikuu ya Vijiji ambavyo ndivyo vyenye maamuzi na badala yake mikutano iliyoitishwa ni ya Hadhara ambayo kisheria havina maamuzi ya kisheria. Huu ni upungufu uliojitokeza. Kuna haja ya Wizara kushirikisha viongozi wa Wilaya kuhakiki jambo hili kwani zoezi zima mwisho wa siku litakuwa na matatizo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado ipo migogoro ya mipaka kati ya hifadhi ya Tarangire na baadhi ya wanavijiji. Bado kuna mgogoro mkubwa kati ya Kijiji cha Mayoka na hifadhi ya Ziwa Manyara. Katika maeneo haya kila mara kumekuwa na migogoro ya hapa na pale.

Nashauri Wizara iweke mwaka huu mpango maalum wa namna ya kutatua migogoro hii ambayo pamoja na kuizimisha kila wakati kwa hatua za dharura, bado ipo na naona kuwa namna pekee ni kushirikisha Viongozi wa Wilaya na Vijiji kwa pamoja na Wahifadhi husika kuwa na vikao vya pamoja mbali na ile ya ujirani mwema inayohusisha Viongozi wa Vijiji husika bila wananchi wao. Ujirani mwema pia uzingatie matakwa ya wananchi.

Utaratibu wa kuhusisha Viongozi wa Wilaya na Vijiji wakati wa kujadili mgogoro wa Kijiji cha Mayoka na Hifadhi ya Ziwa Manyara ulionyesha matumaini lakini mikutano hiyo ilisimama kutokana na sababu mbalimbali.

Katika kipindi hicho migogoro iliendelea kwa kasi na hadi leo uhusiano wa hifadhi ya Ziwa Manyara na Kijiji/wananchi sio mzuri na hasa ikizingatiwa kuwa Hifadhi hiyo ina mashamba ambayo inadai iliyanunua. Tatizo la Hifadhi hiyo kuwa na mashamba ambayo si sehemu ya Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara kisheria huwa ni mpaka wa Hifadhi, bado haujaongezwa na haujapitishwa kisheria. Ni jambo linalohitaji kuamuliwa kwa majadiliano ya pande zote. Nguvu ya dola tu haiwezi kulinda Hifadhi hiyo bila wananchi wa Mayoka. Hivyo natoa ushauri tena kuwa Hifadhi ya Ziwa Manyara/*TANAPA* waitishe vikao vya majadiliano zaidi wakihusisha Halmashauri ya Wilaya ya Babati ili hatimaye utata uishe.

Kuhusu ulinzi wa maisha na mali za wananchi ni muhimu kuwa mikakati ya pamoja kati ya Halmashauri ya Wilaya na Hifadhi husika badala ya mpango wa sasa wa dharura tu kila inapojitokeza tatizo la wanyama kuharibu mali/maisha ya watu. Miradi ya ujirani mwema ni muhimu. Miradi hii ikizangatia usawa wa haki kati ya Wilaya/Vijiji husika kwa sasa naona Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara kwa muda mrefu haijatoa ushirikiano kwa miradi ya Kijiji cha Mayoka na hisa ya wananchi ni kwamba ni kutokana na mgogoro wao na Hifadhi. Nadhani kama ndivyo, si sahihi kwa vile fedha za ujirani mwema ni haki ya Vijiji vyote vinavyopakana hata kama kuna migogoro ya aina gani. Naomba Wizara ichunguze hili kama ndivyo na mimi nitafuatilia mara baada ya Bunge la Bajeti. Naunga mkono hoja.

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Zakia Meghji, kwa kazi nzuri sana anayoifanya. Wote tunakiri na kuthamini kazi nzuri inayofanywa na Waziri huyo.

Napenda kumshukuru pia Katibu Mkuu wa Wizara hii Ndugu Odunga na wataalam mbalimbali kwa maandalizi mazuri ya hotuba hii. Ningependa kutamka wazi kuwa ninaiunga mkono mia kwa mia.

Katika kuchangia hotuba hii nitagusia maeneo mawili tu muhimu, maana sehemu kubwa yaliyo mengi yameshatolewa ufafanuzi ndani ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *speed boat* katika Mwambao wa Ziwa Tanganyika hususan Mkoa wa Rukwa kumekuwa kukijitokeza uvamizi na uvuaji haramu katika Mwambao wa Ziwa hilo hali ambayo inachangia kupunguaza mapato ya Serikali. Mwaka jana wakati nikichangia niliahidiwa kuwa Serikali italiangalia ikiwa ni pamoja na kutafuta *speed boad* kwa ajili ya kudhibiti uhalifu huo. Napenda kufahamu, je, utekelezaji wa suala hilo umefikia wapi? Nitafurahi sana kupata jibu la swali hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ziwa Tanganyika kuna samaki wengi sana na wa mapambo mbalimbali. Tatizo kubwa wanalolipata wananchi hao ni mahali pa kuuza samaki hao pamoja na namna ya kuhifadhi katika Ilani yetu ya Uchaguzi wa CCM imeelezwa kuwa Serikali itajenga Soko la Kisasa katika Tarafa ya Karema ili wavuvi wawe na Soko la Kisasa la Kuuzia Samaki wao. Tunaipongeza sana Wizara hii kwa mipango mizuri ya kujenga Soko la Kisasa la Samaki huko Mwanza. Je, soko hili la kisasa ni lini ujenzi wake utaanza huko Karema? Nitafurahi sana nikipatiwa jibu la suala hili.

Mwisho, nawapongeza kwa kazi nzuri wanayofanya na ninaunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

**MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia katika hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri, nitachangia katika sehemu chache tu kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kuzungumzia kilichokuwa Chuo cha Nyuki katika Mji wa Tabora. Tunashukuru Wizara kwa kukiweka chini ya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori *(TAWIRI)* na kwa mipango yao ya kukiendeleza.

Ombi langu kwa Wizara ni kwamba zoezi la kukiendeleza Chuo hicho liharakishwe, maana majengo na vifaa vilivyoko hapo Chuoni viko katika hali mbaya sana. Nitapenda kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, katika Bajeti hii Wizara imetenga fedha kiasi gani kwa Chuo chetu cha Tabora? Vile vile, ningependa kujua wana mipango gani ya kuwaendeleza wafugaji wa nyuki?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu kuna vivutio vingi vya mambo ya kale, kwa mfano Kijiji cha Makumbusho cha Kwihara, Nyumba ya Mtemi Fundikira, Kaburi la Milambo, Boma la Wajerumani, Mnara wa Uamuzi wa Busara wa Baba wa Taifa, Shule za Sekondari za Wavulana na Wasichana Tabora, Historia ya CCM iliyoko Sekondari ya Wavulana Tabora na kadhalika. Je, Mheshimiwa Waziri atatusaidiaje katika kuviendeleza vivutio hivi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ANTHONY M. DIALLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Maliasili na Utalii. Ili kupunguza tatizo la kupungua kwa misitu hapa nchini, napendekeza yafuatayo yanayohitajika kufanyiwa kazi na Wizara ikishirikiana na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli ya kupata mkaa inahusisha kukata miti na halafu kuchoma miti ili upate mkaa. Kitaalam inaeleweka kuwa ili upate kilogramu moja ya mkaa, unahitaji kuchoma kilogramu kumi za miti. Hii ina maana *destruction* kubwa ya misitu inatokana na kupata mkaa. Mkaa mwingi unatumika Mjini kwa vile wananchi Vijijini hawatumii mkaa. Hivyo basi, Miji na jamii yake ndio chanzo kikubwa cha kumaliza misitu hapa nchini na sehemu nyingine hapa duniani.

Sasa napendekeza kuwa Serikali itoe ilani ya mwaka mmoja ili watu wa Mijini warekebishe nyumba zao ili sehemu za jiko ziwekewe *chimney* ya kutoa moshi na *fumes.*

Baada ya kipindi hiki kupita, Serikali ipige marufuku matumizi ya mkaa pote nchini na waruhusu matumizi ya kuni Vijijini na *chipped logs* sehemu za Mijini. Watu wa Mijini ikiwa watatumia majiko sanifu yaliyopo hapa nchini ina maana matumizi ya kuni yatapungua sana na uharibifu wa misitu utapungua kwa zaidi ya asilimia 70. Hali hii itasababisha *natural growth* ya misitu kuongezeka na hivyo ku-*over shadow or overcome* matumizi ya misitu hiyo bila hata kuendesha kampeni za upandaji miti.

Kuna *argument* nyingi zinaweza kujitokeza kama vile *pollution* ya moshi mjini na kadhalika; kuwepo na misitu kuzunguka Miji itasaidia kumeza *pollution* za Miji *(Carbon Sinks).* Hata hivyo, *pollution* ya kuni ni salama kuliko moshi wa magari na kadhalika. *The level of carbon impurities* kutoka kwenye moshi wa kuni ni *less than fossil fuel* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakazi wa Mjini wasiotaka kurekebisha nyumba zao itabidi watumie umeme kwa matumizi ya kupika na kadhalika. Hii pia itapandisha *demand* ya umeme na hivyo kusababisha bei kupungua na kuwa *affordable.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tusaidiane kuliokoa Taifa kutopata jangwa. Uhuru wa watu kukata miti sio uhuru endelevu na hivyo lazima tuchangamke sasa na sio baadaye.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri na yenye ufafanuzi wa kina kuhusu Wizara yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii napenda kuchangia haya yafuatayo: -

Kwa kuwa askari wa wanyamapori ni wachache ipo haja ya kufundisha Maafisa Wanyamapori wengi ili wapelekwe katika Wilaya zetu ikiwemo Wilaya ya Mpwapwa.

Kwa kuwa wanyamapori wanaharibu sana mazao katika baadhi ya maeneo na kusababisha uhaba wa chakula katika maeneo hayo, je, ni kwa nini Serikali isiwapatie Wananchi risasi za kutosha ili kupambana na wanyama hao?

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha *Central Zone Corridor* kwa ajili ya maendeleo ya wanyamapori na maendeleo ya misitu? Mikoa itakayohusika ni Dodoma, Singida, Tabora na Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilipenda sana niongee ili nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Waziri wa Maliasili na Utalii,

kwa hotuba nzuri na mpango mzuri wa mwaka 2003/2004. Pia, napenda kuwapongeza Katibu Mkuu, Salmon Odunga, Wakurugenzi wa Idara naWakuu wa Asasi zilizopo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ina majukumu mengi na makubwa licha ya upana huu, Wizara ni mfano mzuri wa utekelezaji wa majukumu yake. Hata hivyo, kuna majukumu mengine ambayo wote kama Watanzania tuna jukumu la kutoa mchango wetu ili tuyatatue. Hatuwezi kutegemea Wizara peke yake itoe majawabu yote! Leo nitaandika juu ya moja ya matatizo haya nalo ni kukua kwa jangwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukataji wa miti hapa nchini unatisha na kama haukupatiwa ufumbuzi nchi yetu itageuka jangwa katika kipindi cha miaka 20 hadi 40 ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu kubwa za ukataji miti kiholela ni kama kuchoma mkaa. Hii imeongezeka sana baada ya kupanda sana kwa bei ya umeme na mafuta ya taa, kukausha mazao hasa tumbaku katika Mikoa ya Tabora, Iringa, Ruvuma na Rukwa. Kwa kila hekta moja ya tumbaku inayolimwa katika Mikoa hiyo mkulima lazima akate hekta tatu za msitu wa miombo ili kukausha tumbaku yake. Hivyo, msitu unapotea kwa kiwango cha kutosha katika Mikoa hiyo, kukausha samaki. Tatizo hili lipo katika maeneo ya maziwa ambapo uvuvi unafanyika na kwenye mabwawa makubwa na uchomaji wa misitu na maeneo ya hifadhi. Hili ni tatizo na ni tatizo linalotutia aibu, tutumie kila njia kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jawabu ya matatizo haya ni pana. Pamoja na kuwaelimisha wananchi lazima tuchukue hatua kadhaa pamoja na kupunguza bei ya umeme na mafuta ya taa yanayotumika majumbani, kupanda miti na misitu ya Miji, Vijiji na jamii kwa ajili ya kuni na mkaa na tutumie makaa ya mawe kupikia, kukausha mazao na samaki, kuzalisha umeme na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya mwaka 2001/2002 Mheshimiwa Waziri akifanya majumuisho ya hotuba ya Wizara yake aliahidi kuwa Wizara itachukua hatua ya kuweka mipaka ya misitu ya hifadhi ambayo imeingiliwa sana na Wanavijiji. Mpaka sasa kazi hii haijafanywa!

Naomba Wizara ichukue hatua ya kurekebisha hali hii katika mwaka huu wa fedha. Tunaomba pia Wizara itusaidie kupanda miti *(enrichment planting)* na kupanda miti ya kuhifadhi vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuishukuru Serikali kwa kuanza kulifanyia kazi tatizo la magugu maji katika Ziwa Jipe. Kazi hii tunaomba iendelee ili kuwawezesha Wananchi wa Mwanga kuvua tena katika Ziwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kumekuwa na operesheni ya kukabiliana na uvuvi haramu katika Bwawa la Nyumba ya Mungu. Kazi hii bado haijakamilika na tunaomba uwezeshaji wa Serikali na Wizara yako. Ahsante sana.

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze mchango wangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu wake, Bwana Solomon Odunga na wasaidizi wao kwa yafuatayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kazi nzuri ya uhifadhi endelevu wa maliasili na uendelezaji wa utalii ambao umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa hotuba nzuri na yenye kuleta matumaini kwetu sisi Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kwa ukusanyaji mzuri wa maduhuli ambayo kila mwaka yanazidi malengo wanayojiwekea na pia yanakuwa zaidi ya mgao wa fedha wanayopewa kutoka bajeti ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, ushirikiano mzuri baina ya Wizara na Taasisi zake kwa upande mmoja na sisi wadau kwa upande wa pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, kwa jinsi wanavyosaidia maendeleo ya maeneo na Vijiji vinavyopakana na maeneo ya hifadhi za wanyama na misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo nina maoni yafuatayo ambayo nashauri Wizara iyafanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni kuhusu Sekta ya Uvuvi. Pamoja na azma ya kujenga soko la uvuvi Mjini Mwanza chini ya mpango kamambe wa kuinua uvuvi, ipo haja ya kufanya yafuatayo.

Kwanza, kutayarisha mafunzo ya uvuvi wa kisasa kwa wazalendo. Haitoshi kufanya mikutano ya Kitaifa. Mafunzo kwa mfano katika vyuo kama kile cha Mbegani yatatuhakikishia wavuvi bora wa kizalendo, zibuniwe njia za kuwapatia Wananchi mitaji ya kununulia zana za kuvulia na kuendeleza miradi yao na licha ya masoko ya ndani kama linalotarajiwa kule Kinemba, Wizara isaidie kuwezesha Wananchi kusafirisha bidhaa za samaki nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni Sekta za Hifadhi za Misitu na Wanyamapori. Naipongeza Wizara kwa azma ya kuendesha warsha ya Kitaifa ya kukusanya maoni ya wadau, lakini hatuwezi kutegemea warsha kama hiyo kutuwezesha kupata maoni ya walio wengi. Nashauri kuwa licha ya warsha ya Kitaifa pangekuwa na warsha za Kiwilaya hasa katika Wilaya zenye hifadhi za wanyamapori na misitu.

Kuhusu ulinzi wa maisha na mali za wananchi, nawapongeza kwa jitihada zilizoonyeshwa katika ibara ya 55 ya hotuba. Lakini kwa kuwa tatizo hili limekuwa sugu sana hasa katika maeneo yanayozunguka Mbuga za Selous, nashauri Serikali irejeshe utaratibu wake wa zamani wa kuweka *askari game* wenye silaha katika maeneo hayo wakati wote.

Pia, kwa kuwa sasa wananchi wamehamasishwa kuendesha usasi, Serikali isaidie zaidi kutoa nyenzo za usasi kama kuongeza idadi ya silaha na risasi katika ofisi za Wilaya ambazo zitasimamiwa na Maafisa Wanyamapori wa Wilaya. Sehemu kubwa ya usasi wa wanyama wadogo wadogo kama vile nyani, ngedere, nguruwe na ngiri hufanywa kwa kutumia nyavu, mishale na mikuki. Lakini nyavu za kisasa ni ghali, zinauzwa kwa wastani wa Sh,80,000/= kila moja. Serikali ingetazama uwezekano wa kuwanunulia Wanavijiji vyavu za namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale ambapo Wananchi wamepoteza maisha au mali zao hata kupelekea tishio la njaa, Wizara iunde utaratibu wa kuwapatia Wananchi hao kifuta machozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, ni kuhusu Sekta ya Utalii. Ninaipongeza Wizara kwa kukuza utalii. Lakini naamini kuwa mapato yetu yanaweza kuongezeka zaidi kama tutaongeza mikakati ifuatayo: -

(a) Tuongeze matangazo yetu ya kitalii katika nchi ambazo kihistoria siyo zinazoleta watalii Tanzania. Nchi hizo ni pamoja na Japan, China na nyinginezo za Mashariki ya mbali. Ingawa Wajapani walioanza kuja nchini ni wachache sana. Soko la Marekani pia tunaweza tukalipanua.

(b) Tuhamasishe sana utalii wa ndani na wageni kutoka baadhi ya nchi za Kiafrika. Ingawa kwa sehemu kubwa mazingira ya nchi za Kiafrika yanafanana bado zipo tunazotofautiana nazo kama nchi za Sahel na Afrika ya Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na ninaunga mkono hoja.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na wataalam wake wote kwa kazi nzuri na hotuba inayoeleweka na ya wazi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa Mbunge wa Morogoro Kusini, sitakuwa mtu mwenye shukrani kama sitatoa neno la shukrani. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu, napenda kuishukuru Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kutengeneza barabara ndani ya Mbuga ya Selous hadi kambi ya Matambwe. Baada

ya hapo barabara hiyo imeendelea hadi Milengwelengwe. Hivyo, imeweza kutengeneza madaraja saba ya *Kisaki Station* na daraja kubwa la Mgeta kafa. Tunashukuru sana kwa msaada huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni kuhusu pori la wazi la kuwinda la Ngerengere hadi Tununguo na Selembala. Pori hili linapakana na pori katika Mbuga ya Selous, Serikali kuliweka wazi kwa uwindaji ni sawa, lakini matumizi ya pori hili ni baya sana. Jeshi la wananchi linapiga wanyama malori kwa malori bila kiwango. Wawindaji humiminika na kupiga bila mfano! Kwa kuwa wanyama wa *Selous* hawajui kupigwa hivyo hupigwa ovyo ovyo katika pori hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba eneo hili la uwindaji wazi la Ngerengere ligeuzwe liwe pori la kupiga picha. Mbuga hii inaweza ikaingiza mapato makubwa sana kwa Wananchi na Serikali na hivyo kuwatendea haki wanyamapori. Suala hili ni muhimu sana na nipo tayari kuwa mstari wa mbele kusaidia hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninaunga mkono hoja.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na utekelezaji wa Wizara yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Wizara iangalie uwezekano wa kulifanya pori la Mgori (Singida Vijijini) kuwa Hifadhi ya Taifa chini ya *TANAPA*. Pori hili lina wanyama wengi na uoto wa asili usiopatikana popote duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kwamba pori la Itigi lenye wasifu wa pekee liwe Hifadhi ya Taifa. Pia, napendekeza itengenezwe *Tourism Corridor* chini ya *TANAPA* itakayounganisha Bonde la Ufa la Afrika Mashariki (Arusha, Manyara na Singida).

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Zakia Meghji, Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa hotuba yake nzuri sana yenye takwimu muhimu na ambayo ameisoma kwa ufanisi wa hali ya juu.

Aidha, napenda kuwapongeza Bwana Salmon Odinga, Katibu Mkuu, pamoja na wasaidizi wake Wizarani na katika Asasi chini ya Wizara hiyo kwa kufanya kazi kwa juhudi, uadilifu na ushirikiano mkubwa ambao umeweza kuijengea Wizara heshima humu Bungeni na kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema Wizara iendelee na juhudi zake za kuhakikisha kwamba hoteli ya *Novotel (Mount Meru)* inapata mwekezaji makini na aliye na uzoefu wa kuongoza na ku-*manage* hoteli kubwa. *AICC* ingeungwa mkono ili iweze kusimamia hoteli hiyo na kuihusisha na *program* zake za mkutano. *AICC* ingeweza kutafuta mbia. Hoteli hiyo ni *critical* kwa shughuli wa ushirikiano wa Afrika Mashariki. *AICC* ina mali nyingi zinazoweza kuwa kinga ya mikopo.

**MHE. ESTHERINA KILASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Maliasili na Utalii kwa kazi nzuri ambazo amekuwa akifanya. Vile vile, nampongeza kwa hotuba nzuri ambayo amewasilisha, bila kumsahau Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na watendaji wake kwa kuleta ufanisi mzuri katika kuongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo langu la uchaguzi la Mbarali, wanafurahi na kushukuru kwa mchango mzuri unaofanywa na Shirika la *TANAPA.*Katika Sera ya ujirani mwema wamesaidia vizuri sana hasa kukamilisha ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Madibira iliyoko Kata ya Madibira inayopakana na Hifadhi ya Ruaha na sasa wanaendeleza ujenzi wa hosteli kwa ajili ya Shule hiyo. Kwa hiyo, napongeza sana. Wananchi wamekuwa walinzi wazuri wa majangili.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna matatizo yanayojitokeza eneo la vitaru vya uwindishaji *(Usangu Game Reserve)* kuhusu mipaka iliyowekwa. Inaonekana Wananchi wanaoishi kuzunguka hifadhi hii ya wanyamapori wanaomba irekebishwe kidogo kutokana na kuongezeka idadi ya watu, ongezeko la mifugo ya ng'ombe hadi kufikia 600,000 na kukumbwa na tatizo la malisho ya maji wakati wa kiangazi kumefanya wakimbilie maeneo ambayo yanazunguka hifadhi hiyo. Kwa hiyo, ufumbuzi wa haraka unatakiwa.

Aidha, njia ya kuwatafutia maeneo ambayo watakuwa na uhakika wa maji kwani mpaka sasa bado wanaingia katika maeneo hayo kwa kujificha. Kwa hiyo, naomba ushirikiano wa karibu na haraka ili tutatue tatizo hili na utatuzi uwe wa kudumu, hasa ukizingatia kuwa Wananchi wanaona umuhimu wa kuwa na vitaru hivi vya uwindishaji kwani faida yake wameanza kuiona. Halmashauri pekee uwezo wake ni mdogo sana kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa ufugaji nyuki, nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwani nilipochangia Bajeti iliyopita ya 2002/2003 alianza utekelezaji mapema kwa kutoa majibu ya hoja yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumwomba Mheshimiwa Waziri kuhusu suala hili. Wataalam waletwe, wakae pamoja na wataalam walioko Halmashauri ili utafiti wa kuainisha maeneo yanayofaa kufuga nyuki na mbegu bora ya nyuki wanaofaa kufugwa ufanyike kusudi Sekta hii iendelezwe na wananchi wanaoshughulika na Sekta hii wapewe elimu ya ufugaji bora wa nyuki. Mpaka sasa kuna Kata tatu ambazo zina maeneo ya ufugaji wa nyuki nazo ni Kata za Msangaji, Chimola na Mawindi. Kama haiwezekani basi wawezeshwe tu ili wafanye ufugaji wa nyuki kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kumuomba Mheshimiwa Waziri ni ofisi za wafanyakazi wa *Game Reserve* ya Usangu kwani ziko mbali na maeneo ya hifadhi na ni ofisi za kupanga. Kulikuwa na mpango wa kujenga ofisi za kudumu zitakazokuwa karibu na maeneo haya ya uwindishaji ili iwe rahisi kutatua makosa madogo madogo kwa urahisi, ningependa kujua Mheshimiwa Waziri amefikia wapi.

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, njia mojawapo ya muhimu ya Benki Kuu kujua kiasi cha fedha za kigeni zilizoingizwa na Sekta ya Utalii ni kukusanya takwimu za *Bureau de Change*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo uzoefu unaonyesha kwamba hizo *Bureau de Change* taarifa hii si sahihi kwa sababu hata Watanzania wanaopata mishahara yao na malipo yao humu nchini kwa fedha za kigeni wakienda kubadilisha fedha hizo *Bureau de Change* wao hujaza kwenye nafasi ya utalii, kumbe hawa si watalii. Pia, yapo mabadilisho ya fedha za kigeni mengi ya aina hiyo! Sasa hali hii inapotosha na kuongeza fedha za kigeni zinazoonyeshwa kupatikana na nchi kutokana na Sekta ya Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara/Serikali ichukue hatua za kukabiliana na tatizo hili ili tusiendelee kuonyesha fedha nyingi za kigeni toka kwenye utalii kumbe sivyo.

**MHE. OSCAR T. MLOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Maliasili na Utalii kwa hotuba yake nzuri ya bajeti ya Wizara yake iliyojaa matumaini mengi. Kutokana na hilo, natanguliza kusema kuwa naiunga mkono hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, sasa naomba nijielekeze kwenye hoja kutoa mchango wangu katika kuboresha maudhui yaliyomo. Katika Bajeti ya Wizara ya mwaka 2001/2002, Waziri alizungumzia mpango wa kutoa Hifadhi ya Taifa kwa Milima ya Uluguru ili kunusuru maisha ya viumbe hai waliopo na uhifadhi wa misitu inayotupatia vyanzo vya maji safi na salama kwa Mikoa ya Morogoro, Dar es Salaam na Pwani. Hapa ningependa Mheshimiwa Waziri anieleze mpango huu sasa umefikia wapi na ni nini matumaini ya baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utalii, napenda niipongeze Wizara kwa jitihada zake za kutangaza hazina tuliyonayo nchi za nje kupitia Balozi zetu. Pia, kitendo cha kushiriki kwenye maonyesho katika nchi za Afrika Kusini, Australia, Japan, Marekani na Korea ni changamoto tosha kabisa katika

jitihada za kujitangaza. Bodi ya Utalii iendelee na mikakati yake iliyojiwekea ya kutafuta Wakala wawakilishi katika masoko ya zamani na mapya kama ilivyoyaainisha kama inavyoonekana kwenye hotuba ya Waziri mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache napenda kurudia tena kusema naiunga mkono hoja ya kupitisha Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa asilimia mia moja.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani kwa Wizara yako chini ya Mkurugenzi wa Misitu kwa kushirikiana na *NGO* ya *Coastal Women Environment, Conservation and Poverty Alleviation (COWEPO)* katika kupanga na kutekeleza mradi wa nyuki. Naomba mhusika wa Wizara aliyepewa jukumu la kushirikiana na *COWEPO* awe *serious*. Mradi unaenda polepole kwa sababu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba wakati Mheshimiwa Waziri ana-*windup* atusaidie kutueleza ufumbuzi wa mradi wa kufuga samaki katika mashamba ya mpunga. Mradi huu ulipitishwa na Halmashauri ya Kibaha, lakini tukakwamishwa na Wizara ya Kilimo kwa sababu mradi huu unashirikisha Wizara mbili (Kilimo na Utalii). Naomba Wizara hii iwe na kauli ya mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utalii Mafia, watalii wengi hasa wale wanaopenda *diving* na kuona viumbe vya majini wangependa/wanapenda kwenda Mafia kuona *coral leaf* ya aina yake ambayo ni ya aina chache duniani, lakini kwa kukosa njia ya uhakika kufika Mafia hata watu wa simu wanashindwa kwenda Mafia.

Namwomba Mheshimiwa Waziri awasiliane na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ili kujenga gati Mafia. Mheshimiwa Waziri atakuwa ameisaidia sana CCM katika ushindi wake 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu simba Rufiji, pamoja na jitihada kubwa ya Wizara yake, lakini simba wala watu bado hawajauwawa. Naomba nguvu na utaalamu wa ziada utumike.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usimamizi na uendelezaji wa mashamba ya miti, moja ya mpango wa *COWEPO* wa muda mrefu ni kuwashawishi Wananchi kuwa na mashamba ya miti na kufuga nyuki. Je, Wizara inaweza kushirikiana na *NGO* hii *(COWEPO)* ili mradi huu uweze kutekelezeka? *NGO* hii imeweza kuwahamasisha Wananchi wa Mkoa wa Pwani kupanda miti na kuidhamini, waliweza kufanya hivyo kwa mradi wao wa Panda miti kuzunguka shamba lako ili jirani yako asikuibie neo la shamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Wananchi wa Mkoa wa Pwani wanapanda sana miti kuzunguka mashamba yao. Pia ukiweka vibaya au bila ya ulinzi miche ya miti itaibiwa! Hii inaonyesha kuwa sasa watu wanathamini miti. Miradi wa Kufuga Nyuki Rufiji imefanya Wananchi wengi wapande miti ili wapate mashamba ya miti. Kwa hiyo, naomba Wizara ishirikiane na *COWEPO*.

**MHE. ALI SAIDI SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu unaonyesha kuwa wapo wafanyakazi na wananchi wa kawaida ambao walipata athari ya kuumizwa au kufa kutokana na kushambuliwa na wanyamapori katika nyakati tofauti. Ni vyema Serikali kupitia Wizara hii ikatenga fungu maalum la kutoa fidia kwa watu wa namna hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Wananchi kutozwa kodi zaidi ya mara moja kwa mradi mmoja limekuwa ni kero kubwa kwao. Nashauri Wizara kuliangalia kwa makini suala hili ili kuwapunguzia Wananchi wetu kero zisizokuwa na sababu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Kata Mti Panda Mti ni vyema ikasimamiwa na Wizara ili kuona Wananchi wanashirikishwa kikamilifu katika zoezi hili ili kuimarisha misitu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na taarifa mbalimbali na za mara kwa mara juu ya kuibiwa kwa watalii. Suala hili linaitia aibu nchi yetu mbele ya uso wa Kimataifa. Nashauri Wizara kuchukua hatua madhubuti za kuhakikisha usalama wa watalii na pia kuchukuliwa hatua kali wale wote watakaopatikana wanawaibia watalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara kuchukua hatua za dharura katika kukabiliana na janga la Ukimwi ili kunusuru maisha ya wafanyakazi wa Wizara ambao wamesomeshwa kwa gharama kubwa ya jasho la Watanzania.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi kwa hotuba nzuri na kazi nzuri inayofanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa mapendekezo yafuatayo baada ya kusoma hotuba ya Wizara ukurasa 1 hadi 15.

Tanzania itumie jiografia yake kama mgodi usioondosheka, mbuga, milima, bandari, maeneo ya kihistoria, maziwa na kadhalika. Tujenge miundombinu ili kuvutia wawekezaji na watalii kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, *hinterland* yetu inapakana na Uganda, Rwanda, Burundi, Kongo, Zambia na Malawi, lakini hatuitumii kikamilifu! Afrika ya Kusini kwa kushirikiana na Zambia wanajenga Bandari ya Mpulungu *(Lake Tanganyika)* na reli ya kuunganisha Mpulungu na stesheni ya Kasama katika *TAZARA* ili wachukue biashara yote ya nchi za Maziwa Makuu na Uganda na kuua reli ya kati na Bandari ya Dar es Salaam.

Wizara hii ishirikiane na Wizara nyingine ili kujenga barabara, bandari, reli na barabara za kuunganisha Tanzania na nchi za jirani ili Tanzania ifaidike kutokana na mahali ilipo na kwa Wizara hii kwa kushirikiana na nchi husika ijenge majumba ya makumbusho katika maeneo ya makambi ya wapigania uhuru kutoka Zimbabwe, Angola, Namibia, Afrika ya Kusini, Msumbiji na kadhalika ili yatumike kama maeneo ya Hija kwa raia wa kutoka nchi hizo (Kongwa, Mgagao, Mazimbu, Dakawa, Kurasini, Nachingwea, Bagamoyo na kadhalika).

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ijenge mnara wa kumbukumbu ya Nyumbanitu na Kwilongo, chimbuko la makabila ya Nyanda za Juu za Kusini na pia mkazo uwekwe katika ujenzi wa vituo vya mikutano, viwanja vya michezo na viwanja vya ndege ili kuvutia wageni na kupata fedha ya kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiundwe chombo maalum ili kuhamasisha wawekezaji katika maeneo haya ya kitalii kwa kutumia jiografia yetu. Tukizubaa, tutapuuzwa na kuachwa nyuma kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jiografia yetu na historia yetu ni mgodi usioondosheka. Wizara ikiwekeza katika maeneo haya itakuza sana mapato kutokana na utalii, niko tayari kufafanua mapendekezo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nyumbani (Kibena) maana yake ni nyumba nyeusi. Nyumbani tu ni eneo la msitu wa asili wenye ukubwa wa ekari mbili. Hili ni eneo la matambiko ya jadi ya watu wa koo za Fute, Kiswaga na Mkongwa. Fute, Kiswaga na Mkongwa ni watu wanaotokana na kizazi cha Kahemele.

Historia ya Nyumbanitu inaonyesha kuwa wWatu wajulikanao kwa jina la Wangulube waliishi katika eneo la Nyumbanitu kabla ya miaka ya 1400 A.D. Kipindi kati ya mwaka 1400-1412 Wangulube walihama Ukinga kutokana na ukame na mwaka 1400 watu waitwao Wategeta kutoka lango la Mto Rufiji walihamia Nyumbatu kupitia mabonde ya Mito Rufiji, Kilombero na Ruhudji hadi walipofika kwenye chanzo cha Ruhudji na kuhamia katika msitu wa Nyumbanitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakiwa Nyumbanitu walizaana na kusambaa kuelekea pande zote za dunia wale walioelekea Magharibi waliitwa Wakinga, Kusini, Wapangwa na Walusi, Kaskazini Wahehe asilia, Kaskazini-Magharibi, Wasangu na wengine kuendelea hadi Tukuyu. Wanyakyusa, Undali, Wandali, Karonga (Malawi) Wakaronga na kadhalika. Baada ya muda wengine walirudi Rufiji na wengine Morogoro.

Katika kipindi kati ya 1600 na 1670 (1700), kundi la watu wa Kyando lilihamia Ukinga kupitia Nyumbanitu kutoka Ilongo, kundi la watu wa koo za Kihaule, Mlelwa, Mtweve, Mahenge-walihamia Ukinga kutoka Ilongo kupitia Nyumbanitu, kundi la ukoo wa Sanga kutoka Ilongo walihamia Ukinga

kupitia Nyumbanitu na kundi la Mbena kutoka Idete kupitia Ilongo na Nyumbanitu kuelekea Liganga Upangwa na baadaye kurudi tena Nyumbanitu.

Msitu wa asili wa Nyumbanitu uko kilomita 20 Kaskazini Magharibi katika barabara itokayo Njombe mjini kuelekea Iyayi (Njombe) na unatunzwa na Ndugu Msigwa mtoto wa Vangameli Msigwa chini ya usimamizi wa Mzee Daniel Kiswaga, ambaye anafahamu kwa undani historia ya Nyumbanitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafadhali sana ningependa kujua Serikali ina mikakati gani ya kuenzi na kutunza makambi ya wapigania Uhuru katika Tanzania ili kutunza kumbukumbu za mchango wa Watanzania katika ukombozi wa Bara la Afrika. Viongozi maarufu kama Nelson Mandela, Robert Mugabe, Hayati Oliva Tambo, Joshua Nkomo, Samora Machel, Mkuu wa Pili wa Jeshi la Afrika Kusini na kadhalika waliwahi kuishi katika makambi yaliyoko Tanzania. Mwaka 1964 Hayati Julius Nyerere, alitoa ardhi ya Tanzania Kongwa kwa *OAU* kama eneo la wapigania uhuru wote wa nchi za *SADC* na wote waliishi Kongwa katika siku za mwanzo. Kwa nini Serikali isijenge kumbukumbu Kongwa na mahali pengine?

Kwa nini Watanzania tupoteza historia ya bara hili na ya nchi yetu? Tazama mifano ya makambi ya ukombozi hapa chini. Kongwa Dodoma – Afrika ya Kusini, Namibia, Angola, Msumbiji, Zimbabwe mwaka 1964, Mugagao - Wilaya ya Kilolo Iringa, Zimbabwe, Afrika ya Kusini, Mandela, Mugabe, Nkomo, Mazimbu (Morogoro) Afrika ya Kusini, Dakawa (Morogoro) Afrika ya Kusini na Tunduru – Msumbiji na kadhalika.

Kwa nini Wizara yako isishirikiane na nchi husika, kujenga *monument* za kumbukumbu katika maeneo haya na kufanya utafiti wa majina?

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wa wapiganaji wangali hai kama viongozi wa Afrika ya Kusini, Msumbiji na Namibia wameonyesha nia hiyo lakini wanasubiri sisi tuanze. Hii pia ni njia ya kukuza utalii.

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii ningependa kupata maelezo kuhusu yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mambo ya kale kule Tabora kuna Tembe la Kwihara na Makazi ya Mtemi Milambo (Iselamagazi). Wizara inayafanyia nini? Inaonekana Tembe la Kwihara ameahidiwa Mzee anayeishi hapo na Iselamagazi zamani lilitunzwa na Wanajeshi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Hivi sasa mambo yakoje?

Chuo cha Maliasili (Nyuki) Tabora hakitumiki ipasavyo, je, ubadhirifu wa miundombinu hii inaonekanaje machoni mwa Wizara hii? Je, Mkoa unaruhusiwa kuyatumia vinginevyo?

Misitu ya Hifadhi hasa hasa Ipala ni mwiba uliotukwama kooni Wilaya ya Nzega na Mkoa wa Tabora kwa jumla; kwa kuwa Wananchi wanaendelea kurejea ndani kila wanapohamishwa, je, Wizara ya Maliasili na Utalii haiwezi kufanya utafiti yakinifu wa sababu, kiini cha baadaye tatizo litatuliwaje ili utekelezaji usionekane kuwa kero kama kero nyinginezo tunazozitoa kama vile Kodi ya Maendeleo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naunga mkono hoja na nina haya ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wanajimbo la Mtwara Vijijini, tunaomba tujulishwe kinachoendelea kuhusu Shamba la Mkonge la Kabisera juu ya mzozo wa Wananchi na mwekezaji kwamba mwekezaji anataka kuligeuza shamba hilo zoo ya kufugia simba, chui na kadhalika na Wananchi hawalitaki hilo wanataka ardhi itumike kwa lengo lililoombewa ardhi hiyo yaani kilimo cha mkonge. Kama kilimo hicho kinashindikana ardhi irudishwe kwa wakazi walime mtama, muhogo na korosho. Wananchi wanapenda kujua kinachoendelea na msimamo wa Serikali katika mzozo huu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *Marine Park* Mwambao mwa Jimbo la Mtwara Vijijini katika Vijiji vya Msimbati, Nalingu, Mnawene, Mnazi, Msangamkuu na kadhalika. Wiki tatu zilizopita magazeti yalitangaza kutiwa ndani kwa Wanakijiji wa Nalingu zaidi ya 300 na kutishia kurudisha kadi za CCM wanachama zaidi ya 2000. *DC* pamoja na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mtwara Vijijini na wataalam wa *Marine Park* walifanyiwa fujo walipokuwa mkutanoni huko Nalingu. Sababu ni kwamba Wananchi wa Nalingu hawataki *Marine Park.*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Nalingu wameambiwa kuwa *Marine Park* itawazuia kuvua, kuchokoa na kupita hata kutumia bahari yao na kama wakitumia watafungwa pia kama wataruhusiwa ni kwa masharti mazito na kwa sehemu fulani fulani tu. Pia, watakuwa wavuvi wa madema na aina nyingine watalazimika kuacha na kuvua kwa nyavu inchi kuanzia tano na kadhalika. Tatizo lao wao hawana *boat* za kisasa, nyavu inchi tano zinahitaji maji marefu watafikaje?Kumbadilishia ghafla mvuvi aina ya uvuvi aliozoea bila mafunzo huko unakomuhamishia itawezekana wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, wameambiwa watafute njia mbadala ya kujipatia kipato hii maana yake nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaomba Serikali iwafafanulie mipaka, haki zao na ustawi wao wa baadaye dhidi ya kushamiri kwa mradi huu wa *Marine Park*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nashauri wapelekwe Mafia haraka sana wakajifunze kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DR. BATILDA S. BURIAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Zakia Meghji, Katibu Mkuu na timu nzima ya wataalam, kwa kazi nzuri ambayo Wizara inaifanya na hasa kwa hotuba hii nzuri ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi ningependa kuchangia kwa maandishi katika maeneo machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuhusu Sekta ya Misitu. Kusema kweli pamoja na kupitishwa kwa Sera na Sheria ya Misitu hali ya uvunaji ovyo wa mazao ya misitu na uchomaji moto umekuwa mkubwa sana. Nilitegemea katika Bajeti hii kuwepo kwa kipaumbele cha pekee kwa Sekta hii ili kuwezesha zoezi la doria kwa kuongeza watumishi ambao ni wachache sana katika Sekta hii.

Pia, wataalam wengi wanaohitimu *SUA,* Kitengo cha Misitu ni wachache sana ambao wanapata ajira. Naomba Wizara ihakikishe kwamba wale wote wenye mashamba ya misitu iwe Taasisi, Serikali za Wilaya, Kijiji au hata mtu binafsi wanaajiri wataalam wa misitu. Hii iwe ni sharti la muhimu kama ilivyo kwa wafugaji, wenye maduka ya dawa na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Utalii hii ni muhimu sana na ina mchango mkubwa sana kwa uchumi na maendeleo ya wananchi kwa ujumla.

Pamoja na jitihada kubwa Serikali na Wizara hii iliyokuwa ikifanya, bado Sekta hii ina fursa kubwa ambayo ikishughulikiwa inaweza kuwa na mchango mkubwa zaidi katika Pato la Taifa. Maeneo ambayo yanahitaji kushughulikiwa ni kama ifuatavyo: -

(a) Kushughulikia miundombinu inayo *support* Sekta hii. Nashukuru kwamba Wizara imeshirikiana na Wizara ya Ujenzi na Sekta nyingine katika ujenzi wa barabara ziendazo kwenye vivutio vya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, nashauri hatua ya pili inayotakiwa kuchulikuwa ni kuhakikisha kwamba miundombinu ya mawasiliano inaboreshwa. Wizara hii kwa kushirikiana na ile ya mawasiliano

ihakikishe kwamba inawasaidia watoa huduma za utalii kupata mtandao wa *Internet* (tovuti) ya uhakika, kwani kwa sasa *bookings* nyingi zinafanywa kupitia *Websites.*

Vile vile, kuhakikisha kwamba (kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano) huduma za simu za mikononi au na zile *fixed* zinafika katika maeneo yote ya utalii.

(b) Jambo lingine ni usambazaji wa habari na taarifa muhimu kupitia vipindi vya redio, *Television,* vipeperushi na hata kwenye Tovuti ya Taifa na ile ya Bodi ya Utalii. Pia, ni muhimu taarifa za muhimu za nchi kwa ujumla zipatikane kwenye Tovuti ya Taifa ili hata hawa *operators* binafsi waweze kuweka *link* kupitia *website* zao ili wageni walio nje waweze kupata taarifa za nchi.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie uwezekano wa kuwasaidia wananchi hasa vijana na akina mama wenye uzoefu na utaalam na shughuli za utalii kupitia vikundi vyao. Jitihada hizi za Serikali zitasaidia sana kupunguza wakala bandia *(flycatchers)* ambao wanatia hofu na woga kwa wageni wanapoingia nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo uwezeshaji huu utawafanya vijana wawe na ajira na hivyo kupunguza wizi na ukosefu wa uaminifu wanaofanyiwa baadhi ya wageni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache napenda kusema ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. MWADINI ABASS JECHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kushukuru kupata nafasi ya kuchangia katika hotuba hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ninauelekeza kwenye sekta ya wanyamapori. Kama tunavyofahamu kwamba biashara ya utalii wa wayamapori imeshamiri duniani. Hapa kwetu Tanzania Serikali imefanya juhudi kubwa kuwekeza katika utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, utalii wa wanyamapori umekuwa ni kivutio kikubwa kwa watalii. Kadhalika utalii ho unaipatia nchi fedha nyingi za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tukiri kwamba matatizo mbali mbali yamekuwa yakijitokeza yanayosababishwa na wanyamapori. Imekuwa ni jambo la kawaida kusikia katika vyombo vya habari kwamba wanyamapori wamevamia vijiji. Matokeo yake huwa wanaharibu mazao, wanaua mifugo, wanaua na kujeruhi binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni tatizo na si jambo la hali hii ikaachwa kama ilivyo. Tatizo lingine ambalo pengine Serikali haijalitupia macho ni usambazaji wa maradhi ambao husababishwa na wanyamapori. Kuna maradhi ambayo wanyamapori huambukizana wenyewe kwa wenyewe, na pia kuna maradhi ambayo binadamu huambukizana na wanyama.

Maradhi ya mifugo kama *Anthrax, FMD, CBBP* na kadhalika huwa mara nyingi mlipuko wake huwa unatokana na wanyamapori. Kutokana na matatizo yanayosababishwa na wanyamapori nashauri Wizara kuwadhibiti wanyamapori kwa kuzijengea uzio hifadhi za wanyama hao wasiwe wanazurura ovyo. Kadhalika naishauri Wizara iwe inatoa fidia katika vijiji ambavyo wanyamapori wanafanya uharibifu na kusababisha hasara ya mali, mazao, mifugo na maisha ya binadamu.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii ili niweze kuchangia hoja ya Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Zakia Meghji.

Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa mawasilisho mazuri ya hotuba yake ya Bajeti. Hali kadhalika nawapongeza Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa maandalizi mazuri ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianzie mchango wangu kwa kuangalia kero zinazowakabili wananchi wanaoishi kwenye Kata zinazozunguka Hifadhi ya wanyama ya Lukwika-Lumesule ndani ya Jimbo la Nanyumbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ni wananchi kuuawa na wengine kujeruhiwa na wanyama wakali kama simba, chui, tembo na mamba ni jambo la kawaida sasa. Katika msimu wa 2002/2003 wananchi zaidi ya watatu wameuawa na wengine zaidi ya nane wamejeruhiwa na wanyama wakali kwenye vijiji vilivyoko katika Kata ya Napacho peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kero nyingine kutokana na wanyama kutoka Hifadhi ya Lukwika-Lumesule ni wananchi kukosa mazao baada ya mazao yao kushambuliwa na wanyama kutoka Hifadhi hiyo. Katika msimu wa 2002/2003 idadi ya ekari ambazo zimeshambuliwa na wanyama katika vijiji vitatu vya Kata ya Napacho ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahindi ekari 289, Muhogo ekari 253, Mpunga ekari 137 na Jamii ya mikunde ekari 96.5 na jumla ni ekari 770.5

Vijiji hivyo vitatu ni Mpombe, Mburusa na Chinuka. Hivi sasa wananchi hao wanakabiliwa na njaa baada ya mazao yao kushambuliwa na wanyama kutoka Hifadhi ya Lukwika-Lumesule.

Mheshimiwa Naibu Spika, uharibifu umekuwa mkubwa kiasi hicho kutokana na udhibiti mdogo wa uongozi wa Hifadhi kwa wanyama waharibifu. Aidha, wananchi wanapokwenda kutoa taarifa za uharibifu wa mazao askari wanyamapori huchelewa kuja kutoa msaada hivyo wanapokuja hukuta uharibifu mkubwa tayari umekwishafanyika.

Naomba Serikali kusambaza askari wanyamapori katika kila kijiji na wapewe silaha na risasi za kutosha ili kuweza kudhibiti wanyama waharibifu wa mazao na kulinda wananchi. Aidha, wananchi nao washirikishwe katika ulinzi huo kwa kupewa silaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kero nyingine ni kwa baadhi ya wananchi ambao mashamba yao yaliingizwa ndani ya Hifadhi na hadi leo hawajalipwa fidia ya mazao. Uongozi wa Hifadhi ngazi ya Wilaya ya Masasi unadai kuwa wananchi wote wamelipwa fidia lakini wananchi wenyewe na uongozi wa kijiji na Kata wanadai kuwa wananchi hao hawajalipwa fidia. Hivi sasa kuna wananchi 63 wa Kijiji cha Mpombe ambao wanadai hawajalipwa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya viongozi wa Kata ni kuwa mpaka wa Hifadhi ya Lukwika-Lumesule umesogezwa kwa mara tatu kuelekea Kijijini na kila awamu wananchi kadhaa mashamba yao yameingizwa ndani ya Hifadhi hivyo kustahiki kulipwa fidia kwa mazao yao. Wananchi ambao mashamba yao yalikumbwa kwenye mpaka wa kwanza wamelipwa fidia. Hali kadhalika wananchi ambao mashamba yao yalikumbwa kwenye mpaka wa pili nao wamelipwa fidia. Wananchi ambao mashamba yao yalikumbwa kwenye mpaka wa tatu ndiyo ambao bado hawajalipwa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachogomba ni baadhi ya majina kujirudia rudia kwenye orodha za awamu ya kwanza, pili na tatu, hivyo kuonekana kuwa wananchi hao wanataka walipwe mara mbili au tatu. Maelezo ya viongozi wa kijiji au tatu.

Maelezo ya viongozi wa kijiji ni kuwa kwa sababu mtu alikuwa anahama kutoka ndani ya mpaka wa kwanza na kuanzisha shamba lingine nje ya mpaka huo, wakati wa kuweka mpaka wa pili mtu huyo alijikuta akiwa ndani ya mpaka wa pili. Vivyo hivyo kwa mpaka wa tatu. Ikumbukwe kuwa mipaka hiyo haikuwekwa mwaka mmoja bali baada ya kipindi cha miaka kadhaa kupita. Nashauri Serikali sasa ikalifanyia uchunguzi wa kina suala la fidia wanaodai wananchi hao ili wawe na imani na Serikai yao vinginevyo wananchi wataona kama Serikali yao inawanyima haki yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hifadhi ya Lukwika-Lumesule inajumuisha eneo ambalo wananchi walikuwa wakichimba madini hasa Lumesule Chini. Baada ya kuanzisha Hifadhi wananchi waliondolewa eneo hilo hivyo kuwakosesha kipato kutokana na uuzaji wa madini. Uongozi wa Hifadhi umeruhusu uanzishwaji wa vikundi kwa ajili ya uvuvi, kurina asali, lakini hauruhusu kuanzisha vikundi vya kuchimba madini.

Naomba Serikali ikaruhusu wananchi kuchimba madini katika eneo la Lumesule Chini ili wajipatie kipato na hasa ukichukulia kuwa kilimo ni hasara tupu kutokana na wanyama kushambulia mazao yao. Nina hakika madini yangekuwa kifuta jasho lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, bada ya hayo naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Mwisho nashukuru tena. Ahsante sana.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, maporomoko ya Kalambo hayajatiliwa maanani wakati nchi jirani ya Zambia imeyatumia kama kivutio cha watalii. Halmashauri ya Sumbawanga imetengeneza barabara nzuri kufika maporomoko hayo lakini Wizara yako haijaonyesha juhudi yoyote ku-*promote Kalambo Falls,* yapo pia maporomoko ya maji ya Lyanji ni makubwa lakini hayajulikani.

Ngome ya Kasanza ya Bismark inazidi kuharibiwa hakuna chombo cha kulinda ngome hii Wizara ya Elimu na Utamaduni haijaonyesha nia ya kuhifadhi ngome hii isipokuwa chini yake ni matumaini yangu utaona umuhimu wake na utusaidie tuilinde ngome hii kulinda historia ya Wajerumani katika nchi hii isipotee kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uvuvi katika Ziwa Tanganyika, adha ya wavuvi kuibiwa na wezi toka *DRC* vifaa vyao vya uvuvi hili unalifahamu. Samaki wengi wanauzwa Zambia wakavu na wabichi kisa hakuna soko la uhakika hapa nchini na kwa sababu hiyo tunapoteza mapato mengi mno kwa kutolipa ushuru kwani raslimali hii inatoroshwa Ziwani kwa ukosefu Maafisa Maliasili wenye zana za kufuatilia uvuvi Ziwa Tanganyika eneo la Mpakani. Tutaendelea kupoteza raslimali yetu hii mpaka lini? Naunga mkono hoja.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Zakia Meghji, kwa hotuba nzuri na kamilifu pia ninampongeza Katibu Mkuu pamoja na wataalam waliohusika na utayarishaji wa hotuba hiyo.

Awali ya yote naunga mkono hotuba hiyo 100%. Napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Waziri Zakia Meghji, kwa juhudi zake za kuboresha utalii karibu nchi nzima. Kwa upande wa Jimbo langu la Liwale ambako 53% ya eneo lake 39,000 *square kilometer* ni *Selous Game Reserve,* wananchi wanaendelea kufaidika/kunufaika na michango ya kimaendeleo, baraabara na hata ujenzi wa hosteli ya wasichana ya shule ya Sekondari ya Liwale, Wizara imechangia shilingi milioni 5. Napenda kueleza kwamba ujenzi wa hosteli hiyo umeanza kutokana na fedha hizo na unaendelea vizuri.

Mheshimiwa Waziri wakati wa ziara yako Mkoani Lindi 2001 uliwaahidi wananchi wa Liwale kwamba utawatembelea tena. Kwa niaba ya wananchi wa Liwale nakukumbusha kuhusu ziara hiyo naomba kupata jibu wakati wa majumuisho yako.

Mimi mwenyewe nikishirikiana na wananchi wa Liwale tutaendelea kushirikiana kwa karibu zaidi na Wizara yako pia na miradi ya *Selous* iliyopo Wilayani Liwale. Nampongeza pia Mkurugenzi Wanyamapori Ndugu E.L.M. Severre na Mkuu wa Mradi wa *Selous,* Ndugu Kibonde kwa ushirikiano mzuri tunaopata mara kwa mara kwa lengo la kuboresha miradi mbalimbali ya *Selous.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Liwale kihistoria ndiko kulikotokea chimbuko la vita vya Maji Maji ninakumbuka nilipokuwa Chuo Kikuu mwaka 1967/1968 Dar es Salaam nilitumiwa na Idara ya Historia kwenda kufanya utafiti wa vita vya Maji Maji Liwale kwa kutumia dodoso maalum. Pia kuna makaburi ya Wamisionari waliouwawa wakati wa vita vya Maji Maji katika eneo la Mikukuyumbu kijiji cha Kimambi kilomita 60 kutoka Liwale Mjini. Pia kuna Boma iliyojengwa na Wajerumani ambayo hivyo vyote Mheshimiwa Waziri uliviona wakati wa ziara yako ya 2001. Moja ya shughuli zote nzuri na uwindaji wa kitalii wananchi wa Liwale wanakuomba Mheshimiwa Waziri kumbukumbu hizo kihistoria zitumike katika kutangaza utalii kusini na Boma ya Kijerumani lihusishwe kwa kuboresha miundombinu ili yaweze kuwa vivutio vya utalii.

Mheshimiwa Waziri pamoja na ushirikiano tunaopata kutoka mradi wa *Selous Game Scouts* kudhibiti wanyamapori wanapowashambulia wananchi na kuwauwa bado usalama wa maisha ya wananchi na mazao ni wa kutia wasiwasi mwaka hadi mwaka. Naomba Wizara iongeze nguvu kwa kuongeza idadi ya *Game Scouts.* Pia uongozi uchukue hatua za haraka kwa kwenda maeneo ya matukio ambayo wananchi wamepoteza maisha kwa kuuwawa na wanyamapori. Hii itaondoa dhana kuwa Wizara inajali wanyamapori zaidi kuliko wananchi.

Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho yako ni vema ukatoa pole kwa wananchi waliopoteza maisha yao nchini kote kutokana na wanyamapori ikiwemo Liwale na kadhalika. Napelea kusema naunga mkono 100% kwa mara nyingine. Ahsante.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu nichangie hoja hii iliyoletwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri ya Bajeti.

Nianze na kuunga mkono hoja hii kwa sababu ya mafanikio yaliyojitokeza katika sekta za Misitu na Nyuki, Uvuvi, Wanyamapori, Utalii, mambo ya Kale na Taasisi za Tafiti mbalimbali. Aidha, natoa pongezi zangu kwa Chuo cha Mweka kutimiza miaka 40 tangu kianzishwe. Hali na madhari ya chuo hiki ni ya kuvutia. Nashauri hali hiyo iendelezwe, ili asasi hiyo iendelee kuwa mfano wa kuigwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia eneo la ushirikishwaji wananchi kwa jumla lakini hasa katika maeneo ya Jumuiya ya Uhifadhi wa wanyamapori. Wizara imeandaa utaratibu na mwongozo wa kuendesha maeneo hayo na hili ni jambo nzuri. Lakini utaratibu wa kuchagua maeneo 16 ni mpango wa kurudisha nyuma hamasa ambazo wananchi wamekwisha pata nchi nzima. Nashauri maeneo ambayo wananchi wameamua kuanzisha maeneo kwa ridhaa yao waruhusiwe na iwe ni jukumu la Serikali kuwawezesha. Mheshimiwa Waziri anakumbuka ombi la Mheshimiwa Bakari Mbonde, aliuliza maeneo ya ushirikishwaji katika jimbo lake yapanuliwe.

Mheshimiwa Waziri maombi kama haya yapo kila mahali hasa yale maeneo ambayo hayana hadhi ya kuuhifadhi lakini yana raslimali. Wizara vile vile ikubali kuwashirikisha wananchi wa maeneo ya Jumuiya ya Uhifadhi wanyamapori katika kugawa vitalu vya uwindaji, utaratibu wa sasa hauonyeshi ushirikishwaji wa wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ninalotaka kuchangia ni biashara ya meno ya tembo. Wakati Mheshimiwa Waziri anajibu swali Namba 278 la tarehe 21 Julai, 2003, sikupata nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Namwomba Mheshimiwa Waziri atakapojumuisha atoe maelezo katika maeneo yafuatayo:-

(a) Meno ya tembo yanayohifadhiwa yana uzito wa tani ngapi na yana thamani gani na kama thamani hiyo inaongezeka au inapungua ili kuweza ku-*justify* gharama hizo?

(b) Mheshimiwa Waziri nakupongeza kwa kuwa na mpango mahususi wa kudhibiti ujangili wa tembo. Lakini mpango huo ili uwe bora lazima uwe na kipindi *(time frame)* ili kuwezesha tathmini kufanyika, kwa lengo la kuharakisha uuzaji wa meno ya tembo?

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba wa *CITES,* unaweza ukawa ni chombo cha ukandamizaji kama nchi haitakuwa na msimamo kwa lengo la kutetea maslahi ya Taifa. Asasi hii inapojumuisha *NGOs* za Kimataifa kama *Animal Welfare Group* ambayo ina uwezo mkubwa wa kushawishi ili nchi kama Tanzania kupinga uuzaji wa meno, raslimali yake inabidi maandalizi ya kutosha na msimamo wa pamoja na nchi zenye tembo wengi kama Zimbabwe, Botswana, *South Africa* na Zambia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba kama shehena hiyo ingekuwa ya nchi kubwa kama Marekani shehena hii ingekuwa imeuzwa. Tanzania sharti iwe na kauli katika hili, miaka 14 inatosha kutoa maamuzi kuhusu meno ya tembo. Ongezeko la tembo kutoka 52,000 hadi 83,000 ni kigezo tosha kwamba kumefanyika kazi nzuri kwa kipindi cha miaka 14. Nashauri kwamba meno haya yauzwe ili fedha hizo zitumike kuhifadhi tembo.

Mheshimiwa Naibu Spika, programu nzuri ya kuhifadhi tembo itahifadhi pia viumbe wengine ikiwemo misitu ya asili pamoja na maji.

Mwisho kama tunaona hakuna haja ya kuuza basi tujenge mnara wa meno ya tembo iwe kama kivutio cha utalii, badala ya kuendelea kuhifadhi meno kwa gharama na tahadhari *(risk)* ya kuibiwa.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la mchango wangu kwanza ni kumpongeza Waziri wa Maliasili na Utalii kwa jinsi anavyofanya kazi yake kwa kuimudu na kusimamia. Lakini pia Katibu Mkuu wa Wizara hii pia kuwashukuru wafanyakazi wote kwa kufanya kazi vizuri katika Wizara hii, hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwapongeza Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi kazi kwa zawadi mbalimbali walizozipata kwenye maonyesho ya Saba Saba kuhusu banda bora. Hii inaonyesha hali halisi ya uchapaji kazi na ushirikiano wenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekwisha mwandikia barua Waziri juu ya mbuga za wanyama za Lukwati. Tangu nimeingia Bunge nimeisemea sana mbuga ya wanyama ya Lukwati ambayo pengine kwa miaka ya karibuni imebaki kama Loliondo kwa jinsi wanyama walivyo wengi na jinsi eneo lenyewe lilivyo zuri kwa kuwa na wingi wa ndege na wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo ambayo nimemwandikia kuhusu kuboreshwa kwa mbuga zile za wanyama za *Lukwati Game Reserve.* Mheshmiwa Waziri naomba sana utupatie Meneja wa Hifadhi, ujenzi wa Ofisi na miundombinu na uwekaji wa mipaka ya hifadhi na kadhalika. Pia utupatie gari la Hifadhi ya Lukwati na mafunzo kwa wana kijiji kulinda hifadhi.

Kuhusu mahali pa kujenga Ofisi ya wanakijiji wa kijiji cha Kapalala/Kiminga wananchi wametenga eka 20 pale kijijini kwa ujenzi wa Ofisi. Lakini pia ujenzi wa uwanja mdogo wa ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wapo tayari kwa uzio wa ujenzi wa Ofisi hii na bila shaka huduma za barabara na nyinginezo kuboreshwa. Katika barua yangu nimeomba kusaidiwa juu ya matatizo ya maji katika vijiji vinavyozunguka mbuga hii hasa vijiji vya Gua - visima viwili na Kapalala, visima viwili.

Akinamama maeneo haya wanapata taabu sana kuweza kuchota maji. Huyafuata kwenye hifadhi jambo ambalo ni hatari sana. Lakini hata hivyo huyapata kwa kutumia muda mwingi. Kama nilivyokuomba, naomba sana Wizara yako itusaidie sana kupata visima katika maeneo haya. Naelewa utafikiria juu ya *Council* yetu kwa muda mrefu imeshindwa kabisa kutimiza katika tatizo hili.

Mwisho nakubaribisha katika Jimbo la Songwe hasa kuona mbuga hizi za Lukwati na maeneo mengine ya kale kama vile mlima Kwimba. Mlima ulitumika na *Chiefdoms* mbalimbali. Naomba pia Wizara iorodheshe maeneo ya utalii Mkoani Mbeya ambayo ni jiwe la Kimondo pale Mbozi, daraja la Mungu pale Tukuyu, maji moto Songwe, fukwe nzuri za Matema na Maleza (Matema/Kyela na Maleza/Songwe/Chunya), mbuga za wanyama za Lukwati na maeneo ya ukombozi ya Mazimbu kule Chunya na kadhalika.

Maeneo haya yangeboresha yanaweza kuleta watalii wengi na kuboreshwa kwa ajili ya watalii. Nitapenda uzungumzie juu ya utalii wa kusini na pia tatizo la kuwepo na mamba wengi katika ziwa la Rukwa, kwani imekuwa ni kero kubwa sana. Angalia pia juu ya uwezekano wa kuwapunguza.

Naunga mkono hoja hii lakini nipate maelezo juu ya matatizo ya mbuga za wanyama Lukwati uboreshaji wa utalii, kusini hususan Mbeya uvunaji wa mamba ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nashukuru *TANAPA* hasa Mzee Lusinde kwa kunipatia fedha za kuanza darasa moja, nimekwisha anza na ujenzi unaendelea. Naomba kupitia kwako kuwashukuru *TANAPA* juu ya msaada huo ingawa bado naomba tena msaada wa darasa lingine. Na pia wawindaji wapo nao wachangie mpaka sasa wapo kimya.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja na nawatakia watendaji wa Wizara utekelezaji mwema kwa malengo waliojiwekea kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa ushauri ufuatao. Katika utafiti wa mambo ya kale ni vyema Wizara ikafanya utafiti kuhusu vitu vya thamani ambavyo vilizikwa na Wajerumani mnamo mwaka 1917 na 1918 baada ya Wajerumani kuona kabisa watashindwa vita. Kuna maeneo ambayo yanajulikana kuwa kuna mali za thamani zilizikwa. Mali hii ikipatikana inaweza kukuza mapato ya Serikali.

Pia naomba Idara hii kwa kushirikiana na watalam wa nje hasa Amerika na Ulaya katika kufanya utafiti wa mali zilizozama na shehena ya madini na vitu vya thamani katika pwani ya Bahari ya Hindi. Pwani ya Afrika Mashariki ilianza miaka ya 500 AD kutembelewa na wafanya biashara wa Arabia, India, Persia na China. Ninaamini kabisa utafiti ukifanyika ninayo imani mali za thamani zinaweza kuibuliwa na zikauzwa kwa fedha nyingi ili kuboresha uchumi wetu.

Nawaomba sana mradi wetu wa Hifadhi Ardhi Shinyanga (Hashi), Serikali iendelee kuufadhili kwa kushirikiana na wafadhili. Kazi ya Hashi ni nzuri sana na inaendeleza uboreshaji wa mazingira. Pamoja na kwamba mradi huo ukawa chini ya Manispaa na Halmashauri zetu Serikali iendelee kuunga mkono mradi huu kwa nguvu zote. Matunda yake yameanza kuonekana kimataifa na kitaifa. Hashi inasaidia sana katika kuwahamasisha wananchi wa Shinyanga katika kutunza mazingira.

Nashukuru sana kwa ushirikiano wa Wizara yako kuhusiana na ushauri wangu.

**MHE. MARIAM SALUM MFAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja hii ya Bajeti kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa Bajeti ambayo imeandaliwa kwa uwezo wa hali ya juu na imeweka wazi utekelezaji wa kipindi kilichopita na imeonyesha mwelekeo wa Serikali na Wizara hiyo kwa kipindi kinachofuata. Naomba maelezo kwa mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ingewaelimisha wananchi hasa akinamama na vijana juu ya uchimbaji wa mabwawa ya samaki wa kufuga ili waweze kupambana na suala zima la kuondokana na umaskini. Mpango huu unatufaa sisi wa Dodoma.

Naipongeza Serikali kwa kuhimiza upandaji wa miti. Hata hivyo naishauri Serikali kutoa taarifa ya miti iliyohai na hata namna inavyotunzwa. Vile vile utaratibu wa kupanda miti utegemee majira ya mvua katika maeneo hayo, badala ya kufuata siku ya kupanda miti inayofanyika kwa nchi nzima.

Vile vile Serikali iangalie utaratibu wa kuwaelimisha akina mama na vijana juu ya upandaji miti kwa vikundi au watu binafsi kuwa na mashamba.

Naipongeza Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kusimamia utalii, naomba Serikali kuangalia utalii wa michoro ya zamanik iliyoko Kondoa katika Kijiji cha Muenia ambayo zamani ilikuwa na watalii wengi na sasa hawaendi tena. Tunaomba Serikali ilitangaze tena ili kusaidia Serikali kupata mapato.

Kwa suala la ufugaji nyuki naipongeza Wizara kwa juhudi inayofanya ila naishauri Serikali kuongeza juhudi ili zao hili lijitokeze kwa wingi hasa kwenye maeneo ya mapori na hususan kuelimisha wananchi kutengeneza mizinga ya kisasa. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba kumpongeza Waziri wa Maliasili na Utalii kwa hotuba yake na juhudi zake za kuendeleza na kuongoza Wizara hii. Ni Waziri anayejituma na anafanya kazi bila kuchoka. Kutokana na juhudi zake ameiletea sifa nchi yetu kwa kuhakikisha sekta ya Utalii inazidi kuimarika na kuiongezea kipato nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu nitauelekeza zaidi upande wa ufugaji nyuki na mazao yake yaani nta na asali. Mimi nilikuwa nikifuatilia kwa karibu sana utafutaji wa soko la asali na nta. Kwa

kuwa sasa hivi Watanzania wanajihusisha na ufugaji nyuki hasa hasa Mikoa ya Kigoma, Tabora, Singida, Arusha na kadhalika, wakati umefika wa kuhakikisha ufugaji huu unawapatia kipato cha uhakika.

Kwa sasa soko la asali ni kubwa, mfano Afrika ya Kusini, Ujerumani na Uingereza. Kwa mfano, Afrika Kusini wako tayari kupokea tani 3,000 kwa mwaka huu. Katika soko la Ulaya, ambalo ni kubwa, wako tayari kununua asali yetu ikiwa itakuwa na ubora wa kimataifa. Ni soko la ushindani. Tanzania inaweza kuingia katika soko hili ikiwa tutawahakikishia ubora wa asali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubora huu tutaufikia iwapo tutaweza kuwa na mashine za kuchuja asali na baadaye kuifanyia *analysis* kupitia maabara zinazotambuliwa kwa mfano, *APPLICA GmbH and Quality Service International GmbH,* zote za Ujerumani. Ni gharama kubwa kwa mtu binafsi lakini kama kungelikuwa na ushirika inawezekana. Hivyo ningelishauri kuwa na ushirika wa wafuga nyuki kwa mfano, *Tanzania Beekeepers Association* ili tuweze kupenya na kuingia soko la Ulaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa soko ni kubwa na ni msimu wa asali. Huko *United Kingdom* walikuwa wakinunua asali ya Zimbabwe. Lakini kwa sasa kutokana na mgogoro wa mashamba, hawachukui asali yao. Huu ndiyo ungelikua wakati muafaka kwa Tanzania. Nashauri Wizara iangalie uwezekano wa kuwapatia mikopo wafugaji ili waweze kununua mashine za kuchuja asali, kufunga *analysis* na kununua *container* maalum za kufungashia asali. Ninazo*Proforma Invoice* za mashine za kuchuja asali toka England. Serikali iwasaidie wananchi kuzipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa tayari kuonana na wataalam wa Wizara ili tuone ni namna gani tunaweza kuwasaidia wananchi kupenyeza katika soko la Kimataifa la asali na nta ili kujiongezea kipato na hivyo kinua Pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. Naitakia Wizara mafanikio na kuomba ushirikiano.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Naibu Spika, natanguliza pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Zakia Meghji, Waziri. Pia Bwana Solomon Odunga, Katibu Mkuu, pamoja na wataalam wao kwa jinsi wanavyoendesha vizuri Wizara hii pamoja na kushughulikia mara moja masuala yanayoletwa na Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Jimbo la Masasi, tumefaidika na msaada wa kuletewa greda ambalo limelima barabara zetu zilizo pembezoni mwa Hifadhi ya Wanyamapori wa Msanjesi. Natumaini mwezi ujao, Agosti greda litakuja kumalizia kazi hiyo inayoleta mshikamano mkubwa baina ya wananchi na Wizara ya Maliasili. Namshukuru Waziri na Wizara yake kwa ushirikiano huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimkumbushe Waziri kuwa ile kazi ya kuhamisha jiwe la mpaka katika Hifadhi ya Msanjesi kama tulivyokubaliana mwaka 2001 bado haijatekelezwa na Idara ya Wanyamapori. Tulikubaliana mpaka uhamishiwe ndani ya Hifadhi ili kuondoa utata uliopo kati ya Hifadhi na Kijiji. Suala hili tulikubaliana bila matatizo yeyote na hata Mkurugenzi wa Wanyamapori pamoja na mimi binafsi tulizungukia eneo hili kwa ndege ya Wizara na kuona vizuri zaidi ni nini hasa wananchi walikuwa wanakiomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ifanye marekebisho yanayohusika ili mpaka huu sasa uonekane rasmi. Naunga mkono hoja.

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri sana yenye mwelekeo na upeo mkubwa. Pia nampongeza kwa jitihada ambazo amezifanya hata Wizara hii muhimu kujulikana vizuri Kitaifa na Kimataifa na kuinua Pato la Taifa. Nasema kwa dhati kabisa hongera sana.

Mchango wangu katika Wizara hii ni kuwaomba wataalam wa Maliasili na Utalii walio karibu na hifadhi za Taifa, wawe watumishi waungwana sana hasa wakishirikisha wananchi walio kando kando na

maeneo ya hifadhi zetu. Hii ni pamoja na watumishi ambao huajiriwa na makampuni ya uwindaji ambao huwajali tu waajiri wao na kuwasumbua wananchi waishio karibu na maeneo ya hifadhi.

Aidha, wakuu wa makampuni ya uwindaji nchini washirikiane vizuri na Halmashauri zinazohusika na maeneo ya uwindaji ili kuboresha mahusiano na uhifadhi pia. Bado kuna haja kubwa ya kuelimisha jamii nchini ili jamii iweze kufahamu maana ya utalii na maliasili.

Napenda vile vile, kuwapongeza Mkurugenzi wa Utalii Ndugu Peter Mwenguo kwa kazi zake nzuri, Mkurugenzi wa Wanyamapori ndugu Emmanuel Severe, Mkurugenzi wa Misitu na Nyuki, Profesa Idd na wataalam wote walio chini ya Kurugenzi za Maliasili na Utalii kwa kazi zao nzuri na usimamizi wao wa siku kwa siku. Nasema hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, kwa maelezo hayo naunga mkono hoja ya Bajeti yako. Ahsante sana.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kwa njia ya maandishi kumpongeza dada yangu Mheshimiwa Zakia Meghji, Waziri wa Maliasili na Utalii, Katibu Mku pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa Bajeti hii ambayo imeonyesha uwajibikaji wa kiwango cha juu. Nasema hivyo kwa sababu wanajitahidi kusimamia sekta mbalimbali ndani ya Wizara yake na kukusanya fedha nyingi sana kwa watalii kutembelea vivutio mbalimbali zikiwemo mbuga za wanyama, uwindaji wa kitalii, ufugaji nyuki na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Wizara ina dalili zote za kujiendesha kulingana na mapato yake. Hivyo nina kila sababu ya kumpongeza sana Mheshimiwa Zakia Meghji, kwa umahiri wake na mshikmano na watendaji wake. Huu ni mfano wa kuigwa na yeyote yule anayeithamini nafasi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana serikali kwa juhudi za awali kwa kupeleka wataalamu Mkoani Singida kufanya tathmini ya vivutio vya watalii ni matumaini yangu kuwa tathmini hii itazaa matunda kwani vivutio vipo vingi tu ambavyo vinaweza kuwafanya watalii kuja kuona.

Mfano, Maziwa mawili yaliyoko Singida Mjini yaani Ziwa Singida na Ziwa Kindai yenye sura ya mvuto, hewa safi ya kimwambao, samaki wa aina yake na ziwa Singida hutoa chumvi nzuri ya chakula. Vile vile Mkoa una Ziwa Kitangiri, magofu yaliyoachwa na wakoloni, ambayo yapo huko Mkatama Iramba ya Mashariki, Misitu yenye miti mizuri na itoayo mbao na inayofaa kwa ufugaji wa nyuki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yangu tathmini hii wataalam wakimaliza basi watutafutie na kuwashawishi wawekezaji kuja kujenga hoteli za kimataifa/kitalii ili watalii wapate maeneo ya kufikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufanya hivi tutasaidia sana kuongeza Pato la Mkoa, Taifa, pamoja na vijana wetu kupata ajira. Vile vile naiomba Serikali itafute uwezekano wa kunusuru misitu iliyopo mkoani Singida kwani kuna dalili za kumalizika kwa ajili ya wananchi kuchoma mikaa na akina mama kukata kuni na kupata tabu ya kutembea mwendo mrefu porini.

Naiomba Serikali kushirikisha Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Nishati na Madini kuona uwezekano wa kupunguza gharama za umeme kwa *unit* ili wanawake waweze kutumia umeme kwa kupika. Hii itasaidia sana kunusuru misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile wanyama wengi wanahama na kutafuta maeneo mengine kwa sababu ya msitu kupungua kwa miti kukatwa. Hata suala la ufugaji wa nyuki Mkoa wa Singida upo sambamba hasa Wilaya ya Manyoni, Singida Vijijini na Iramba. Wananchi wanafuga nyuki baridi na nyuki wakali wote hao wanatoa asali nzuri sana kwa matumizi ya binadamu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali wafugaji hawa wapewe changamoto kwa kupewa mikopo ili kupanua ufugaji wao na kuufanya uwe wa kisasa zaidi. Hii itasaidia kuvuna asali nyingi na nzuri zaidi kwa kukuza vipato vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa asilimia inayotoa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni kutokana na uwindaji wa kitalii. Hii inasaidia sana kuendeleza miradi ya maendeleo ndani ya Halmashauri ikiwa ni pamoja na kutenfeneza barabara wanazopita wawindaji hawa na mingine mingi kwa faida ya Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huu, nirudie tena kwa kutamka rasmi kuwa naunga mkono Bajeti hii asilimia mia kwa mia. Nawatakia utekelezaji mwema. Ni matumaini yangu nitapata maelezo yenye kutoa faraja kwa wana Singida.

**MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwanzo wa kikao hiki nilikuandikia kuhusu malalamiko ya wananchi wa Nachingwea katika Vijiji vya Chimbendenga, Mtua, Kitongoji cha Liimbanyama (Mtua) na Matekwe kutokana na utekelezaji mbovu wa *project* ya *Game Reserve* ya Kipindimbi inayo-*overlap* kati ya Wilaya ya Masasi na Nachingwea. Sehemu kubwa ya eneo liko Nachingwea lakini uongozi wa Nachingwea hawahusishwi kikamilifu. Matokeo *Project Manager* yuko *closed up* Masasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wangu wa Vijiji nilivyovitaja hapo juu wananyanyaswa na *Project employees* kuwakataza kuteka maji katika eneo lao, kuwaacha wanyama waharibifu na wakali kuzagaa hovyo kwenye mashamba yao na kadhalika. Mheshimiwa Waziri hujanijibu.

Kuhusu *Royalty* ya mbao aina ya Mninga, Mkongo, Mvule na kadhalika ni juu mno. Wizara inachukua hatua gani?

**MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na wataalam wake kwa kutayarisha hotuba nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mawazo yafuatayo kuhusu Wizara hiyo, kwanza ni kuhusu utalii wa ndani. Ni jambo la wazi kuwa utalii wa ndani ni mchanga sana. Hii inatokana na sababu nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imetilia mkazo utalii wa mbuga za wanyama na baharini. Kwa wazalendo ambao idadi kubwa wanaishi vijijini na wanayo maisha duni, hawavutiwi na utalii huu. Kwa hiyo, iko haja ya kutafuta nyanja nyingine za utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, utalii unashamiri pale ambapo watu wana-*leissure time* au wanaweza kujitegemea muda wa kupumzika. Uchumi wetu ni duni kiasi hakuna ziada ya kutumia kwa utalii. Iko haja ya kujenga sera za uchumi za kuhakikisha hali hii inabadilika.

Kuhusu mambo ya kale, Wizara inatupa moyo katika jitihada zake za kuhifadhi mambo ya kale. Hata hivyo hili jambo likiachiwa Serikali tu, mambo mengine yataharibika kabisa. Kwa mfano, Magofu ya Kunduchi yanakaribia kupotea kabisa. Wananchi wa Kunduchi Mtakuja wako tayari kushirikiana na Serikali kuyakarabati na kutengeneza maktaba na makumbusho ya kuingia kwa Waarabu Dar es Salaam kupitia Kunduchi. Sehemu hiyo pia ni muhimu kihistoria kwa kuwa ndipo penye njia ya watumwa waliokuwa wanapelekwa pwani ya Kunduchi kusafirishwa kwenda Zanzibar na kwingineko.

Nashauri Serikali ikubali kuwateua wananchi wa Kunduchi kupitia *Kunduchi Mtakuja Development Associatoin* waendeleze na wasimamie magofu haya. Ipo pia haja ya kupata mawakala/wabia watakaokuwa tayari kukarabati magofu ya Kaole-Bagamoyo, Marungu-Tanga na Pangani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha *David Livingstone* kilichopo Kigoma Ujiji kina historia kubwa sana na kinahitaji matunzo ya karibu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kusikitisha kuona kuwa majengo ya zamani na ya kihistoria yanabomolewa na badala yake kunajengwa *concrete boxes.* Tunapoteza historia ya miji yetu,

kama maeneo ya barabara za *Garden, Ohio, Shaaban Robert* na *Ocean Road* za Dar es Salaam. Ikiwa iko haja ya kupanua Jiji, basi lipanukie kwa nje na sio majengo ya zamani yabomolewe. Mfano wa kuhifadhi mandhari ya zamani ni ujenzi mpya wa Mahakama ya Kivukoni (sasa Mahakama ya Biashara). Utaratibu huu ufuatwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na msimamo wa Serikali kuwa ujenzi usifanyike kiasi cha mita 60 kutoka ufukweni mwa bahari, jambo hili halisimamiwi ipasavyo. Bado ujenzi huo unaendelea. Pia, maeneo ya Kunduchi Mtongani kuna shamba la chumvi ambalo linaathiri mikoko na mandhari ya ufukwe. Tunaomba Wizara ya Maliasili na Utalii, ishirikiane na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Viwanda na Biashara, kuzuia shughuli hii kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahoteli ya Embassy, Dar es Salaam, na Moshi (Moshi) yaliuzwa kwa mfanyabiashara mmoja. Kumekuwa na habari kuwa huyu mfanyabiashara amenyang'anya *Moshi Hotel,* lakini hivi karibuni kumekuwa na habari kuwa huyu huyu mfanyabiashara amemshtaki mtu mwingine kuhusu kiwanja cha jirani.

Naomba Serikali itoe tamko juu ya mustakabali wa *Moshi Hotel* na *Embassy Hotel* na ieleze imekuwaje mfanyabiashara huyu anaendelea kuuziwa mali ya umma pamoja na kwamba amedhihirisha wazi kuwa yeye siye mwekezaji wala mwendelezaji. Kwa hayo, narudia kuiunga mkono hii hoja.

**MHE. EDWARD N. NDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuchangia kwa kuzungumza katika hoja ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba nijielekeze katika upanuzi wa sekta ya utalii ukanda wa Magharibi, hususan katika mwambao wa Ziwa Tanganyika.

Uimarishaji wa miundombinu (barabara) toka Kigoma hadi mbuga ya hifadhi ya Mahale. Kukosekana kwa barabara ni sababu kubwa ya idadi ndogo ya watalii kutembelea mbuga hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, safari kwa meli ni kiasi cha saa 12, mara moja kwa wiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, safari kwa boti ya kienyeji ni zaidi ya saa 15. Ni muhimu Wizara hii ikaunganisha nguvu na Wizara ya Ujenzi katika kutatua tatizo hili ili Taifa liongeze kipato toka Sekta ya Utalii.

Kuhusu utekelezaji wa sera ya ujirani mwema baina ya mbuga ya Mahale na jamii zinazopakana nayo. Vijiji hususan Kalilani, Sibwesa, Kallya na Kashagulu. Sera ya ujirani mwema ni suluhisho la hifadhi ya mbuga zetu na rasilamali zake, hususan sokwe mtu. Utekelezaji wa sera hii utaimarisha uchumi wa vijiji tajwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishaji wa utalii wa kitamaduni kwa kuanzisha vituo kwa shabaha hiyo *Cultural Tourist Modules* katika mwambao wa Ziwa Tanganyika. Kulingana na jiografia ya ukanda huu, kama sehemu ya kati ya nchi za maziwa makuu na kutokana na mwingiliano wa utamaduni wa wakazi wa mwambao wa ziwa na tamaduni za makabila mbalimbali toka nchi za maziwa makuu, uanzishaji wa vituo vya utalii wa kitamaduni utakuwa kivutio kikuu kwa watalii wa kitamaduni.

Kuhusu uanzishaji wa *Marine Park* katika fukwe za mbuga ya wanyama ya Mahale na sehemu ya Ziwa Tanganyika inayopakana na mbuga hiyo.

Uanzishaji wa uvuvi wa kitalii na upigaji picha wa kitalii katika Marine Park itakayoanzishwa. Eneo hili la ziwa lina hazina kubwa ya samaki wakiwemo wa mapambo na wengineo ambao yamkini wanapatikana katika sehemu hiyo tu duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya yote hayo Taifa litaongeza kwa kiasi kikubwa sana Pato lake la pesa za kigeni na kuchangia kwa kiasi kikubwa na kwa namna ya peke kuondoa umaskini miongoni mwa jamii za mwambao wa Ziwa Tanganyika.

**MHE. JOHN P. MAGUFULI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja hii. Pia nampongeza Waziri wa Maliasili na Utalii, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote kwa kazi nzuri wanazofanya. Mungu awajalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nawapongeza tu. Endeleeni hivi hivi, *your are doing fine* wewe Waziri na watu wako wote hongera na ninaunga mkono hoja.

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naunga mkono hoja ya Waziri wa Maliasili na Utalii kwa asilimia mia moja.

Hata hivyo naomba kujenga hoja kuwa *Rudi Game Researve* kwa sifa na madhumuni ya kuianzisha sasa imepoteza sifa hizo na hivyo kuna haja ya kuangalia upya kuendelea kuwepo kwa *Game Researve* hii. *Game Researve* hii ipo Wilaya ya Mpwapwa katika Jimbo la Kibakwe. Siyo kweli kama Wizara ilivyodai huko nyuma eti kuna wanyama. Wanyama waliokusudiwa kuwepo na kuhifadhiwa hawapo tena na kuwepo kwa Bwawa la Mtera kumebadilisha kabisa *ecology* ya eneo hilo kuendelea kuwepo kwa *researve* hii imekuwa kero kwa wananchi wanayoizunguka. Ni vizuri kero hii ikaondolewa kwa kutazamwa upya kuwepo kwa *researve* hii.

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Waziri Mheshimiwa Zakia Meghji, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoifanya katika mwaka 2002/2003. Ninawatakia wote kila la kheri na kazi nzuri zaidi 2003/2004. Aidha, napenda kutamka wazi kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja ninayo yafuatayo.

Kwanza, uhamasishaji wa upandaji miti nchi nzima Wizara hii inatakiwa iendeshe kampeni ya kudumu hasa kuzitaka Serikali za Vijiji kupanda miti maeneo ambayo yako wazi ili kuinusuru nchi yetu na janga la ukame. Vilele vya milima viko wazi, lazima vifunikwe kwa kupanda miti. Tarehe 1 Januari, kila mwaka haitoshi kwa kampeni hii. Ifanyike kipindi chote cha masika na ikiwezekana Wizara itoe miche ya miti na motisha kwa yeyote atakayepanda miti mingi katika kipindi fulani. Yule asiyepanda miti aadhibiwe.

Pili, maeneo ya hifadhi pembezoni mwa Vijiji vya Jimbo la Kasulu Mashariki. Karibu vijiji vyote vya upande wa kulia katika Jimbo la Kasulu Mashariki ukitokea Kigoma kuanzia Kwanga kuelekea Kibondo, vinapakana na Hifadhi ya Taifa. Vijiji hivi vilianzishwa mwaka 1973/1974 na hivyo vina umri usiopungua miaka 30. Bila shaka katika kipindi hiki kumekuwa na ongezeko la watu katika vijiji hivi na wananchi wanakabiliwa sasa hivi na upungufu wa ardhi kwa ajili ya shughuli ya kilimo. Naomba Wizara iangalie uwezekano wa kumega ardhi ya hifadhi ili wapewe wananchi kwa shughuli hizo.

Tatu, utangazaji wa maeneo ya utalii magharibi mwa Tanzania, yapo maeneo kadhaa ya kuvutia watalii magharibi mwa nchi yetu ambayo hayajatangazwa vya kutosha ili kuvutia watalii. Maeneo kama Gombe, Mahale, Muyovosi/*Kigosi Ramsar site* za mengine mengi hayajatangazwa vya kutosha kama vile *Selous,* Serengeti na Mikumi. Serikali iyatangaze zaidi maeneo hayo ili kuvutia watalii wengi zaidi.

Nne, kuhusu nishati mbadala na vifaa vya nishati. Ukataji miti na kuni na uchomaji wa mkaa unazidi kuangamiza misitu ya nchi yetu. Hivyo basi Serikali lazima ichukue hatua za makusudi kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala ya kuni na mkaa. Aidha, Wizara ihamasishe utafiti wa matumizi ya majiko ya nishati mbadala au yatumiayo kuni na mkaa kidogo zaidi au yatumiayo nyenzo nyingine kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia kila la kheri na naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. JUMA MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naunga mkono hoja hii asilimia mia moja. Wanyama waharibifu na wanyama wakali kwa maeneo yaliyo karibu na mapori ya hifadhi kama vile *Selous* bado hawajadhibitiwa. Kule Rufiji katika eneo la Magharibi wameliwa watu 26 na simba mpaka sasa na Serikali bado haijapeleka kikosi cha mabwana wanyama pori ili kuua wanyama hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni kwamba Wizara ipeleke kikosi cha mabwana wanyama pori kusaka wanyama hao na pia Serikali iwape waathirika kifuta machozi. Pia katika maeneo yanayopakana na mapori ya hifadhi uwekwe ulinzi wa kutosha ili wananchi wanaoishi katika maeneo hayo waishi kwa usalama. Vile vile Wizara ipeleke mabwana wanyamapori katika vijiji vinavyoshambuliwa na wanyama waharibifu na kuwasaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sekta ya uvuvi. Meli zilizoruhusiwa kuvua katika Pwani ya Bahari ya Hindi zinavua katika maeneo ambayo wavuvi wadogo wadogo wanavua na kuwaharibia zana zao kama vile nyavu. Kulifanywa utafiti na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo cha Mpunga sambamba na ufugaji wa samaki katika maeneo hayo hayo. Je, Wizara imeliendeleza jambo hilo vipi?

**MHE. ELIZABETHI BATENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa ufasaha aliotumia katika kuwasilisha hotuba yake. Aidha, nawapongeza watendeji wa Wizara yake chini ya uongozi wa Katibu Mkuu kwa namna wanavyofanya kazi kwa ushirikiano na hatimaye kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni kubwa ina shughuli nyingi na mashirika mengi ikiwa ni pamoja na Hifadhi za Taifa. Nampongeza Mheshimiwa Zakia Meghji, kwa namna anavyozimudu kazi nyingi hizo pamoja na kwamba hana Msaidizi yaani Naibu Waziri. Ningeshauri Mheshimiwa Rais, aone umuhimu wa kuweka Naibu Waziri kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kagera ndiyo wa mwisho katika mambo ya utalii, lakini kwa kadri inavyojulikana Mkoa wa Kagera una mambo mengi ya kuvutia kama vile Ziwa Victoria na viumbe vingi vilivyomo, mito, maziwa madogo madogo kama vile Ziwa Ikimba lenye samaki wa ajabu, Ziwa Burigi, maporomoko ya Rusumo, ndege wa aina nyingi na kadhalika. Wanyama katika mapori ingawa si wengi kwa sasa lakini kuna nyoka wakubwa wasiopatikana sehemu nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kujua na kuamini kwamba miundombinu ni nyenzo muhimu kwa utalii wananchi wenye uwezo wameanza kujenga hoteli za kisasa sehemu ambazo watalii wanaweza kufikia na hata kuunda kampuni za kuhudumia watalii. Hii inaonyesha kwamba sasa hali inavutia kuanzisha shughuli za utalii Mkoani Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, sera ya misitu na sera ya ufugaji nyuki ni nzuri sana na hata sheria husika ni nzuri kwa kuwa zinalenga ushiriki na ushirikishwaji wa wananchi. Kwa kuzingatia hayo ili kujikwamua katika hali ya umaskini wananchi katika sehemu mbalimbali za nchi kama Singida, Tabora, Kigoma na hata Kagera wana miradi ya kufuga nyuki ili kupata asali. Soko la asali ni kubwa katika nchi mbalimbali Uingereza, Afrika Kusini, nakadhalika. Lakini gharama za kukamua, kupakia na kusafirisha ni kubwa sana kiasi ambacho hawa wananchi hawawezi kumudu. Je, Wizara inafanya nini kuwasaidia wananchi hawa? Namwomba Mheshimiwa Waziri alione hili ili asali iweze kuuzwa na watu wajikomboe katika umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja.

**MHE. SULEIMAN A. SADIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naunga mkono hoja hii. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayofanya ndani ya Wizara hii na pia kwa umakini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie katika eneo la misitu ya *Teak* hasa *Mtibwa Teak,* msitu huu upo katika Wilaya mpya ya Mvomero Tarafa ya Turiani. Msitu huu Mheshimiwa Waziri anaufahamu sana maana alifika na kujionea hali halisi. Serikali kupitia Wizara hii imeweka utaratibu wa mnada wa kuuza magogo ya aina hii katika misitu kama hii hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa minada ni mzuri lakini wananchi wa vijiji jirani na msitu wa Mtibwa wana malalamiko ya muda mrefu sana wao kama wadau na watunzaji wa eneo hili utaratibu wa mnada unawanyima haki ya kununua magogo yale kwa sababu ya uwezo wao mdogo. Mnada unaofanyika *Mtibwa Teak* unakuwa na Magogo mengi na thamani yake ni kubwa mno huanzia milioni kumi hadi ishirini na wanakijiji hiki ni kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kuna kipindi wananchi wa maeneo hayo walituma ujumbe hapa Bungeni na Waziri alionana nao na alikubali ombi lao na walishiriki. Katika mnada na kununua *Lot* moja kwa shilingi milioni 16. Kiasi ambacho ni kikubwa sana na waliyumba mno mpaka wakaangukia kwa wale wale wanunuzi wa kila siku. Mnunuzi wa magogo ya *Mtibwa Teak* ni mmoja tu ambaye yupo Dar es Salaam huyu ndiye anayefaidika na *Mtibwa Teak* na mara zote anashinda yeye, wapo kama watatu, wananchi wa maeneo hayo huambulia kuni tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ombi maalum kwa Waziri atupie tena jicho lake la huruma katika eneo la *Mtibwa Teak,* tukae na wanakijiji, Serikali itoe kipaumbele angalau mara moja kwa mwaka ili wananchi nao waweze kununua magogo yale na waendelee kuwa askari wazuri wa msitu wa *Mtibwa Teak* kama hilo ni tatizo basi nashauri wanakijiji wapewe kibali ili wavune wao na wauzwe ili kupunguza gharama za uvunaji. Nashauri suala hili ikibidi iundiwe kamati na ije Mtibwa ikae na wadau ili tuone jinsi ya wao kufaidika na msitu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho ni mapato ya msitu huu mpaka leo vijiji jirani havipati asilimia yoyote ya mauzo ya magogo ya msitu wa Mtibwa. Naomba Mheshimiwa Waziri alione pia hili suala la asilimia kwa vijiji jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalam wake wote, mimi binafsi nianze kwa kuunga hoja mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natoka Wilaya ya Kilolo ndiyo Wilaya ambayo ipo Hifadhi nzuri ya Taifa yaani *Udzungwa National Park.* Hifadhi hii bado haijatangazwa vya kutosha kwani hata hapa Tanzania Watanzania hawaifahamu Udzungwa. Kwenye hifadhi hiyo kuna miti, ndege, wanyama wadudu, mapango ambayo hakuna sehemu nyingine duniani, sasa ni vipi haitangazwi vizuri?

Nichukue nafasi hii nipongeze Wizara hii kwa juhudi kubwa ya ujenzi wa barabara, shule, hii itasaidia sana kuitangaza Hifadhi hii hongera sana Waziri. Kando kando ya milima ya Udzungwa kuna vitu vya muhimu vikiwamo vyanzo vya maji ambavyo vinamwaga maji katika Bwawa la Kihansi kuna vyanzo 7 ambavyo kama havitatunzwi vizuri basi bwawa hilo litakauka namwomba sana Mheshimiwa Waziri anipe wataalumu wake niende nikawaonyeshe vyanzo hivyo. Wananchi wanaozunguka vyanzo hivyo wanahitaji elimu ninaomba Mheshimiwa asipuuze hilo. Vyanzo vipo katika Kata ya Bomalang'ombe, Tarafa ya Kilolo na Wilaya ya Kilolo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mapango ya Kale (Nyumba Niitu). Kule Udekwa karibu kabisa na Hifadhi ya Udzungwa yamegundulika mapango mazuri kuliko yote katika Afrika. Mimi kama Mbunge wa eneo hilo tumeomba Kijiji cha Udekwa kiweke ulinzi wa kutosha. Hivyo ninaomba sana Mheshimiwa Waziri ama yeye au watalaamu wake wafike huko mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atoe taarifa kuhusu wale vyura waliopelekwa *USA* maendeleo yao. Nimekuwa nikufuatilia sana habari ya vyura hao kwani wanatoka katika vile vyanzo 7 vya maji toka Kilolo.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote wa uvuvi, wanyamapori, misitu na nyuki, utalii, Mambo ya Kale na watendaji wote wa Wizara yako kwa kazi nzuri mnayofanya ambayo inaleta mabadiliko makubwa kama vile upandaji na utunzaji misitu hifadhi za wanyamapori, maendeleo ya uvuvi, utalii, Mambo ya Kale na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri kasi iongezwe katika kuanzisha *WMAs* maana hiyo ndiyo itakuwa ukombozi wa kuhifadhi, kuyamiliki na kuyatumia maeneo machache yaliyobaki kwa faida ya wananchi wetu.

Pia *WMAs* zikianzishwa maeneo wanayoishi ndugu zetu Wahadzabe Wilaya za Iramba, Mbuhi, Karatu na Meatu kwa sababu kuna maeneo ambayo wataanza kupata mapato toka kwa watalii wanaopiga picha, kuwinda, kuona utamaduni na kadhalika.

Mheshimiwa Waziri nashauri kasi ya kufanya doria iongezwe kwenye mapori yote kwani kuna dalili zinaonyesha ujangili unaoongezeka sana. Mheshimiwa Waziri, mpaka leo Mkoani Singida Wilaya za Iramba, Singida Vijijini, maeneo ya Mlandala, Tope la Wembere, baadhi ya Waarabu wa Mjini Singida wanawinda sana wanyamapori na hata wanatumia semi automatic rifles zinazoingizwa kwa magendo. Wanachukua mwanya wa kikosi chetu cha kuzuia ujangili ambacho kipo mbali na eneo husika uhaba wa watumishi wa maliasili Mkoani Singida, hasa Wilaya hizi mbili.

Pia naomba Wizara iwasiliane na *DED* wa Iramba, ambaye ana nafasi ya Afisa Wanyamapori ili apatikane Mtumishi mwenye uwezo wa kuendesha shughuli hizo kwa manufaa ya Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, Mkurugenzi wa Idara ya uvuvi aongeze kasi ya kutembelea Mkoa wa Singida au kutuma watalaam wake maana kuna maeneo mengi ya uvuvi ambayo yanahitaji utaalam, vitendea kazi na ushauri. Ziwa Kitangili linatoa samaki wengi sana kwa ajili ya matumizi Mkoa wa Singida na maeneo mengine mengi nje ya Mkoa hata hivyo uangalizi wa uvuvi unalegalega sana kutokana na kuwa na Afisa mmoja tu wa uvuvi anayekaa Makao Makuu ya Wilaya na hana vitendea kazi.

Nashauri Wizara ianze utaratibu wa kusaidia maeneo husika. Mheshimiwa Waziri, Wilaya ya Iramba inayo maeneo mengi sana ambayo bado kuna misitu ya asili ambayo inahitaji juhudi ya kuifadhi, wananchi wako tayari kufanya hivyo naomba kile kitengo cha kutoa elimu kwa umma cha Wizara au Idara zote wapange muda wa kupita Mikoani na Wilayani kuwahamasisha wananchi kwa kuonyesha senema, kuwapatia vipeperushi na kadhalika. Hii itasaidia sana kuwapa hamasa ambayo hutolewa kidogo sana na Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Iramba Mashariki, kuna mambo mengi sana ya Kale, picha kwenye mapango mengi makubwa, ngoma kubwa za zamani, shanga, majembe, mishale na kadhalika. Naomba sana Idara ya Mambo ya Kale ipate muda wa kutembelea maeneo haya kujifunza na pia kutafuta njia nzuri ya kuhifadhi maeneo haya na pia kuyatangaza nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ALHAJ SHAWEJI ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Mbunge, Mjumbe wa *NEC* na Waziri wa Maliasili na Utalii, pamoja na watendaji wake ambao ndiyo wasaidizi na washauri wa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwa kuandaa Bajeti nzuri na yenye ufafanuzi mpana wenye kina katika kuelezea masuala ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii, kwanza kwa kupendekeza sheria ya hifadhi ya wanyamapori sheria Na. 12 ya mwaka 1974 ifanyiwe mapitio na kufanyiwa marekebisho kama ifuatavyo:-

*Part 1 Preliminary, Section 2, Interpretation: "Authorized Officer"* hapa napendekeza *Village Game Scout (VGS)* aongezwe katika kifungo hicho. *Convervation area* yaani *Wildlife Management (WMAS)* ziongezwe katika kifungu hiki cha sheria *dangerous animals.*

Napendekeza mamba na viboko waongezwe katika kifungu hiki. *Weapon muzzle loader* iongezwe katika kifungu hiki cha Sheria *Part III of this Act* inazungumzia *Protected Areas and General Restriction* nayo napendekeza *section 6* ya sehemu hii isomeke kama ifuatavyo:-

*"The Minister may by order in the Gazette declare any area of Tanzania Mainland to be game controlled area* yaani iwe *Wildlife Management Areas."*

Mheshimiwa Naibu Spika, *Section 10* napendekeza *Wildlife Management area and game ranching* iongezwe katika kifungu hiki.

*Section 12* ya sheria hii kifungu hiki ambacho kinaruhusu *grazing of livestock* napendekeza kifanyiwe marekebisho kwenye maeneo ya wafugaji wenye *Wildlife Management areas.*

*Part VIII, Section 81(d) compounding* napendekeza kifungu hiki *fine* kiongezwe. *Part (ix) section 83 (I) Rewards,* zawadi iongezwe na hivyo napendekeza isomeke *(i) fifty thousand.*

*Section 50 (i)* kifungu hiki kwa maoni yangu kinatoa mwanya kuua wanyamapori ovyo kwa kisingizio cha kuzuia uharibifu. Napendekeza kifungu hiki kitungiwe sheria ya kufanya zoezi hilo hasa umbali kutoka maeneo yaliyohifadhiwa kama vile hifadhi za Taifa, *game controlled areas wildlife management areas* na ranchi za wanyamapori iwe umbali wa kilomita mbili hadi kilomita tano.

*Part (iv) (a) hunting of animal* katika sehemu hii *Section 21* hadi *Section 31 (b) capture of animals* kutoka *Section 32* hadi *Section 35 (c) commercial game photograph Section 36* mpaka *Section 37* utekelezaji wa hizo *Section* zote katika sehemu hii ya sheria *Part IV,* napendekeza zinapotekelezwa zifuate mila na desturi za wenyeji wa maeneo hayo kama vile Wahazabe, Wamasai nakadhalika. Kwa hiyo, *section* zote napendekeza zibadilishwe kuwezesha pendekezo hili kuleta maana inayokusudiwa.

Katika *subsidiary legislation* chini ya kifungu cha 29(8) napendekeza kisomeke na kifungu cha 48 cha *Wildlife Management Area Regulation* za mwaka 2002. Napendekeza vifungu hivyo vifanyiwe marekebisho katika kuuza nyara zitokanazo na wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kifungu cha 77 cha Sheria ya Uhifadhi wanyamapori Na. 12 ya mwaka 1974 iweke mkazo na kisisitize ukaguzi na uwekaji vizuizi vya ukaguzi wa mazao ya maliasili hii iwe pamoja na watu wenye tabia mbaya, kupiga vita uwekaji wa vizuizi kwa kisingizio cha hoja kwamba ni usumbufu kwa wananchi ili waweze kupitisha nyara za Serikali kwa faida zao binafsi.

Katika kuipitia sheria hii naomba kupendekeza tena kwa maneno mazito sana utaratibu wa kukodisha mapori ya wanyamapori kuwindia au kuleta wawindaji kutoka nchi nyingine za nje kuja kuwinda katika mapori ya wanyamapori yetu uangaliwe upya. Kwa maoni yangu haileti busara hata kidogo kiuchumi au kisiasa mtu mmoja apewe pori la kuwindia wanyamapori lenye ukubwa wa karibu theluthi mbili ya ukubwa wa Wilaya nzima ambaye haonyeshi hata nia ya kuwekeza miradi ya maendeleo katika Wilaya hiyo.

Napendekeza sehemu ya sheria hii ifutwe mara moja kwa faida ya uchumi wa Taifa letu. Nilidhani pori la wanyamapori linapotolewa au kukodishwa kwa wawindaji wengi kunachochea ushindani wa kibiashara wa mazao ya wanyampori wetu.

Kwa hiyo, kiuchumi hoja ya kumkodisha mtu mmoja pori la wanyamapori lenye ukubwa wa eneo la theluthi mbili ya Wilaya inakaribia kabisa kisiasa kutamka mtu huyu anakaribia kununua Wilaya hiyo. Napendekeza katika jambo linalohusisha mapato ya Taifa letu tusifanye mzaha hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo juu ya *frame work* ya idara ya wanyamapori ni kama ifuatavyo:-

(a) Muundo wa Idara ya wanyamapori uzingatiwe kuwa uhai wake unategemea sana utunzaji wa misitu na mazingira na kwa kuwa watunzaji misitu na mazingira wenye uhakika na wenye kuaminika ni jamii kule misitu iliko, nashauri sera ya wanyamapori iwe na vipengele vitakavyotamka kuwa kila Mkoa, Wilaya, Tarafa, Kata na Kijiji kuwe na Kamati ya kusimamia utunzaji wa misitu na mazingira, kuzuia uwindaji na kuua wanyamapori. Idara ya wanyamapori iwe na utaratibu wa kuwawezesha kufanya kazi zao kwa ufanisi

(b) Sera ya wanyamapori muundo wake utamke uundaji wa Kamati za uhifadhi wa mazingira za vijiji na wanakamati wapatiwe mafunzo.

(c) Sera ya wanyamapori itamke muundo wake kupewa uwezo sheria ndogo ya kuhifadhi mazingira.

(d) Sera ya wanyamapori itamke muundo wake utafundisha maaskari wanyamapori wa vijiji *(Village Game Scout).*

(e) Sera ya wanyamapori itamke muundo wake uwepo na utaratibu wa kufanya doria kwa kushirikiana na wanavijiji mara kwa mara.

(f) Sera ya wanyamapori itamke muundo wake utapendekeza itungwe sheria itakayomkataza mtu mmoja kuhodhi eneo kubwa la karibu theluthi mbili ya ukubwa wa eneo la Wilaya.

(g) Kwa kuwa wanyamapori wanagusa sehemu zote muhimu za uchumi wa taifa letu na kwa kuwa vyanzo vya mito mingi inatoka maeneo yenye misitu ya wazi na mikubwa ambako ndiko wanyamapori wanakoishi na kwa kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii ndiyo yenye dhamana ya usimamizi wa Maliasili na Utalii napendekeza kuwa kitengo hiki cha Idara ya Wanyamapori katika muundo wake Waziri apendekeze iundwe Bodi ya Wanyamapori kwa lengo la kusimamia na kuendeleza sekta hii ya wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa wanyamapori. Naomba kuchangia umuhimu wa wanyamapori katika maeneo makubwa matatu. Nchi yetu ya Tanzania ni moja ya nchi chache katika Bara la Afrika na pengine duniani kote ambayo tumebahatika kuwa na utajiri mkubwa wa maliasili na wanyamapori. Kwa kweli wanyamapori ni moja ya vyanzo muhimu vya uchumi wa Pato la Taifa letu kupitia Utalii. Licha ya utalii pia wanyamapori wanatupatia lishe sisi wananchi wenyewe na watalii. Hifadhi hizi za wanyamapori, hifadhi za Taifa, hifadhi za wanyamapori na mbuga za misitu ya wazi huwapatia makazi mazuri ndege, wanyama na mimea.

Hata hivyo napendekeza Wizara ya Maliasili na Utalii ijaribu kuona matatizo yanayowakumba wanyamapori. Kwa njia hiyo nina hakika itaweza kuwa na msingi mkubwa wa kuandaa mikakati ya kuimarisha sera ya Wanyamapori. Kwa mfano, yapo matatizo mengi ambayo yanapatikana kwa kuwepo wanyamapori. Matatizo haya mara nyingi husababishwa na jamii. Kwa ajili hii ni muhimu Wizara ya Maliasili na Utalii ikaweka mikakati itakayotoa njia ya kutatua matatizo hayo. Pamoja na kuwepo kwa matatizo yanayosababishwa na jamii napendekeza Wizara ya Maliasili na Utalii iangalie pia matatizo mengine kwa mfano kutoshirikiana kwa wadau wengi wa wanyamapori na hasa wanavijiji ambao ndiyo wengi na ndiyo wanaoishi karibu na maeneo yaliyo na wanyamapori na elimu kwa jamii ya hifadhi ya wanyamapori haijatolewa inavyostahili kwa maana ya kuwafikia walengwa.

Pia uharibifu wa mazao unaofanywa na wanyamapori kama vile tembo, nyani, nguruwe, viboko, nyati, ndege na wengineo unachangia kwa kiasi kikubwa kwa wakulima hata baadhi ya wakulima wanafikia kuamini hakuna sababu ya kuhifadhi na kuwatunza wanyamapori.

Katika hoja hii ni muhimu sana kwa Wizara ya Maliasili na Utalii ikatafute njia ya kubadilisha imani za baadhi ya wakulima hawa. Maafa makali kwa binadamu yatokanayo na wanyama wakali kama vile simba, chui, viboko, mamba na wengineo inasaidia kasi ya kuamini kuwa kweli hawa wanyamapori hawana umuhimu kwa jamii. Hii inatokana kwa sababu hakuna fidia inayolipwa kutokana na maafa ya namna hiyo. Wizara ya Maliasili na Utalii lazima itafute njia ya suluhu ili wanyamapori waongezeke.

Matatizo mengine ni yale yanayosababishwa na umaskini hali hii inatokea kwenye maeneo yaliyo kandokando ya mbuga ya hifadhi. Wananchi wengi hujitosa katika uvunaji wa maliasili na wanyamapori ikiwa ni njia mojawapo kwa ajili ya kupata kitoweo na pia kujikimu kimaisha.

Kama nilivyoanza kushauri Wizara ya Maliasili na Utalii iwe na mikakati thabiti kuwezesha wanyamapori wawe endelevu. Njia moja ambayo ni rahisi wala hahitaji mtaji mkubwa kuanzishwa katika hatua za mwanzo. Njia hii ni ya ufugaji wa nyuki. Karibu misitu yote wanayopendelea kuishi wanyamapori ufugaji wa nyuki unawezekana. Kitaifa makisio ya uzalishaji wa asali unakadiriwa kufikia tani 138,000 na uzalishaji wa nta unakadiriwa kufikia tani 9,800. Lakini uzalishaji halisi wa asali ni tani 4,800 na nta 380 kutokana na idadi ya nyuki milioni 11.9 (milioni kumi na moja na laki tisa). Kiwastani uzalishaji wetu ni asilimia 3.5% ikilinganishwa na uwezo tulionao.

Kwa kuwa jamii inaua wanyamapori ili wajikimu na maisha yao, tahadhari na mikakati mipevu isipochukuliwa mapema ya kuwalinda na kuwaendeleza wana jamii wanaoishi katika maeneo ya misitu hiyo upo uwezekano mkubwa baada ya muda mrefu wanyamapori watatoweka kama ilivyo sasa katika Hifadhi ya Mikumi wanavyotoweka kidogo kidogo.

Kwa hiyo, napendekeza Wizara ya Maliasili na Utalii kuwatafutia shughuli mbadala wanavijiji ili wasiwe na tamaa ya kuwinda wanyamapori. Nina hakika Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na hao wanaowakodisha mapori ya wanyamapori mnaweza kabisa kupata fungu la kuwawezesha wafugaji wa nyuki wafuge kisasa hata kuwajengea viwanda vya ku-*process* asali na nta. Ni kwa njia hiyo wataongeza kipato na kuachana kabisa na hoja ya kuwinda wanyamapori kwa ajili ya kujitatulia matatizo ya namna ya kujikimu.

Kwa njia kama hizi uwindaji haramu kwa ajili ya kupata kipato cha chakula na upunguzaji wa wanyamapori nao utafutika. Kadhalika vipusa ambavyo pembe za faru huhitajika kama dawa na kwa hiyo kuchangia ujangili nao utatoweka.

Ajli nyingi hutokea kwa magari kugonga wanyamapori waliopo ndani ya Hifadhi ya Mikumi ambapo hali hii inapoteza wanyamapori wengi kutokana na kugongwa na kukanyagwa. Kwa mfano tembo, simba, chui, twiga, nyati, pundamilia, swala, nyoka, mijusi na wengine. Katika vifo hivi vinavyosababishwa kwa kugongwa au kukanyagwa jambo baya zaidi ni pale wanyama kama simba kuacha utamaduni wao wa asili wa kuwinda, kuua na kula yule mnyama waliyemuwinda.

Simba katika eneo la barabarani kwa sababu ya uwingi wa mizoga simba wameacha ile mila na desturi yao ya simba jike kuwinda kukamata na kumwita simba dume kula mnyamapori aliyemuua. Jambo hili si mzaha. Ukipenda unaweza kwenda Kituo cha *TANAPA* pale Mikumi kuthibitisha haya ninayosema mimi inawezekana kimtizamo jambo hili likawa la kuchekesha lakini Mheshimiwa Waziri, naelewa unataka kupata mawazo ni njia zipi zitawezesha wanyamapori wakawe endelevu katika uchumi wa Taifa letu. Hivyo mambo ambayo yanaweza kuchochea wanyamapori hasa katika Hifadhi ya Mikumi kutoweka pale watakapoona hata mila na destrui zao hazitekelezeki, napendekeza Wizara ya Maliasili na Utalii itoe kipaumbele kujenga mkakati kwa kulinda mila na desturi za wanyamapori.

Katika barabara ya Mikumi kwa sasa kila siku wanakufa wanyamapori watano. Wanakufa kwa kugongwa au kukanyagwa na mbaya zaidi mara nyingi hutokea wanyamapori wanaogongwa na kufa huwa majike na tena wenye mimba. Pia watu wengi hupoteza maisha yao kutokana na ajali za magari na wanyamapori.

Jambo lingine baya zaidi ni pale tabia ya wanyamapori inapoharibika kutokana na baadhi ya wasafiri wa kutoka nchi za jirani wanapowalisha wanyamapori vyakula vyao ambavyo vimewekwa sumu ya aina ya ulevi. Wanyamapori wanapolewa wanabebwa na kuwapeleka kwao bila shaka wanawachukuwa ili wakawaweke kwenye zuu zao. Kitengo hiki kinachangia sana kupunguza mno idadi ya uwingi wa wanyamapori katika hifadhi yetu.

Napenda ieleweke kwa kuwa Hifadhi ya Mikumi kwa ukubwa wa eneo ni ya tatu katika nchi yetu itakuwa jambo la kijinga kabisa kama wanyamapori wetu wote watatoweka. Ukiangalia sababu kubwa ni barabara ya Mikumi ambayo kuibadilisha kwake ni jambo ambalo limo ndani ya uwezo wako ndani ya Wizara yako ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchafu wa mazingira *(pollution)* kutokana na wasafiri wanaopita kwenye maeneo hayo ya barabara ya Mikumu. Wasafiri hawa hutupa mifuko ya *plastic,* chupa za maji waliyokwisha kunywa, makopo ya pombe za bia na soda. Bila kufahamu madhara ya kula vitu hivyo wanyamapori wanapokula vitu hivyo vinashindwa kuwa *digested* yaani vinashindwa kubadilika tumboni na hatimaye kusababisha vifo kwa wanyamapori hao. Vifo vya aina hii vinatokea mara kwa mara kwa sababu mabasi ya abiria yanapita katika barabara ya Mikumi ambayo inapita katikati ya hifadhi ya wanyamapori ya Mikumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mikumi inatumika na magari mengi na mazito ambayo mengi ni magari ya nchi jirani. Magari hayo mazito yakipita katika barabara hiyo kwenye maeneo ya wanyamapori kwa miungurumo yao na honi zao hutishia wanyamapori na kuwakosesha amani. Kupita kwa magari katika hifadhi huathiri miendo ya wanyamapori kutoka sehemu nyingine kutafuta malisho na maji.

Kwa hali ya barabara ya Mikumu ilivyo sasa, fedha nyingi za kigeni zinapotea kutokana na wasafiri kutolipa ada za kuangalia wanyamapori. Hali hii inaweka Taifa letu kushindwa kuelewa umuhimu wa wanyamapori wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, watalii wengi wasio rasmi wanaopita katika barabara ya Mikumi ambayo ipo katikati mwa Hifadhi ya Mikumu hutumia muda wao mwingi katika barabara ya Mikumi kuchukua mikanda ya video za wanyamapori wetu bila kulipa fedha za kufanya biashara hiyo. Wakati mwingine husingizia magari yao yameharibika kwa kufungua *bonet* za magari huku wakiendelea kupiga picha za *video* za wanyamapori wetu kwa hoja za kiuchumi napendekeza barabara ya Mikumi ifungwe.

Kwa ajili ya uchumi wa wanyamapori katika mapato ya uchumi wa taifa letu ninapendekeza yafuatayo:-

(a) Kwa kuwa wanyamapori wanaingizia Taifa letu fedha za kigeni kupitia utalii napendekeza sehemu ya fedha ziwe *ploughed back* katika Idara ya wanyamapori. Ingekuwa bora zaidi kama utekelezaji wa pendekezo hili ungekuwa *reflected* katika mapitio ya Bajeti ya Wizara mwaka 2003/2004.

Napendekeza hivyo kwa sababu kwa maoni yangu idara hii ya wanyamapori inahitaji lazima pawepo na usimamizi shirikishi wa hifadhi ya wanyamapori na usafiri wa uhakika kutoka Mkoani, Wilayani, kwenye tarafa na kwenye kata hadi vijijini. Usimamizi huu shirikishi napendekeza uwe wa dhati kabisa na kusiweko na woga wa watendaji wakidhani kuwa watanyang'anywa kazi zao. Kwa maana hii napendekeza ni muhimu baada ya vifungu vya sheria vifutwe au vibadilishwe na au vifanyiwe mabadiliko ili kukidhi mahitaji ya sasa.

(b) Napendekeza barabara kuu ipitayo katikati ya hifadhi ya Mikumi sasa ihamishwe na ipite Morogoro, Dumila, Madudu, Msowero, Mvumi, Rudewa, Gongoni, Madoto, Kimamba, Chanjuru, Kilosa, Magomeni hadi Mikumi na huko itaendelea kutumika barabara ya zamani hadi Iringa, Njombe, Songea, Mbeya, Malawi, Zambia mpaka Afrika ya Kusini na pia Mkoa wa Rukwa.

(c) Kwa hatua za mwanzo naomba nichukue nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kutoka katika kina cha kifua changu kwa Mheshimiwa John Magufuli, Waziri wa Ujenzi, kwa namna alivyokuwa mkweli katika kutekeleza mambo anayoweza kufanya chini ya Wizara ya Ujenzi.

Mambo niliyomwomba ni kuangalia *alternative road* badala ya barabara kupitia katikati ya mbuga ya wanyamapori. Nashukuru sana ahadi ya kupeleka wataalam wake ili wakamfanyie *Preliminary Survey* ametekeleza. Mapendekezo ninayoyatoa kwako Mheshimiwa Waziri msingi wake mkubwa ni kujaribu kutafuta mawazo yatakayowezesha wanyamapori kama chanzo cha mapato ya Taifa letu kuwa endelevu.

(d) Kwa sababu hii tuna kila sababu za kuamini barabara ya Mikumi ni chanzo kikubwa cha kupoteza raslimali yetu ya wanyamapori katika Hifadhi ya Mikumi. Kwa hiyo, napendekeza Wizara ya Maliasili na Utalii wakishirikiana na hao watu wanaokodishwa pori yetu il iwawinde wanyamapori wetu, nguvu itakuwa kubwa sana ya ujenzi wa hiyo barabara niliyoipendekeza mkishirikiana na Wizara ya Ujenzi.

(e) Zipo faida nyingi lakini hatua ya kubadilisha barabara ya Mikumi, Taifa litaokoa na kupunguza vifo vya wanyamapori vinavyosababishwa na kugongwa na malori au kukanyagwa na malori hasa pale wanyamapori majike wenye mimba wanapokutwa na mikasa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanyama majike wanapogongwa na kufa matumaini ya kuongezeka wanyamapori yanakuwa mashakani. Kadhalika kwa uamuzi huo taifa litaongeza pato lake kutokana na kuzuia watu waliokuwa wanafanya utalii wa barabarani na kwa uamuzi huo sasa itawalazimu waingie rasmi kwenye hifadhi ya Mikumi kama watalii.

(f) Pamoja na maelezo hayo, ili kuwezesha maisha ya wanyamapori uchumi wake kwa taifa uwe endelevu, napendekeza kwako Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwa kuwa tayari ipo *alternative road from* Morogoro kupitia Dumila, Madudu, Kitete, Msowelo, Mvumi, Rudewa, Madoto, Kimamba, Chanjulu, Kilosa, Magomeni hadi Mikumi tamko lako la kufunga barabara hiyo haitaathiri usafiri na usafirishaji wa magari kwenda Mikoa ya nyanda za juu na nchi za jirani, barabara ipitayo katikati ya hifadhi ya Mikumi uifunge na utamke kwa watalii kuwa watakuwa wanatembelea rasmi hifadhi hiyo ya Mikumi.

(g) Napendekeza mipango ya matumizi bora ya ardhi iwe wazi katika Wizara ya Maliasili na Utalii na iheshimiwe kwa sababu mara nyingi uwingi wa njia za wanyamapori *migratory routes* zinatumika kwa matumizi mengine.

(h) Baadhi ya wanyamapori walioko katika Mbuga ya Mikumi husafiri hadi kwenye milima ya *Eastern ARC* ambayo ina viumbe hai wa kipekee na hawapatikani kwingine kokote duniani.

Kwa mfano, katika Msitu wa Mandege Kata ya Mandege, Tarafa ya Nongwe Wilaya ya Kilosa ameonekana kinyonga mwenye pembe mbili. Katika hali hii tuna kila sababu ya kuazimika kutunza misitu yetu na hifadhi zetu kwa kuelewa na kuamini umuhimu wa wanyamapori katika uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kutoa shukrani kwako kwa kunipa nafasi hii ili niweze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Pili, napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia kwa kuzungumza ama kwa maandishi kwenye hoja ya Wizara yangu ya Maliasili na Utalii. Kama ninavyosema siku zote kwa kweli hoja hizi mnazozizungumza ni nyingi na mawazo ambayo mnatupa ni makubwa sana na ndiyo mawazo ambayo tunayachukua na kuyatafakari, na baadaye kuangalia ni jinsi gani ya kurekebisha hizi dalili. Kwa hiyo, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaelewa kwamba muda ni mfupi ninayo saa moja ya kujibu hoja zote za maandishi na hoja zilizozungumzwa hapa Bungeni na hata wakati nainuka kulikuwa na karatasi nyingine ambazo wamechangia kwa maandishi zilikuwa zinakuja. Kwa vyovyote vile mtakubaliana na mimi hata ningekuwa na kompyuta namna gani na macho ya aina gani ya kuweza kusoma ingekuwa vigumu. Kwa hiyo, nitakuwa si mkweli nikisema kwamba nimesoma hoja zote ambazo zimefika kwangu. Lakini labda niseme kwamba kwa hoja zile za maandishi tutafanya kama vile tunavyofanya siku zote kwamba tutaweza kuzijibu kwa maandishi ili muwe na kumbukumbu sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia ni 67 na kati ya hao Waheshimiwa Wabunge 16 wamechangia kwa kuzungumza hapa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge 37 wamechangia kwa maandishi. Lakini pia kulikuwa na Waheshimiwa Wabunge 14 ambao walichangia wakati wa kujadili Bajeti za Wizara zingine ambazo zilitangulia. Kwa hiyo, zote tumezichukua na zote katika kujibu kwa maandishi tutazifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwatambua Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa kuzungumza. Kwanza kabisa ni Mheshimiwa Anne Makinda, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira na ni Mbunge wa Njombe Kusini. Pili, Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani na Mbunge wa Mtambile. Wengine ni Mheshimiwa Maria Watondoha, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, Mheshimiwa Mathew Ole-Timan, Mheshimiwa Edward Ndeka, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri na Mheshimiwa Ireneus Ngwatura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa maandishi ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Salim Omar Ali, Mheshimiwa Frank Mussati, Mheshimiwa Paul Ntwina,

Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Venance Mwamoto na Mheshimiwa Hassan Kigwalilo.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengine ni Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Maria Watondoha, Mheshimiwa Anthony Diallo, Mheshimiwa Jackson Makwetta. Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Suleiman Ahmed Sadiq, Mheshimiwa Alhaji Ahamadi Mpeme, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Mwandini Abass Jecha, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Dr. Zanaib Gama, Mheshimiwa Philip Marmo, Mheshimiwa Christopher Wegga, Mheshimiwa Prof. Juma Mikidadi, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Prof. Daimon Mwaga, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Ally Karavina, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, Mheshimiwa Abu Towagale Kiwanga, Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Mheshimiwa John Magufuli, Mheshimiwa Edward Ndeka, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Perseko Kone, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte na Alhaji Shaweji Abdalah. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge ambao walichangia kupitia Wizara nyingine ni Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mheshimiwa Christopher Wegga, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Maria Watondoha, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Janet Bina Kahama, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, Mheshimiwa Martha Wejja na Mheshimiwa Omar Chubi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajaribu kujibu kwa muda huu hoja zile, na kama nilivyosema kwamba kwa zile ambazo sitaweza kuzijibu siyo kwa sababu siyo muhimu. Lakini ni kwa sababu ya muda zote zina umuhimu sawasawa na zote zitatusaidia katika Wizara yetu hii ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala moja ambalo lilizungumza hapa ni juu ya kushirikiana na nchi husika ili kujenga majumba ya makumbusho katika maeneo ya wapigania uhuru. Kwa mfano, kutoka Zimbabwe, Angola, Namibia, Afrika ya Kusini, Msumbiji na kadhalika. Kwa hili ningesema kwamba wazo hili ni nzuri na pia wale ambao wamezungumzia masuala ya kumbukumbu mbalimbali. Kwa hiyo, tunalichukua kama wazo nzuri ambalo kwa kweli tutalifanyia kazi na baadaye mapendekezo yetu tutawaletea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni juu yaWizara kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya kujenga mnara wa kumbukumbu ya nyumba mbalimbali ili kuonyesha makabila ya aina mbalimbali katika Nyanda za Juu Kusini. Wizara kimsingi inakubaliana na pendekezo la Mheshimiwa Mbunge, na kama nilivyosema kwamba tutalifanyia kazi, lakini pia kwa kumshirikisha Mheshimiwa Mbunge aliyetoa mawazo haya pamoja na Halmashauri husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo limezungumzwa ni kuhusu uendelezaji wa uhifadhi wa mapango ya Kipatimu. Niseme kwamba mimi mwenyewe binafsi nimeishafika kwenye pango hili Kipatimu na niliteremka mpaka chini katika pango hilo. Wizara hivi sasa inaandaa utaratibu wa namna bora ya kuhifadhi na kuweza kuyaendeleza mapango hayo. Wataalam wa Wizara yangu wataendelea kuyatembelea na kushirikiana na uongozi wa maeneo hayo katika kutekeleza azma hiyo. Labda niseme kwamba kwa kushirikiana na Wizara zingine hasa hasa Sekta ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa sababu suala la mawasiliano pia katika eneo hili limeonekana ni suala la umuhimu mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwamba pawepo mahali ambapo historia ya Marehemu Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere inatunzwa na niseme kwamba hivi sasa kuna makumbusho ya Marehemu Baba wa Taifa ambayo yapo Butiama. Lakini tunakubali kwa wazo lile ambalo tumepewa kwamba kuna haja ya kuweka mambo zaidi ili kuonyesha mchango wa Kitaifa wa Marehemu Mwalimu Julius Nyerere. Kwa hiyo, hili nalo pia tutalifuatilia ili kuleta mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo limezungumzwa ni kuhusu takwimu za utalii, na Mara nyingi sana suala hili la takwimu za utalii linajitokeza. Hata hivi leo nilipokuwa nasoma Bajeti yangu nimeeleza kwa kweli takwimu za utalii tulizozipata na jinsi gani ambavyo tumeshirikiana. Kwa mfano,

Benki Kuu, Idara ya Uhamiaji na sekta nyingine ili kuhakikisha kwamba takwimu hizi ni sahihi. Suala ni kwamba takwimu hizi labda pengine siyo sahihi, kwa maana labda tunachukua takwimu zile za *Bureau De Change,* pale ambapo Watanzania pia wanaweza kubadilisha fedha za kigeni. Labda niseme kwamba takwimu za mapato haya ya fedha za kigeni zimepatikana kutoka vyanzo vifuatavyo:-

Kwanza, mahoteli, huduma za kulala na vyakula. Ada za viingilio katika hifadhi zetu moja kwa moja. Manunuzi mbalimbali ya maduka ya zawadi yaani *Curio and gift shops,* huduma za usafiri wa ndani yaani *ground operation kupitia Tour Operators* wetu, gharama za vyakula katika migahawa. Kwa hiyo, takwimu hizo zote ukusanywa kupitia *banking systems* na kusimamiwa na Benki Kuu za mapato. Kwa hiyo, suala la kusema kwamba zinakusanywa kutoka *Bureau De Change* moja kwa moja siyo sahihi *in such,* kwa maana ya *statistic* zile ambazo tunazipata kwa hivi sasa.

Lakini tutakuwa tayari na wataalam wangu watakuwa tayari kama Mheshimiwa Mbunge atapenda kujua zaidi ili waweze kukaa na wataalam wangu kuzungumza pengine ana mawazo zaidi tutaweza kuyachukua hayo. Kwa hiyo, nashukuru sana Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo limezungumzwa ni kuhusu kuboresha afya za wananchi kwa kuwafanya wajishughulishe na kuvuna samaki walioko kwenye mito, maziwa na bahari hapa nchini hata kujipatia fedha zaidi. Labda nieleze kwamba hili ndilo ambalo Wizara ya Maliasili na Utalii inafanya na kwa Mheshimiwa Mbunge ambaye amelizungumzia hili ni wa upande wa Upinzani, nafikiri baada ya kusoma Bajeti yetu ameliona kwamba tumezungumzia juu ya uvuvi endelevu katika Mikoa yote ya Tanzania Bara, hasa katika mwaka 2001/2002 na pia ziweze kupatikana zana za kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili la zana za kisasa na wavuvi wadogo wadogo nalo pia limezungumzwa sana. Labda niseme kwamba tunatambua kuna matatizo makubwa ya wavuvi wadogo wadogo wanayoyapata kutokana na kutokuwa na zana za kisasa. Sheria yetu ya uvuvi ina Mfuko wa Uvuvi. Kazi mojawapo ambayo Mfuko huu wa Uvuvi utafanya ni kusaidia mbali ya kutoa elimu kwa wavuvi wadogo wadogo, lakini pia utasaidia kupatikana kwa zana hizi. Lakini mbali ya hivyo Mheshimiwa Waziri wa Fedha alitamka hapa Bungeni kwamba kutakuwa na Mfuko wa kuwasaidia wananchi wenye kuanzisha biashara ndogo ndogo. Tunaamini kabisa na tumezungumza hili na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba kwa upande wa Sekta ya Uvuvi, wavuvi wadogo wadogo pia wataweza kusaidiwa ili waweze kudhaminiwa na Serikali na kuweza kununua vifaa hivi vya kisasa, na kwa maana hiyo kujiondolea umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo limezungumziwa ni kwamba Wizara ya Maliasilia na Utalii ina mpango gani katika kuongeza kiwango cha elimu katika Vyuo vya Utalii. Labda niseme na nimesema hili katika *Budget Speech* yangu ni kwamba mwaka 2003/2004 kwa maana ya mwaka huu Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa inatarajia kujenga upya Chuo cha Taifa cha Utalii. Tunaishukuru Serikali ya Ufaransa na kwa kweli tumeishapata viwanja viwili ambavyo viko pamoja ambapo Chuo hicho cha Utalii cha Kisasa kitaweza kujengwa. Kwa maana hiyo tunaamini kwamba hili litapunguza ile adha ya kuajiri vijana kutoka nje ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo limezungumzwa linahusu ni kwa nini Mashirika mengi ya kigeni yanayotoa huduma wanapenda kuajiri watumishi kutoka nje ya nchi. Labda niseme kwamba kufuatana na Sheria ya Uwekezaji Kampuni inaruhusiwa kuajiri wataalam watano tu katika *Departments* muhimu. Lakini ajira za ziada zinaweza kujazwa iwapo hakuna mwananchi mwenyewe sifa. Kwa mfano, kama hakuna mwananchi wenye sifa wanaweza kuajiri zaidi. Lakini tunaamini kwamba katika sekta hii ya utalii baada ya kujenga hicho Chuo pengine tatizo hilo litakuwa halipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo limezungumzwa ni suala la viwango maalum vya bei ya huduma za utalii kwa wenyeji. Suala la *Domestic Tourism* nalo limezungumzwa na ni jambo ambalo hivi sasa tunalitilia mkazo. Kama vile tunatilia mkazo utalii wa Kusini mwa Tanzania na utalii wa wenyeji wananchi wenyewe nao pia tunatilia mkazo. Tunaelewa kwamba watu wengi sana hawajawahi kuona simba, kwa mfano hawajawahi kuona chui na hata hivi majuzi wakati wa Saba saba kwa kweli viwanja vilifurika watu wengi sana, vijana wa shule na kadhalika ili kuona Wanyamapori katika maeneo hayo. Kwa hiyo, hili ni eneo ambalo tunalitilia mkazo mkubwa sana. Na ada katika kuingia katika hifadhi hizi

kwa upande wa wananchi ada ni ndogo sana. Kwa mfano, ada ya shilingi 1,500/= kwa wananchi wengine ni kubwa. Lakini kwa kweli kwa wananchi wengi shilingi 1,500/= wanaweza kuitumia kuweza kuingia katika hifadhi zetu. Lakini pia niseme kwamba zipo hosteli za bei nafuu katika hifadhi zetu kwa wananchi pia na wanafunzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, limezungumzia juu ya suala la wafanyakazi wa hoteli *Seventy Seven.* Labda niseme kwamba wafanyakazi wa hoteli ya *Seventy Seven* walipunguzwa kwa taratibu zote za kisheria na Tume tatu zimepelekwa katika Hoteli ya *Seventy Seven* kuweza kuchunguza madai ya wafanyakazi hao. Tume hiyo ilihusisha pia *PSRC,* Hazina na pia Wizara yangu. Ilionekana kwamba hakuna mapunjo yaliyofanyika. Wahusika hawakuridhika na kwa maana hiyo wamepeleka kesi Mahakamani. Kwa hiyo, sasa hivi kesi iko Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo limezungumziwa ni kwamba hatua gani zitachukuliwa kuzuia wizi unaofanywa dhidi ya watalii kama ilivyotokea hivi karibuni huko Dar es Salaam na Wilayani Ulanga. Labda niseme kwamba kwa kweli matukio kama haya huwa Serikali haiyapendi na yanaleta sifa mbaya kwa nchi yetu. Ili kuzuia matukio hayo mabaya Wizara kupitia chombo chake cha Bodi ya Utalii huwa inatoa tahadhari kwa watalii na kuwataka kuwa waangalifu kama ilivyo katika nchi nyingine. Tahadhari hizo hutolewa kupitia Tovuti ya Bodi ya Utalii. Aidha, watalii wameishauriwa kutumia Wakala wanaoaminika na kuishi katika hoteli zinazotambulika na kuthibitishwa na Wizara. Hata hivyo, kuhusu majaribio ya hivi karibuni Wizara ikishirikiana na Jeshi la Polisi tumeweza kufuatilia matukio hayo na tuweza kupata baadhi ya mali na fedha zilizoibiwa. Mhusika Mjapan alilipwa fedha zake na mmiliki mwenye hoteli wa *Pop Inn* kwa hiyo fedha zake huyo Mjapan zote alilipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine lililozungumziwa ni juu ya mikakati ya kuepushwa kugongwa kwa wanyamapori Mikumi nalo hili pia limezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge kwamba labda pengine kuna haja ya kuweka *gate* katika maeneo hayo au kubadilisha barabara iende sehemu nyingine. Ningependa kusema kwamba matuta yaliyopo yamepungua urefu kutokana na uzito mkubwa wa magari yaliyotumia barabara ile. Kwa hiyo, matuta yale yaliyowekwa kwa wakati ule yamekuwa hayawezi kukidhi magari makubwa ambayo yanapita kwa hiyo yamedidimia chini. Kwa hiyo, magari yanapita tu kwa haraka sana sasa.

Sasa na joto la jua huyenyusha lami iliyotumika kujenga matuta hayo na kurahisisha kupunguza urefu wake kwa magari yanayopita na matuta pia ni machache. Sasa mikakati ambayo tumefikiria labda ni kwamba Shirika liweze kubadilisha matuta na kuweka yaliyo imara zaidi na makubwa zaidi. Tumesikia kwamba kuna utaalam zaidi wa kuweka matuta makubwa zaidi na imara zaidi na pia kuweza kuongeza matuta kwenye maeneo korofi ili kuepuka ugongwaji wa wanyamapori. Suala la kuchepua barabara kwenda sehemu nyingine ni suala ambalo tumelizungumza na Kamati ya Maliasili na Mazingira na tutashirikiana na Wizara ya Ujenzi ili kuangalia kama hili litafanyika namna gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini labda niseme kwamba suala la gate Mheshimiwa Wabunge mimi ninaliogopa kidogo. Lakini nyie ndiyo Waheshimiwa Wabunge na mtatoa mawazo. Kwa sababu tukiweka *gate* pale ile ni *highway,* halafu inatakiwa mtu alipe fedha pale. Watanzania wengine watasema aah hata kuona Pundamilia basi wanatukataza! Halafu wanaweza kuuliza je, treni zinazopita katika maeneo ya *Selous* na kadhalika na watu wanaona wanyama hao nao pia walipe na inaweza kuleta *corruption* huku Askari kakaa anasema basi sikupitishi mpaka hutoe chochote hapa. Kwa hiyo, mimi nina wasiwasi sana isije ikatuletea matatizo hayo. Lakini Waheshimiwa Wabunge ndiyo ambao mtaamua na nyie ndiyo wawakilishi wa wananchi na ndiyo wananchi watawauliza nyie.

Kulikuwa na suala la migongano ya wananchi na Hifadhi kutokana na mipaka isiyo wazi. Labda niseme kwamba hili lilikuwa ni tatizo, lakini tatizo hili limeanza kufanyiwa kazi kwenye baadhi ya Hifadhi. Kwa mfano, Mikumi na Mahale. Jitihada zitaendelea kufanywa kuainisha na kuweza kufyeka mipaka ili kupunguza hata kuondoa kabisa tatizo hilo. Zoezi hilo litazingatia ushauri wa Kamati kama wananchi husika washirikishwe katika kuimarisha mipaka. Kwa hiyo wananchi husika watakuwa sasa hivi wanashirikishwa katika mipaka hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lile la kuchomewa na kubomolewa nyumba huko Ngaruma Kijiji cha Sengerema namshukuru Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, kwamba amelijibu kwa ufasaha. Kwa maana hiyo sitokuwa na haja ya kulijibu mimi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala lile la kwamba Twiga kama *national emblem* kwamba Twiga ni *docile* na mpole sana, na pia kulikuwa na *issue* ile kwamba wale wanaopita kwenye maeneo ya wanyamapori wanasitupe karatasi na takataka ovyo. Labda niseme kwamba katika hili la kutupa takataka ovyo tulifikiria labda tungeweza kushirikiana na wenye mabasi, lakini pia kuweza kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo inahusika na masuala ya Mazingira ili tutaweza kulifanyia kazi. Lakini ningesema kwamba kwa kweli Twiga ni mpole, lakini nafikiri ni imara unaweza kuwa mpole lakini ukawa imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo limezungumzwa ni suala la meno ya tembo kwamba yana uzito gani na thamani yake ni kiasi gani na je, thamani hiyo inapungua au inazidi na kwamba tuweze kuweka mkakati wa kuweza kuyauza meno ya tembo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili nalo pia liliulizwa jana bahati mbaya muda ulikwisha na Mheshimiwa Mbunge hawakuweza kuuliza swali la nyongeza. Labda niseme kwamba thamani ya meno ya tembo Kimataifa haijulikani. Kwa sababu haijulikani ni kuwa hayana soko maalum isipokuwa Japan ambapo bei ya kule Japan ni maelewano kati ya anayeuza na anayenunua. Kwa hiyo, hakuna bei maalum ya kusema kwamba kilo moja ya meno ya tembo ni kiasi gani ni kwamba mnakubaliana tu. Nchi zilizouza meno ya tembo kwa mfano, Botswana Zimbabwe, *South Africa* ni kwamba waelewana na Wajapan wakakubaliana bei kadhaa. Hata hivyo, kufuatana na thamani ya Mahakama hapa kwetu kwa tani 80 tulizokuwa nazo hivi sasa ni sawa na shilingi bilioni 3.5 kwa bei ya Mahakama, inawezekana kwa makubaliano tunaweza kupata bei zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa Ireneus Ngwatura kama alivyoeleza ni sahihi kabisa kwamba yeye amekuwa katika Wizara hii kwa miaka mingi sana, na hata mimi nilipofika pale Wizarani nilimkuta katika Idara ya Wanyamapori na analielewa vizuri sana suala hili. Amesema kwamba nitoe tamko kwamba tufanye biashara hii.

Labda niseme kwamba na kama nilivyojibu jana kwamba kuna mambo kadhaa ambapo lazima yafanyike kabla ya nchi haijaruhusiwa kuuza. Huwezi tu kuuza bila ya kupata kibali cha *CITES* kwa sababu sisi ni *Members* wa *CITES* huwezi kwa vyovyote. Kama vile biashara yoyote ile ya wanyamapori tunafanya ni lazima tupate kibali cha *CITES.* Ukichukua nchi ya Botswana kwa mfano, katika suala hili ambalo tunalizungumza sasa la *Wildlife Management Areas,* suala la kushirikisha wananchi nchi ya Botswana imekuwa na ushirikishwa wa wananchi kama miaka 10 hivi. Tanzania ndiyo tumeanza tu hata sheria yetu ya mwaka 1974 bado haikupitishwa kuweka hii element ya ushirikishwa. Kwa hiyo, tukifananisha kwa mfano, Tanzania na Botswana, *South Africa* na Zimbabwe kwa maana ya biashara hii ya tembo siyo sahihi, kwa sababu wao walikuwa mbele na masuala mazima ya *monitoring* kwa mfano, una *monitor* tembo *movement* zao, ujangili unatokea tembo wangapi na kadhalika.

Kwa hiyo, sisi ndiyo tumeanza hivi juzi hata nikisema kwamba kuna programu inaitwa *MIKE A Monitoring of illegal killing of Elephants* Hii *MIKE* imekuwa *put inplace* mwaka 2000 na *CITES.* Lakini kama nilivyosema *already* wenzetu walikuwa nayo, sasa sisi ndiyo tumeanza kuweka in *inplace* mwaka 2002 kwa maana ya mwaka jana. Sasa tukisema tu kwa hivi sasa tuuze tunaweza kupata matatizo. Lakini nafikiri mimi kwamba kwa sababu tumeishaweka hiyo *inplace monitoring* kwa sababu *WMAs* sasa hivi ziko na tunaanza na 16. Kwa sababu katika fedha za *rentetion* tutaweza kuzitumia kwa ajili ya mambo ya ujangili.

Kwa hiyo, nafikiri tuko katika nafasi nzuri na pengine tunaweza na tunapokea wazo la Mheshimiwa Ireneus Ngwatura kwa mambo haya yote kwamba tunaweza tukaomba *CITES* tukasema kwamba tuko tayari au tukasikiliza ni kitu gani ambacho watatueleza. Tutakuja kuwajibu watakavyotueleza ni kitu gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala la hili kugeuza Shamba la Mkonge la Kibisela kuwa shamba la kufugia simba. Suala hili kwa kweli limekuja mara nyingi tu na tumejaribu kulijibu. Lakini

kwa faida ya Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge w na wananchi wapiga kura wa Mheshimiwa Abdillahi Namkulala tunasema kwamba suala la kubadili matumizi ya ardhi ni suala la Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi siyo suala la Wizara ya Maliasili na Utalii.

Wizara ya Maliasili na Utalii haijapokea ombi lolote kutoka kwa mwekezaji juu ya kutaka kufuga simba Mtwara Vijijini. Kwa hiyo, kama atataka kufuga simba itabidi akaombe mabadiliko ya matumizi ya ardhi, kwa sababu ardhi ile ilikuwa inatumika kwa ajili ya kilimo kama nilivyoeleza.

Aidha mabadiliko ya matumizi ya ardhi itabidi aombe Wizara ya Ardhi na hapo ndipo aje kuomba Wizara ya Maliasili na Utalii. Kama nilivyosema kwamba sisi hatukupata maombi yoyote yale. Kwa hiyo, kama ana taarifa zaidi ya huyu kama ameanzisha kule tungependa kupata taarifa kamili ili tuweze kushughulikia ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala hili la misitu ambalo limezungumzwa kwamba katika Sera ya Misitu na katika Sheria ya Misitu ni kwamba tutaweza kukabidhi usimamizi wa misitu mingine kwa wananchi. Kwa maana kwamba kwa Vijiji, Halmashauri na kadhalika badala tu ya kusimamiwa na labda Serikali Kuu na Halmashauri.

Mheshimiwa Mbunge mmoja alikuwa na wasi wasi juu ya hili kwamba pengine linaweza kuleta matatizo juu ya usimamizi ya misitu hii na kukawa na matatizo yakajitokeza. Labda niseme kwamba tutaangalia ni jinsi gani ambavyo tutaanza. Tutaanza kidogo kidogo na matatizo yatakapojitokeza yataweza kutatuliwa kwa jinsi ambavyo yanajitokeza, hatutoweza kuingia kichwa kichwa kama wanavyosema Waswahili, lakini tutaanza kidogo kidogo.

Lingine ambalo limezungumzwa ni juu ya usimamizi shirikishi wa misitu ufanyike nchi nzima. Nimejibu kwamba tutakuwa na tahadhari katika suala zima la ushirikishwaji na hasa hasa usimamizi wa misitu.

Suala lingine lilikuwa ukataji wa miti na utengenezaji wa mkaa usio wa kawaida ni mkubwa sana. Niseme tu kwamba Serikali itaendelea jitihada za kudhibiti ukataji miti ovyo ikiwa ni pamoja na kupitia usimamizi shirikishi wa misitu. Suala hili la muhimu sana kwa sababu hatusemi kwamba wananchi wasitumie mkaa au wananchi wasikate miti, haiwezekani. Lakini matumizi ya misitu hii lazima yatumike kiendelevu. Kwa maana kuwe na programu maalum hata katika Vijiji vyetu kutenga baadhi ya maeneo kwa ajili ya miti. Miti hii ambayo itatumika kwa ajili ya mkaa. Kwa hivyo, nafikiri hili likifanyika kutakuwa utaratibu mzuri ambako kutakuwa hakuna ukataji ovyo wa miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine lilikuwa Bwanamiti wana miradi ya kuuza mikaa. Sasa niseme kwamba pale ambapo tutabaini hivyo Serikali itawachukulia hatua za kinidhamu watumishi wote hawa wanaofanya hivyo kwa sababu ni kinyume na taratibu za kazi na kinyume cha taratibu za sheria.

Ushauri uliotolewa na Mheshimiwa Mbunge ambalo niliosema hivi kwamba kila kijiji, taasisi, mji uwe na shamba la miti kwa ajili ya nishati. Nafikri ni ushauri mzuri sana na Wizara yangu inajitahidi kuhamasisha wananchi mmoja mmoja vikundi, vijiji, sekta binafsi na Mashirika yasiyo ya Kiserikali kuanzishwa misitu yao ili iwapatie mazao mbalimbali ya misitu ikiwa ni pamoja na kuni na mkaa.

Suala lingine lilikuwa ni kwamba Wizara iendeleze ufugaji nyuki ili wananchi wanufaike na shughuli hiyo. Hili nalo pia nasema kwamba nakubaliana kabisa na ushauri huu na kwamba nakubali kwa mwaliko tutapanga wakati muafaka wa kutembelea vikundi hivyo vya ufugaji nyuki. Nafikiri lingine pia ni la ukataji miti ambalo linajibu lile ambalo nililoeleza hivi karibuni.

Lingine lililozungumziwa juu ya Serikali itoe elimu kwa wananchi wanaolima tumbaku wapande miti, wanafyeka miti kwa ajili ya kilimo cha tumbaku. Nakubaliana kabisa na ushauri huu na Wizara kupitia programu ile ya *HASHI, IKRAF* inawahamasisha wananchi kutumia kilimo misitu ili kupunguza ukataji wa miti kwa ajili ya kilimo cha tumbaku. Aidha, wanahamasishwa pia kupanda miti.

Lingine ni kwamba vyanzo vya maji vitunze, upandaji miti uhamasishwe na kuhamasisha matumizi ya majiko sanifu. Wizara inahamasisha uhifadhi wa vyanzo vya maji na pia upandaji miti.

Lakini kama nilivyosema kwamba Wizara peke yake au sheria peke yake haiwezi kufanya kazi. Wananchi wenyewe wakishirikiana ndipo ambapo kwa kweli tutaleta mabadiliko katika sekta hii ya misitu.

Lingine ambalo nililoulizwa juu ya *speed boat* kwa Ziwa Tanganyika. Niseme kwamba *speed boat* ambayo imepelekwa Ziwa Tanganyika sasa hivi limetengemaa na linafanya kazi. Nina hakika hata kama sasa hivi mtu akitoka nje akipiga simu basi ataambiwa kwamba *speed boat* inafanya kazi. Mheshimiwa Mbunge ni hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo limezungumzwa ni kwamba Wizara inasimamia vipi suala la utafiti wa kina juu ya ufugaji, uvunaji na ulaji wa samaki nchini ili iweze kuleta mafanikio kwa bidhaa zitokanazo na samaki. Ningependa kusema Wizara imeweka mikakati ifuatavyo katika kusimamia utafiti wa uvuvi nchini. Kwanza kuwapatia mafunzo nje na ndani ya nchi wataalamu zaidi katika fani ya uendelezaji na ufugaji wa samaki na ukulima wa samaki. Suala hili kwa kweli hivi sasa tunalitilia mkazo mkubwa sana juu ya ufugaji wa samaki. Ufugaji wa samaki kwa kweli unaweza kufanyika popote pale na unaongeza fedha kwa wananchi na kwa maana hiyo unaondoa umaskini. Kwa hivyo hatutakuwa tutagemea tu bahari au maziwa. Imenunua vifaa vya kisasa vya Maabara, kituo cha kuendeleza ufugaji cha samaki cha Kingolwira, kimeimarisha kituo cha kuendeleza ufugaji samaki pia nchini na kuimarisha shughuli za ugani za uvuvi. Pia kushirikiana na Mashirika ya Kimataifa kufanya tathmini ya hali ya ufugaji samaki nchini kwa mfano *DFID* na Serikali ya Ufaransa. Pamoja na hayo tumeboresha vitendea kazi na kuimarisha ukusanyaji wa takwimu za uvuvi na *finally* kuwezesha utafiti kufanyika kwa kuongeza Bajeti ya utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala la wavuvi wanaopatwa na majanga baharini na maziwani. Labda niseme kwamba sheria na kanuni za uvuvi zinazotumika zinawataka wavuvi wanapokuwa baharini au katika maziwa wawe na vifaa vya kuokolea maisha na honi inayofanya kazi na kadhalika. Aidha, kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi jitihada zinaendelea za kudhibiti usalama wa vyombo vya wavuvi. Vyombo vinatakiwa kuwa si watu kwa hivyo vyombo viwe *checked* kabla ya kupewa leseni. Pia lingine ni kwamba utoaji wa taarifa juu ya hali ya hewa na taarifa mbalimbali utaendelezwa kwa kushirikiana na Idara ya Hali ya Hewa ili wavuvi wapate kuelewa hali ya hewa iko namna gani. Lingine ni kuhamasisha sekta binafsi katika kuanzisha huduma za kuokolea wavuvi kwa mfano kuwa na boti ya kuokolea wavuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo limezungumziwa ni juu ya kwamba mikakati ya kusaidia wavuvi wadogo wadogo katika ziwa. Aidha, ipo hali ya kutokuelewana kati ya wavuvi wakubwa na wale wadogo na pia tatizo la ujambazi ambalo lililokuwepo ziwani. Ningependa kusema kwamba Wizara yangu inahamasisha wenye viwanda katika kuweka utaratibu wa kuwakopesha wavuvi wadogo wadogo zana na vyombo vya uvuvi, hili linafanyika hasa katika Ziwa Victoria.

Pili, katika Ziwa Victoria tunaweza kusema hakuna wavuvi wakubwa. Katika upande wa bahari ndipo ambapo tunao wavuvi wakubwa. Kwa sababu tunacho kile ambacho tunasema *deep sea fishing.* Lakini kwa upande wa Ziwa Victoria hakuna wavuvi wakubwa vyombo vyote vikubwa yaani *trailers* vilipigwa marufuku tangu mwaka 1994. Wenye Viwanda vya Kusindika Samaki hawaruhusiwi kuendesha uvuvi wao wenyewe. Kwa hivyo wale wenye viwanda wenyewe kwa kweli kazi yao ni kununua samaki kutoka kwa wavuvi wadogo wadogo.

Kuhusu ujambazi ziwani wavuvi wameshauriwa kuunda vikundi vya ulinzi wa raslimali. Ningependa kusema kwamba hadi sasa wavuvi hawa wameitikia wito na hadi sasa vikundi 511 vimeshaundwa. Aidha, Wizara yangu inategemea kuvitambua vikundi hivi kisheria. Jukumu kubwa kwa kweli ni kulinda wavuvi na dhana zao. Katika kudhibiti wizi na vyombo na dhana za uvuvi kila mvuvi hutakiwa kukata leseni kwenye Wilaya anayokusudia kuendesha uvuvi. Upo utaratibu maalum kwa wavuvi wanaohamia maeneo mengine. Wale ambao wanahamia maeneo mengine ni lazima watoe taarifa kwa Afisa Uvuvi wa Wilaya ile. Bila ya kutoa taarifa kwa Afisa Uvuvi katika Wilaya ile anaweza kukamatwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la utafiti labda niseme kwamba Wizara inatilia mkazo mkubwa sana pia katika suala la utafiti na utafiti hapa tunazungumzia utafiti wa samaki. Tunacho chuo

*Tanzania Fisheries Reaseach Institute(TAFIRI)* ambacho kwa kweli kinafanya tafiti mbalimbali katika maziwa yetu pia katika bahari. Pia inashirikiana na Mashirika ya Kimataifa ya Nje kwa mfano *FAO*. Kwa mfano taarifa ya utafiti wa *FAO* ambayo imetajwa, wameitaja kwamba kuna idadi ya samaki katika Ziwa Tanganyika ambao Mkoa wa Kigoma ni tani 98,000, Mkoa wa Rukwa ni tani 24,000 je wavuvi wadogo watasaidiwaje? Kama nilivyosema kwamba pale mwanzo kutakuwa na Mfuko wa Uvuvi lakini hapo hapo kwa kupitia Wizara ya Fedha kutakuwa na utaratibu wa kusaidia wavuvi wadogo wadogo. *(Makofi)*

Kulikuwa na suala lingine juu ya Wanamnalingu ilitangazwa kwamba hawataki *Marine Parks* ya *Mnazibay* kwa vile itawazuia kuendesha shughuli zao za kutumia na shughuli zile za kutumia bahari katika maeneo yao. Labda niseme kwamba napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge Namkulala na uongozi wa Serikali wa Wilaya na Mkoa kwa kweli kwa kushughulikia suala hili. Labda niseme kwamba si kweli kwamba katika *Marine Parks* wananchi hawaruhusiwi kuvua katika maeneo yale au kutumia *Marine Park* kwa shughuli zao. Kuna utaratibu maalum ambao unaweka. Lakini nafikiri kwamba tatizo linatokea na si tatizo hili pia hata Mafia. Mafia pia tumelipata kwamba kuna baadhi ya wavuvi wakubwa ambao pengine wanaona wanakosa manufaa yale ambayo wangeyapata kwa hivyo wanaanza kupiga kampeni hizi za kusema kwamba kwa kweli *Marine Parks* si sawa na kadhalika pingeni na mambo kama hayo. Lakini napenda kwa kweli kuwahakikishia wananchi kwamba *Marine Parks* ni baharini kama vile *National Park* katika nchi kavu. Tunajua kwamba Wabunge wengi sana na wananchi wengi sana wanataka kuwa na *National Parks* na kwa maana hiyo *Marine Parks* zitasaidia na kuondoa umaskini kwa wananchi wale ambao watakuwa na *Marine Parks.* Sasa napenda kutoa wito kwa wananchi kwa kweli wasibabaishwe kabisa na watu wachache ambao wanataka kujaza matumbo yao kwa haraka sana. Wananchi waingie kwenye *Marine Parks* ili kuweza kuondoa umaskini wao. *(Makofi)*

Kulikuwa na suala la kuendelezwa fukwe za Lindi na Mtwara ili zichangie maendeleo na utalii kwa ujumla. Ningependa kusema kwamba Wizara yangu kwa kupitia *Marine Parks* ya *Mnazibay* inaandaa mpango shirikishi wa usimamizi, uendelezaji, uhifadhi wa fukwe katika jitihada za kuinua utalii wa Mwambao na kuzitumia kiendelevu.

Kwa hiyo, tuna programu hizi kwa kweli ambapo hivi sasa wiki ijayo nitazungumza na watu wa *World Bank* kuangalia ni jinsi gani hizi *Marine Parks* lakini maeneo ya fukwe pia ni jinsi gani ambapo kutakuwa na programu mbalimbali za kuweza kuondoa umaskini.

Programu za kuwapa mikopo wananchi, programu za utalii, programu za elimu, programu za kuwaongezea uwezo wa vyombo vyao na kadhalika. Hii ni programu ambayo naweza kusema ni kabambe ambayo tunashirikiana na Benki ya Dunia. Kwa hivyo, hivi karibuni kwa kweli tutaona mabadiliko makubwa kwa wananchi ambao wanaishi katika maeneo ya bahari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa makofi hayo kwa hivyo baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja na naomba kuomba fedha zile ambazo nimezitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Hoja imetolewa na imeunga mkono hatu a inayofuata.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 69 - Wizara ya Maliasili na Utalii**

Kif. 1001-*Administration and General* ........... Shs. 1,331,543,906/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge nadhani mmeona *mood* iliyopo humu ndani, hata hivyo nitawapa nafasi ili kila mtu apate nafasi yake, wako watatu.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama tunasema Waziri ni mzuri, hata mimi najua Waziri ni mzuri na anastahili kupongezwa sio kama tunasema mtu asichangie chochote. Ila nilikuwa nasema kwamba kwa kweli Waziri amejibu vizuri, nilikuwa naomba ufafanuzi katika mambo mawili. Jambo la kwanza ambalo ni muhimu sana linatuharibia katika nchi yetu ni jinsi Kenya wanavyotumia jina la Mlima wetu wa Kilimanjaro kwa ajili ya kujinufaisha na Waziri analitolea kauli gani? Pili mwaka jana katika Bunge hili nilizungumzia kuhusu maongezi na mimi na watu wa *TANAPA*. Na Waziri alikubali nikazungumze nao na nilikwenda Arusha kuzungumza nao. Lakini baadaye yakavunjika vunjika mazungumzo yale. Na kwa kuwa wananchi wananisukuma kwamba nije nihoji hapa Bungeni ni vizuri wakasikia nikihoji, imefikia wapi yale mazungumzo. Mkurugenzi tulizungumza naye lakini sikupata matokeo ya mazungumzo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kabla sijampa Mheshimiwa Waziri naomba nitoe ufafanuzi kidogo. Waziri alikuwa na muda wa kuendelea kujibu wote mnajua. Alikuwa na saa nzima lakini mkamshabikia amalize. Kwa hiyo, nadhani pengine yote haya yangepatiwa majibu. Sasa ni sisi wenyewe tumemwambia akae. Kwa hiyo, naomba mzingatie hilo pia.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kutangaza utalii kwa upande wa Kenya. Suala hili limezungumzwa mara nyingi sana. Lakini niseme kwamba sisi upande wetu tunalitangaza Mlima wa Kilimanjaro uko Tanzania na kama nilivyoeleza kwamba katika maonyesho ya utalii nje kwa kweli Kenya hawatangazi kwamba uko Kenya. Wakisema kwamba wanauona kutoka Kenya ni sahihi. lakini na sisi tunasema kwamba unauona kutoka Tanzania na pia unaweza kupanda Mlima wa Kilimanjaro kutoka Tanzania tu. Suala la *TANAPA* labda niseme kwamba ni suala ambalo tumewasiliana na Mheshimwia Mbunge na kuna wakati ambapo Waziri wa TAMISEMI alitoa maagizo kwa sababu kulikuwa na tatizo la suala la kisheria. Hivi sasa *TANAPA* kwa kweli inasaidia katika shughuli za Kimaendeleo pale Kilimanjaro. Lakini kulikuwa na suala ambalo ni la kisheria, pale ambapo kuna sheria ndogo basi sheria kuu ndiyo inakuwa na msimamo. Sasa labda niseme kwamba hivi sasa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi Vijijini kwa taarifa ambazo tulizokuwa nazo ni kwamba bado wako Mahakamani. Kwa hiyo, kama wako Mahakamani kuishtaki *TANAPA* sifikiri kama tunaweza kueleza zaidi ya hapo. *(Makofi)*

**MHE. KISYERI W. CHAMBIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuona *mood* ya Wabunge wenzangu kwa hiyo nimeamua nitamfuata Waziri mwenyewe. *(Makofi)*

**MHE KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia kwa kuzungumza nilimkumbusha Mheshimiwa Waziri juu ya barabara ile inayotoka Chubi, Itaswi, Kisaki ambayo ina ushirikiano baina ya Halmashauri na *TANAPA*. Nikasema tatizo kubwa ni tuta. Likishatengenezwa hilo tuta basi wananchi watafaidika na barabara hiyo. Sasa maelezo hayakutolewa kwa hiyo naomba yatolewe maelezo ili niweze kupeleka majibu kwa wananchi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mheshimiwa Suru. Ni kwamba mwanzo kabisa maombi ambayo yaliyoletwa ni ya kutengeneza sehemu ya barabara ambayo *TANAPA* walikubali kilomita 14. Lakini baada ya hapo Mkurugenzi wa Halmashauri alileta barua kwamba hilo sio *priority* na sasa hivi *priority* ni tuta. Kwa hivyo labda niseme kwamba nimezungumza na Mkurugenzi wa *TANAPA* na Mwenyekiti na kwamba hili sasa hivi watajaribu kuliangalia ni jinsi gani wataweze kumsaidia Mheshimiwa Suru.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kif. 1002 | - | *Finance and Account* ........... | Shs. 610,860,400/= |
| Kif. 1003 | - | *Policy and Planning*............. | Shs. 481,653,700/= |
| Kif. 2001 | - | *Wildlife* .............................. | Shs. 7,838,987,520/= |
| Kif. 3001 | - | *Forestry and Beekeeping*.... | Shs. 7,657,482,216/= |
| Kif. 3002 | - | *Fisheries* .......................... | Shs. 4,558,104,958/= |

Kif. 4001 - *Tourism* ............................Shs. 2,711,920,900/=
Kif. 4002 - *Antiquities Unit*...............Shs. 1,184,497,800/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 69 - Wizara ya Maliasili na Utalii**

Kif. 1003 - *Policy and Planning*....................Shs. 4,372,500,000/=
Kif. 2001 - *Wildlife* .......................................Shs. 7,979,635,500/=
Kif. 3001 - *Forestry and Beekeeping*...........Shs. 16,445,166,000/=
Kif. 4001- *Tourism* ......................................Shs. 2,117,086,300/=
Kif. 4002 - *Antiquities Unit* .........................Shs. 563,400,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii ya mwaka 2003/2004 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali makisio hayo. Naomba kutoa hoja

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Wizara ya Maliasili na Utalii Yalipitishwa na Bunge)*

*(Saa 12.54 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano Tarehe 23 Julai, 2003 Saa Tatu Asubuhi)*